Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

EQUIPPING CHURCH LEADERS
• EAST AFRICA •

KITABU CHA UFUNUO

na
Jonathan M. Menn
B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974
J.D., Cornell Law School, 1977
M.Div., Trinity Evangelical Divinity School, 2007
Equipping Church Leaders-East Africa
3701 N. Gillett St., Appleton, WI 54914
(920) 731-5523
jonathanmenn@yahoo.com
www.eclea.net

Disemba 2017

Kitabu cha Ufunuo ni moja kati ya vitabu vya Biblia ambavyo havieleweki vizuri na hutumiwa vibaya. Hata hivyo, ni moja kati ya vitabu muhimu sana vya Biblia. Ufunuo kina kama dokezo 630 za Agano la Kale tu. Kiliandikwa kwa, na kuhusu kanisa, ambalo linaonekana katika kitabu chote katika namna ya mifano. Kinafungamanisha pamoja na kukamilisha Biblia yote. Kitabu cha Ufunuo kiliandikwa kulielewesha kanisa namna Mungu anavyoshughulika na dunia, kuwaita Wakristo kustahimili katika mapambano dhidi ya nguvu za uovu, na kufariji na kutia moyo waamini kwa sababu Kristo ni mshindi. Kitabu hiki kwa kuendelea huzungumzia maswala: Uaminifu wangu wa msingi unaegemea wapi? Na ni nani ndiye Bwana wangu wa kweli? Kwa kutupa sisi mtazamo wa Mungu kuhusu dunia, Ufunuo kinasaidia kutuwezesha sisi kufanya uhakiki wa jamii zetu na tamaduni zetu.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

I. Aina……...…….....3
A. ***Barua (waraka)***……3
B. ***Unabii***……...3
C. ***Mafunuo***……...3
D. ***Mwongozo wa kutafsiri ishara kwenye Ufunuo***…….....5

II. Mbinu za tafsiri……...7
A. ***Mbinu ya Utangulizi***…….....7
B. ***Mbinu ya Kihistoria***…….....9
C. ***Mbinu ya Kinabii***……....10
D. ***Mbinu ya mawazo au njozi***……10
E. ***Ufupisho wa mbinu nne za hapo juu***……11
F. ***Mbinu ya Wateule***……...11

III. Hali ya makanisa mwishoni mwa karne ya kwanza……12
A. ***Ufalme na Utamaduni***……12
B. ***Suala la mateso***……...12
C. ***Matatizo ya ndani***……...13

IV. Kusudi na mada……...13
A. ***Kulielezea kanisa ni jinsi gani Mungu anavyojihusisha na dunia***……..13
B. ***Mwito wa kuvumilia kwenye kung'ang'ana na nguvu za uovu***……...13
C. ***Kuwafariji na kuwatia moyo Wakristo kwa sababu Kristo ni mshindi***……14

V. Muundo……...14
A. ***Utata, Umoja, na umuhimu wa muundo***……...14
B. ***Kujirudia kwa misemo na mawazo***……14
C. ***Msingi wa muundo wa yaliyomo***……15
D. ***Msingi wa muundo kifasihi***……16
E. ***Mpangilio wa kimuundo wa uwakilishi***……16
F. ***Muundo: sambamba hatua kwa hatua; siyo kwa mpangilio madhubuti wa wakati***……18
G. ***Ufunuo 1:19 na muundo wa kitabu***……...23

VI. Kanisa kwenye kitabu cha Ufunuo……24
A. ***Kitabu cha Ufunuo kiliandikwa kwa, kwa ajili ya, na kuhusu kanisa***……24
B. ***Umuhimu kwenye kitabu cha Ufunuo wa matumizi ya maumbo ya Agano la Kale kulielezea kanisa***……..25
C. ***Kanisa kwenye kitabu cha Ufunuo: takwimu kuu na ishara***……25

VII. Mtazamo wa mawazo makuu na vifungu……42
A. ***Ufu 1:1-20: Utangulizi***……42
B. ***Ufu 2:1-3:22: Barua kwa makanisa saba***……..42
C. ***Ufu 4:1-5:14: Kiti cha enzi, kitabu (gombo), na Mwanakondoo***……...44
D. ***Ufu 6:1-8:5: Mihuri saba***……45
E. ***Ufu 8:6-11:19: Tarumbeta saba***……..50
F. ***Ufu 12:1-15:4: Mwanamke, Joka, na Mnyama***……56
G. ***"Wanyama" wa Ufu 11:7; 13:1-18; 14:9; 15:2; 16:2, 10, 13; 17:3-17; 19:19-20; 20:10***……58
H. ***Ufu 15:5-16:21: Hukumu za vitasa saba***……...64
I. ***Ufu 17:1-19:10: Hukumu ya mwisho ya Babeli***……..66
J. ***Ufu 19:11-21: Kurudi kwa Kristo mara ya pili***……...72
K. ***Ufu 20:1-15: Kufungwa kwa Shetani, kutawala kwa Watakatifu, hukumu ya Shatani, na hukumu ya mwisho***……...74
L. ***Ufu 21:1-22:5: Mbingu mpya nan chi mpya: Yerusalemu Mpya***……..83
M. ***22:6-21: Hitimisho***……..89

VIII. Ufunuo umefungwa pamoja na kukamilisha Biblia yote……...89
A. ***Uumbaji mpya wa Ufunuo umeungana na uumbaji asili wa Mwanzo***……89
B. ***Uumbaji mpya wa Ufunuo ni zaidi ya uumbaji wa asili wa Mwanzo***……90

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

XII. Maana ya Kitabu cha Ufunuo……90

BIBLIOGRAFIA……..……..……...……..91

MWANDISHI..…….....98

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Kitabu cha Ufunuo

I. Aina

Karibia watafsiri wote wanatambua kwamba Ufunuo umejumuisha aina tatu: barua (waraka); unabii; na mafunuo (Osborne 2002: 12). Aina hizo zimeunganishwa au zimechanganywa pamoja. Kwa hiyo, "mtazamo unaofaa zaidi ni kwamba Ufunuo ni 'unabii uliotolewa kwenye umbo la mafunuo na kuandikwa kwenye muundo wa barua au waraka' ili kuwahimiza wasomaji au wasikilizaji wake kubadilisha mienendo yao kwenye nuru ya ukweli uliyoinuka kupitia ujumbe wa kitabu" (Beale 1999: 39).

A. *Barua (waraka)*

"Ufunuo umefungwa kwa mfumo wa ki-barua (1:4-8 na 22:10-21). Patano hili pekee linakiondoa kutoka kwenye vitu vinavyotakiwa kwa ajili ya mafunuo. Kanuni (1:4-8) zimebeba vipengele vya aina ya ki-nyaraka—mtumaji, anwani, salaam, na kuongezewavipengele vya nyimbo. Machapisho (22:10-21), kwenye muundo mzuri wa barua za kale, ikifupisha muundo wa uandishi, pamoja na uhalali wa Yohana kama mtunzi aliyevuviwa Uungu." (Pate 1998a: 12) Umuhimu wa tafsiri ya Ufunuo kuwa barua ni kwamba kitabu kiliandikwa kuwa wazi na cha kueleweka na wasomaji wake wa karne ya kwanza. Kwa hiyo, watu ambao husema kwamba Ufunuo ni "msimbo wa siri" hili linatumika tu kwa matukio ambayo yalitokea mara kabla ya kurudi mara ya pili kwa Kristo, miaka elfu moja baada ya karne ya kwanza, siyo sahihi.[1]

B. *Unabii*

Tangu mwanzo na mwisho wa kitabu Yohana anauita Ufunuo kitabu cha "unabii" (**Ufu 1:3; 22:7, 10, 18, 19**). Vifungu vingine vinazumgumza kuhusiana na manabii, au watu wakitoa unabii (**Ufu 2:20; 10:7; 11:3, 6, 10, 18; 16:6; 18:20, 24; 19:10; 22:6, 9**). Hili halimaanishi kwamba Ufunuo kinahusiana na mambo ya wakati ujao tu. Kwa mfano, **Ufu 10:11** na **11:3** vyote vinatumia neno "unabii." Hata hivyo, katika kesi zote mbili neno linaashiria kulitangaza neno, matendo ya haki, na hukumu za Mungu, kama kinyume na "kutabiri mambo yajayo."

Tunapaswa kukumbuka asili ya unabii wa Kibiblia, i.e., unabii wa hukumuna unabii wa wokovu, viliandaliwa kubadilisha tabia za watu. Huu pia ni ukweli wa Ufunuo.[2] TUkweli kwamba kitabu chote kinalenga kwenye wakati uliopo, kilikusudiwa kuwa wazi kwa wasikilizaji wa Yohana wa karne ya kwanza, na kimeandaliwa kuathiri tabia za wasomaji, yaweza kuwa imetolewa kutokana na ukweli kwamba vyote tokea mwanzoni (**Ufu 1:3**) na hata mwishoni (**Ufu 22:7**) msomaji anashauriwa "kuchukua tahadhari" kwa maneno ya unabii. Hivyo, kama ilivyo kwa nabii zote za kibiblia, kipengele cha unabii wa Ufunuo kinatambua au kufahamuasili na kusudi la Mungu kwenye mazingira ya sasa ya Makanisa, kuona ni jinsi gani kusudi la Mungu la wakati wote linavyohusiana na hali ya sasa, na kutaka majibu kupitia kwa watu. Ukweli kwamba kitabu cha Ufunuo kiliandaliwa kueleweka na wasomaji au wasikilizaji wa Yohana kwenye karne ya kwanza kumeonyeshwa kupitia **Ufu 22:10** ambayo inasema, *"Usiyatie muhuri maneno ya unabii wa kitabu hiki, kwa maana wakati huo umekaribia."* Hili ni kinyume na **Dan 8:26** pale Danieli alipoambiwa *"yafunike maono hayo; maana ni ya wakati ujao baada ya siku nyingi."*

C. *Mafunuo*

Mafunuo ni aina fulani ya unabii. "Ni vizuri zaidi kuuelewa mafunuo kama mkazo wa unabii. . . . Mafunuo haupaswi kuonekana kama uko tofauti sana na unabii, ingawaje una kina mkusanyiko wa maandishi wenye upeo mkubwa zaidi na ukali zaidi na kiini cha nabii za kipekee." (Beale 1999: 37) "Katika kutofautisha

---

[1] "Usomaji halisi wa Ufunuo kama kitabu cha fumbo kwa kufafanua ramani kwenye historia ni kuuvuruga na kuusaliti ujumbe wake" (Stylianopoulos 2009: 31). Richard Bauckham anaandika kwamba tafsiri inayojulikana ya waamini wa msingi wa mpito ya Ufunuo kimsingi hawaelewi aina ya unabii wenyewe: "Kinyume chake, tafsiri ya Waamini wa msingi, ambao unapatikana kwenye unabii Kibiblia huweka alama ya fumbo kwenye utabiri wa matukio maalum karne nyingi baadaye kuliko nabii, kutokuuelewa unabii kwa umuhimu kuliendelea kwa kupuuza kuuliza hiki kilimaanisha nini kwa wasikiaji wake wa kwanza" (Bauckham 1993b: 152-53).

[2] "Ufunuo unathibitisha uhalisia wa maelezo ya awali ya unabii wa Kikristo. . . . Wakati ambao ujumbe wa Wakristo wa mwanzo ulilenga juu ya tafsiri na kuyafunua maandiko na tamaduni, unabii wa awali wa Kikristo ulitangaza hukumu au wokovu" (Schüssler Fiorenza 1980: 109). Uchambuzi wa David Aune wa "barua saba kwa makanisa saba" (**Ufunuo 2-3**) unafunua kwamba "muundo wa hotuba ya kinabii ambayo sehemu ya kati ya matangazo saba mengi yanafanana ni kinywa cha wokovu na hukumu, mwendelezo wa unabii wa baada ya uhamisho wa Wanawa Israeli" (Aune 1983: 277; angalia pia Ulfgard 1989: 13; Schüssler Fiorenza 1991: 46-47; Schnabel 2011: 13).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mafunuo na unabii, tofauti iliyo dhahiri kabisa inahusu ile njia ambayo kwayo ujumbe unatumwa. 'Neno la Bwana' la kinabii hutoa nafasi kwa ufunuo kwa njia ya maono na ndoto. Uashiriaji, maandishi picha, namba—huonekana tayari katika vifungu vya kinabii—huja mbele pamoja na ufafanuzi mkuu wa kiufunuo. Maandishi ya mafunuo wakati mwingine hutafsiri tena unabii wa hapo nyuma. . . . La muhimu zaidi, hata hivyo, ni utofauti wa fokasi ya ujumbe. Manabii walizitangaza kazi za Mungu katika na kupitia kipindi cha historia. Wenye ufunuo waliutarajia mkono wa Mungu kuingilia kwa nguvu mwishoni na baada ya kipindi cha historia." (Green 1984: 62) Neno la kwanza la kitabu, *apokalupsis* (mafunuo; ufunuo), linaonyesha aina ya mafunuo wa kitabu. Hili linathibitishwa kupitia maono ya hali ya juu na asili ya mifano ya kitabu chote.[3]

1. <u>Kiini cha kitabu ni mifano.</u> Ufunuo kama wote, kuanzia na **Ufu 1:1** hutumia *sēmainō* ("mawasiliano kwa njia ya mifano") na *deichnumi* ("kuonyesha"), pamoja na kurudiwa kwa kanuni ya utangulizi "Nikaona" au maelezo sawa na hayo (**Ufu 4:1; 12:1-3; 13:1-3; 14:1; 17:1-3**, **20:1**) huchangia "asili ya jumla ya mawasiliano kwa njia ya ishara" (Beale 1999: 973). "Ufunuo 1:1 ni njozi ya Danieli 2:28-29, 45 [ambayo] inathibitisha kwamba hapa neno linamaanisha 'ishara.' . . . Kwenye mwanga huu, mbinu maarufu ya maelezo ya kitabu cha Ufunuo—kilitafsiriwa kiuhalisia isipokuwa umelazimishwa kukitafsiri kwa ishara—lazima kigeuzwe kichwa chake. Badala yake, maelezo ya kiprogramu sahihi kuhusiana kitabu na aina ya mawasiliano kwenye 1:1 ni hii kukunjwa na kufunikwa kwake ni ishara, ili kwamba maelezo yanayoendelea yaweze kugeuzwa na kusema 'kutafsiriwa kwa ishara isipokuwa umelazimishwa kukitafsiri kiuhalisia.' Bora kuliweka, msomaji atarajie kwamba maana kuu ya ufunuo wa Mungu kwenye kitabu hiki ni ishara." (Beale 2006: 54, 55)

2. <u>Vyanzo vya ishara za mafunuo.</u> Yohana alitumia ishara kwa sababu aliona maono ambayo yasingeelezeka kwa maneno pekee yake, hivyo aliyaweka kwenye picha. "Vyanzo kwa kuyatafsiri inatoka kwenye Agano la Kale, fasihi ya Agano shirikishi, na ulimwengu wa Rumi ya Kigiriki—kwa maneno mengine, kwenye ulimwengu wa kawaida wa wasomaji halisi kwenye eneo la Asia" (Osborne 2002: 17). Kiwango cha uhitaji wa Ufunuo kwenye Agano la Kale kwa ishara zake kinaonekana kwenye kweli kwamba Ufunuo imebeba na kugusia takribani ishara 630 kutoka kwenye Agano la Kale pekee. Vivyo hivyo, ili tuweze kuelewa picha za Yohana ni lazima kuangalia, siyo kwenye siasa na matukio mengine ya siku zetu, bali fasihi na hali ya siasa ya jamii ya siku za Yohana.

3. <u>Asili ya ishara za mafunuo.</u> "Picha za ufunuo hazimaanishi kuwa ni picha ya mnato inayolenga kweli halisi; mara nyingi ni ishara zinaziwakilisha karibia kweli za Kiroho ambazo hazielezeki kirahisi kwa picha" (Ladd 1972: 102). Hii ndiyo sababu moja kwanini mara nyingi manabii "huelezea maono yao kwa uangalifu na kwa wasi wasi na mifano . . . tusije kusahau uwezo wenye kikomo wa uzoefu wa mwanadamu na lugha inayowakilisha kweli za mbinguni" (Johnson 2001: 216n.24, e.g., *"palikuwa na <u>mfano</u> wa kiti cha enzi, kuonekana kwake <u>kama</u> yakuti samawi"* [**Ezek 1:26**]; *"Nikaona <u>kitu mfano</u> wa bahari ya kioo iliyochangamana na moto"* [**Ufu 15:2**]).

Ishara tofauti zaweza kutaja kitu kile kile lakini kikatupa sisi mtazamo tofauti au msimamo kwenye somo hilo. Kwa mfano, kwenye **Ufu 4:1** mbingu zimeonyeshwa kama chumba cha kiti cha enzi, na kwenye **Ufu 6:9** zimeonyeshwa kama hekalu. "Ni mtiririko wa mawazo ya kimafunuo ambayo yanafanya hili liwezekane. . . . Kwa uhakika, Mungu hakai kwenyye kiti cha enzi; yeye ni Roho wa milele ambaye ama hasimami au kukaa au kulala. Picha ya Mungu kukaa kwenye kiti chake cha enzi ni njia ya ishara ya kusisitiza Ufalme na mamlaka ya Kiungu." (Ladd 1972: 102) Sambamba na hilo, Kristo ameonyeshwa kama simba (**Ufu 5:5**) na kama Mwanakondoo (**Ufu 5:6**). Kwenye kitabu chote, kanisa limeelezewa kwa njia tofauti tofauti, mara nyingi kwa njia ambayo inaonekana ngumu kueleweka. Kwa mtiririko huu, Ishara pia yaweza kuwa safu mbali mbali. Kwa mfano, kwenye **Ufu 17:1-4** Yohana alimwona mwanamke ambaye ni kahaba; **17:8** inasema kwamba alikuwa ni *"mji mkubwa, ambao unatawala juu ya wafalme wa dunia"*; **17:5** inamwita huyo mwanamke *"Babeli mkuu."* Babeli yenyewe siyo ukomo wa mji mmoja lakini ni ishara ya ulimwengu wote wa uchumi wa kijamii na tamaduni za kidini au za kistaarabu.

Kwa nyongeza, "kitendawili ni kiini cha ishara." (Johnson 2001: 9). Hivyo, mara kwa mara mfano kwenye kitabu chote ni kwamba "vitu siyo kile kilichoonekana kuwa." Kwa mfano, Kanisa la Filadelfia lilikuwa na *"nguvu kidogo"* (**Ufu 3:8**); hata hivyo, *kwa sababu* ya ukweli huo Kristo

[3] Mfululizo wa sehemu tatu za mhadhara wa sauti wa D. A. Carson kuhusiana na asili na utendaji wa kimafunuo, pamoja na msisitizo maalum juu ya kitabu cha Ufunuo, wenye kichwa cha habari "Kuhubiri kiufunuo," inaweza kusikilizwa au kupakuliwa bure kutoka kwenye wavuti ya: http://thegospelcoalition.org/index.php?/resources/name-index/a/DA_Carson/topic/End+Times.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

atawafanya wale wa "sinagogi la Shetani" waje *"kusujudu mbele ya miguu yako, na kuwafanya wajue ya kwamba nimekupenda"* (**Ufu 3:9**). Kwa namna nyingine, kwa kanisa lililoko Loadikia alisema, *"Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu"* (**Ufu 3:17**); hata hivyo, ukweli, kulingana na Kristo, ni kwamba wao ni *"mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini , na kipofu, na uchi"* (**Ufu 3:17**). Kupitia kitabu chote, Wakristo wanaonekana kama kwamba wameshambuliwa na kushindwa na nguvu za Shetani na uovu (e.g., **Ufu 11:7; 13:7**); bado kivitendawili, ni vifo vyao halisi, kwa sababu ya uaminifu wao kwa injili, ambao unafunua ushindi wao (e.g., **Ufu 6:9-11; 12:11; 20:4-6**).

D. ***Mwongozo wa kutafsiri ishara kwenye Ufunuo***

1. Baadhi ya ishara hutafsiriwa kwenye Ufunuo wenyewe. Nyota saba ni malaika wa makanisa saba (**1:20**); vinara saba vya taa ni makanisa saba (**1:20**); taa saba za moto ni Roho saba za Mungu (**4:5**, i.e., Roho Mtakatifu); mabakuli ya manukato ni maombi ya watakatifu (**5:8**); joka kuu ni Shetani (**12:9**); Kitani nzuri, ing'aayo, safi, ni matendo ya haki ya watakatifu (**19:8**). Wakati kitabu chenyewe kinapofafanua baadhi ya ishara, kasha popote ishara hizi zilizofafanuliwa zitakapojitokeza baadaye kwenye kitabu bila maelezo, upo uwezekano kwamba zinamaanisha jambo lile lile lililofafanuliwa mwanzoni. Vinara viwili vya taa kwenye Ufunuo 11:4 ni simulizi iliyojitokezaya hili (hivyo, mashahidi wawili bila shaka siyo manabii binafsi lakini ni ushirikiano wa kanisa kwenye utukufu wake na majukumu yake ya kushuhudia)." (Beale 2006: 55-56)

2. Ishara zingine zinaonyesha mwendelezo pamoja na vitabu vingine vya Agano la Kale au Agano Jipya. Ingawaje picha za Yohana zina msingi wake kwenyeulimwengu wa kawaida wa wasomaji wa karne ya kwanza, picha hizo siyo kumbukumbu ndogo ya kihistoria. "Kwa sababu picha za Yohana ni picha zilizoandaliwa kupenya tabia muhimu ya nguvu itendayo kazi kwenye ulimwengu wake na mambo ya mwisho yanayofuatana nayo, kwa kiwango kikubwa aliachili mbali tu vipengele dhahiri vya ulimwengu wake" (Bauckham 1993b: 156). Kanuni hii inaonekana kwa jinsi Yohana alivyolitendea Agano la Kale. Yohana, kama manabii wote wa Kibiblia, alitafsiri kile kilichokuwa kimeandikwa kabla kwa nyakati mpya na mazingira mapya. Hatua ya msingi ya kuunganishwa ni kuja kwa Yesu Kristo mara ya kwanza, ambako kwa kina kulibadilisha mazingira ya kitheolojia. Kama matokeo ya umuhimu wa Kristo, ingawa picha iliyochorwa kutoka kwenye Agano la Kale hubaki inatambuliwa, Dennis Johnson anaonyesha kwamba "zilibadilishwa na kuundwa tena kwa maandalizi mapya—kama ambavyo tungetarajiat, kwakuwa sadaka na ufufuo wa mwanakondoo ulileta vita ya nyakati kwenye awamu mpya na uwanja wa shughuli" (Johnson 2001: 13). Kutolewa kwa hali mpya ya ukombozi kihistoria na mazingira ya mkristo ya Ufunuo, kama vyombo vya Agano la Kale na picha kama hekalu, madhabahu, na manukato vilipewa maana mpya.

3. Zile ishara ambazo hazikufafanuliwa kwa wazi kwenye kitabu zinahitaji kutafsiriwa kulingana na mazingira, wazo kuu ambalo Yohana aliliwasilisha, na kusudi la jumla la unabii wa ki-ishara. "Bila shaka ni kwamba Mungu alichagua ishara za sirikutoka kwenye ghala la kawaida la ishara za ki-mafunuo kwenye karne ya kwanza ili *kuwaweka wasomaji mbali na kile halisi anachoenda kukifanya na kuelekea maana ya Kitheolojia* ya ni jinsi gani atakavyokifanya. Hatujui ni nini kitakachoenda kutokea nyuma ya picha ya mapigo la nzige, kuanguka kwa nyota, milipuko ya volkano, na dhoruba ya kutisha. Baadhi yaweza kutokea kiuhalisia, mengi hayatakuwa. Ni muhimu kutambua kwamba hatujui mengi kuhusiana na kurudi mara ya pili kuliko walivyofanya wanafunzi Wayahudi wa Yesu kuhusiana na kuja kwa mara ya kwanza." (Osborne 2002: 16, msisitizo umeongezwa)

Kwa mfano, **Ufu 16:16** (angalia pia **20:9**) inalitaja kusanyiko la wasiomcha Mungu kwa ajili ya vita kwenye eneo liitwalo Har-Magedonia. "Kwanini Har-Magedonia? Palikuwepo, tunayo kila sababu ya kuamini, hakuna eneo kama hilo. Jina ni ishara. Ni neno tata lililotolewa kutoka Kiebrania na likiwakilisha mlima wa Megiddo. Kwa hili tunarudishwa nyuma kwenye historia ya Agano la Kale, Katika hiyo ambayo kuna uwanda mkubwa wa Megiddo, lililo maarufu zaidi Palestina, lililoonyeshwa zaidi ya tukio moja sehemu maarufu. Kwa uhalisia, eneo hilo lilikuwa maarufu kwa mauaji makuu mawili, lile la Wakaanani walioalikwa na Baraka, kusherehekea kwenye wimbo wa Deborah [**Waamuzi 5**], na lile ambalo mfalme Yosia alianguka [**2 Nyakati 35:22**]. Mwanzoni bila shaka lilielezwa, kwa kuwa maadui wa Israeli waliokuwepo pale waling'olewa kabisa." (Milligan 1896: 272; angalia pia Schnabel 2011: 233, 237) Hivyo, kumbukumbu kwenye **Ufu 16:16** (angalia pia **20:9**) haiyangazi kwamba kutakuwepo na vita ya mwisho ya kimwili kwenye eneo halisi (ambalo halipo) mlimani, uwandani, au kambini, bali inachora *muunganisho wa kitheolojia* kuonyesha kile kitakachotokea kwa

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

maadui wote wa Kristo.[4]

Zaidi, kwenye kutafsiri ishara za Ufunuo ni lazima wakati wote kuweka akilini kusudi la kinidhamu na maadili lililoko nyuma ya nabii zote, ikijumuisha na mafunuo: kuwafanya watu wa Mungu waone kweli za Kiroho kutoka kwenye msimamo wa Mungu na majibu ya mapenzi na makusudi yake. Hivyo, Hakan Ulfgard, kwenye kuzungumzia ishara na mihuri ya Ufunuo, tarumbeta au parapanda, na mabakuli, anasema kwamba "maana ya uandishi huu wa unabii wa kimafunuo ni *kuwafariji* wasomaji kwenye mtazamo wa mateso ambayo tayari yalishaanza na kwamba yangekuwa hata yangesisitizwa zaidi, na *kuwatia changamoto* kuvumilia" (Ulfgard 1989: 29). Beale anaongeza, "Maonyo ya kiishara huwashtua waamini wa kweli nje ya uvivu wao wa Kiroho kwenye kuenenda pamoja na hali hiyo ya dhambi ya wengi wasioamini" (Beale 2006: 59).

4. Mifano miwili ya kawaida ya matumizi yasiyo halisi ya lugha kwenye ufunuo.

a. *Hesabu kwenye Ufunuo.* "Hesabu zilitumika kwenye fasihi ya mafunuo kama ishara za mawazos. Hili limedhihirika wazi kwenye uchunguzi linganishi ndani ya fasihi." (Summers 1960: 180) Matumizi yao ya kiishara kwenye fasihi ya mafunuo, ikijumuisha na kitabu cha Ufunuo, ni ya "kunyumbulika" (Johnson 2001: 15). Hesabu au namba kuu nne ambazo zinatoka kwenye wingi wa namba kitabuni zilitotumika ni 4, 7, 10, na 12. Ingawa baadhi huziangalia namba kwenye Ufunuo kama halisi, "bila shaka inaonekana zaidi kwamba namba kwenye kitabu zina maana yak i-ishara, kama ilivyokuwa kawaida kwenye ufunuo wa zamani. Kila namba moja inakusudia kumaanisha ukamilifu kwenye andiko lote. . . . Hili halimaanishi kwamba hakuna namba inayoweza kuwa halisi. Bila shaka zilikuwepo kabila kumi na mbili na Mitume kumi na wawili, lakini hata namba hizo zilichaguliwa na Mungu kwa sababu za kitheolojia." (Osborne 2002: 17)

Kwa mfano, mwanzoni Kristo alionekana kama *"mtu mfano wa wanadamu . . . namacho yake [mwaili yaliyokamilika, kama pamoja na watu] yalikuwa kama mwali wa moto"* (**Ufu 1:13-14**). Kwenye Ufu **5:6** Kristo anaonekana kama *"Mwanakondoo amesimama, alikuwa kana kwamba amechinjwa, mwenye pembe saba na macho saba."* Saba, kama namba ya ukamilifu au utimilifu, ikimaanisha mamlaka makamilifu ya Kristo ("pembe saba") na mjuvi wa yote ("macho saba" = ukamilifu wa maono). Kwenye mifano hii tunaziona ishara na matumizi mtambuka ya namba au hesabu zihusianazo na aina ya mafunuo. "Ishara hizi za kihesabu zinaeleza kwamba isipokuwa kipo kiashiria cha wazi kwa tafsiri halisi, namba au hesabu kwenye ufunuo wa Yohana zinatakiwa kujulikana kuwa na maana ya ki-ishara" (Schnabel 2011: 63).

b. *Kumbukumbu za wakati kwenye Ufunuo.* "Kwa kuwa 'saa moja' la utawala wa wafalme kumi pamoja na mnyama (17:12) haiwezekani kuonekana kuwa kulikusudiwa kiuhalisia, hatupaswi kutarajia kipindi chochote cha muda kwenye Ufunuo kuwa halisi" (Bauckham 1993a: 449). Sambamba na hilo, "siku kumi" za dhiki (**Ufu 2:10**) kwa wazi hazimaanishi uhalisia. Kama zilivyo nyingine nyingi kwenye kitabu, Yohana anafanya maunganisho ya Kitheolojia, hatupi kilicho halisi, "historia iliyoandikwa kabla ya wakati."

Katikati ya kitabu tunaona kipindi cha wakati kikijirudia, vikizungumziwa kwa njia tofauti: *"miezi arobaini na miwili"* (**11:2; 13:5**); *"siku elfu na mia mbili na sitini"* (**11:3; 12:6**); *wakati, nyakati, na nusu wakati"* (**12:14**). Vipindi hivi vya wakati ni msimbo au fumbo, siyo halisi. Ikiwa vipindi hivyo vya wakati vitachukuliwa kwa uhalisia, na ikiwa kanisa lilijua ni lini kipindi halisi cha wakati kinaanza, basi Wakristo wangekokotoa ni lini mwisho utakuja. Kwakuwa hili ni kinyume na maelezo mengi ya Yesu kwamba mwisho haujulikani, tafsiri "halisi" haitakuwa sahihi (angalia Schnabel 2011: 83). Zote zimeibuka kutoka au ni mbadala wa nyakati ulioanzia kwenye **Dan 7:25; 9:27; 12:7, 11-12**. Kumbukumbu ya wakati kwenye kitabu cha Danieli kiasili ilitumika kwa miaka mitatu na nusu ya vikwazo vya Antiochus Epiphanes

[4] Meredith Kline anasema, kwa mazingira na sababu za kisarufi, kwamba "Har-Magedon" ilipaswa kuwa ilitafsiriwa kama *"Har Mō'ed"* ("Mlima wa kusanyiko"). Hili lingependekeza kwamba Har Magedon ni Mlima Sayuni na kwamba vita vya Har Magedon ni mgogoro wa Gogu na Magogu wa **Ezekieli 38-39**, ambao ulielezwa kwenye **Ufu 16:12-16; 19:11-21; 20:7-10** kama kilele cha jitihada za kuliangamiza Kanisa ambacho kiliondolewa na *kurudi kwa Kristo mara ya pili.* (Kline 1996: 207-22) Kwenye Ufunuo, Mlima Sayuni ulitumiwa kwa mfano kuonyesha "Kanisa kama maelezo ya kidunia ya Mlima Sayuni wa Mbinguni" (Johnson 2001: 235). Wanatheolojia vivyo hivyo huelewa asili ya picha ya Megido lakini huitumia kwenye kuangamizwa kwa Yerusalemu mwaka BK 70 (angalia DeMar 1999: 317-19).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

dhidi ya Israeli mpaka uasi wa Wamakabayo ulipofanikiwa. Kwenye aina hii ya mbinu ya kinabii, hata hivyo, agano shirikishi la maandiko ya Kiyahudi huchukulia kipindi hiki cha wakati kumaanisha "wakati wa jumla ta majaribu kwa waamini, kama wakati unaofuatana na utumwa wa Waisraeli Babeli, au kipindi ambacho ni lazima kipite kabla ya ukombozi wa mwisho wa Israeli" (Beale 1999: 565; angalia pia Carson 2011: 25-27; Storms 2013: 483 [vipindi vyote hivi vya wakati "vyote ni vya *Kitheolojia*, siyo nafasi ya mfuatano au mtiririko wa wakati. Kwenye mtazamo wao wanayo *aina au ubora* wa wakati, lakini siyo muda wake."]). Yohana anachukulia kipindi hiki cha miaka mitatu na nusu kwenye uwakilishi wa ufahamu wake wa wakati wa majaribu makali mpaka pale Mungu atakapowapa watu wake msaada wa mwisho na analitumia kwa kanisa. **Ufu 12:5-6** inaonyesha kwamba kipindi hiki cha kujaribiwa kilianza wakati wa kufufuka na kupaa kwa Kristo. Kitaishia na kurudi kwake kwenye utukufu wakati wa *parousia.*

Lipo la ziada kwenye "miaka mitatu na nusu" kuliko tu kuharibiwa kwa urefu wa wakati ambao umeongezeka kutoka kupaa kwa Kristo mpaka *parousia.* Hili linaonekana kwa jinsi Yohana alivyotengeneza vipindi vya wakati. Wakati wa watu wa mataifa kuukanyaga "mji mtakatifu" (**11:2**) = wakati wa kutoa unabii kwa "mashahidi wawili" (**11:3**) = wakati wa "mwanamke" kuwa nyikani (**12:14**). "*Miezi arobaini na miwili"* (**11:2; 13:5**), *"siku elfu na mia mbili na sitini"* (**11:3; 12:6**), na *"wakati, nyakati na nusu wakati"* (**12:14**) zote ni njia tofauti za kukitaja kipindi kile kile, lakini njia tofauti ya kukitamka kipindi hiki cha wakati huashiria mtazamo tofauti au msisitizo wa Kitheolojia. Kwenye utaratibu wao wa mwonekano na umuhimu, zimepangwa kwa mpangilio wa muda: *"miezi arobaini na miwili"* inawataza maadui wa kanisa na hasira zao juu ya Kanisa; pale ambapo *"siku elfu na miambili na sitini* na *"wakati, nyakati na nusu wakati"* hutazama kwenye mashahidi wa kanisa na ulinzi wa Mungu, kama ifuatavyo:[5]

A. *Miezi 42*: "Mji mtakatifu" utakanyagwa na mataifa (**Ufu 11:1-2**).
  B. *Siku 1260*: "Mashahidi wawili" watatoa unabii na hawatadhuriwa (**Ufu 11:3-6**).
  B'. *Siku 1260 [Kama zilicyoongezwa kwa "wakati, nyakati na nusu wakati"]*: "Mwanamke" atasitawi na kulindwa nyikani (**Ufu 12:6, 13-16**).
A'. *Miesi 42:* "Mnyama" atanena makufuru na kufanya vita dhidi ya "watakatifu" (**Ufu 3:5**)

Mateso na usalama, majaribu na shuhuda, kutenganishwa na kusitawi vyote vimefungwa kwenye maelezo ya wakati wa kujaribiwa kwa Kanisa. Kupitia hayo yote, maelezo haya pia yanaonyesha au kudhihirisha mamlaka ya Mungu juu ya Kanisa, Shetani, mateso, na uovu.

II. <u>Mbinu za tafsiri</u>

Maswali muhimu kuhusiana na kitabu cha Ufunuo ni: Ni kwa kiwango gani kitabu hiki kinahusiana na karne ya kwanza (i.e., wakati kilipokuwa kinaandikwa, na mazingira na wasikilizajiau wasomaji ambao waliandikiwa)? Kwa kiwango gani kinahusiana na kipindi mara kabla ya Yesu kurudi tena? Na kwa kiwango gani hasa cha mpito wa kihistoria (i.e., kuhusiana na kanuni ambazo zilitumiwa kipindi chote cha historia, bila kuyataja matukio maalum hasa ya kihistoria)? Majibu tofauti kwa maswali haya yanatuongoza kwenye mbinu kuu tano za utafsiri wa kitabu.

A. *Mbinu ya Utangulizi*

Mbinu ya utangulizi inang'ang'ania kwamba kitabu kinasimulia matukio kwenye karne ya kwanza. Yohana alikuwa akiyaambia makanisa ni jinsi gani wangechukuliana na ukatili na jinsi Mungu atakavyowaokoa na watesi wao. Ipo misingi miwili tofauti ya mbinu ya Utangulizi: Nafasi ya awali ya watangulizi ni kwamba Ufunuo "hauhusiani na ama wigo wa historia ya Dunia au mwisho wa Dunia, lakini unahusiana na matukio ambayo yalikuwa karibu na hatima ya Mtakatifu Yohana na wasomaji wake. . . . Kitabu cha Ufunuo ni 'mashtaka ya agano,' kikitabiri kumwagwa kwa hasira ya Mungu juu ya Yerusalemu. Ni unabii wa kipindi

[5] Angalia Johnson 2001: 172; angalia pia Silva 2014: 4:673 (Vifungu hivi vyote "huzungumzia kipindi kile kile, nyakati za Kanisa, ambazo ni moja ya mashahidi wa kinabii wakati uo huo ni moja ya mateso. Kwenye mwanga wa umilele ni ulinganifu wa kiwango kifupi cha wakati, ingawa wakati kinapoelezewa kwa kigezo cha siku huonekana kuwa kirefu"); Bauckham 1993a: 401 (42 na 1260 zote ni namba "mstatili", i.e., hata jumla ya mfululizo wa namba, "kuonyesha kipindi hiki cha wasiwasi ambacho mnyama na watakatifu wanapingana,"kama kupingana kwa namba "mstatili", i.e., jumla ya mfuatano wa namba, ikijumuishwa 666 ambayo inamwakilisha mnyama, na namba "mraba", i.e., jumla ya mfuatano wa namba usiokuwa wa kawaida, ikijumuishwa 144 ambayo inawawakilisha watakatifu.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kijulikanacho kwenye maandiko kama ‘Siku za Mwisho,’ kikimaanisha siku za mwisho za taifa la agano la Israeli, ‘kizazi’ cha miaka arobaini (Math. 24:34) baina ya kupaa kwa Kristo mwaka (BK 30) na Yerusalemu kuangukia kwa Warumi mwaka (BK. 70). Kilitabiri matukio ambayo Mtakatifu Yohana alitarajia wasomaji wake kuyaona ghafla.” (Chilton 1987: 51-52; angalia pia Preston 2010: 17-18, 230) Muundo wa pili wa utafsiri wa Utangulizi unashikilia kwamba Ufunuo ni unabii wa ushindi wa kanisa dhidi ya maadui wake: Waisraeli wasioamini na Dola ya Rumi (Chilton 1985: 165-66; Bahnsen 2015: 9-22).

1. Nguvu ya mbinu za utangulizi. Nguvu kubwa sana ya mbinu hii ni umakini ambao kwa pamoja umechukuliwa na kuwekwa kihistoria kwa kile Yohana alichokiandika, kwa makanisa saba ambayo kwa hakika aliyaandikia, na kumbukumbu ya wakati kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kitabu (**Ufu 1:1, 3; 2:10, 16; 3:10; 22:7, 10, 12, 20**).
2. Udhaifu wa mbinu ya utangulizi.
    a. *Kitabu cha Ufunuo kiliandikwa lini.* Toleo la Utangulizi ambalo linaona Ufunuo kama ulitimizwa kwenye mwaka BK70 ungeweza tu kuwa na uhalali kama kitabu kiliandikwa kabla ya mwaka BK 70. Hoja zenye nguvu zilifanywa kwa msimamo huo (Gentry 1989; Noe 2006: 781-84). Hata hivyo, zote zikiwa na msingi juu ya ushahidi wa ndani na wa nje, makubaliano ya wasomi walio wengi, wa kihistoria na wa leo, ni kwamba kitabu kiliandikwa wakati wa utawala wa Domitian, karibia mwaka BK 95 (Beale 1999: 4-27).
    b. *Kumbukumbu za wakati.* Kumbukumbu za wakati, kuanzia kwenye **Ufu 1:1** (*“mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi”*) yanatokana na **Dan 2:28-29, 45**. Kwenye **Ufu 1:1** Yohana anabadilisha “upesi” kwa “*siku zijazo”* za Danieli “Upesi” kwenye mazingira haya “haimaanishi ama jinsi ya haraka ambayo unabii wa Danieli utatimizwa wala uwezekano mdogo ambao utatimizwa wakati wowote, bali kwa wazi, wakati wa karibu sana kutimizwa, ambao bila shaka tayari ulishaanza kwenye wakati huu uliopo. . . . Mbadala ya Yohana wa [‘upesi’] hudokeza matarajio yake kwamba dhiki za mwisho, kushindwa kwa uovu, na kuimarishwa kwa ufalme, ambao Danieli alitarajia kwamba utatokea kwa haraka ‘kwenye siku zinazokuja,’ zingeanzia kwenye kizazi chake mwenyewe, na, ni ukweli, kwamba zilikuwa tayari zilishaanza kutokea.” (Beale 1999: 181-82) Kumbukumbu ya wakati wa Yohana inaunganisha wakati uliopo na ujao. Wanaonyesha kwamba kanuni kuhusiana na kile ambacho alikiandika tayari kilikuwepo na kikitenda kazi. Walikuwa thabiti na asili ya ufalme ya “tayari, lakini bado”, pamoja na “ishara” Yesu alizozitoa kwenye hotuba ya Mlimani, ambayo ilitokea kikanuni kwenye kizazi chake Mwenyewe, bado aliruhusu utimilifu kutukia kwa wakati ujao ambao haukutabiriwa.
    c. *Nyakati za mwisho na mambo ya jumla ya Ufunuo.* Labda tatizo lililo kuu kwenye mbinu ya Utangulizi ni kwamba haichukulii kwa umakini nyakati za mwisho na mambo ya jumla ya Ufunuo. Mwonekano wa Ufunuo wa “wanyama” kwa sehemu kubwa yanatokana na **Danieli 2, 7** (angalia chini, sehemu **VII.G.**1). Wanyama wa Danieli wanaelezea *dola nne za dunia*, ambazo pia zitanyenyekeshwa kwenye hukumu ya mwisho ya Mungu na kubadilishwa na ufalme wake Mwenyewe (**Dan 2:34–35, 44–45**). Zaidi, **Danieli 2** na **7** zote hutafakari hukumu ya *jumla*, siyo tu hukumu ya mahali pamoja kama ilivyotokea mwaka BK 70 (Beale 1999: 44-45). Mtazamo wa Utangulizi wa **Ufu 19:11-21**—kwamba Kristo alimtaliki mke wake asiyemwaminifu (Israeli) na kumchukua Bibi arusi mpya (kanisa) (Gentry 1998: 80-81) pia haiunganishwi na mazingira ya mafunuo wa kifungu hicho wa hukumu ya jumla (angalia Payne 1980: 624n.150).

        Sawa na, **Ufu 1:7** inasema kwamba wakati Kristo atakapokuja *“kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili Yake.”* Kulifupisha hili kumaanisha “kabila zote za *nchi* [ya Israeli]” wakati alipokuja kwenye hukumu juu ya Yerusalemu mwaka BK 70 ni kwa kikabila, kijiografia, na kwa muda “kutaja kifungu kisichoeleweka kwa ahaadi za Mungu ya Baraka za mataifa kwa na kupitia kwa Abraham (Mwanzo. 22:18). Mzunguko wa waombolezaji hautajumuisha Waisraeli tu bali pia mataifa ya wasioamini.” (Johnson 2001: 52-53) Kweli, wakati baadaye Ufunuo unapotaja*“kila kabila”* (ambayo inalingana na*“makabila yote”*) kwa wazi inazungumzia makabila mbali mbali, mataifa mbalimbali kusanyiko la waaminifu (**5:9; 7:9**), au waasi dhidi ya Kristo (**11:9; 13:7**).

        Tena, **Ufu 3:10** inazungumza kuhusiana na *“saa ya kujaribiwa”* ambayo itaujilia *“ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi.”* Neno lililotafsiriwa “ulimwengu” ni la Kigiriki *oikoumenē,* ambalo linautaja ulimwengu wote na hao wakaao ndani yake, au wakati

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mwingine, kwa Dola ya Rumi (Danker 2000: *"oikoumenē,"* 699). Neno lililotafsiriwa "nchi au dunia" ni *gē,* ambalo linataja dunia yote au, wakati mwingine, baadhi ya sehemu zake, kama vile nchi ya Israeli (Ibid.: *"gē,"* 196). "Kuingiliana kwa *gē* na *oikoumenē* ni moja ya kiashiria cha kutokujitosheleza kwa tafsiri ya wanatheolojia ambayo huwekea mipaka nabii za Ufunuo za hukumu kwa kuharibiwa kwa Yerusalemu na 'nchi' ya Yudea, tukio lililoishia mwaka 70" (Johnson 2001: 88n.35).

Toleo la utangulizi ambalo linaona Ufunuo kutimizwa na anguko la Dola ya Rumi linakabiliana na tatizo sawa na hilo. "Unabii wa Ufunuo unaenda mbali kupita hali yoyote ya kihistoria inayojulikana kwenye karne ya kwanza. Wakati Rumi ya siku za Yohana ilifanyika kuwa na tabia ya mpinzani wa ukristo, mwonekano wa Mpinga Kristo kwenye Ufunuo13 ni mkubwa sana kuliko Rumi ya kihistoria." (Ladd 1972: 9) Kifupi hukumu ya mwisho haikutimizwa kwa anguko la Rumi kwenye karne ya tano.

Utangulizi siyo tu umekosa wigo au upana wa hukumu yote, lakini umekosa wigo wote wa mpango wa Mungu wa kuufanya upya uumbaji katika hali ya haki kamilifu. Huitazama ishara ya Yerusalemu mpya kama patakatifu pa patakatifu na jinsi gani mbingu mpya na nchi mpya zitakavyogeuka na kupita au kushinda nguvu iliyoanza mwendo wake kwenye kitabu cha **Mwanzo 1-3** na hivyo ni utimilifu wa mpango wa Mungu wa kihistoria ulimwenguni kote na mchezo unaoendelea kurudi nyuma hadi kwenye bustani ya Edeni (angalia hapo chini). Kama Marko Stephens alivyoliweka, "Yohana aliisukuma mipaka yake ya nyakati za mwisho zaidi sana kuliko manabii wengi wa Israeli, kwa kujumuisha matokeo. Kwa Yohana, 'mwisho' haukuwa tu nchi ya Israeli, wala watu wa Israeli. Azimio lake la nyakati za mwisho lilikumbatia watu kutoka kila kabila (Ufu 7:9; 21:3), na 'nchi' ambayo inaathirika ni dunia yote. Zaidi ya hayo, Maono ya Yohana ni maono ya umilele, kama yanavyopingana na maono ya maisha marefu (angalia, kwa mfano, Isa 65:17-25)." (Stephens 2011: 259) Kwa ufahamu au akili ya utendaji, kwa hiyo, mitazamo yote ya Utangulizi hupunguza ukubwa wa kitabu kuwa maelezo ya kihistoria ambayo yana umuhimu mdogo kwa kanisa tangu angalau karne ya tano, na ambayo haitoi tumaini lolote kuhusiana na wakati ujao.

B. ***Mbinu ya Kihistoria***

Mbinu hii huutazama Ufunuo kama unabii wa ki-ishara wa historia yote ya kanisa, toka mwanzo wake hadi *parousia*. Ishara tofauti za kitabu huonyesha harakati tofauti za kihistoria na matukio kwenye ulimwengu wa Magharibi na Kanisa la Kikristo, kama vile Goths, Waislamu, Upapa wa zamani, Marekebisho au Uamsho, nk.

Tofauti za mbinu hizi huona "barua saba kwa makanisa saba" (**Ufunuo 2-3**) kama zinazoelezea historia ya umri kanisa lote kwenye nyakati saba zilizopitiwa na makanisa saba, i.e., Kanisa lililoko Efeso likifanana na kanisa la kwanza hadi alipokufa Yohana (c. BK 99); Smirna inawakilisha kanisa kutoka karne ya pili hadi karne ya nne; Pergamo ni mwanzo wa mfumo wa kanisa kama nchi chini ya mfalme Constantino na kuingiza Ukatholiki wa Rumi; Thiatira ni Kanisa la Katholiki la Rumi la nyakati za kati; Sardi linawakilisha kanisa la Kiprotestantu la matengenezo; Filadelfia kanisa lenye uaminifu la kwenye siku za mwisho; na Laodiki ni kanisa la uasi kwenye siku za mwisho. (Smith 1980b: 24-36; angalia pia Scofield 1967: 1353n.4; Ironside 1943: 123-24; Pentecost 1958: 153; MacDonald 1995: 2355) Mtazamo huu ulikuwa maarufu sana kwenye karne ya kumi na tisa, hasa hasa miongoni mwa wamini wa mpito, ingawa lilikuwa na wafuasi kurudi nyuma hadi kwenye nyakati za kati.

1. <u>Nguvu za mbinu ya Kihistoria.</u> Mbinu hii huchukulia kwa umakini ukweli kwamba Ufunuo unatumika na uko wazi kwa vipindi vyote vya historia mpaka kurudi kwa Kristo.
2. <u>Madhaifu ya mbinu ya Kihistoria.</u> Wengi wa wanahistoria huwa na tabia ya kuona mpangilio wa fasihi wa *maono* ya kitabu kama mpangilio wa nyakati ambazo matukio yakini yalitukia *kwenye historia* na kukusudia kupuuza ushahidi wa kurejea kwenye Ufunuo (angalia hapo chini, kipengele **G. *Muundo: sambamba hatua kwa hatua; siyo kwa mpangilio madhubuti wa wakati***). Mbinu ya Kihistoria kwa ujumla na tofauti ya"makanisa saba" yameangukia nje ya kibali kwa sehemu kubwa kwa sababu yalikuwa ya kibinafsi na ya kiholela (Thomas 1967: 323-27; Thomas 1992: 507-11; Osborne 2002: 105; angalia pia Hamstra 1998: 131). Aina za upinzani wa kihistoria ni zifuatazo:
    - "Hakuna mwongozo imara kama ni kwa matukio gani ya kihistoria yanayomaanisha" (Ladd 1972: 11).
    - "Hakuna mtu aliyewahi kuwa na uwezo wa kuandaa mpangilio wa nyakati angalau kuifanya

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mbinu kukubaliwa kwa ujumla. Historia ya kanisa haiwezi kutengwa kwenye vipindi saba vilivyofuatana vilivyowekewa alama na wahusika wale ambao walibainishwa kwenye kusoma nyaraka saba." (Milligan 1893: 269)

- "Kwenye kuzitazama namba na urefu wa vipindi [vya historia ya kanisa, iliyowakilishwa na makanisa saba] kwa uhakika, hakuna mwafaka; ndogo zaidi, kwenye maelezo mbalimbali ya madhehebu tofauti yakiimarisha msimamo wa mtazamo tofauti, hasa kuanzia karne ya kumi na sita" (Schaff 1990: 1:14).
- Wanahistiria "hijaribu kuzitambulisha harakati za kihistoria kwa njia maalum sana na kuuwekea ukomo unabii wa ufunuo kwa historia ya kanisa la Magharibi, kuiachilia mbali historia ya kanisa ulimwenguni kote" (Beale 1999: 46).
- "Mawakili wa shule ya utafsiri wa kihistoria wakati wote hugundua kilele cha unabii kwenye siku zao wenyewe—uthibitisho wa uhakika wa udhalimu wa mbinu hii" (Payne 1980: 593).

C. ***Mbinu ya Kinabii***

Kimsingi manabii huchukulia **Ufu 4:1-22:5** kama kuonyesha "kipindi cha dhiki" na matokeo yake (i.e., kipindi cha wakati ujao mara kabla na baada ya *parousia*). Kuna mitazamo miwili muhimu ya kinabii ambayo inalingana na mitazamo miwili mikuu ya Waamini wa kabla ya milenia: wastani mkubwa wa waamini wa unabii wa baadaye hulingana na ile wa waamini wa kihistoria kabla ya milenia; Waamini wengi wenye msimamo mkali wa unabii wa baadaye hulingana na wale waamini wa mpito kabla ya milenia. Kwa sababu waamini wa unabii wa baadaye wenye msimamo wa wastani hufanya tofauti kubwa baina ya Israeli na Kanisa, haioni "unyakuo wa kabla ya dhiki" kama ilivyoeleweka kwenye Ufunuo. Wakati inaona vitabu vingi kama vinazingatia mwishoni mwa historia, haioni kwa umadhubuti maono ya kitabu kama matukio ya mfuatano wa nyakati ambao utatokea. Kwa namna nyingine, waamini wa mpito wanaamini kwamba kanisa litanyakuliwa wakati au kabla ya **Ufu 4:1** na halitakuwepo mpaka **19:7** (wakati litakapoonekana mbinguni). Kulingana na mtazamo huo, **Ufu 4:1-19:7** inasisistiza kabisa juu ya Israeli ya baadaye na nyakati zinazoelezea miaka saba ya dhiki. Mpinga Kristo atajitambulisha mwenyewe na ataanzisha "dhiki kuu" dhidi ya wale Wayahudi 144,000 waliomgeukia Kristo na dhidi yaw engine ambao hawasaidii utawala wake (angalia Osborne 2002: 21; MacDonald 1995: 2361; Smith 1980a: 17-21; Smith 1980b: 39-40, 68-75, 120-24). Baada ya hayo *parousia,* milenia halisi, hukumu juu ya wasioamini, na mbingu mpya na nchi mpya (**Ufu 19:11-22:21**).

1. Nguvu ya mbinu ya Unabii. Nguvu kubwa na mbinu hii ni kwamba inatambua kuwa Ufunuo unajishughulisha na matukio mara kabla, kwa wakati, na baada ya *parousia.*
2. Udhaifu wa mbili ya kinabii. Waamini wengi wa unabii hutamani kuona mpangilio halisi wa *maono* ya kitabu kama mpangilio wa nyakati ambao kwenye huo matukio ya uhakika yalitukia *kwenye historia.* Kwa nyongeza, Waamini wa unabii wa baadaye hufifisha karibia kitabu chote cha Ufunuo kuwa hakikuwa wazi kwa wasikilizaji halisi wa Yohana kwenye karne ya kwanza na kwa wale wote waliofuata kwa kipindi cha miaka elfu mbili ya mwisho. Kwenye kuunganisha na hili, Gentry kwa usahihi anaelezea kwamba waamini wa unabii wa baadaye "wanapaswa kuyatafsiri tena matukio kwenye siku za Yohana kuyafanya yafae kwa nyakati za sasa. Huangalia kwa makini madai ya ukaribu wa matukio kwenye Ufunuo." (Gentry 1998: 92) Tatizo hilo limekuzwa sana kwenye tolea la waamini wa mpito wa unabii wa baadaye kwa kuwa waamini wa mpito hudai kwamba kanisa "litanyakuliwa" kwenda mbinguni na halitahusika na matukio yoyote ya duniani yanayoonekana kwenye **Ufu 4:122:5**. Hatimaye, waamini wa unabii wa baadaye, hasa hasa kwenye muundo wake wa kuamini mpito, mara nyingi hutupeleka kwenye ubazazi au uvumi ambao uliachwa tangu karne ya kwanza na mazingira ya kiini cha kanisa ya kitabu. Kwa matokeo hayo, umuhimu na nguvu ya kitabu, na maana ya kitheolojia ya picha zake, imepotea.

D. ***Mbinu ya mawazo au njozi***

Wakati wanahistoria na waamini wa unabii wa baadaye wanapoegemea kuelekea utambulisho maalum na wa mapema wa vifungu vya Ufunuo na picha pamoja na matukio hasa ya kihistoria (yanayodhaniwa kuwa ya baadaye), kinyume chake ni mawazo au njozi za kweli. Mbinu ya mawazo huuona Ufunuo kama mwonekano wa ishara ya mgogoro baina ya mema na mabaya, ufalme wa Mungu na nguvu za Shetani. "Kwa ujumla, mtazamo wa mawazo umewekewa alama kwa kukataa kwake kuitambua picha yoyote ile na matukio maalum ya baadaye, ama kwenye historia ya kanisa au kuhusiana na hatima ya mambo yote" (Johnson 1981: 410). Kwa uthabiti mawazo yanalenga kwenye kanuni ya mpito wa kihistoria ambao ishara zinawakilisha. Kwa hiyo, mnyama anawakilisha uovu wa kishetani popote anapotokea kupingana na kanisa, na muhuri, na parapanda, na

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mabakuli huwakilisha hukumu ya Mungu juu ya uovu kwenye historia yote.

1. Nguvu ya mbinu ya mawazo au njozi. Mawazo, zaidi ya mbinu nyingine yeyote, kwa usahihi inatambua kwamba theolojia na ishara ndicho kiini cha Ufunuo. Inaona kwamba kitabu kinajihusisha na masuala na kufundisha kanuni ambazo ni muhimu kwenye maisha yote ya kanisa kuanzia karne ya wanza hadi kurudi mara ya pili.
2. Udhaifu wa mbinu ya mawazo. Udhaifu wa msingi wa mawazo "safi" ni kushindwa kwake kuunganisha unabii wowote wa kitabu na historia, ama wakati uliopita, uliopo, au ujao, ingawa kitabu chenyewe huonekana kufanya hivyo mara kwa mara. Kwenye muundo wake wa kiradikali, kitabu kinaonekana tu kama maelezo ya kung'ang'ana kusikoisha baina ya mema na maovu. "Tatizo la m-badala huu ni kwamba hushikilia kwamba Ufunuo hauonyeshi hitimisho lolote la mwisho wa historia, ama kwenye ushindi wa Mungu wa mwisho au kwenye hukumu ya mwisho ya utawala wa uovu." (Beale 1999: 48)[6]

E. ***Ufupisho wa mbinu nne za hapo juu***

Mtu anaweza kuratibisha na kwa kiasi kikubwa kufanya tathmini ya mitazamo hiyo hapo juu pamoja na umuhimu wa shoka kwa kanisa la leo na tumaini la suluhisho la milele kwa wakati ujao, kama ifuatavyo:[7]

	Utangulizi	***Wanahistoria***	***Waamini wa unabii wa baadaye***	***Mawazo***
Umuhimu	Karne ya kwanza—Ndiyo Baada ya karne ya kwanza—Hapana	Ndiyo	Karne ya 1st —Ndiyo (sura ya. 2-3 pekee) Baada ya karne ya 1st —Hapana Mara kabla ya *parousia*—Ndiyo	Ndiyo (kwenye kanuni, lakini siyo kihistoria)
Tumaini	Hapana	Ndiyo	Ndiyo	Hapana

F. ***Mbinu ya Wateule***

Kila moja ya mbinu hizo hapo juu ina nguvu Fulani, lakini pia inao udhaifu. Kwahiyo, wengi wa watafsiri wa Kiinjili na wanamabadiliko hutumia vipengele mbali mbali vya mbinu hizi zote kwenye kutafsiri kitabu cha Ufunuo. (Beale 1999; Johnson 1981; Osborne 2002; Smalley 2005). Beale anaielezea mbinu hii m-badala ya tano kwa kitabu kama "mawazo yaliyobadilishwa" au "kufanya maamuzi" (Beale 1999: 48-49). Mbinu hii ni thabiti pamoja na unabii wa kibiblia na mafunuo kwa ujumla: nabii zina msingi kwenye matukio maalum yenye matokeo kwenye mada na kanuni ambazo hutumika kwenye historia yote; Manabii hupeleka unabii unaohusiana na tukio moja , wakati, na mahali, na kulifanyia kazi upya na kulitumia kwenye matukio mengine, nyakati, na mahali; matukiop maalum mara nyingi hutumika kama kielelezo au mfano matukio yajayo au kanuni. "Malengo ya "Ufunuo wa Yohana ni kwa wasikilizaji wake wa Asia, lakini mifano aliyotumia ni mtambuka kiasi cha kutosha kwamba zinaweza na zitaweza kutumiwa kwa usahihi kuelezea hali zingine za migogoro kwenye maisha ya kanisa" (Witherington 2003: 25). Wachambuzi wafuatao wamelifafanua hili:

- Ufunuo wa Yohana ni kwa wasikilizaji wake wa Asia, lakini mifano aliyotumia ni mtambuka kiasi cha kutosha kwamba zinaweza na zitaweza kutumiwa kwa usahihi kuelezea hali zingine za migogoro kwenye maisha ya kanisa" (Witherington 2003: 25).
- "Ni muhimu kwenye mchakato wa kutafsiri ufunuo kutokuweka ukomo wa utambulisho wa 'Rumi', au kwa hakika 'Babeli'. Yohana kwa ujumla aliyaona haya yote, siyo kwa maneno ya kiraia au kifalme; kwa kuwa ni mawazo wakilishi au mawazo mbadala, na picha ambazo zinasimama kwa ajili ya wasio haki wakipingana na Mungu kwenye kila jamii au mfumo wakati wowote." (Smalley 2005: 3)

[6] Chakushangaza, hili pia ni tatizo la wanatheolojia kamili ambao huona Ufunuo 21-22 kama maelezo siyo la matumizi ya mwisho lakini ya Kanisa. Inaonyesha nyakati za Kanisa kama "hazina mwisho" (Preston 2010: 54-55). Hivyo, kulingana na wanatheolojia kamili, hakuna mwisho wa dhambi, ukandamizaji, au mauti (Ibid.: 262-63, 266; Preston 2013: 22).

[7] Kubainisha jibu la "Hapana": Juu ya "umuhimu" wa mhimili, mtazamo wa wanatheolojia wa Ufunuo hufanya kitabu kutokuwa na umuhimu wa moja kwa moja kwa Kanisa leo kwa sababu wanang'ang'ana kwamba ni Kanisa la karne ya kwanza pekee (au kufikia kwa juu sana karne ya tano) waliokuwa wakizungumziwa; kwa kuwa waamini wa wakati ujao hudai kwamba Kanisa lilinyakuliwa kwenye **Ufu 4:1** na ukubwa wa kitabu (**Ufu 4:122:5**) inahusu Israeli tu na miaka saba kabla ya *parousia,* mtazamo huu vivyo hivyo hupunguza ukubwa wa kitabu kutokuwa na maana kwa Kanisa leo. Juu ya mhimili wa "Tumaini", Mitazamo yote ya Waamini wote wa theolojia haitoi tumaini kwa wakati ujao kwa sababu wanaona kimsingi Ufunuo kama historia iliyoishia mwaka BK 70 au kwa kuchelewa sana pamoja na kuanguka kwa Warumii kwenye karne ya tano; mawazo safi hawatoi tumaini kwa wakati ujao kwa sababu hukitazama kitabu tu kama ambacho kina kanuni zisizokuwa na mwisho lakini siyo kama kuonyesha matumizi yoyote ya wakati ujao.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

- “Kama ilivyo kwa matukio mengine mengi, [Yohana] anaanzia kutoka kile ambacho kina ukomo na cha kieneo au mtaa tu kuelekea kile4 ambacho hakina ukomo na cha kidunia. Yerusalemu yake, Babeli yake, siyo majina ya miji halisi. Ni mwanamke ‘kahaba mkuu aketiye juu ya maji mengi;’ na ‘na maji ambayo unayaona,’ malaika alimwambia mwonaji, ‘ni watu au jamaa, na makutano, na mataifa, na lugha [**Ufu 17:1, 5, 15**].’” (Milligan 1896: 295)

Mada na picha za Ufunuo siyo kumbukumbu tu za matukio hasa lakini zina umuhimu unaoendelea kwa ajili ya kanisa. Kanuni za mawazo, hutumiwa kwenye mbinu ya maamuzi, zikitolewa kivitendo kwa imani na maisha ya kanisa kutoka karne ya kwanza mpaka *parousia.* Kwa namna nyingine, mbinu ya maamuzi inatambua kwamba hufanya zaidi ya kuandaa kanuni endelevu. Kitabu hakielezei tu matukio ya karne ya kwanza lakini pia utimilifu wa wakati. Vivyo hivyo, mbinu hii hutoa tumaini la mwisho kwa waamini, majaribu ya namna yoyote wanayoweza kuwa wanayapitia kwa sasa. Hii ni mbinu ambayo itakuwa imewakilishwa pale.

III. <u>Hali ya makanisa mwishoni mwa karne ya kwanza</u>

“Kitabu cha Ufunuo kinaashiria mgogoro miongoni mwa Wakristo, mgogoro baina ya Wakristo na Wayahudi, na baina ya Wakristo na wawakilishi wa Rumi. Kazi inajaribu kuitafsiri migogoro hii na kuisuluhisha kulingana na mitazamo yake yenyewe.” (Yarbro Collins 1998: 400)

A. *Ufalme na Utamaduni*

Ufunuo unaibua swali la msingi lililowakabili Wakristo wengi: Kwakuwa Mungu ni mtawala na Kristo tayyari alishauzindua ufalme wake, kwanini, tamaduni ni za kipagani kiasi hiki na zinatutesa? Karne ya kwanza dini ya Wagiriki wa Rumi ilikuwa imeunganishwa na tamaduni mbalimbali, kijamii, kiuchumi, na vitendo vya kisiasa. Wakati mwingine Wakristo walikabiliwa na uchaguzi mgumu kuhusiana na ni lini watakubaliana kwenye vitendo vya kushinda ni lini jinsi gani watazuia. Mambo yay ohayo, bila shaka, Wakristo wanakabilia na hayo leo.

Zipo kwa kiwango kidongo kweli tatu za kidini zinazoyakabili makanisa ya karne ya kwanza ambazo zilikuwa na athari za kisheria. Kwanza, kwenye jamii ya Kirumi, makundi yote tofauti ya kibiashara yalikuwa na miungu yao wasimamizi. Athari za miungu hiyo wasimamili zilionyeshwa na Beale: “Ilivyoonekana, makundi muhimu miongoni mwa makanisa ya Asia ndogo hawakulifikiria hili kuwa dhambi ya kaburi kuonyesha waziwazi utii wao kwa miungu hiyo inayosimamia biashara. Hili lilikuwa kesi hasa pale walipokuwa wanahitajika kulipia “madai” kwa makundi yao ya biashara kwa kuhudhuria kwenye chakula cha jioni cha kila mwaka kilichofanyika na kuandaliwa kwa heshima au kwa miungu wasimamizi wa makundi. Heshima kwa mtawala kama mungu ilikuwa ikijumuishwa pamoja na kuiabudu miungu kama hiyo ya kienyeji. Kwa tamaduni kwa ujumla kuonyesha utii huku kulikuwa sehemu ya kuwa mzalendo. Baada ya hayo yote, miungu wasimamizi wa makundi pamoja na mungu mtawala wa Rumi walidaiwa kuwajibika kwa Baraka za kijamii na za kiuchumi ambazo tamaduni zilizifurahia. Kukataa kuonyesha shukurani kwa miungu hii ilikuwa ni kuwa uraia mbaya.” (Beale 1999: 30)

Pili, makanisa yalikabiliwa na kuinuka kwa kuabudiwa kwa mtawala. Hili lilikuwa na athari za kidini na kijamii: “Ufunuo wa Yohana ulimjia wakati ibada za kumwabudu mtawala zilipokuwa zimeongezeka kutumiwa kuunganisha jamii na kuunganisha kila mji mkubwa wa Waasia, lakini pia mikoa, pamoja. . . . Maandiko kama vile Ufu. 13.4; 15-16; 14.9-11; 15.2; 16.2; 19.20; 20.4, ambayo yanataja au kusema kumwabudu Mnyama, bila shaka yanaashiria ushawishi wa ibada ya mtawala kwa Yohana na Wakristo wengine wa kwanza.” (Witherington 2003:25)

Tatu, kama ambavyo ilijadiliwa kwa kuunganishwa na Hotuba ya Mlimani, udhaifu wa kisheria wa makanisa ulizidi kuongezeka kwa kubadilisha hali ya kisheria ya Ukristo kwenye mahusiano na Uyahudi baada ya mwaka BK 70. Kwenye mwanga wa mabadiliko haya ya hali ya kisheria, iliwezekana kwamba baadhi ya viongozi wa Wayahudi kuwajulisha viongozi wa serikali za mitaa kwamba Wakristo siyo kundi la Wayahudi na kwa hiyo hawana kibali cha kuendesha masuala yao ya kidini nje ya Palestina pale ambapo Ukristo ulianzia. Kwenye kila tukio, Ufunuo huasdhiria kwamba upinzani kwa Ukristo haukutoka kwa Warumi tu lakini kutoka kwa Wayahudi pia (**Ufu 2:9; 3:9**).

B. *Suala la mateso*

Linalohusiana na suala la ufalme na tamaduni ni suala la mateso. Uchunguzi unaonyesha kwamba, ingawa kwenye miaka ya mwisho ya utawala wake Nero kwa utaratibu aliwatesa Wakristo Rumi peke yake, “hakuna ushahidi kwamba kipindi cha miaka ya mwishoni mwa karne ya kwanza kulitokea mateso yoyote ya wazi au ya kuratibiwa ya Wakristo” (Ladd 1972: 8). Hata hivyo, Ufunuo unaonyesha kwamba kufikia mwishoni

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mwa karne ya kwanza makanisa yaliyokuwa Asia yalipitia angalau mifano ya mateso mara kwa mara (**Ufu 1:9; 2:10, 13**). Bila shaka Yohana alionyeshwa mwendo huo uliokuwepo kwenye jamii ungepelekea kuongezeka kwa mateso kwa wakati ujao. Hivyo, Ufunuo umejawa na mifano ambayo inawaonya waamini ujio wa mateso na kuwasihi kuwa mashahidi waaminifu hata kifoni (angalia, e.g., **Ufu 3:10; 6:9-11; 7:13-17; 11:3-12; 12:1-17; 13:7; 17:14; 19:7-10; 20:4-6**).

C. *Matatizo ya ndani*

Kama ambavyo barua kwa makanisa saba (**Ufunuo 2-3**) ilivyoweka wazi, "Matatizo ya moja kwa moja yaliyoyakabili makanisa wakati wa Yohana, na kutengeneza muundo wa yaliyomo kwenye Ufunuo, yaliinuka kutoka *ndani* ya jamii yake, na siyo tu kutoka nje au mbali yake" (Smalley 2005: 4). Matatizo hayo yalijumuisha; kukosekana kwa upendo (**2:4**); mafundisho ya uongo (**2:14-15**); uasherati uliokuwa na msingi kwenyemafundisho ya uongo na unabii wa uongo (**2:20-21, 24**); kufa kiroho, kukosekana kwa uaminifu, kukosekana kwa subira (**3:1-4**); uvuguvugu na kiburi (**3:15-17**).

IV. <u>Kusudi na mada</u>

Kama tunavyoiona hali ya makanisa ya karne ya kwanza na kutafakari uchambuzi wa Yesu kwa makanisa hayo kwenye **Ufunuo 2-3**, tutaona usambamba wa majaribu na masuala tunayokabiliana nayo siku hizi. Makusudi na mada za kitabu hutusaidia sisi kuona mwelekeo wa kitabu na kutupa ufahamu wa jumla wa kinahusiana na nini hasa. Makusudi na mada hizi zinahusiana na zimeelezwa kwa njia tofauti. Njia zifuatazo zinawakilisha nyingine.

A. *Kulielezea kanisa ni jinsi gani Mungu anavyojihusisha na dunia*

Wilbur Smith alionyesha vipengele muhimu vya muundo wa Ufunuo na maana ya muundo huo: "Maeneo mengi ya kitabu hiki yapo mbinguni, wakati hukumu zenyewe zinafanyika hapa duniani; na wakati wote maeneo ya mbinguni huenda mbele ya matukio ya kidunia ambayo yamehusishwa nayo. . . . Ninasikia wakati wote kwamba zipo kweli mbili kuu ambazo zaweza kuandikwa kutoka kwenye ajabu hili. Kwanza, kile kinahusika kufanyika hapa duniani, ingawa hakijulikani kwa mwanadamu na kisichotarajiwa kwake, kinaeleweka kikamilifu kwa wale walioko mbinguni—Bwana aliyepaa, malaika, wazee ishirini na wanne, viumbe wenye uhai, na wengine. Pili, kile kinachotokea hapa duniani kinaongozwa kabisa na kupewa maelekezo na mbingu, hivyo kwa usalama kunaweza kusema kwamba, hukumu kwenye kitabu hiki, sawa na zile za kutoka kwenye vitabu vingine vya kinabii kwenye maandiko, chochote kile kinachotokea duniani hapa tu hutimiza neno la Mungu." (Smith 1962: 1497)

Sawa na hilo Walter Elwell anaeleza, "Wakati wote kusudi la Ufunuo ni kulielezea kanisa ni jinsi gani Mungu anavyojihusisha na ulimwengu. . . . Mada ya msingi ambayo inaendeshwa kupitia kitabu cha Ufunuo ni kwamba maisha na historia yanaweza kuangaliwa kutokana na upeo wa mitazamo miwili. Tunaweza kuangalia kwenye matatizo, mateso, huzuni, uovu na maumivu ambayo yanatuzunguka sisi na kutuvunjwa moyo; au tunaweza kuangali zaidi ya hilo kwenye ukweli wa utukufu wa milele ambao pia unatuzunguka sisi—Mungu, Kristo, Watakatifu wa zamani, malaika, kiti cha enzi cha Mungu, muziki, rangi, sauti, na uzuri wa mbingu, Yerusalemu mpya pamoja na mitaa yake ya dhahabu, na ushindi ambao tayari tulishashinda. Uchaguzi ni wetu; mitazamo yote ni ya kweli." (Elwell 1989: 1200-01) Yohana anaelezea kupitia maono na ishara kwamba Mungu anatimiza mpango wake wa milele. Upeo wa kitabu hiki "siyo zaidi sana kuyawezesha [makanisa saba ambayo Yohana aliyaandikia] kuuona wakatiwao ujao kama kuwawezesha wao kuuona wakati wao wa sasa kutoka kwenye mtazamo wa wakati ujao" (Bauckham 1993b: 167) Haitaonekana wazi kwetu kwenye ulimwengu huu kwamba Mungu anatimiza mpango wake. Hata hivyo, "moja ya mada kuu ya kitabu hiki ni kwamba vitu siyo kama vile vinavyoonekana" (Johnson 2001: 9).

B. *Mwito wa kuvumilia kwenye kung'ang'ana na nguvu za uovu*

Maadili ya tamaduni za kigeni, mateso ya mara kwa mara, udhaifu wa kisheria na kijamii, na shinikizo toka kwenye serikali na Wayahudi kungewajaribu Wakristo kukubaliana imani na utendaji wao. Ufunuo umeweka wazi kwamba, kutoka karne ya kwanza hadi *prousia,* kutakuwa na uovu na jitihada za kuukandamiza ushuhuda wa kanisa. Mpango wa Mungu unahusisha mauaji ya kiimani ya watu wake. Kwa hiyo, watu wa Mungu wanabaki wakiwa waamini bila kujali magumu na kuyashika maneno ya unabii ambao umeandikwa kwenye kitabu (**Ufu 1:3; 22:7**). "Kama mwanzo wa ufalme wa Yesu, ufalme wa kanisa unahusishwa kwenye kushinda kwa kudumisha uaminifu wake kwenye kukabiliana na majaribu (e.g., 2:9-11, 13; 3:8; 12:11); kwenye kuzishinda nguvu za uovu (e.g., 6:8 kwenye mahusiano na 6:9-11); kwenye kuitiisha dhambi kwenye maisha ya

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

wanachama wake (angalia sura ya. 2-3); na kwenye mwanzo wa utawala juu ya kifo na shetani kwa utambulisho na Yesu (cf. 1:5–6, 18). Uvumilivu wa kanisa, ni sehemu ya mchakato wa ushindi" (White 2000: 175). Elisabeth Schüssler Fiorenza anafupisha "Yohana alikuwa anatafuta kuwahamisha [wasikilizaji wake] kutawala hofu zao, kuhuisha kujitoa kwao, na kuendeleza maono yao" (Schüssler Fiorenza 1991: 37).

C. ***Kuwafariji na kuwatia moyo Wakristo kwa sababu Kristo ni mshindi***

Ufunuo unadhihirisha kwamba Mungu ni mtawala juu ya historia yote, juu ya uovu wote, na kupanga matukio yote ya historia kulitukuza jina lake na kuleta kwenye kutukuzwa, hitimisho la milele la watu wake. Ufunuo "unatuonyesha sisi Mungu wa upendo na nguvu, ambaye hushangilia utawala wake juu ya maadui zake na juu ya maadui zetu. Historia ya mwanadamu, kama tuijuavyo, itaishia wakati Shetani atakaposhindwa milele na Bwaba Arusi atakapomkumbatia mkewe. TKanisa litafurahia furaha ya milele pamoja na Yesu." (Hamstra 1998: 127) William Hendriksen anaihitimisha mada hii muhimu kama ifuatavyo: "Kwenye ukubwa wake, kusudi la Ufunuo ni kuwafariji wapiganaji wa kanisa kwenye kung'ang'ana kwao kinyume cha nguvu za uovu. Kimejawa na msaada tele na faraja kwa Wakristo wanaoteswa na kuumizwa. Kwao wamepewa uhakika kwamba Mungu ameyaona machozi yao (7:17; 21:4); maombi yao yana nguvu kwenye mambo ya dunia (8:3, 4) na kifo chao ni cha thamani machoni pake. Wamehakikishiwa ushindi wao wa mwisho (15:2); damu yao itapatilizwa (19:2); Kristo wao anaishi na kutawala milele na milele. Anautawala ulimwengu kwa matakwa ya Kanisa lake (5:7,8). Atarudi tena kuwachukua watu wake mwenyewe kwenye 'chakula cha jioni cha Arusi ya Mwanakondoo' na kuishi pamoja nao milele kwenye ulimwengu uliohuishwa (21:22). . . . Mada ni ushindi wa Kristo na kanisa Lake juu ya joka (Shetani) na wasaidizi wake. . . . Kupitia kwenye unabii wa kitabu hiki cha ajabu Kristo ameonyeshwa kama Mshindi (1:18; 2:8; 5:9ff.; 6:2; 11:15; 12:9ff.; 14:1; 15:2ff.; 19:16; 20:4; 22:3). Alishinda kifo, Kuzimu, joka, mnyama, nabii wa uongo, na watu ambao wanamwabudu mnyama. *Yeye* ni mshindi; kwa sababu hiyo, *sisi* pia ni washindi*,* hata wakati tunapoonekana walioshindwa na wasio na msaada." (Hendriksen 1982: 7-8)

V. <u>Muundo</u>

A. ***Utata, Umoja, na umuhimu wa muundo***

Kwa jinsi ambavyo mtu anazidi kukisoma kitabu cha Ufunuo, ndivyo mtu anavyohisi utata wa muundo wake. "Ushirikiano kwenye Ufunuo unaweza kuwa na utata sana kwamba mfumo wa muundo mmoja hauwezi kutoa haki kamili. Hapa hatuwezi kuwa na fumbo la vipimo viwili lakini vipimo vitatu mchemraba" (Johnson 2001: 35) Bila kujali fasihi yake tata, uchunguzi wa Richard Bauckham wa Ufunuo unafunua kwamba "kwa hakika ni moja ya kazi zilizounganishwa vizuri kwenye AganoJipya. . . . Ni dhahiri kwamba Ufunuo umeundwa kuubeba ujumbe wake kuashiria viwango kwa wasikiaji wake wa kwanza (cf. 1:3), lakini pia hatua kwa hatua kuvuna maana kamili kwa marafiki wa karibu na wasomaji wavivu au wenye mashaka." (Bauckham 1993a: 1n.1, 1)

Mchoro huu wa kubuni ni muhimu kwa kukielewa kitabu chetu, hasa kutupa mafunuo na asili ya ishara zake. Ranko Stefanovic anafupisha umuhimu wa muundo wa kitabu kwa kuyaelewa yaliyomo: "Inaonekana kwamba utajiri wa muundo wa kitabu cha Ufunuo ulipangwa vizuri na mwandishi aliyevuviwa. Mchoro huu ni, muhimu sana kwa uelewa wa kuenea kisaikolojia kwa maendeleo ya kitabu. Kinawaonya wasomaji kujifunza kinyume na kutafsiri kifungu au eneo kwa kulitenganishana kitabu chote. Tafsiri yoyote ya andiko ni lazima iwe imekubaliana na kusudi a jumla la kitabu chote." (Stefanovic 2002: 43)

B. ***Kujirudia kwa misemo na mawazo***

Sehemu ya utata wa Ufunuo, umoja wa muundo wa fasihi umefunuliwa kwenye mifano yake ya kurudia misemo na mawazo. Misemo baadhi na mawazo imejirudia, mara nyingi kwenye vifungu vipana vilivyotenganishwa, na wakati mwingine kwenye miundo tofauti midogo. "Kujirudia huku hutengeneza mtandao tata wa rejea ya kimaandishi, ambao husaidia kutengeneza na kupanua maana ya kila kifungu kimoja kwa kukipa mahusiano maalum kwa vipengele vingine vingi." (Bauckham 1993a: 22) Sababu moja ya kujirudia kwa misemo ufunguo yaweza kuwa kwa sababu Yohana alikuwa akiwaandikia *wasikilizaji* sambamba na wasomajini (**Ufu 1:3**). "Kwenye ujumbe uliokusudiwa kwa uwasilishaji wa mdomo muundo ni lazima uashirie kwa wazi ustadi wa lugha." (Ibid.: 3)

1. <u>Kujirudia kwa misemo na mawazo husaidia kukiweka kitabu pamoja na kuimarisha msingi wa ujumbe wake.</u> Misemo, kipengele cha mawazo, na ahadi kwa kanisa zimeelezwa mwanzoni mwa kitabuna kupatiwa utimilifu wake mwishoni mwa kitabu:

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

1:1; 22:6-*"kuwaonyesha watumishi Wake"*	**2:7, 11, 17, 26; 3:5, 12, 21; 21:7-***"ambaye atashinda"*
1:1; 22:6-*"mambo ambayo hayana budi kuwako upesi"*	**2:7; 22:2, 14-***"mti wa uzima"*
1:1; 22:6, 16- Yesu alimtuma malaika wake	**2:10-11; 20:6; 21:4-**kuokolewa kutoka kwenye mauti ya pili
1:2; 19:10; 20:4-*"ushuhuda wa Yesu"*	**2:16; 3:11; 22:7, 12, 20-***"Naja upesi"*
1:3; 22:7-*"heri ni wale . . . wasikiaao"*	**2:17; 19:12-**A Jina *"asilolijua mtu"*
1:3; 22:7-*"maneno ya unabii"*	**2:23; 20:12; 22:12-***"kulingana na . . .matendo"*
1:3; 22:10-*"wakati u karibu"*	**2:27; 19:15-***"Atawachunga kwa fimbo ya chuma"*
1:4; 22:16-*"makanisa saba"*	**2:28; 22:16-***"nyota ya asubuhi"*
1:6; 20:6-*"makuhani wa Mungu"*	**3:4, 5, 18; 19:8, 14-**vazi safi, jeupe
1:8; 21:6; 22:13-*"Alfa na Omega"*	**3:5; 20:12, 15; 21:27-***"kitabu cha uzima"*
1:8; 21:22-*"Mwenyezi"*	**3:12; 21:22-**hekalu
1:14; 2:18; 19:12-macho *"kama mwali wa moto"*	**3:12; 22:4-**Jina la Mungu juu ya washindi
1:16; 2:16; 19:15-upanag kutoka kinywani mwa Kristo	**3:12; 21:2, 10-**Yerusalemu mpya ukishuka toka mbinguni
1:17; 22:13-*"wa kwanza na wa mwisho"*	**3:21; 20:4-**Washindi wakikalia citi vya enzi
1:18; 20:14-*"mauti na kuzimu"*	

2. Kijirudia kwa misemo kunaimarisha usambamba wa kitheolojia na tofauti ambazo Yohana alitaka wasomaji wake wazione. **Ufu 17:1-19:10** na **Ufu 21:9-22:9** vipo zambamba moja na kingine. "Kwenye 17:1-19:10 alimwona kahaba wa Babeli na anguko lake; kwenye 21:9-22:9 aliona mke wa Mwanakondoo, Yerusalemu mpya, ambao unashuka kutoka mbingni. Kwa pamoja maeneo haya mawili yanatengeneza kilele kuelekea kitabu chote kinachokilenga: kuangamizwa kwa Babeli na nafasi yake kuchukuliwa na Yerusalemu mpya." (Bauckham 1993a: 4-5) Vivyo hivyo, maeneo yote mawili huanza na kuishia karibia kwa kufanana:

17:1-3: *"Akaja mmoja wa wale malaika saba, wenye vile vitasa saba . . . akanena nami, akisema, 'Njoo huku, nitakuonyesha' . . . Akanichukua katika Roho."*	**21:9-10:** *"Akaja mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na vitasa saba . . . akasema name a, akisema, 'Njoo huku, nami nitakuonyesha' . . . Akanichukua katika Roho."*
19:9b-10: *"Akaniambia, Manenohaya ni maneno ya kweli ya Mungu. Nami nikaanguka mbele ya miguu yake, ili nimsujudie; akaniambia, Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Msujudie Mungu."*	**22:6-9:** *"Kisha akaniambia, 'Maneno haya ni amini na kweli . . . Na hapo nilipoyasikia na kuyaona, nalianguka, ili nisujudu mbele ya miguu ya malaika yule mwenye kunionyesha haya. Naye akaniambia , 'Angalia usifanye hivi; mimi ni mjoli wako, na wa ndugu zako manabii, na wa wale wayashikao maneno ya kitabu hiki. Msujudie Mungu."*

Ubora wa muundo wa kitabu hiki unaonekana kwamba maadui wakubwa wa Mungu na watu wake walijifanyia kanuni ya mwonekano wao kwenye utaratibu huu: Mauti na kuzimu (**6:8**); joka (**12:3**); mnyama na nabii wa uongo (**13:2; 13:11** [kutokuendelea na kumbukumbu tarajiwa kwenye **1:7**]); Babeli (**17:1** [kutokuendelea na kumbukumbu tarajiwa kwenye **14:8**]). Kuangamizwa kwao kupo kwenye utaratibu ulio kinyume, kutengeneza mpangilio unaoenda kinyume na ule wa kwanza: Babeli (**18:1–24**); mnyama na nabii wa uongo (**19:20**); joka (**20:10**); mauti na kuzimu (**20:14**)[8]

C. *Msingi wa muundo wa yaliyomo*

Wachambuzi wengi kimsingi huona sehemu mbili za muundo wa yaliomo kwenye kitabu: **sura za 1-11** na **12-22**. Maeneo haya mawili makuu yanaweza kuonekana kama yanayofungua jumbe za vitabu viwili (vitabu) vya Ufunuo: kitabu chenye muhuri **5:1-5**, ambacho ujumbe wake umefunguliwa kwenye **6:1-11:9**; na "kitabu kidogo" cha **10:2, 8-10**, ambacho ujumbe wake umefunguliwa kwenye **12:1-21:8**. Maoni ya ziada ya Hendriksen kwa yaliyomo kwenye nusu ya pili ya kitabu: "Mgawanyo mkuu wa kwanza (sura za 1-11) zinafunua Kanisa, kuishi na Kristo, kuteswa na ulimwengu. Lakini Kanisa lililipiza kisasi, kulindwa na kushinda. Mgawanyo mkuu wa pili (sura za12-22) zinafunua kina cha Kiroho cha historia ya kung'ang'ana huko. Ni mgogoro baina ya Kristo na Joka ambao kwenye huo Kristo, na kwa hiyo Kanisa ake, ni washindi."

[8] Beale anaona, "Mabadiliko haya huonyesha mapungufu zaidi kuhusiana na mfuatano wa nyakati kwenye ufunuo. Maadui wane wameondolewa wakati uo huo, kama ulivyo ushahidi kutokana na kurudiwa kwa maneno na kutajwa kwa Agano la Kale kwenye maelezo ya kushindwa kwao (e.g., 'kukusanyika pamoja kwa vita' [**16:14; 19:19; 20:8**])." (Beale 1999: 812) Kwa nyongeza, **Ufu 14:8** inaarifu, *"Umeanguka, umeanguka Babeli mji ule mkubwa,"* lakini "Babeli mkuu" hata haukuelezwa mpaka **17:1-5**. *"Umeanguka, umeanguka"* kwenye **Ufu 14:8** imechukuliwa kutoka **Isa 21:9**.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

(Hendriksen 1982: 23; angalia pia Payne 1980: 594)[9]

D. ***Msingi wa muundo kifasihi***

Kumekuwa na mapendekezo mengi ya miundo ya fasihi ya Ufunuo. "Baadhi ya mapendekezo hutumia viashiria vya wazi kama waandaaji wa muundo. Baadhi ya mifano ya mbinu hizi huhusisha mpangilio ulio tofauti na ule wa awali, kuingiliana, uhakikisho na kuzunguka. Mapendekezo mengine yamesisitiza matumizi ya viashiria vya maandishi ya wazi kama vile: 'kwenye Roho'; 'kipi cha sasa na kipi kitakachofuata baadaye'; 'njoo uone'; 'tetemeko la ardhi'; na, bila shaka, namba '7.' Kuhusiana na matumizi ya namba 7, baadhi ya wasomi hupendekeza mpango wote wa kitarakimu kwenye ufunuo pamoja na ambao umejumuisha kumbukumbu za wazi za makanisa 7, mihuri 7, parapanda 7 na vitasa 7. Baadhi hupangilia na chini ya maeneo makuu saba kutupatia muundo wa kitarakimu kwa kila kifungu au seneo kuu la maandiko tu. Na hatimaye, baadhi yao huunganisha mbinu hizo mbili hapo juu kuleta matokeo kwenye mpangilio wa kitarakimu kwenye ufunuo ambao ndani yake huunganisha mafungu saba ya miundo kwa namba ambazo ni za maeneo yanayofanana yenyewe." (Korner 2000: 160-62)

E. ***Mpangilio wa kimuundo wa uwakilishi***

Moja ya sababu kwanini wachambuzi wengi hupendekeza miundo tofauti kwa kitabu ni kwamba vipengele vyote vya maudhui ya kitheolojia na viashiria vya kifasihi lazima kuchukuliwa kwenye maelezo. Wachambuzi baadhi hutoa umuhimu kwenye maudhui, wakati wengine hutoa uzito mkubwa kwenye kweli za kifasihi. Yafuatayo yanawakilisha baadhi ya mengi ya mawazo makuu yanayofikiriwa zaidi kuwa muundo wa kitabu.

1. G. K. Beale (Beale 1999: x-xvi).
   - **1:1-20:** Utangulizi
   - **2:1-3:22:** Barua kwa makanisa saba: Kristo anayatia moyo Makanisa kushuhudia, akiwaonya kuhusiana na kukubaliana au kuafikiana na dunia, na kuwasihi kusikia na kushinda mwafaka ili kwamba warithi uzima wa milele.
   - **4:1-5:14:** Mungu na Kristo kutukuzwa kwa sababu kufufuka kwa Kristo kulidhihirisha kwamba wao ni watawala juu ya uumbaji kuhukumu na kukomboa.
   - **6:1-8:5:** Mihuri saba
   - **8:6-11:19:** Parapanda saba
   - **12:1-15:4:** Mgogoro wa kina
   - **15:5-16:21:** Hukumu ya vitasa saba: Mungu akiwaadhibu wasiomwamini wakati wa kipindi cha majilio na kuhitimishwa siku za mwisho kwa sababu ya mateso yao na uasherati
   - **17:1-19:21:** Hukumu ya mwisho ya Babeli na mnyama
   - **20:1-15:** Kuzinduliwa kwa milenia wakati wa kipindi cha Kanisa wakati Mungu atakapokomesha nguvu ya udanganyifu wa Shetani na kama Wakristo waliokufa wakithibitishwa na kutawala mbinguni. Milenia itahitimishwa kwa kurudi kwa udanganyifu na unajisi wa Shetani kinyume na Kanisa na hukumu ya mwisho.
   - **21:1-22:5:** Uumbaji mpya na Kanisa kukamilishwa kwenye utukufu.
   - **22:6-21:** Hitimisho
2. Utangulizi wa mfano wa eneo la mahali patakatifu (Stefanovic 2002: 32-35).
   - Utangulizi (**1:1-8**)
   - 1. Utangulizi wa mahali patakatifu (**1:9-20**)
     Ujumbe kwa makanisa saba (**2:1-3:22**)
   - 2. Utangulizi wa mahali patakatifu (**4:1-5:14**)
     Kufunguliwa kwa mihuri saba (**6:1-8:1**)
   - 3. Utangulizi wa mahali patakatifu (**8:2-5**)
     Kupigwa kwa tarumbeta saba (**8:6-11:18**)
   - 4. Utangulizi wa mahali patakatifu (**11:19**)
     Hasira ya mataifa (**12:1-15:4**)

[9] TaWarumibeta ya saba (**Ufu 11:15-19**) huondoa mwisho wa nyakati hizi na mwanzo wa nyakati zijazo na kuzungumzia matukio yale yale ya nyakati za wisho kama yalivyozungumziwa mwishoni mwa kitabu. Ukweli kwamba ta Warumibeta ya saba ilipigwa katikati, badala ya mwishoni, mwa kitabu, ni kiashiria kingine ambacho mpangilio wa *maono* ya Yohana hayawakilishi matukio ya kinyakati kwenye *historia.* (Schüssler Fiorenza 1991: 75-76)

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

5. Utangulizi wa mahali patakatifu (**15:5-8**)
Mpigo saba ya mwisho (**16:1-18:24**)
6. Utangulizi wa mahali patakatifu (**19:1-10**)
Utimilifu wa nyakati za mwisho (**19:11-21:1**)
7. Utangulizi wa mahali patakatifu (**21:2-8**)
Yerusalemu mpya (**21:9-22:5**)
Hitimisho (**22:6-21**)

3. Kuyarudia mawazo kinyume na mpangilio wake wa awali (Stefanovic 2002: 38-40).

A. Utangulizi (**1:1-8**)
B. Ahadi kwa washindi (**1:9-3:22**)
C. Kazi ya Mungu kwa Wokovu wa mwanadamu (**4:1-8:1**)
D. Hasira za Mungu zikichanyikana na Huruma zake (**8:2-9:21**)
E. Yohana kuagizwa kutoa unabii (**10:1-11:18**)
F. Mgogoro mkuu baina ya Kristo na Shetani (**11:19-13:18**)
E'. Kanisa kuhubiri injili ya wakati wa mwisho (**14:1-20**)
D'. Hasira ya mwisho ya Mungu isiyochanganywa na huruma (**15:1-18:24**)
C'. Kukamilika kwa kazi ya Mungu kwa wokovu wa mwanadamu (**19:1-21:4**)
B'. Utimilifu wa ahadi kwa washindi (**21:5-22:5**) A'.
A'. Hitimisho (**22:6-21**)

4. Richard Bauckham (Bauckham 1993a: 21-22).

1:1-8: Utangulizi
1:9-3:22: Uzinduzi wa maono ya Kristo na makanisa ukijumuisha ujumbe kwa makanisa saba
4:1-5:14: Uzinduzi wa maono ya mbingu ukiongozwa na mifululizo mitatu ya saba na miingiliano miwili [kuingizwa kwa kifaa kingine]:
6:1-8:1; 8:3-5: Mihuri saba, ikihesabiwa 4+1+(1+mwingiliano)+1
8:2; 8:6-11:19: Tarumbeta saba, zikihesabiwa 4+1+(1+mwingiliano)+1
12:1-14:20; 15:2-4: Simulizi ya watu wa Mungu kwenye mgogoro na uovu
15:1; 15:5-16:21: Vitasa saba, vikihesabiwa (4+3) bila mwingiliano
17:1-19:10: Ukahaba wa Babeli
19:11-21:8: Kuhamishwa kutoka Babeli hadi Yerusalemu mpya
21:9-22:9: Yerusalemu mpya mke
22:6-21: Hitimisho

5. William Hendriksen (Hendriksen 1982: 16-18).

1. Kristo katikati ya Kinara cha taa (**1:1-3:22**)
2. Maono ya mbinguni na mihuri (**4:1-7:17**)
3. Tarumbeta saba (**8:1-11:19**)
4. Kuteswa kwa Joka (**12:1-14:20**)
5. Vitasa saba (**15:1-16:21**)
6. Kuanguka kwa Babeli (**17:1-19:21**)
7. Hitimisho kuu (**20:1-22:21**)

6. Elisabeth Schüssler Fiorenza (Schüssler Fiorenza 1991: 35-36; tarakimu za Kirumi zinaashiria wazi kuhesabiwa kwa mfululizo wa namba saba)

A. **1:1-8:** Utangulizi na salaam za waraka
1:1-3: Andiko au cheo
1:4-6: Salaam
1:7-8: Utambulisho
B. **1:9-3:22:** Hali ya kejeli kwenye miji ya Asia ndogo
1:9-10: Mwandishi na hali
1:11-20: Uzinduzi wa maono ya kinabii
I. **2:1-3:22:** Ujumbe wa kinabii kwa Jamii saba
C. **4:1-9:21; 11:15-19:** Kufunguliwa kwa kitabu kilichotiwa muhuri: Mapigo ya kutoka
4:1-5:14: Mahakama ya kimbingu na kitabu kilichotiwa muhuri
II. **6:1-8:1:** Mapigo ya Kiulimwengu: Mihuri saba
III. **8:2-9:21; 11:15-19:** Mapigo ya kiulimwengu: Tarumbeta saba

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

D. **10:1-15:4:** Kitabu kichungu-Kitamu: "Vita" dhidi ya jamii
10:1-11:14: Kuagizwa kwa unabii
12:1-14:5: Kutafsiriwa kwa unabii
14:6-15:4: Uhuru au ukombozi wa nyakati za mwisho
C'. **15:5-19:10:** Safari ya kutoka kwenye ukandamizaji wa Babeli/Rumi
IV. **15:5-16:21:** Mapigo ya kiulimwengu: Vitasa saba
17:1-18: Rumi na nguvu zake
18:1-19:10: Hukumu ya Rumi
B'. **19:11-22:9:** Ukombozi kutoka kwenye Uovu na Mji wa Mungu hapa ulimwenguni
19:11-20:15: Ukombozi kutoka Nguvu za Uovu
21:1-8: Ulimwengu wa Mungu Ulikombolewa
21:9-22:9: Tofauti za Mungu za kisiasa
A'. **22:10-21:** Hitimisho na sura ya kiwaraka
22:10-17: Misemo ya mafunuo
22:18-21: Hitimisho la kiwaraka

F. ***Muundo: sambamba hatua kwa hatua; siyo kwa mpangilio madhubuti wa wakati***

Ili sote tuweze kuelewa jinsi gani kitabu cha Ufunuo kilivyowekwa pamoja na kinamaanisha nini tunalazimika kuelewa kwamba kitabu hiki siyo simulizi ya nyakati tu. Stephen Travis anasisitiza wazo muhimu kwamba kwenye Ufunuo "ukweli kwamba *maono* yanafuatana kwenye mtiririko siyo sababu ya lazima ya kutuaminisha kwamba yanawasilisha mfuatano endelevu wa *kihistoria*" (Travis 1982: 142). Vitabu vya Kinabii (e.g., Isaya) Wakati wote kimeweka kumbukumbu za maono au unabii kwenye mpangilio tofauti kutoka kwenye mpangilio wa historia ambao yalifanyika. Sambamba na hilo, vitabu vya kinabii (e.g., Danieli) mara nyingi kimehusisha maono tofauti ambayo hujirudia au hurudia matukio yale yale kutoka kwenye mitazamo tofauti.

Kwa sehemu kubwa kitabu cha Ufunuo kimechukulia kutoka kwenye vitabu hivyo vya Agano la Kale kama Isaya, Ezekieli, na Danieli. Beale ameelezea umuhimu wa mfanano wa *kimuundo* baina ya Kitabu cha Ufunuo na Danieli: "Muundo wa maono matano sambamba na yaliyo sawasawa ya Danieli (sura za. 2, 7, 8, 9, 10-12) waweza kuwa ushawishi mkubwa kwenye muundo wa kitabu cha Ufunuo, Kwa kuwa kitabu cha Danieli kimetumika sana kwenye kitabu cha Ufunuo na kimetumika kuashiria migawanyiko mipana ya muundo wa Ufunuo. . . . Maono sambamba matano ya Danieli ni mitazamo ya ziada kuhusiana na wakati huohuo wa kipindi cha wakati ujao kwa ujumla; ni kitu kisichotarajiwa kwa kitabu kama Ufunuo kujifananisha chenyewe na Muundo sambamba wa Danieli na bado kuwa na vifungu vyake sambamba ambavyo pia havihusiani na kipindi kile kile cha wakati ujao kwa ujumla. Badala yake, ingeonekana ya kiasili zaidi kwa usambamba huo kuashiria mtazamo wa kinyakati wa 'tayari na bado', hasa kwa kuwa baadhi ya maono muhimu ya wakati ujao ya Danieli yalianza kutimia kwenye ujio wa kwanza wa Kristo. Kwamba matukio hay ohayo ya kujirudia yanayopatikana kwa Danieli pia yalitokea kwenye vitabu vingine vya ki-mafunuo vya Wayahudi . . . vivyo hivyo huonyesha matukio ya kufanana kwenye kitabu cha Ufunuo." (Beale 1999: 135-37)

Kwa mtazamo huo hapo juu, wachambuzi wengi hutazama vifungu tofauti kwenye kitabu kuwa mfanano muhimu kwa kila kimoja na kingine: matukio yel yale muhimu au makubwa yanaweza kurudiwa kwenye maono tofauti (kwa kutumia picha tofauti) na kwenye sehemu tofauti za fasihi. Vifungu hivi mfanano huhusisha nyakati zote za Kanisa; huunganisha matukio ya muda na yale ya heshima (i.e., kurudiana moja na jingine); na kuhitimisha pamoja na mwisho wa nyakati, *parousia,* hukumu, na mbingu mpya nan chi mpya. Ingawaje hujirudia moja na jingine, vifungu mfanano huonyesha baadhi ya nyakati na mwendelezo wa kisaikolojia, i.e., mwanzoni kwenye kitabu mwisho umefikiwa, lakini inakuja kuelezewa kwa kina zaidi kwenye maelezo ya baadaye yanayofanana.

William Hendriksen mwanzoni aliliita hili "mfanano endelevu," kwa sababu vifungu tofauti vya kitabu: "vimepangwa kwenye mpangilio wa kukua, kufikia kileleni. Upo mwendelezo kwenye msisitizo wa nyakati. Hukumu ya mwisho mwanzoni *ilitangazwa* kisha *kuanzishwa* na hatimaye *kufafanuliwa.* Sawa na hilo, mbingu nan chi mpya zimeelezwa kwa kina zaidi kwenye kifungu cha mwisho kuliko kwenye vifungu vilivyotangulia." (Hendriksen 1982: 36) Huu ni mtazamo uliochukuliwa na Victorinus wa Pettau (alikufa mwaka c.304), Askofu wa Poetovio (Ptuj, Slovenia ya sasa), mwandishi wa ufafanuzi ya awali iliyokamilika ya Kitabu cha Ufunuo ambayo ilitufikia (Bruce 1938: 352-53).[10]

[10] Kwenye sura ya 8 ya ufafanuzi wake, kuhusiana na uhusiano wa taWarumibeta na vitasa, Victorinus anaeleza,

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Mfanano endelevu unaonekana kwa wazi kwa jinsi mihuri kwenye Kitabu cha Ufunuo (**Ufu 6:1-17; 8:1-5**) inavyoenda sambamba na Hotuba ya Mlimani ya Kristo, na kuishia na maelezo au ufafanuzi wa nyakati za mwisho (**Math 24:3-31; Marko 13:3-27; Luka 21:7-28**). Sawa na hilo, tarumbeta (**Ufu 8:6-9:21; 11:15-19**), mwanamke na Joka kwenye (**Ufu 12:1-14:20**), na vitasa (**Ufu 16:1-21**) vyote vimefanana na kuishia na maelezo au mafafanuzi ya nyakati za mwisho:

Math 24-Hotuba ya Mlimani	***Ufu 6/8:5-Mihuri***	***Ufu 12-14-Mwanamke na Joka***	***Ufu 8-9/11-Tarumbeta***	***Ufu 16-Vitasa***
Vita: **24:6** Kukosekana utulivu: **24:7** Matetemeko: **24:7** Njaa: **24:7** Mateso: **24:9** Makristo wa uongo: **24:23**	Vita: **6:3-4** Kukosekana utulivu: **6:3-4** Njaa: **6:5-6** Mateso: **6:9-11** Kristo wa uongo: **6:1-2**	Vita: **12:7; 13:7** Ole wa nchi: **12:12** Ole wa bahari: **12:12** Mto: **12:15** Mateso: **12:13** Mungu wa uongo: **13:4, 12-14**	Nchi: **8:7** Bahari kuwa damu: **8:8-9** Mito na chemchemi: **8:10** Mto Frati: **9:14**	Nchi: **16:2** Bahari kuwa damu: **16:3** Mito na chemchemi: **16:4** Mto Frati: **16:12**
Kupatwa kwa Jua: **24:29** Kupatwa kwa Mwezi: **24:29** Kuanguka kwa nyota: **24:29** Kutikiswa kwa nguvu za mbinguni: **24:29**	Kupatwa kwa Jua**:** **6:12** Mwezi: damu: **6:12** Kuanguka kwa nyota: **6:13** Tetemeko; kutikishwa mbingu: **6:12, 14**		Kupatwa kwa jua: **8:12** Kupatwa kwa mwezi: **8:12** Kuanguka kwa nyota: **8:10** Kupatwa kwa nyota: **8:12** Tetemeko: **11:13**	Kuunguzwa na jua: **16:8** Kiti cha enzi cha mnyama: giza: **16:10**
Mwanawa adamu & mawingu: **24:30** Malaika kukusanya: **24:31**	Hasira ya Mungu na Mwanakondoo: **6:16-17** Sauti kuu: **7:2** Radi: **8:5** Sauti: **8:5** Umeme: **8:5** Tetemeko: **8:5**	Hasira ya Mungu: **14:10** Mwana wa Adamu & mawingu: **14:14** Sauti kuu: **14:15** Malaika kuvuna: **14:17-20**	Hasira ya Mungu: **11:18** Sauti kuu: **11:15** Radi: **11:19** Sauti: **11:19** Umeme: **11:19** Tetemeko: **11:19** Dhoruba: **11:19**	Hasira ya Mungu: **16:19** Sauti kuu: **16:17** Radi: **16:18** Sauti: **16:18** Umeme: **16:18** Tetemeko: **16:18** Dhoruba: **16:21**

1. <u>Mitazamo tofauti ya viwango vya harakati za nyakati dhidi ya kujirudia miongoni mwa mihuri-tarumbeta-vitasa.</u> Kuna baadhi ya kutokukubaliana miongoni mwa wachambuzi kuhusiana na kiwango cha ambavyo mihuri, tarumbeta, na vitasa vinavyohusiana.Moja ya ukweli unaochanganya umetajwa na Johnson: “Kama ilivyo aina ya maono mara nyingi hufunga pamoja nyakati mbalimbali kwenye picha za ishara ambazo hupita kama kufumba na kufumbua macho (angalia Ufu. 12:1-5, ambayo hurefusha historia ya ukombozi kutoka Mwanzo 3 hadi Matendo ya Mitume 1), hivyo pia mpasuko wa pili kwenye wakati kwaweza kupanuliwa kwenye maelezo ya mwonaji na kilele cha matukio ya wakati huo huo kuwakilishwa kama yanayofuatia, ili kuwasaidia wasikilizaji kuona pande tofauti za ushindi wa Kristo.” (Johnson 2001: 176)

Wale ambao wanafikiri mihuri, tarumbeta, na vitasa ni utaratibu wa kawaida kwenye aina ya nukuu ya wakati: (A) mpangilio wa mapigo umetofautiana; (B) viwango vyake vimeongezeka kutoka ¼ ya kibinadamu kwenye mihuri (**6:8**) hadi 1/3 kwenye tarumbeta (**9:15**), hadi kuwa ya kiulimwengu kwenye vitasa (**16:1-11**); (C) kutokuwepo (kwenye mtiririko wa vitasa) ya “kuingiliana au kuchelewa ambako huzuia mwendelezo wa mzunguko wa tarumbeta kufikia kwenye kilele chake” (Ibid.: 36); (D) vitasa vimeelezwa kama kuwa*“vya mwisho, kwa sababu ndani yake hasira ya Mungu imeisha”*

“TaWarumibeta ni neno la nguvu. Na ingawa kuna marudio ya maeneo kwa vitasa, hili halikuzungumziwa kana kwamba matukio yalitokea mara mbili. Badala yake, kwa kuwa matukio ambao ni ya wakati ujao kwao yalikuwa yametangazwa na Mungu kutokea, mambo haya yamezungumzwa mara mbili. Na kwa hiyo, chochote alichokisema kifupi kwa njia ya taWarumibeta alikisema kwa ukamilifu zaidi kwa njia ya vitasa. Hakuna sababu ya kutafakari sana juu ya utaratibu wa kile kilichosemwa. Kwa mafungu saba Roho Mtakatifu, wakati alipopita kwenye tathmini ya matukio ya wakati wa mwisho, hata mwisho, alirudia tena wakati uo huo na kurutubisha au kuongezea kile alichokisema pasipo ukamilifu. Wala hatulazimiki kuuliza mengi juu ya mpangilio wa Ufunuo. Badala yake, tunapaswa kuuliza juu ya maana, kwa kuwa pia upo uwezekano uelewa batili.” (Victorinus 2012: 8.2). Mtazamo huu huu wa kujirudia rudia ulitumiwa na Tyconius kwenye maoni yake yenye ushawishi juu ya Ufunuo (sasa yamepotea kwetu), yaliyoandikwa takriban mwaka BK 385 (angalia Yarbro Collins 1998: 388).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

(**15:1**) (angalia Beale 1999: 116-21; Resseguie 2009: 56-59; Smith 1962: 1515-16; Thomas 1998: 191-93; Johnson 2001: 36-37, 46-47, 223n.4). Thomas anaziona mihuri, tarumbeta, na vitasa kama kuwa muhimu, lakini siyo kwa ujumla wa nyakati. Kama alivyoziona, zilikuwa na uhusiano wa "kiona mbali au darubini ya kukuzia" ambayo kwayo hukumu ya vitasa ilibebwa humo na "suala kutoka hukumu ya mwisho ya tarumbeta ya saba ambayo, kwa namna nyingine, ni matokeo ya muhuri wa saba kwenye hukumu ya mihuri saba" (Thomas 1994: 73) Kwa maana nyingine, Elisabeth Schüssler Fiorenza anachora mpaka baina ya muhuri wa tano na kile kilichofuata. Aliona mihuri ya kwanza mitano kama maandalizi, kama inapingana na muhuri wa sita na saba, tarumbeta, na vitasa, ambavyo aliviona kama hitimisho, matukio ya majanga ya kidunia ya "siku iliyo kuu ya Bwana" (Schüssler Fiorenza 1991: 65, 71, 93). Kisha tena, Dennis Johnson anaonekana kuutazama wingi wa mihuri na tarumbeta siyo kama mfuatano bali kama kuingiliana moja kwa moja na nyakati hizi (Johnson 2001: 122, 146, 223). Umuhimu wa mipaka yake ni baina ya tarumbeta na vitasa. Alivitazama vitasa saba tu kama vinaashiria hukumu ya mwisho, lakini kimsingi anakubaliana na Thomas kwamba zilikuwa "zilikuwamo pamoja na kufafanuliwakwenye tarumbeta ya saba na muhuri wa sita" (Ibid.: 223n.4).

Wengine huona mwendelezo wa matukio kwenye kitabu cha Ufunuo siyo kama uthibitisho wa nyakati au wa kihistoria lakini kama uwakilishi wa mwendelezo wa *kifasihi*. Kwa maneno mengine, mahusiano baina ya mihuri, tarumbeta na vitasa kimsingi ni ya kisaikolojia. Kujirudia na tukio la msisitizo au fafanuzi mpya. Kwa mfano, Beale, anang'ang'ania kwamba wingi wa vitasa kurudia mihuri na tarumbeta nyakati zote, vyote vina hitimisho la kawaida (hukumu ya mwisho). Alieleza, "Hakuna mawasiliano ya moja kwa moja baina ya mwingiliano wa tarumbeta na kitasa. Lakini vinafanana kiasi cha kutosha kuzingatia kuwa sehemu ya mpango wote wa hukumu ya Mungu itakayotokea wakati wa kipindi hicho hicho cha jumla." (Beale 1999: 810) Kwenye mtazamo wake, mihuri mitano ya kwanza, tarumbeta sita, na vitasa vitano hufunika wakati baina ya kufufuka kwa Kristo na *parousia;* mihuri miwili ya mwisho, tarumbeta ya saba, na vitasa viwili vya mwisho huonyesha hukumu ya mwisho (Ibid.).

2. Maelezo ya kina zaidi ya hatua kwa hatua ya "tetemeko" kwenye sura ya **8:5; 11:19; 16:18-21** na janga la kiulimwengu kwenye sura ya **6:12-17** na **20:11** ni la *kisaikolojia, siyo la kinyakati*. Matumizi ya tetemeko ya kitabu cha Ufunuo yamechukuliwa kwenye Agano la Kale, ambayo yanaelezwa kutikisika kwa nchi wakati Mungu atakapojidhihirisha mwenyewe. Kwenye suala hili wakati wote tetemeko ni sehemu ya kutikisika kwa ulimwengu wote wakati Mungu atakapoonekana.

Hili lilitokea kwenye Mlima Sinai na kwenye matukio mengine wakati uliopita (**Kut 19:18**; **Waam 5:4-5; Zab 68:8; 77:17-18; 114; Isa 64:3; Hab 3:3-15**). Agano la Kale huelezea zaidi kwamba kutikisika huku kutatokea kwenye wakati ujao "siku ya Bwana" (**Isa 13:13; 24:18-23; 34:4; Yoeli 2:10; Mika 1:3-4; Nah 1:5-6**). Kwa kiasi kikubwa, Kristo alitumia lugha ya aina hiyo hiyo kuelezea kurudi kwake mara ya pili kwenye hotuba yake ya Mlimani (**Math 24:29-30; Marko 13:24-25; Luka 21:25-26**). Historia hii hutupa mazingira ya tafsiri ya**Ufu 4:5; 8:5; 11:19; 16:18–21; 6:12–17;** na **20:11**:

> **4:5—***umeme na sauti na radi*
> **8:5**—*radi na sauti na umeme na tetemeko la nchi*
> **11:19**—*umeme na sauti na radi na tetemeko la nchi na dhoruba kuu*
> **16:18-21**—*umeme na sauti na radi na tetemeko kuu la nchi . . . na dhoruba kuu*
> ---
> **6:14**—*Unga kupasuliwa vipande . . . na kila mlima na kisiwa kiliondoka kutoka mahali pake*
> **16:20**—*kila kisiwa kilikimbia, na milima haikuonekana*
> **20:11—***nchi na mbingu zilikimbia, na mahali pake hapakuonekana*

"Kanuni, ambayo msingi au kiini chake kimetajwa kwenye tokeo la Sinai [**Kut 19:16**], kumepanuliwa kwa vipengele vya ziada kwenye 8:5 na 11:19, wakati kwenye 16:18-21 tetemeko la nchi na dhoruba kumeelezewa kwa mapana zaidi. Kwenye 4:5 kanuni inaeleza kwamba tokeo limefungwa mbinguni, ambalo kwenye tukio la baadaye litakuwa tokeo litakalopelekea hukumu ya nchi. Hivyo kanuni hutumika kuwa msingi wa hukumu ya Mungu kwenye sura za 6-16 kwenye maono ya mwanzo ya utawala wa Mungu mbinguni kwenye sura ya 4. Pia hutengeneza aina halisi ya mahusiano baina ya mifululizo mitatu ya hukumu saba. Hukumu za kufunguliwa kwa muhuri ya saba, hitimisho au kilele cha mfululizo wa kwanza, ulioelezwa na kanuni hii kwenye 8:5, huhusisha mwendelezo wote wa hukumu za tarumbeta saba, na sawa sawa na hukumu ya tarumbeta ya saba, imeelezwa na kanuni hii kwenye11:19b, huhusisha mfululizo wote wa hukumuza vitasa, kuhitimisha kwenye kilele, mafafanuzi

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kamili ya kanuni kwenye 16:18-21. Hivyo kanuni huashiria kwamba ni hukumu ile ile ya mwisho ambayo ilifikiwa kwenye saba ya kila mfululizo wa tatu. Pamoja na kila saba mbili za kwanza tunapata kiashiria cha awali cha hukumu ya mwisho, ambao hatimaye mfululizo ufuatao hufikiwa tena kutoka kwa kiwango cha karibu zaidi, kama kilivyokuwa. . . . Vifungu viwili vimebaki kwa ajili ya kufikiriwa. Vyote 6:12-17 na 20:11 ni vifungu vya wazi ambavyo tetemeko la nchi hufuatana na tokeo la Mungu Mhukumu. Zaidi ya hayo kwenye mambo hayo mawili Yohana ameazima asili ya kutikisika kwa ulimwengu, ambako mbingu kama vile nchi zilikimbia kwenye uwepo wa Mungu. Kifungu cha kwanza huashiria maelezo mbali mbali ya Agano la Kale la Siku ya Bwana. La pili linaonekana kujumuisha mtazamo au wazo la kuangamizwa kwa ulimwengu wa kale na kubadilishwa na mpya (cf. 21:1)." (Bauckham 1993a: 8, 208)

Ufu 6:14 (*"kila mlima na kisiwa kikahamishwa kutoka mahali pake"*), **16:20** (*"kila kisiwa kikakimbia, wala milima haikuonekana tena"*), na **20:11** (*"nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana"*) yote ni mistari iliyo sambamba kwa wazi, maelezo yanayokaribiana kufanana, haya yanaweza tu kuelezea tukio moja: kuangamizwa kwa nchi mwishoni mwa nyakati; hukumu ya Mungu na *parousia*. Kumbukumbu iliyo kwenye **6:14** kwa *"kila Mlima na kisiwa"* sambamba na **16:20**. Zote **16:20** na **20:11** zinasema kwamba kila kisiwa (**16:20**), au nchi na mbingu (**20:11**), *"zitakimbia."* Zote zinatumia neno lile lile, hata ikihusisha mtu yule yule na wakati, kwa *"kukimbia"* (*pheug*ō). Vifugu vyote vinaongezwa kwamba Milima (**16:20**), au nchi na mbingu (**20:11**), "havikupatikana." Tena, vifungu vyote vinatumia neno lile lile kwa kutokupatikana (*heurisk*ō). Matukio yote yanayoelezewa kwenye vifungu vyote hivyo ni lazima view sambamba, nan i lazima viwe vinazungumzia *parousia,* kwa sababu *visingeweza kutokea mara mbili*. "hatua ya Yohana ya msisitizo, kutoka sura ya. 6 kuendelea, imekuwa kwamba hakuna mtu juu ya nchi atakayesalimika wakati wa parousia. . . . Chukulia kwenye thamani ya uso, mageuzi ya sura ya. 6 na 16 ni mabaya kama vile yale ya Ufu. 20.11" (Mealy 1992: 160; angalia pia 158-62, 194; Schüssler Fiorenza 1991: 64). "[Matokeo ya tetemeko kuu la nchi ni] yakushangaza hasa kwakuwa tayari hili lilikwisha kutokea mapema nyuma kama kwenye 6:14b kama moja ya matokeo ya kufunguliwa kwa muhuri ya sita. Kujirudia huku ni moja ya viashiria kwamba mfululizo wa mapigo tofauti kwa uhakika hayapaswi kuangaliwa kama ya kufuatana moja baada ya jingine, lakini bila shaka kutazamwa kama toleo tofauti la mfululizo ule ule wa ole za nyakati za mwisho kuandaa njia ya mwisho wa ulimwengu huu na nyakati" (Rist na Hough 1957: 488).[11]

3. <u>Mifano ya hukumu iliyorudiwa inaonyesha kwambaUfunuo siyo mmoja, simulizi ya nyakati, lakini ni mwendelezo wa muundo wa vifungu vinavyofanana.</u> Kwenye kitabu chote cha Ufunuo ipo mifano ya hukumu iliyojirudirudia. Hukumu zilizojirudia hufuata mfano au muundo wa mhusika: zinatoka mbinguni lakini athari zake kuu ni juu ya nchi. Hivyo, mihuri inafunguliwa, tarumbeta zinapigwa, na vitasa vinamwagwa mbinguni, lakini athari zake hutokea juu ya nchi au duniani. Maelezo ya baadaye yameimarishwa na kuongeza kina kwa maelezo ya awali ya tukio lile lile. Kwenye nyongeza kwa mihuri-tarumbeta-vitasa, mifano hii pia ilionekana penginepo. "Kwenye 14:14-20 kuna kuvunwa mara mbili kwa nchi. . . . Mfano ni sawa na ule wa muhuri ya saba, tarumbeta na kitasa. Hukumu inatoka mbinguni, lakini athari zake kuu—hasa hukumu—zinaangukia juu ya nchi. Kipengele kingine kipya kimeelezewa, hata hivyo: Siyo tu hukumu inayoonekana juu ya nchi, lakini pia Baraka za watakatifu ambao walichukuliwa duniani kwenye hukumu ya kwanza zinaonekana. Mfano huu umerudiwa kwenye 19:1-21. . . . Hukumu inatoka mbinguni, na matokeo yake yanajidhihirisha juu ya nchi. Hapa, hata hivyo, mada ya Baraka za watakatifu imeelezewa kwenye hukumu ya mavuno mara mbili iliongezwa kwenye "sherehe ya ndoa" mahali Baraka za watakatifu kwenye hukumu ya mwisho siyo tu zitadokezwa bali zitaonekana wazi. Limebaki eneo moja la hukumu ya mwisho, lile la 20:9-22:5. . . . Muundo ni sawa kama hukumu nyingine. Zinaanzia mbinguni, lakini matokeo ya hukumu yanaangukia juu ya nchi. Kwenye nyongeza, kama kwenye sura ya. 19 kuna kifungu kilichoongezwa kwenye Baraka za watakatifu, kwenye suala hili kwenye Yerusalemu mpya." (Steinmann 1992: 77-78)

[11] **Ufu 6:12-17** na **7:3** pia unatupa mfano ulio wazi wa ukweli kwamba mpangilio wa maono Yohana aliyokuwa nayo *hayawezi* kuwakilisha mpangilio wa matukio kwenye historia ambayo yanaashiria. Kwenye **7:3** Malaika anasema kwamba msiidhuru nchi hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu. Hata hivyo, **6:12-17** aliona kuangamizwa kwa nchi na anga wakati wa "siku ya mwisho." Vivyo hivyo, **7:3** lazima kuitangulia **6:12-17** kwenye *historia* ingawa inafuata **6:12-17** kwenye mfuatano wa maono.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

4. Kumbukumbu iliyorudiwa kwenye "hasira" ya Mungu na Mwanakondoo huonyesha kurejewa. **Ufu 6:17** inasema, *"Kwa maana siku iliyo kuu, yahasira yao, imekuja, naye ni nani awezaye kusimama?"* Hili ni, bia shaka, swali la dhihaka, jibu kwa hili ni "*hakuna hata mmoja*" (angalau miongoni mwa wasioamini). Swali hilo na jibu "huongeza ujumla, kukamilisha asili ya eneo" (Beale 1999: 124). **Ufu 11:18** ni saw: *"Hasira yako nayo ikaja, na wakati ukaja wa kuhukumiwa waliokufa . . . na kuwaharibu hao waiharibuo nchi."* **Ufu 14:9-11** inazungumzia asili ya milele ya *"mvinyo wa ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa maji, katika kikombe cha hasira yake"* (i.e., *"moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele"*). "Kisha surah ii inahitimisha na maeneo mawili ambayo yanaweza kutokea tu mwishoni mwa nyakati. La kwanza (mistari ya. 14-16) inawakilisha mavuno, kuzivuna nafsi, na kuonekana kusanyiko la walikombolewa, ambao Bwana wetu aliwataja kwenye Mt 13:30, 39; 24:30, 31. . . . La pili [**14:17-20**], ambalo siyo mavuno bali eneo la mavuno [malaika *"kusanya vichala vya zabibu ya nchi, maana zabibu zake zimeiva, akazitupa zabibu katika shinikizo hilo kubwa la hasira ya Mungu"*], lazima kuona kusanyiko la wasioamini na waovu wa nchi." (Smith 1962: 1514)

Ufu 19:15, ambayo ni wazi kuwa ni kifungu cha kurudi mara ya pili, tena inataja kwenye *"shinikizo la hasira kali ya Mungu"* hivyo huunganisha **14:19-20** pamoja na **19:15**. **Ufu 16:19** hutumia picha ile ile ya hasira ya Mungu kama **14:10**, wakati inapozungumzia *"kikombe cha mvinyo wa ghadhabu Yake."* Farasi wa **14:20** wanaonekana tena kwenye **19:18**. Sawa, cheo sahihi cha Mungu "Mungu Mwenyezi" imetokea kwenye Ufunuo tu kwenye **16:14** na **19:15**. Kusanyiko la wafalme kwenye **16:14** limetokea tena kwenye **19:19**. (Bauckham 1993a: 20). Mazingira ya vifungu vyote hivi vyaweza tu kuwa utimilifu na hukumu ya mwisho.

5. Maelezo ya Mungu na Kristo yanaonyesha mfanano endelevu. Mungu na Kristo wameelezewa kwenye **Ufu 1:4, 8**, na **4:8** kama mmoja *"ambaye yupo na ambaye alikuwepo na ambaye atakuja."* Kwenye **Ufu 11:17** na **16:5** Mungu na Kristo wametajwa moja kwa moja kama mmoja *"uliyeko na utakayekuwako."* Kumbukumbu ya *"na ambaye atakuja"* imeondolewa. Sababu za mabadiliko ni kwamba sauti ya tarumbeta ya saba kwenye **11:15** na kitasa cha tatu kwenye **16:4** imetangaza au zina matarajio ya kuja kwa ufalme, hukumu, na utawala wa Mungu na Kristo. Melezo hayo ya Mungu ni sambamba na maelezo ya kuja kwa Mungu na Kristo na kuonyesha mwendelezo kabla ya kuja kwake.

6. Lugha iliyorudiwa ya kuimba na kufurahi mbinguni huonyesha mfanano endelevu. Kwenye **Ufu 11:17**, eneo la kusifu na kuabudu mbinguni linafuatiwa na kuhakikishwa kwa "mashahidi wawili," wazee ishirini na wanne wakitangaza, *"Wewe Bwana Mungu, Mwenyezi, . . . Wewe . . . umeanza kumiliki na kutawala."* Kwenye **Ufu 19:6** makutano makuu mbinguni nao wakatangaza *"Bwana Mungu wetu, Mwenyezi, amemiliki."* Neno lile lile la (Kigiriki = *basileu*ō) limetumika kwa "kumiliki" kwenye mambo yote mawili. Kwenye mambo hayo vitenzi vipo kwenye utendaji wa kibinadamu wa dalili ya wakati. Johnson anaelezea umuhimu wa hili: "Wakati wa kibinadamu wa kitenzi hiki [hasa kwa kuwa ni kitenzi 'kigezo'] kinaashiria kuanzishwa kwa utawala au umiliki wa Mungu, kuanzishwa kwa ukombozi wake na ufalme wa nyakati za mwisho kwenye kwenye utimilifu wake na awamu ya mwisho, pamoja na kutiishwa kwa maadui na wapinzani wake wote. . . .Biblia iitwayo (New American Standard Bible) NASB kwa usahihi inaashiria kuanzishwa kwa matokeo ya muundo wa kibinadamu, *ebasileusas*, kwenye Ufu. 11:17: 'wewe . . . umeanza kumiliki au kutawala.' Muundo ule ule wa kibinadamu wenye kitenzi kwenye19:6 kinachukulia nguvu ile ile ya kuanzishwa na kinapaswa kutafsiriwa sambamba." (Johnson 2001: 262, 262n.32, 263n.33)

Kwenye **Ufu 15:3-4**, kifungu mfanano cha kusifu na kufurahi mbinguni, waliokombolewa *"wakiimba wimbo wa Musa, mtumwa wa Mungu na wimbo wa Mwanakondoo."* Kwa sehemu kubwa wimbo huu umechukuliwa kwenye Agano la Kale "nyimbo za Musa" (**Kut 15:1-18; Kumbukumbu la Torati 32:1-43**) sawa na vifungu vingine vya Agano la Kale kama vile **Zab 86:8-10; 111:1-3; Isa 66:23; Yer 10:7**. Nyimbo zote hizi zinaonyesha utimilifu wa "wimbo mpya" ulioimbwa na wazee ishirini na wanne kwenye **Ufu 5:9-10** ambao kwa huo walielezea tena Sadaka ya kifo cha Mwanakondoo, kuwafanya waliokombolewa kuwa ufalme na Makuhani, na kuwawezesha waliokombolewa kutawalajuu ya nchi. Kufuatiwa na kutupwa kwa Babeli mkuu, makutano wakifurahia juu ya Mungu kulipiza *"kisasi juu ya damu ya Mtumishi wake"* (**Ufu 19:2**). Hili ni kukumbukwa kwa "wimbo wa Musa" (**Kumb 32:1-43**) ambao unahitimishwa kwa kusema kwamba Mungu *"atalipiza kisasi kwa damu ya mtumishi wake"* (**32:43**).

Nyimbo hizi zote zinaonyesha maono tofauti ya kushindwa kwa uovu, kuhakikishwa kwa watakatifu, na kuambatana na furaha mbinguni kwenye utimilifu wa mpango wa Mungu, ushindi

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

wake, na kumiliki kwake. Muunganiko miongoni mwa vifungu hivi tene vinadhihirisha muundo wa mfanano endelevu wa kitabu.

7. Lugha iliyorudiwa ya mwisho inaonyesha mfanano endelevu. **Ufu 10:7** (wakati malaika alipokuwa tayari kupiga tarumbeta ya saba) alisema, *"Siri ya Mungu imetimizwa."* **Ufu 15:1** (wakati malaika alipokuwa tayari kumwaga vitasa) sawa na lile alisema, *"hasira ya Mungu imetimizwa."* Kwenye mambo hayo yote mawili neno la Kigiriki *etelesthē* ("imetimizwa") limetangulia "siri ya Mungu" na "hasira ya Mungu." Kukiweka kitenzi kwenye nafasi hiyo kwenye mambo yote hayo kunasisitiza "mwisho na ukamilifu wa mpango wa Mungu" (Johnson 2001: 162n.9). Sawa na hili, **Ufu 16:17** inasema, *"Sauti kuu ikatoka katika hekalu, katika kile kiti cha enzi, ikisema, Imekwisha kuwa.'"* Kwenye mtindo mfanano, **Ufu 21:6** inasema, *"Kisha Aliniambia, 'Imekwisha kuwa.'"* Mifanano hiyo pia huonyesha asili ya mfanano"endelevu" wa kitabu: **Ufu 10:7** iliinuka wakati wa mwingiliano wa hukumu za tarumbeta; **Ufu 15:1** ni mara kabla ya mwishoni mwa "mapigo saba" (hukumu ya vitasa); **Ufu 16:17** ilitokea wakati kitasa cha saba kilipomwagwa; na **Ufu 21:6** inasema wakati Yerusalemu mpya utakaposhuka kutoka mbinguni.

G. ***Ufunuo 1:19 na muundo wa kitabu***

Waamini wa mpito huchukulia mtazamo kwamba kanisa litanyakuliwa na siyo hata kuwepo juu ya nchi, bali mbinguni tu, baada ya **Ufu 3:22**. Wameweka msingi wa mtazamo wao juu ya **Ufu 1:19**, ambao wanauona kama kuanzishwa kwa sehemu tatu za muundo wa kitabu: *"mambo hayo uliyoyaona"* (ambayo wanayatafsiri kuwa ni maono ya Kristo kwenye **Ufu 1:1-18**); *"mambo ambayo yapo"* (ambayo wanatafsiri kuwa makanisa saba ya **Ufu 2:1-3:22**, ambayo kasha hutafsiri kuonyesha "nyakati za kanisa" zitakazoishia kwenye unyakuo wa kabla ya dhiki wa kanisa; na *"mambo yatakayotokea baada ya mambo haya"* (ambayo hutafsiri kuwa mambo yatakayotokea baada ya unyakuo wa kanisa). (Smith 1980a: 17-20; Smith 1980b: 1, 17-18; Thomas 1998: 186-87; MacDonald 1995: 2354, 2361) Mtazamo huo siyo endelevu kwa sababu mbalimbali:

1. Kuomba swali. Mtazamo wa waamini wa mpito *husadiki kabla* kwamba kanisa litanyakuliwa kabla ya dhiki kwa sababu hili lilidaiwa na mpito wenyewe. Kwamba, bila shaka, ni uongo wa *petitio principii* au "kuomba swali" (i.e., kuchukulia kwa urahisi au kusadiki kila kitu kwamba kinahitaji kuthibitishwa). Zaidi ya hayo, wazo kama hili halijaonyeshwa popote kwenye Kitabu cha Ufunuo.
2. **Ufu 1:19** haijaandaliwa au kubuniwa kuanzisha sehemu tatu za muundo wa nyakati kwa matukio ambayo yatatokea kwenye historia. "Kwanza, 'mambo ambayo umeyaona' kwenye 1:19 probila shaka haizungumzii tu kuwa mwanzo wa maono kwenye 1:12-18 na kwa hiyo kukigawanya kitabu ambacho kinajihusisha na yaliyopita kwenye sehemu tofauti ambazo zinajihusisha na yaliyopo na yajayo, hutajwa kwenye maneno yanayofuata kwenye 1:19. Inaelezea, badala yake, maono yote ya kitabu ('yale uyaonayo,' wakati wa kibinadamu wa *eides* hauashirii muda wa maono bali ujumla wake). Uwezekano huu hudhibitishwa na mtazamo kwamba mstari wa 19 hausimami wenyewe bali ni sehemu ya kifungu chote (mistari ya 9-20) huku ni kutazamwa kuliko bora kama kunaruhusu simulizi, ili kwamba 'andika kile uonacho' ni marudio tu ya agizo kwenye 1:11 kuweka kumbukumbu ya maono ya kitabu chote. Pili, 'mambo yaliyopo' bila shaka haizungumzii tu mambo yaliyopo kama ilivyoelezwa kwenye sura za 2-3 lakini kwa kumbukumbu yay ale yote yaliyopo kwenye kitabu chote. Kwa uhakika, haiwezi kuwa kumbu kumbu ya muda kabisa, bali kumbukumbu ya asili ya mafumbo ya kitabu ambayo yanahitaji kutafsiriwa (kwa hiyo, baadhi hutafsiri *ha eisiv* kama kumaanisha 'Nini wao [maono ya picha]'." (Beale 1999: 162-63)

Msemo wa tatu, *"baada ya mambo haya,"* hakumaanishi "baada ya mambo ya kanisa kukamilika" kama, kwa mfano, Chuck Smith alivyolichukulia (Smith 1980a: 17-20; Smith 1980b: 17-18). Baadala yake, **Ufu 1:19** (sambamba na **1:1; 4:1**; na **22:6**) inaashiria kwa **Dan 2:28-29, 45.** Mazingira haya ni muhimu kwa kutafsiri *"baada ya mambo haya."* Hasa, **Dan 2:29** imetumia maneno *"baada ya mambo haya"* (Kigiriki = *meta tauta*) kama sawa na msemo *"kwenye siku za baadaye"* (**Dan 2:28**). Kama vile, wakati Yohana anatumia msemo uleule kwenye **Ufu 1:19**, kipindi cha wakati ambacho kinazungumziwa kinajumuisha kipindi chote kutoka kuja kwa Kristo mara ya kwanza mpaka kuanzishwa kwa mbingu mpya na nchi mpya.[12]

[12] Kwa nyongeza, maneno *meta tauta* yametokea mara nane nyingine kwenye kitabu cha Ufunuo (**4:1; 7:1; 7:9; 9:12; 15:5; 18:1; 19:1; 20:3).** Msemo unaashiria "mpangilio ambao Yohana aliona maono lakini siyo lazima kuwa mpangilio wa kihistoria ya kutokea kwake kama matukio" (Beale 1999: 316–17).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

3. *“Mambo yaliyopo”* na *“mambo ambayo yatatokea baada ya mambo haya”* yameunganishwa na hayawezi kutenganishwa kabisa. Yote mawili *“mambo yaliyopo”* na *“mambo ambayo yatatokea baada ya mambo haya”* yanaelezea yaliyomo kwenye “Ufunuo mmoja” ambao Yesu Kristo alimpa Yohana (**Ufu 1:1-2**). Kama vile, “barua saba kwa makanisa saba” (**Ufunuo 2-3**) kuhusiana na mazingira ya sasa ya kanisa lakini pia anaweka ahadi kwa heshima ya wakati ujao. Kwa kweli, mengi ya kile kilichojumuishwa kwenye hizo “barua saba” kilikuwa cha wakati ujao wakati Yohana akiandika kitabu cha Ufunuo lakini kwa sasa ni wakati uliopita kwetu. Sawa na hilo, ukweli kwamba maono kwenye **Ufunuo 4-22** hutuonyesha matukio ambayo yalikuwa ni ya wakati ujao wakati Yohana alipopokea maono, hayatuambii sisi ni yapi ya maono hayo ambayo ni ya wakati ujao kwetu. Mengi ya matukio ya **Ufunuo 4-22** yalitukia kwenye historia yote na yanapitisha historia. Hivyo, rahisi na ya kueleweka “wakati uliopita-uliopo ujao” muundo wa nyakati wa Ufunuo siyo sahihi.

VI. Kanisa kwenye kitabu cha Ufunuo

A. *Kitabu cha Ufunuo kiliandikwa kwa, kwa ajili ya, na kuhusu kanisa*

Kitabu cha Ufunuo kiliandikwa kwa kanisa (**Ufu 1:4; 22:16**). Kama tulivyoona hapo juu, kiliandikwa kwa ajili ya kanisa na kinashughulika na maswala yanayolihusu kanisa. Kwa hiyo, kama tutakavyoona, kanisa lipo katika kitabu chote.

Kwa upande mwingine, waamini wa mpito huamini kwamba kanisa litanyakuliwa mwanzoni mwa sura ya 4, kwa sehemu kwa sababu “neno *kanisa,* ambalo limekuwa maarufu sana kwenye sura za 2 na 3, halikutokea tena hadi 22:16” (Walvoord 1966: 103). Tena, mtazamo huo *unasadiki kabla* kwamba kanisa litanyakuliwa kabla ya dhiki kwa sababu hilo limedaiwa na mpito wenyewe. Mtazamo huu siyo endelevu kwa sababu mbali mbali.

1. Kutokuwepo kwa neno “kanisa” hakuthibitishi chochote kabisa. “Kwanza, ni lazima ikumbukwe kwamba neno ‘kanisa’ (*ekklēsia*) kama maana ya mwili wote wa Kristo halijaonekana kabisa kwenye kitabu. Matumizi pekee ya neno kwenye kitabu ni kutumika kwenye kanisa hasa la mahali au kwa ‘makanisa.’ . . . Kwakuwa istilahi haikutumiwa kabisa kwenye kitabu, itakuwa wazi kwamba kutokuwepo ushiriki wa ‘kanisa’ kwenye baadhi ya sura hakutakuwa na maana yeyote kuliko kuktokwepo kwake kwenye kitabu kizima.” (Bell 1967: 318-19) Pili, nano“kanisa” halijatumiwa kwenye maono ya Yohana kuelezea watu wa Mungu walioko mbinguni pale waamini wa mpito wanaposema kanisa limewekwa baada ya **Ufu 3:22**. Hata **Ufu 19:7-9**, ambayo inataja au kuzungumzia “arusi ya Mwanakondoo,” haikutumia neno “kanisa,” bali waliliita kanisa “bibi arusi” na “watakatifu.” Tatu, injili mbali mbali na nyaraka pia hazikulitumia neno “kanisa” lakini kwa wazi zimezungumzia kuhusiana na waamini (i.e., kanisa).[13]
2. Kitabu kizima kinahusu Kanisa. Vyote utangulizi wa Yohana (**Ufu 1:1-4**) na kumbukumbu ya hitimisho lake kwa kanisa kwenye **Ufu 22:16** (*“Mimi, Yesu, nimemtuma malaika wangu kuwashuhudia ninyi mambo hayo katika makanisa”*) inaweka wazi kwamba kitabu *kizima* ni kuhusiana na kanisa. “Ufunuo 1:4 unatuambia kwamba yote yaliyomo kwenye kitabu kimeandikiwa makanisa haya,na ukweli huu pekee humaanisha barua zile [i.e., **Ufunuo 2-3**] hazikusudiwi kusimama zenyewe na kutenganishwa na kitabu chote” (Goldsworthy 2000: 217). Kwenye **Ufu 22:16** pale Yesu anaposema *“Nimemtuma malaika wangu kuwashuhudia ninyi mambo haya,”* somo la ushuhuda wa malaika ni kitabu chote, siyo tu sehemu yake. Waamini wa mpito hukifanya kitabu chote *kutokueleweka* kwa kanisa. Tafsiri ya Waamini wa mpito kwamba kanisa halikuwepo kitabuni kutoka baada ya sura ya 3 ni ajaqbu ya mbali kutajwa. Wazo kwamba “kwenye utimilifu wa kitabu cha Agano Jipya, kimeelekezwa hasa kwa makanisa saba ya kihistoria yaliyokuwa yakikabiliwa na mateso makali na uhitaji wa makusudi maneno ya matumaini kutoka kwa Mtume, badala ya Yohana kuelekeza sura tatu tu kwao na kutumia muda wake mwingi kukusanya kitabu kirefu cha nyakati za mwisho kuhusiana na matukio ambayo yatatokea juu ya nchi baada ya kanisa kuondolewa . . . kunafunua utepetevu au kukosa kwake kina cha maelezo na kushindwa kwake kujihusisha na yaliyomo kwenye kitabu kwa njia yoyote ile inayoleta maana” (Bell 1967: 317).

[13] Neno *Ekklēsia* halikuonekana kwenye injili ya Marko, Luka, na Yohana. Halikuonekana pia kwenye nyaraka za 2 Timotheo, Tito, 1 Petro, 2 Petro, 1 Yohana, 2 Yohana, na Yuda.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

B. ***Umuhimu kwenye kitabu cha Ufunuo wa matumizi ya maumbo ya Agano la Kale kulielezea kanisa***

Mwanzoni kabisa mwa kitabu (**Ufu 1:6**) Yohana anasema, *"Kutufanya kuwa ufalme na makuhani wa Mungu na Baba."* Hili lilitumika kwa kanisa lugha ya **Kut 19:5-6**, ambayo mwanzoni ilitumiwa kwa Israeli ya Agano la Kale (cf. **1 Pet 2:5, 9**). **Ufu 5:9-10** inatumia lugha sawa na ile na pia kuelezea *"kila kabila na lugha na jamaa na taifa."* "Kama lugha iliyotumika hapa ya *watu hawa wa kila kabila, na lugha, na jamaa, na taifa,* wakati waliposema wamefanywa *kuwa ufalme na Makuhani wa Mungu,* ni aina ileile kama ile ya [**1:6**], tunaona ikiruhusiwa kuhitimisha kwamba, hata kutoka kwenye aya zake za mwanzo kabisa, Ufunuo ulikuwa na mtazamo wa jumla wa kanisa." (Milligan 1896: 82)

Matumizi ya maumbo ya Agano la Kale kwenye Ufunuo kwa ajili ya taifa la Israeli kwa kanisa kuna matokeo muhimu sana kwa uelewa wa kitabu na kuona kiini cha mahali kanisa lilipo ndani yake: "Mwenendo wote wa kitabu, kutoka rejeo la utangulizi hadi kwenye Makanisa ya Kikristo yaliyoko Asia chini ya ishara ya patakatifu pa Wayahudi, hadi kwenye maono ya mwisho ya Yerusalemu mpya, kunashuhudia kwenye kweli ambazo zilikuwepo kwenye mawazo ya mwonaji, Kanisa la Kristo limechukua nafasi ya Israeli halisi. . . . Kutoka kwenye kanuni hii kunaibuka *bado* nyingine. Ikiwa mambo ya Israeli sasa yanatumika kwa Kanisa la Kristo ni lazima yawe moja kwa moja na matumizi ya kiulimwengu badala tu ya eneo dogo la mahali. Israeli ya kweli ilitawanyika kwenye kila taifa, na sawa na hilo Babeli pia ilikuwa ya kiulimwengu. Vinara saba vya taa vinaonyesha muunganiko wa waamini kiulimwengu, bali kwa asili matawi yake saba ya kinara cha taa yapo au yanadumu mahali patakatifu Palestina. Kwenye kitabu chote hiki Yohana alichukulia vifaa kutoka kwenye maono ya manabii wa Agano la Kale kwa asili yakieleweka kwenye eneo dogo la mahali, na kuyatumia kwenye matukio ya kiulimwengu." (Ford 1979: 257, 258)

C. ***Kanisa kwenye kitabu cha Ufunuo: takwimu kuu na ishara***

Kwa kuwa kitabu cha Ufunuo ni*"Ufunuo wa Yesu Kristo"* (**Ufu 1:1**), Mwili wa Kristo, kanisa, lipo kwenye kitabu chote. Limeelezewa kwa ishara mbalimbali karibia kila sura. Yohana anaukubali ukweli wa Agano Jipya kwamba, "kama mwili wa Kristo, na kwa hiyo inatarajiwa kwamba mwili utashiriki uzoefu wa kichwa" (Ibid.: 259). Hivyo, kupitia kitabu chote tunaona kanisa likipitia vyote mateso, na kuhakikishwa na ushindi, wa Kristo. Zifuatazo ni ishara kuu zilizotumika kuelezea kanisa kote kwenye kitabu cha Ufunuo:

1. <u>"Mtumishi au mtumwa wangu" (**Ufu 1:1; 2:20; 7:3; 11:18; 19:5; 22:3, 6**).</u> Kila kumbukumbu kwa "Mtumishi wangu" (Kigiriki = *doulos*, mara nyingi hutafsiriwa "mtumwa" au "mtumishi") kwenye Ufunuo (isipokuwa **15:3** pale istilahi ilipotumiwa na Musa) bila shaka liliwataja Wakristo (i.e., kanisa). Kwa kweli, wakati wote istilahi hii ilipotumika kwenye Agano Jipya kwa watu walioishi baada ya kufufuka kwa Yesu, lilitumika kwa Wakristo. Siyo Wayahudi. Kwenye **Ufu 7:3** "mtumishi wangu" ni njia nyingine ya kuelezea 144,000 wa **7:4**. Kwa kuwa hakuna mahali kwenye Agano Jipya ambapo istilahi "mtumishi wangu" lilitumika kutofautisha "Wayahudi walioamini" kutoka kwa Wakristo wa kawaida wa wakati wowote, lazima ichukuliwe kwa njia ileile, kama inavyotumika kwa kanisa, kwenye **7:3** (kwa mengi zaidi ya 144,000, angalia hapo chini).
2. <u>Makanisa saba (**Ufu 1:4; 2:1-3:22**).</u> Makanisa saba yalikuwa ya kweli, makanisa ya kihistoria kwenye mkoa wa Rumi ya Asia (Uturuki ya sasa). Barua kwa makanisa saba inaonyesha kwamba kanisa ni Israeli ya kweli ya Mungu. Tofauti baina ya nje, Israeli ya kimwili na ndani, Israeli ya Kiroho ni wazi kutoka kwenye kumbukumbu **2:9** na **3:9** kwa *"wale wasemao ni Wayahudi na siyo, bali ni Sinagogi la Shetani."* Kwenye maneno mengine, "wapo watu ambao kweli na kwa nje ni Wayahudi—Israeli halisi—lakini kwa uhakika siyo Wayahudi wa kweli—Israeli ya Rohoni—lakini hufuata njia za Shetani badala ya njia za Mungu" (Ladd 1972: 116).

   Ingawa waliandikiwa kwa umaalum, hali ya kihistoria kwenye makanisa tofauti, jumbe saba zilikuwa na umuhimu wa jumla. Ziliandika mambo na matatizo ambayo yalikuwa ya kila siku kwa makanisa yote na kutengeneza kanuni za kutumiwa kwenye makanisa yote. "Barua saba" zilikuwa na kusudi la pamoja: "Mpangilio wote ni mkusanyiko wa fasihi iliyoandaliwa kulishawishi kanisa la kiulimwengu juu ya ulazima au umuhimu wa uvumilivu na subira kwenye kukabiliana na mateso ya wakati ujao" (Mounce 1998: 65). Vivyo hivyo, karibu wachambuzi wote (isipokuwa wanatheolojia) huyatazama makanisa saba kama wawakilishi wa makanisa kwenye historia yote mpaka kurudi mara ya pili. Hata waamini wa mpito huyatazama makanisa saba kama "wawakilishi siyo tu wa makanisa yote ya wakati wao, lakini pia ya wakati wote mpaka Kristo atakapokuja" (Thomas 1998: 216). Baadhi ya wataalamu wa lugha na kweli za kimazingira ndani ya Ufunuo zinaona kwamba makanisa saba ya **Ufunuo 2-3** yalichaguliwa kufanya au kutumika kwa kanisa la kiulimwengu:

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

- *"Makanisa saba."* Kwanza, hata kanisa la awali kwa kuzingatia namba "saba" kama inayoashiria utimilifu au ukamilifu. Hivyo, makanisa "saba" yanamaanisha kanisa la kiulimwengu (Aune 1997: 130; angalia pia Johnson 2001: 14; Schüssler Fiorenza 1991: 53). Pili, kwenye **Ufu 1:4** makala fafanuzi ("the") kabla ya "makanisa saba" ni kiashiria kwamba makanisa saba yaliandaliwa kuwa na matumizi ya kiulimwengu: "Yohana aliyaandikia mwenye siyo kwa saba, lakini kwa '(the) makanisa saba ambayo yapo Asia,' kama vile hayakuwepo makanisa mengine kwenye eneo au mkoa huo. Zaidi, hata hivyo, kwa uhakika yalikuwepo. . . . Umuhimu ni lazima uambatanishwe na namba saba. Kila msomaji wa kitabu cha Ufunuo ni mzoefu na sehemu ya matumizi mamoja kwa namba hiyo kwenye muundo wake, na pamoja na ukweli kwamba (isipokuwa sura ya. xvii. 9 kuwa ya kipekee) kamwe haikumaanisha tarakimu hiyo pekee. Ni namba ya umoja kwenye utofauti. . . . Namba yao—saba—hiyo lazima izingatiwe kama kiwakilishi cha umoja, na makanisa saba kama wawakilishi wa kanisa moja la kiulimwengu." (Milligan 1896: 28-29)
- *Yaandike kwenye "kitabu" (au gombo la chuo).* Ukweli kwamba jumbe saba kwa makanisa saba zilitakiwa kuandikwa kwenye kitabu kimoja tu au kwenye gombo la chuo (**Ufu 1:11**) ni muhimu: "Ukweli kwamba kulikuwa na gombo moja tu, badala ya saba, kunathibitisha kwamba kitabu ni kwa ajili ya kanisa lote la Kikristo" (Hamstra 1998: 101).
- *Kwa "makanisa."* Kwa njia ambayo Yesu alimalizia kila ujumbe kwa makanisa saba kwenye **Ufunuo 2-3** kunaonyesha kwamba kila ujumbe haukuwa na ukomo kwa lile kanisa la mahali lakini ni kwa matumizi ya kanisa pana zaidi. Sababu ni kwamba, hata ingawa kila moja ya "barua saba" iliandikwa kwa kanisa maalum, mwishoni mwa kila barua ni kwa makanisa yote, i.e., *"Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa"* (**2:7, 11, 17, 29; 3:6, 13, 22**).
- *Utimilifu wa ahadi mwishoni mwa kitabu.* Kile kilichoahidiwa kwa makanisa saba kwenye **Ufu 2:1-3:22** kilipata utimilifu wake baadaye, hasa mwishoni mwa kitabu (angalia hapo juu, kifungu **E. Muundo*: mtazamo wa jumla***). Hili linaashiria uwepo endelevu wa kanisa kwenye kitabu chote na asili ya uwakilishi wa makanisa saba.

3. <u>"Watakatifu" (**Ufu 5:8; 8:3-4; 11:18; 13:6-7, 10; 14:12; 16:6; 17:6; 18:20, 24; 19:8; 20:9**).</u> Mahali penginepo popote Agano Jipya lilipotumia neno "Watakatifu" madhihirisho yake ni kuwataja Wakristo (kanisa) (angalia **Math 27:52; Mdo 9:13, 32, 41; 26:10; Rum 1:7; 8:27; 12:13; 15:25, 26, 31; 16:2, 15; 1 Wakor 1:2; 6:1, 2; 14:33; 16:1, 15; 2 Wakor 1:1; 8:4; 9:1, 12; 13:13; Efe 1:1, 15, 18; 2:19; 3:8, 18; 4:12; 5:3; 6:18; Wafil 1:1; 4:22; Kol 1:2, 4, 12, 26; 1 Wathes 3:13; 2 Wathes 1:10; 1 Tim 5:10; Filemoni 5, 7; Waeb 6:10; 13:24; Yuda 3**). Picha nyingi kwenye kitabu cha Ufunuo huonyesha "watakatifu" juu ya nchi (**Ufu 5:8; 8:3-4; 11:18; 13:7, 10; 14:12; 16:6; 17:6; 18:24; 20:9**). Nyingine huwaonyesha wakiwa mbinguni (**Ufu 13:6; 18:20; 19:8**). Hili linathibitishwa na Agano Jipya lote, ambalo limeanzisha muunganiko baina ya kanisa lililopo duniani na kanisa lililopo mbinguni. Kwa mfano, **Wafilipi 3:20** inatuambia *"wenyeji wetu uko mbinguni."* **Efe 2:6** inathibitisha kwamba kanisa ni *"Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa Roho"* (angalia pia **Kol 3:1**). Kama kwenye **Ufu 14:1** pale wale 144,000*"waliposimama kwenye Mlima wa Sayuni"* pamoja na Mwanakondoo, hivyo kwenye **13:6-7** watakatifu wliopo juu ya nchi pia ndio*"wale ambao wanakaa [au 'hema'] mbinguni."*

Kwenye kitabu cha Ufunuo muunganiko baina ya watakatifu waliopo juu ya nchi na walioko mbinguni umeonekana angalau kwa njia mbili: kwenye mateso na kushindwa; na kwenye ushindi wa milele hatimaye. Watakatifu waliopo usoni pa nchi wanakandamizwa "kwa sababu utiifu kwa uwenyeji wao wa mbinguni hutegemea kutokutii au kutokuuheshimu uwenyeji wao wa hapa duniani" (Beale 1999: 697). Hata hivyo, ingawa wananyanyaswa hapa duniani, watakatifu kiroho wameunganishwa na ulimwengu wa kimbingu kubakia kuwa watendaji na wenye ufanisi. Kwenye **Ufu 5:8** na **8:3-4** chetezo cha uvumba au manukato huashiria *"maombi ya watakatifu."* Kwenye **8:5** malaika anakijaza chetezo na moto wa madhabahu na akautupa juu ya nci. "Picha ina nguvu sana: Maombi ya Wakristo ni muhimu kwa anguko la maadui wa injili" (Johnson 2001: 142).

4. <u>Wale ambao *"walinunuliwa . . . kutoka kila kabila na lugha na jamaa na taifa [ambao walikuwa wamefanywa] Ufalme na Makuhani kwa Mungu wao"* (**Ufu 5:9-10**).</u> "Wimbo mpya" wa **Ufu 5:9-10** ni wimbo wa ushindi na ukombozi. Wale walionunuliwa kutoka kila kabila, lugha, jamaa, na taifa, sasa wanaanzisha ufalme na Makuhani (kwa mengi kwenye "walionunuliwa" angalia hapo chini kwa "Wale 144,000 wa **Ufu 7:4-8; 14:1-5**"). Kumbukumb kwa*"Ufalme na Makuhani"* umechukuliwa kutoka kwenye ahadi alizopewa Israeli kwenye kitabu cha **Kut 19:6** na **Isa 61:6**: "(a) Kwanza kabisa, vitenzi vya maandiko yote mawili ya Agano la Kale ni vitenzi vya wakati ujao—vimejawa na ahadi za Mungu

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kwa watu wake kwa ajili ya wakati ujao. Kwa kulithibitisha hili Yesu alitufanya sisi kuwa Ufalme na makuhani, kwa uwazi mwandishi aliona matendo ya Kristo ya ukombozi kama utimilifu kwa ahadi hizo za Mungu. (b) Pili, ahadi zilizofanywa kwa 'nyumba ya Yakobo,' au 'watu wa Israeli' [**Kut 19:3**] au 'wao waliao katika Sayuni' [**Isa 61:2–3**] wapo kwenye Ufunuo zikionekana kuwa zimetimizwa kwenye kanisa la Kikristo." (Bandstra 1992: 16; hili pia limethibitishwa kwenye **1 Pet 2:5, 9; Ufu 1:6**)

Pamoja na heshima kwa *"kutawala kwao juu ya nchi"* (**Ufu 5:10**), wote kwa wakati huu (*"wanatawala"*) na kwa wakati ujao (*"watatawala"*) wakati umesaidiwa kwa ushahidi wa mazingira mazuri. Wakati uliopo bila shaka ulipendelewa kwa kuwa **5:9-10** inaonekana kuelezea "uzinduzi wa utimilifu wa ufalme uliotabiriwa wa watakatifu na 'mwana wa adamu' kwenye Danieli 7 na kwa uhakika kwamba 1:5b-6a, ambayo huwatazama watakatifu kama ufalme *wa sasa*, umeendelezwa kwenye 5:9b-10a. . . . Zote 1:5-6 na 5:9-10 inaweka wazi kwamba kufanywa kwa watakatifu kama ufalme ni matokeo ya moja kwa moja ya kifo cha ukombozi cha Kristo, hivyo upo uwezekano kwamba ufalme huu ungeanza mara baada ya kifo hiki. Zaidi sana, 'wimbo mpya,' ambao unajumuisha kweli za ukombozi za 'tayari- na-bado, zikijumuisha kumbukumbu za mamlaka ya sasa ya Kristo ('kufungua kitabu'), ili kwamba utawala wa watakatifu, pia sehemu ya wimbo, inawezekana kujumuisha kumbukumbu za kuzinduliwa kwa tukio." (Beale 1999: 362-63) Kwa maneno mengine, "Watakatifu ambao sasa wameangamizwa juu ya nchi tayari wametambuliwa mbinguni kama wale ambao ni watawala, na kusimama hata sasa mbele ya kiti cha enzi cha Aliye juu" (Hooker 1967: 29).

5. <u>Waliouawa au kuchinjwa kwa ajili ya neno la Mungu (**Ufu 6:9-11**).</u> Baadhi hushikilia kwamba waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu ni watakatifu wa Agano la Kale, kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya "kutokuwepo kiasi kikubwa cha maneno 'ushuhuda wa Yesu' kwenye Ufu. 6:9" (Mealy 1992: 85n.1), na ukweli kwamba hawakupokea vazi lao jeupe kabla, bali tu walilipokea kwenye **6:11** (Milligan 1896: 98-102). Hata hivyo, upo uwezekano mkubwa kwamba waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu wanawakilisha Wakristo, labda inajumuisha watakatifu wa Agano la Kale.

Kwanza, mazingira kwenye Ufunuo yanahusu kanisa na mateso ya Wakristo kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu (angalia **Ufu 1:9; 2:9; 2:13; 3:10**, na karibia kila kitu kutoka **Ufu 7:1-20:10**). Pili, "Moja ya msisitizo uliorudiwa kwenye Agano Jipya lote ni kwamba ni asili ya kanisa kuwa watu walio au wanaouawa kwa ajili ya neno la Mungu. Wakati Yesu alipowafundisha wanafunzi wake kwamba mtu ni lazima ajikane mwenyewe na kuuchukua msalaba wake (Math. 10:38; 16:24), hakuwa anazungumzia kujikana mwenyewe au kubeba mzigo mzito; alikuwa akizungumzia utayari wa kuteswa na kuuawa kwa ajili ya neno la Mungu. Msalaba siyo chochote zaidi ya chombo cha kifo. Kila mwanafunzi wa Yesu yupo kwenye nafsi ya kuuawa kwa ajili ya neno la Mungu; na Yohana aliwaona waamini wote waliokuwa wakiteseka." (Ladd 1972: 104; angalia pia Bauckham 1993b: 155; Milligan 1896: 102, 192) Kwa hiyo, wakati inawezekana kwamba ni wale waliouawa kwa ajili yaneno la Mungu halisi waliokuwa kwenye ufahamu, upo "uwezekano mkubwa 'kuchinjwa' ni fumbo na wale wanaozungumziwa huwakilisha kundi kubwa au pana la watakatifu ambao wanateswa kwa ajili ya imani yao. . . . Mahali pengine pekee kwenye Ufunuo ambapo waamini waliokufa wanatiwa moyo 'kupumzika' kunaonekana kuandikiwa watakatifu wote kwa ujumla ambao walivumilia kwa 'kuzishika amri . . . na imani yao' na kufa katika Bwana' (14:12–13)." (Beale 1999: 390-91)

Kama isivyokuwa wazi kusema *"wa Yesu"* baada ya *"ushuhuda"* kwenye **6:9** baadhi ya maandiko ya kale hujumuisha neno *"wa Mwanakondoo"* baada ya *"kwa sababu ya ushuhuda"* (Ibid.: 391). Kwenye kila tukio, ushuhuda*"wa Yesu"* limekuzwa kutoka **1:2, 9**. Zaidi, **12:11**, ambalo kwa wazi huzungumzia Wakristo wanaouawa kwa ajili ya neno la Mungu, vivyo hivyo huzungumzia tu juu ya*"neno la ushuhuda wao,"* ambalo ni sawa na*"ushuhuda wa Yesu"* (**12:17**). Hatimaye, kupokea vazi jeupe ni thawabu ya mbinguni kwa waaminifu (**3:4, 5, 18; 6:11; 7:9, 14; 19:8, 14**).

6. <u>"144,000" (**Ufu 7:4-8; 14:1-5**).</u> Wengi wanakubali kwamba 144,000 wa **Ufu 7:4-8** na **Ufu 14:1-5** huwakilisha kundi lile lile (e.g., Beale 1999: 733; Ladd 1972: 114-17, 190; MacDonald 1995: 2371).

Kuna mitazamo miwili mikuu kuhusiana na utambulisho wa 144,000:

(1) Walikuwa kundi la kikabila la Wayahudi ambao walikuwa walimwamini Yesu Kristo kipindi cha dhiki muda mfupi kabla ya *parousia.* Utambulisho wa 144,000 pamoja na kabila la Israeli msingi wao ni kuchukulia idadi na utambulisho wa kikabila kiuhalisia, na kwenye fikra potofu za mpito kwamba kanisa litakuwa limenyakuliwa kabla ya kutiwa muhuri kwa wale 144,000 kutokea (Pate 1998b: 164-65; Thomas 1998: 196-97; MacDonald 1995: 2364. Gentry anaamini sawa na hilo kwamba hawa ni wa kabila la Wayahudi ambao walikuwa waamini lakini, kamaUtangulizi, aliamini kwamba hili lilitokea kabla ya mwaka BK70, Gentry 1998: 5657).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

(2) Mtazamo mwingine mkubwa (ambao tunaamini ndio uliosahihi) ni kwamba "Chini ya muundo wa Kiyahudi, walijumuisha wafuasi wote wa Kristo, au kanisa la kiulimwengu" (Milligan 1896: 117; Ladd 1972: 114; angalia pia Beale 1999: 412-23; Hamstra 1998: 106-07; Hendriksen 1982: 110-11; Ngundu 2006: 1559; Schüssler Fiorenza 1991: 67). Mtazamo huu ni thabiti pamoja na kusudi la kitabu chote: kutoa taarifa, kusihi, na kulifariji kanisa. Ni thabiti pia pamoja na mada ya vifungu vya kitabu ambavyo kwavyo144,000 wanapatikana (i.e., **Ufu 6:1-8:5** na **12:1-14:20**), ambavyo vyote vinahusika na kanisa kukabiliana na mateso.

Zipo sababu mbalimbali za kuzingatia kwanini144,000 huanzisha kanisa lote (Beale: 1999: 409-23; Milligan 1896: 114-21):

a. *144,000 ni sawa kama "mtumishi wangu" ya **Ufu 7:3.*** Istilahi kwa "mtumishi wangu" (Kwa Kigiriki = *doulos*) "halikutumiwa kabisa na Wakristo Wayahudi popote pale kwenye kitabu, lakini wakati wote hutumiwa na waamini kwa ujumla" (Beale 1999: 413). Kwa kweli, Agano Jipya lote limeweka wazi kwamba ndani ya Kristo *"hakuna tofauti baina ya Myunani wala Myahudi, kutahiriwa wala kutokutahiriwa* (Wak**ol 3:11;** angalia pia **Wagal 3:28**). Kristo *"aliyafanya makundi yote kuwa moja na akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga . . . ili kwamba kwake yeye Mwenyewe aweze kuwafanya wawili kuwa mtu mpya mmoja* (**Eph 2:14, 16**).

Kumchagua mmoja kutoka kwenye kabila la Waisraeli kwa upendeleo maalum ni kinyume kwa utendaji wote wa injili, Agano Jipya, na Ufunuo kwa ujumla: "Hakuna mahali pengine kwenye Ufunuo pameonyeshwa tofauti yeyote baina ya Wayahudi na watu wa Mataifa waliomjia Kristo. Kwenye Ufu. 2-3, Yesu alitembea miongoni mwa kila sehemu ya makanisa saba ya Ki-Asia, ambayo yafanywa . . . kwa waote Wayahudi wa kwanza *na* waamini ambao hapo awali walikuwa ni watu wa mataifa. Maandiko yaliyotiwa muhuri ya Ufunuo 5.1-8.1 yamejaa hukumu na kusudi la Mungu liletalo wokovu kwa ulimwengu wake wote na kwa kanisa lake lote. . . . Sifa za Mungu ambazo zinazunguka kwenye mchezo wote wa Ufunuo, na kuishia kwenye maono ya mji mtakatifu wa Yerusalemu mpya (Ufu. 2122), zinatolewa kwa watakatifu wote wa Mungu, bila kujali kabila lake na dini na historia yake; na wao wote walivaa vazi lile lile jeupe (3.4, 5, 18; 6.11; 7.9, 13)." (Smalley 2005: 187)

Muhuri kwenye vipaji vya uso (**Rev 7:3**) unathibitisha kwamba kanisa lote limetiwa muhuri kwa hiyo kama kusivyokuwa na kiashiria cha ukomo wowote miongoni mwa Waamini ambao wameshatiwa muhuri.[14] Kutiwa muhuri kwa kanisa lote la kuilimwengu kumethibitishwa kwa **Ufu 7:1** ambako malaika wanne wamesimama kwenye *"pembe nne za nchi au dunia"* wakizizuia *"pepo nne za nchi"* mpaka kazi ya kuwatia muhuri itakapokuwa imekwishafanyika. "Hizo pepo za dhoruba ni ulimwengu, na siyo maalum, kwenye asili yake; zinafanya uwezekano wa madhara makubwa kwa viumbe wote, siyo tu sehemu yake, na Wakristo wote, siyo tu kundi fulani la waamini wenye upendeleo" (Smalley 2005: 188).

Historia ya msingi ya Agano la Kale kwa muhuri kwa kanisa kwenye **Ufu 7:3** bila shaka ni **Ezek 9:3-10**, Mungu alipomwaagiza malaika kutia alama kwenye vipaji vya nyuso za wale wote ambao wanalia na kuugua juu ya machukizo ya Yerusalemu; watabakizwa wakati wa hukumu ya mji. "Kuhifadhiwa kwa waaminifu katikati ya hukumu juu ya waovu ni mada ya maono ya Agano la Kale, na kwa maana iyo hiyo ni mada ya maono haya ya Mtakatifu Yohana" (Milligan 1896: 114).

b. *Kutiwa muhuri kwa hao 144,000 ni tofauti na kutiwa muhuri kwa wafuasi wa Shetani.* Kutiwa muhuri kwenye vipaji vya nyuso zao huonyesha umiliki wa Mungu nan i sawa na kuwa na jina la Kristo na Mungu *"limeandikwa katika vipaji vya nyuso zao"* (**14:1; 22:4**). Imetofautiana na muhuri ambao Shetani huweka kwa wafuasi wake. "Alama" ya mnyama kwenye vipaji vya nyuso za wasioamini (**13:16-17; 14:9-11**) inatambuliwa kwa jina la mnyama.

Kwenye Ufunuo wanadamu wote wanatambuliwa kwa moja kati ya kambi mbili: ulimwengu au kanisa; wote wanafaa ama kwa Kristo au kwa mnyama. Hivyo, kwa kuwa Shetani huweka muhuri juu ya wafuasi wake wote (**Ufu 13:16-17; 14:9-11**), Mungu vile vile

[14] Ulfgard anaonyesha, "Watu hawa wanapaswa kutiwa muhuri ili kuepuka hasira ya Mungu iliyotangazwa kwenye 6:16f, siyo ili kuepuka hasira ya nguvu zisizo za Kimungu. Muhuri wa 7:4-8 kwa uwazi inakusudiwa kwa Wakristo wote watu wa Mungu." (Ulfgard 1989:72)

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

huweka muhuri kwa wafuasi wake wote (Beale 1999: 413). Ujumla wa muhuri umethibitishwa kwenye **Ufu 20:4** ambayo inasema *"hao wasiomsujudia yule mnyama, wala sanamu yake, wala hawakuipokea ile chapa katika vipaji vya nyuso zao."* Hili halizungumzii msingi wa kundi la kikabila au jamaa. **Ufu 22:4** vivyo hivyo huzungumza kuhusiana na wale ambao wana *"Jina lake . . . kwenye vipaji vya nyuso zao"* na kwa wazi inazungumzia Wakristo wote.

Kimsingi muhuri huashiria ulinzi wa Kiroho. Ingawa wanaweza kuteseka na kuuawa kwa ajili ya neno la Mungu na imani yao, kwa kuwa wamebeba muhuri na Jina la Kristo, siyo chapa ya Shetani na mnyama, watabaki wakiwa waaminifu hata kufa, na wanalindwa kutokana na hasira ya Mungu kwenye hukumu. Hili ni kwa Wakristo wote, bila kujali ametokea kwenye kundi au kabila gani. Ikiwa muhuri hapa ni kwa kundi la Wakristo lililochaguliwa tu [i.e., Wayahudi walioamini tu, kama baadhi ya wachambuzi wanavyoshikilia] basi, kwa sababu hakuna mahali kwenye Ufunuo aina hii ya muhuri imepewa nafasi, itafuatiwa kwambawaamini waliosalia wa kanisa hawajawekewa muhuri na kulindwa (Smalley 2005: 186, 188).

c. *Maelezo ya makabila ya Israeli (**Ufu 7:4-8**) yanaonyesha kwamba ni kanisa la kiulimwengu, siyo tu Wayahudi walioamini, walioko kwenye mtazamo.* Agano Jipya linaonyesha kanisa kuwa, Israeli ya kweli ya Kiroho. Kwenye Ufunuo, hata kabla ya sura ya 7, Wakristo walishaonyeshwa kama Israeli ya kweli. **Kut 19:6** inatumika kwenye **Ufu 1:6** na **5:10** kwa kanisa; **Dan 7:18, 22** kwenye **Ufu 5:9**; **Isa 62:2** na **65:15** kwenye **Ufu 2:17** na **3:12**; **Isa 43:4; 45:19; 49:23**; na **60:14** kwenye **Ufu 3:9** (angalia Beale 1999: 418). "Yohana anatofautisha baina ya Israeli halisi nay a Kiroho, ingewezekana kwake kuzungumzia makabila kumi na mawili ya Israeli na kwa kufanya hivyo kuwachagua wale ambao ni Wayahudi halisi—yaani kanisa. Na aliashiria maana hii [kwenye **Ufu 7:4-8**] kwa kuyaorodhesha makabila kumi na mawili kwenye muundo siyo kwa kufanana pamoja na nadharia." (Ladd 1972: 116)

Baadhi ya vipengele vya orodha ya makabila kwenye **Ufu 7:4-8** siyo vya kawaida kabisa: Kabila la Dani halipo. (2) Manase lipo lakini Ephraim halipo. (3) Yusufu amekuwa mbadala kwa Ephraim, lakini hili litatengeneza kurudufiwa kwa sababu Yusufu angewajumuisha wote Ephraim na Manase kwa kuwa Yusufu alikuwa baba yao. (4) Mpangilio wa makabila haushabihiani na orodha yoyote kwenye Agano la Kale: Gadi, Asheri, na Naftali—ambao walikuwa watoto wa wajakazi— wameorodheshwa juu ya watoto wengine wote isipokuwa Yuda (ambaye ameorodheshwa wa kwanza) na Ruben. (5) Makabila yenyewe hayakuwepo tena kwa sababu ya utumwa wa Waashuru mwaka 722 KK, kuanguka kwa Yerusalemu mwaka BK 70, na ndoa za mchanganyiko.

Christopher Smith anaonyesha kwa wazi ni jinsi gani Yohana alivyoasili orodha isiyokuwa kwenye mtiririko au isiyokuwa halisi ya makabila kulionyesha kanisa kama Israeli mpya. Yeye alionyesha: "Yuda alionyeshwa wa kwanza kwenye orodha kwa sababu Kristo, ambaye ni kichwa cha Kanisa, alitoka kwenye kabila hili. . . . Kuinuliwa kwa watoto wa wajakazi kunaonyesha kuingizwa kwa watu wa mataifa kwenye agano jipya . . . Ruben hakuhamishwa, hata hivyo. Kama mzaliwa wa kwanza, aliwawakilisha Waisraeli walioamini, wale ambao, ni kama wazaliwa wa kwanza kwenye Agano la Kale, "wao ni mali ya Bwana" (Kut. 13.2). . . . Dani hasa aliondolewa, kama ambavyo wachambuzi wengi walipendekeza, kwa sababu kabila hili kwa muda mrefu limejihusisha na sanamu [na uasi], na kwa sababu ya tamaduni za Kiyahudi kwamba Mpinga Kristo atatoka kwenye kabila la Dani." (Smith 1990: 114-15)

Mazingira ya kina yanathibitisha kwamba 144,000 kutoka "makabila ya Israeli" kwenye **Ufu 7:4-8** wanawakilisha umbo la Wayahudi kwa ishara ya kanisa. Kina cha maono kinaonyesha kwamba maono haya ni ya mbinguni—uhalisia wa mbinguni uhakika wa kanisa (angalia **Efe 2:6; Ufu 20:4**). Yohana alisikia sauti za mbinguni (**Ufu 14:2**), na wale 144,000 walikuwa wakiimba *"wimbo mpya mbele ya kiti cha enzi na mbele ya wenye uhai wanne na wazee"* (**Ufu 14:3**; angalia pia **Ufu 5:8-10**). Wa**eb 12:18, 22** inasema kwamba Wakristo *"mmeufikilia Mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu ya Mbinguni."* Kanisa tayari limekwisha kuwa *"kuufikia Mlima sayuni"* umeonyeshwa kwenye 144,000 ya **Ufu 14:1** ambao ni *"wasimamao juu ya Mlima Sayuni."* Wanatofautiana na wale ambao *"wanakaa juu ya nchi,"* ambao wote ni wafuasi wa mnyama (**Ufu 13:8, 12, 14**). Maelezo kwenye **Ufunuo 13** na **14** yanakusudiwa kuhusishwa yote. Kudai kwamba 144,000 pekee hujumuisha sehemu ya waamini huharibu tofauti Yohana anayoifanya baina ya makao ya watu wa kwenye **Ufunuo 13**

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

na wale kwenye **Ufunuo 14**.

d. *Wale 144,000 wa **Ufu 14:1-5** ni sawa na wote waliokombolewa wa **Ufu 5:9***. Kwenye **Ufu 14:3-4** wale 144,000 ni wale ambao *"walinunuliwa kutoka duniani"* na wale ambao walikuwa *"wamenunuliwa miongoni mwa watu . . .kwa Mungu."* Kwenye **Ufu 5:9** Mwanakondoo *ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa."* Mfanano baina ya makundi hayo mawili ni wa karibu sana kwamba makundi yote mawili yametajwa kama "yalinunuliwa" bila shaka yanafanana. "Hili linamaanisha kwamba wale 144,000 kwenye 14:1-3 siyo baadhi ya masalia wachache wa tamaduni za Ki-Israeli lakini ni njia nyingine ya kuzungumzia kundi kubwa la masalia ya kibinadamu walioishi kipindi cha nyakati za kanisa ambao Kristo aliwakomboa kutoka ulimwenguni kote" (Beale 1999: 412). Hili linathibitishwa na matumizi mengine ya Agano Jipya ya watu "kununuliwa" (**1 Wakor 6:20; 7:23**; Kigiriki = *agorazō*). Kwenye hivyo vifungu vingine Kristo pia aliwanunua Wakristo kwa ujumla (i.e., Kanisa).[15]

e. *Kwenye **Ufu 14:1-5** wale 144,000 wameelezewa kama mabikira au wanawali.* Hapa tena, mtu ni lazima awe makini asianguke kwenye mtego wa kutafsiri picha za mafunuo kiuhalisia, kama Payne alivyofanya wakati alipowaelezea wao kama "kundi la vijana Wakristo waliowekwa wakfu" (Payne 1980: 612). Hakuna mahali ambapo Biblia inaonyesha kwamba tendo la ndoa ndani ya ndoa kama ni dhambi. Ikiwa picha ya **Ufu 14:4** itachukuliwa kiuhalisia na siyo ki-ishara kiwakilishi cha Waamini wote, basi yohana angewahitaji wajane na kuwa mume kwa kanisa lote. Hili, bila shaka, ni kinyume na kila kitu kingine kwenye Agano Jipya.

Suala la **Ufu 12:1-14:20** ni mateso ya kanisa kupitia Shetani na mfumo wa ulimwengu. Hata ingawa waamini wanaweza kuuawa (**13:7, 15**), **14:1** inaonyesha waamini waaminifu wakisimama pamoja na Mwanakondoo katika Mlima Sayuni. Kwa maneno mengine, kama vile Mwanakondoo alivyomshinda Shetani kupitia kifo chake, vivyo hivyo watu wake watakaofuata nyayo zake (**14:4**).[16]

"Neno 'mwanamwali' (au 'bikira') laweza kuzungumzia hali ya Kiroho, siyo tu kwa mahusiano ya kimwili" (Ladd 1972: 191). Manabii kwa kurudia rudia wamelinganisha sanamu na kutokuwa waaminifu kwa Mungu na uasherati (e.g., **Isa 57:3; Yer 2:7-3:10; Ezek 23:48-49**). Yesu alilinganisha kukataliwa kwake na uzinzi (**Math 12:38-39; 16:1-4; Marko 8:38**). **Yak 4:4** inapanua wazo la uzinzi wa Kiroho zaidi ya ibada maalum za sanamu au matendo, kwa kuwaita watu "wazinzi" wale wenye *"urafiki na dunia,"* au hata wale walio na *"matarajio ya kuwa rafiki na dunia."* Kwa upande mwingine, Wakristo wote wanaitwa kutumiwa na Kristo kama *"bikira safi"* (**2 Wakor 11:2**). Wazo hili limeletwa kwenye Ufunuo kwenye picha ya kanisa kama Bibiarusi au mke (**Ufu 19:7-9; 21:2, 9**).

Kwenye mazingira maalum ya 144,000, Yohana anazungumza juu ya ibada ya sanamu ya mnyama kama uasherati (**Uf 13:4, 6, 8, 11-18; 14:8; 17:2, 4: 18:3, 9; 19:2**). Tayari tumekwisha kuona jinsi ambavyo sura za 13-14 zilivyo kwa ukaribu sana kwenye istilahi ya ni wapi wale wanaomfuata mnyama watakapokuwa (*"watakaa juu ya uso wa nchi"*), ukilinganisha na wale ambao wannamfuata Mwanakondoo watakakokaa (*"watasimama juu ya Mlima Sayuni"*). Mwanakondoo na mnyama wenyewe pia wako kwa karibu sana kwenye **Ufunuo 13-14** ambao, tena, tumeonyesha tofauti baina ya hao wawili. Kwenye **14:1** tunamwona Mwanakondoo halisi, kwenye **13:11** tunamwona mwanakondoo wa uongo. Tofauti inaonyesha ukweli kwamba watu wote watamfuata ama mmoja au mwingine kati ya hao "wanakondoo" wawili. Hivyo, ni wazi kwamba wale 144,000 siyo "vijana wa Kikristo

[15] **2 Pet 2:1,** aya ya mwisho pale Kristo aliposema "kuwanunua" watu, inaonekana kuwa jambo ambalo Petro alitumia lugha ya ajabu, kwa kuwa alikuwa akizungumzia *"waalimu wa uongo miongoni mwenu . . . wakimkana hata Bwana aliyewanunua."* "Kwa maneno mengine, aliwaelezea waalimu wa uongo kama waaminio kwa sababu wanaikiri imani na kutoa kila mwonekano wa awali wa kuwa waaminio halisi" (Schreiner 2003: 331). Hata kifungu hiki kinathibitisha kwamba popoteKristo kweli alipowanunua watu, alilinunua Kanisa kwa ujumla, siyo daraja maalum la watu.

[16] Bauckham anaona kumbukumbu ya wanawali kama mali ya picha ya jeshi: "Wafuasi wa Kristo wanafananishwa kama jeshi la wanaume watu wazima ambao, hufuata mahitaji ya kale ya desturi za utakaso kwa wale ambao wanapigana vita vitakatifu (Kumbu. 23:914; 1 Sam. 21:5; 2 Sam. 11:9-13; 1QM 7:3-6), lazima aepuke unajisi wa kitamaduni unafanyika kupitia kujamiiana. Utakaso huu wa kitamaduni ni picha ya jeshi: ulinganifu wake halisi kwenye ubora wa Yohana kwa Kanisa siyo kujinidhamisha mwenyewe na kujiepusha na uasherati, lakini ni utakaso wa kimaadili." (Bauckham 1993b: 78; angalia pia Yarbro Collins 1998: 405-8; Johnson 2001: 202-3)

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

waliowekwa wakfu” au kikundi kingine chochote kanisani; 144,000 ni umbo la kanisa lote. Vivyo hivyo, wao ni “mabikira na wasiojinajisi kwenye ufahamu kwamba walikataa kujinajisi wenyewe kwa kushiriki kwenye uasherati wa kumwabudu mnyama lakini walijiweka safi wenyewe kwa ajili ya Mungu” (Ladd 1972: 191).

f. *“144,000” ni ishara, siyo halisil.* Wachambuzi wengi wanakubali kwamba idadi ya144,000 ni ishara. “Kwenye Ufunuo kikamilifu maelfu yanayozunguka pande zote yameonekana kuwa ni ishara.” (Gentry 1998: 56) “Idadi ya 144,000 imeelezewa kwa ubora zaidi kwa kuingiza ishara zake—12 x 12 x 10 x 10 x 10 inaelezea utimilifu uletao wokovu, hisia za agano—kuliko sense halisi ya mabaki ya Wayahudi” (Smith 1990: 116). Beale anahitimisha kwa kuelezea msingi wa mfano wa 144,000: “Mraba wa kumi nambilikwa kiasi kidogo unaweza kuwa idadi ya makabila ya Israeli kwa kuyazidisha yenewe au, zaidi kama, makabila kumi na mawili ukizidisha na Mitume kumi na wawili. Sura ya. 21 inathibitisha pendekezo hili, pale majina ya makabila kumi na mawili na Mitume kumi na wawili wanapounda sehemu ya muundo wa fumbo wa mbinguni mji wa Mungu. . . . Mji pia una kuta zenye urefu wa mia moja na arobaini na nne kwennda juu pamoja na mawe ya msingi kumi na mawili juu yake kumeandikwa majina ya Mitume kumi na wawili (cf. pia fumbo sawa na hilo la ‘kumi na mbili’limetumika mata mbili kwenye 22:2). Ikiwa waamini wa mataifa wametambuliwa kwa wazi pamoja na ‘makabila kumi na mawili ya wana wa Israeli’ kama sehemu ya Yerusalemu mpya (21:12, 14, 24; 22:2-5), basi siyo kitu kisichokuwa cha kawaida kwamba Yohana lazima aliwazungumzia wao pamoja na Wakristo Wayahudi kwenye 7:4 kama ‘makabila kumi na mawili ya wana wa Israeli.’ Hili linapokea uthibitisho kutoka uchunguzi wa awali kwamba ‘kutiwa muhuri’ ya 7:2-3 ni sawa na waamini kupokea ‘jina.’ Na ni wazi kwamba moja ya majina yaliyoandikwa kwenye vipaji vya nyuso za Wakristo wa mataifa, kwenye nyongeza ya majina ya Mungu na Kristo, ni ‘jina la Yerusalemu mpya’ (3:12), ambayo ni kumbukumbu muhimu kwa Wakristo wote kama Israeli ‘mpya’.” (Beale 1999: 417)

7. “Makutano makuu” (**Ufu 7:9-17; 19:1, 6**). Suala la msingi kuhusiana na “makutano makuu” ni ama ni kundi tofauti na lile la 144,000, au ni sawa na lile la 144,000 linaloonekana kwa mtazamo tofauti. Wale wanaofikiri kwamba 144,000 ni Waisraeli walioamini hushikilia kwamba“makutano makuu” ni watu wa mataifa waliookoka kupitia Wayahudi Wakristo 144,000 kipindi cha “dhiki kuu” (Pate 1998b: 165), au ni wale waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu kutoka kwenye makabila au tamaduni zote (Payne 1980: 610-11; angalia pia Johnson 1981: 484). Msingi wa imani hizo hujumuisha ukweli kwamba wale 144,000 wapo juu ya uso wa nchi, ni waliohesabiwa maalum, na kuchukuliwa kutoka “makabila kumi na mawili ya Israeli,” wakati ambao “makutano makuu” wapo mbinguni, hawawezi kuhesabiwa, na kuja*“kutoka kila taifa na makabila yote na jamaa na lugha”* (**7:9**) (Pate 1998b: 165-66; angalia pia Resseguie 2009: 137; Smalley 2005: 185). Hata hivyo, asili ya ishara ya idadi ya144,000, na maelezo ya kitheolojia ya kanisa kama Israeli ya kweli, yanaashiria kwamba“kile baadhi wanachokiona kama tofauti [baina ya makundi yaliyozungumziwa kwenye **7:4-8** na **7:9-17**] kwa uhakika yaweza kukusudiwa kuongezewa kila kimoja na kuonyesha mwendelezo wa kundi la kwanza pamoja na la pili” (Johnson 1981: 484). Ukweli kwamba “makutano makuu,” kama yale ya 144,000, yanawakilisha kanisa lote yanaonekana kwenye njia zifuatazo:

a. *Uhusiano baina ya 144,000 na “makutano makuu” yanaenda sambamba na uhusiano wa Simba na Mwanakondoo kwenye **Ufu 5:5-6**.* Kuna mfanano muhimu baina ya maelezo ya kanisa kwenye sura ya 7 na maelezo ya Kristo kwenye sura ya 5. Kwenye kesi zote mbili Yohana anatumia mfano wa “kusikia-kuona”, na kwenye kesi zote mbili zile ambazo amezitambulisha, amezitambua kwa ishara mbili tofauti. Hili halikutokea kama ajali. Hivyo, kwenye **Ufu 5:5** Yohana “alisikia” mmoja wa wazee akimzungumzia Kristo kama *“Simba ambaye anatoka kabila la Yuda.”* Hata hivyo, kwenye **5:6** Yohana “aliona,” siyo Simba, lakini *“Mwanakondoo asimamaye, kama kwamba amechinjwa.”* Mwanakondoo ni Simba, siyo mtu au kitu kingine. Yohana anashirikisha kwamba mbinu ileile ye utambulisho kwenye sura ya 7 kwa kulitambulisha kanisa kwanza na kile “alichosikia” (144,000) na kisha kwa kile “alichokiona” (makutano makuu): “Picha zote mbili zinaonyesha uhalisia ule ule. Ni sambamba na picha mbili zinazomtofautisha Kristo kwenye 5:5-6.” (Bauckham 1993b: 76)

Aina hizi mbili za utambulisho zina umuhimu wa kitheolojia kwenye hizi zinafunua vipengele tofauti vya kanisa, kama vile “Simba” na “Mwanakondoo” zinafunua vipengele tofauti vya utu na kazi ya Kristo: “Yohana aliona matukio hayo ya kufanana kutoka kwenye

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

upeo wa mitazamo miwili tofauti. Upeo mmoja wa mtazamo—alisikia nini [**7:4**]—ni uhakika au uyakinifu wa ndani au mtazamo wa kitheolojia. Upeo mwingine wa mtazamo—aliona nini [**7:9**]—ni uhakika au uyakinifu wa nje. Kwa namna nyingine, Yohana alisikia ishara ya idadi ambayo inawakilisha hesabu kamili ya wale ambao ni mali ya Mungu [i.e., Israeli ya kweli ya Mungu]. . . . Kwa namna nyingine, Yohana aliona makutano makuu kutoka kila kabila na taifa na lugha na jamaa (7:9). . . . Huu ni uhakika wa nje: Israeli ya Mungu imejumuisha wale wote waliomfuata Mwanakondoo, wote Wayahudi na watu wa Mataifa." (Resseguie 2009: 137-38) Ulfgard anaongeza, "Wakati 7:4-8 (kwenye ukaguzi na kutoka kwenye mtazamo wa kidunia) unatupa ishara ya namba 144,000 kwa wale ambao wataokolewa kupitia ishara ya ulinzi wa Mungu, 7:9–17 (kwenye mtazamo wa mbinguni) unaonekana ulinzi wao na kufarijiwa katika Mungu" (Ulfgard 1989: 105).

Sawa sawa na mfano wa "kusikia-kuona" (au "kuona-kusikia") kuelezea kitu kilekile unapatikana kwenye kitabu chote cha Ufunuo. Hivyo, kwenye **Ufu 9:13-16** Yohana alimsikia malaika akipiga tarumbeta ya sita na kwamba hili linafaa nini; kwenye **9:17-21** aliona kwenye maono kile kilichotokea kama sehemu ya ukweli uleule aliokuwa ameusikia muda mfupi. Kwenye **Ufu 14:1** Yohana alimwona Mwanakondoo na 144,000 juu ya Mlima Sayuni; kasha alisikia ukweli uleule ulioelezwa kwenye **14:2-5**. Kwenye **Ufu 15:2** aliwaona washindi wamesimama juu ya bahari ya kioo; kwenye **15:3-4** alisikia kile kilichoimbwa na kundi lile lile. Kwenye **Ufu 17:1-6** Yohana alimwona "kahaba mkuu"; kwenye **17:7-18** alisikia malaika akielezea utambulisho na maelezo ya ukweli ule ule aliokuwa ameuona.

b. *Kama vile 144,000 hutambulisha kanisa la kweli, Israeli ya Kiroho, vivyo hivyo msemo "makutano makuu ambayo hakuna mtu awezaye kuwahesabu."* Msemo *"makutano makuu ambayo hakuna awezaye kuwahesabu"* (**Ufu 7:9**) unaibua ahadi kwenye Agano la Ibrahimu kwamba Mungu angekuinulia*"hakika nitauzidisha uzao wako* [lit. 'mbegu'] *wala hautahesabika"* (**Mwanzo 16:10;** angalia pia **Mwanzo 13:16; 15:5; 22:17; 26:4; 32:12**). Agano Jipya kwa kurudia limeeleza kwamba Agano la Ibrahimu, na hasa ahadi ya kuizidisha mbegu au uzao wa Ibrahimu, imetimizwa kwa Kristo na kanisai (**Yohana 8:31-58; Rum 4:11-18; 9:6-8; Wagalatia 3-4**). "Kwa hiyo, makutano kwenye Ufu. 7:9 ni ukamilifu timilifu wa ahadi ya Ibrahimuna kuonekana kuwa njia nyingine kwa mara nyingine ambayo kwayo Yohana aliwataja Wakristo kama Israeli" (Beale 1999: 427).

c. *Matumizi ya "makutano makuu" penginepo kwenye Ufunuo.* **Ufu 19:1** na **6** ni wakati mwingine pekee ambao msemo *"makutano makuu"* ulitumika kwenye kitabu. Kwenye kesi zote mbili ni wazi kwamba zinazungumzia kanisa lote, siyo tu sehemu yake. Kwenye maeneo yote matatu kwenye kitabu wakati *"makutano makuu"* yanapopatikana, msemo ule ule wa kigiriki (*ochlos polus*) limetumika.

8. <u>"Hekalu" na "mji mtakatifu" (**Ufu 11:1-2**).</u> Ipo mitazamo tofauti juu ya maana ya hekalu na mji mtakatifu, ambazo (kama zilivyo nying ya picha za Yohana) huangukia kwenye makundi mawili makuu: mitazamo ya "uhalisia" na "fumbo au ishara".

a. *Hekalu na mji mtakatifu kama uhalisia.* Utangulizi hutazama hekalu kama uhalisia, hekalu la kihistoria lililokuwa Yerusalemu ambalo liliharibiwa mwaka BK70 (Gentry 1998: 65-67; Bahnsen 2015: 18). Kumbukumbu kwenye **11:2** kwa behewa iliyo nje ya hekalu*"mataifa wamepewa; naowataukanyaga mji mtakatifu miezi arobaini na miwili"* inaonekana kama kuwa imechukuliwa kutoka kwenye utabiri wa Kristo kwenye **Luka 21:24** kuhusiana na kuhusuriwa na kuangushwa kwa Yerusalemu na Warumi (Payne 1980: 616; Bahnsen 2015: 18-19). Kwa namna nyingine, Mitazamo ya Mpito na baadhi ya wengine wa wakati ujao huendeleza **Ufunuo 11** kwenye wakati mara kabla ya *parousia.* Vyote hakalu na madhabahu vilichukuliwa kama kuzungumzia uhalisia, kujengwa tena kwa hekalu kwenye "mji mtakatifu" halisi wa Yerusalemu."Wale wanaoabudu ndani yake" wanaonekana kama waamini wa kabila la Kiyahudi. (Thomas 1998:198; MacDonald 1995: 2367; Smith 1980b: 99-100; angalia pia Ladd 1972: 149-51)

Nafasi zote "halisi" zina uhusika mdogo kwa *kusudi* la kitabu (ambalo ni wazi na moja kwa moja kwa kanisa kwa muda wote, kutoka karne ya kwanza hadi *parousia*); *muundo* wa kitabu (ambao hatua kwa hatua vifungu sambamba hurudia changamoto zinazolikabili kanisa kwa kipindi chote cha historia, kutoka karne ya kwanza hadi *parousia*); au asili ya *ishara* kwenye kitabu (kwenye mwanga ambao "maelezo ya mbinu maaarufu ya Ufunuo—hutafsiri

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kiuhalisia isipokuwa umelazimishwa kuitafsiri ki-ishara—italazimika kugeuka kwenye kichwa chake" [Beale 2006: 55]). G. B. Caird labda analeta wazo lenye kukabiliana na lenye umaizi (angalau kwa "uhalisia" wa mawazo ya Kimagharibi) kwamba, wakati tunapochukulia aina ya mafunuo wa kitabu cha Ufunuo kwa makini, "Ni vigumu sana kusema kwamba, kwenye kitabu ambacho vitu vyote vimeelezwa kwenye ishara, mambo ya mwisho kabisa hekalu na mji mtakatifu ungemaanisha kuwa hekalu la kimwili na Yerusalemu ya kidunia. Kama Yohana angetaka kuyazungumzia hayo, angepata baadhi ya picha kuielezea maana yake bila kupotea kwenye uhalisia usiothabiti" (Caird 1966: 131)

b. *Hekalu kama fumbo.* Msemo halisi *"hekalu la Mungu"* unapatikana mara kumi na moja kwenye Agano Jipya nje ya 2 Wathesalonike (**Math 26:61; 1 Wakor 3:16, 17a, 17b; 2 Wakor 6:16a, 16b; 2 Wathes 2:4; Ufu 3:12; 7:15; 11:1, 19**). Wakati mwingine wowote msemo huu ulitumika kuelezea kanisa.[17] Hivyo, "hekalu" n bora kueleweka kama fumbo au ishara ya kanisa. Kwa nyongeza, yapo mazingira mazuri na sababu za kitheolojia ndani ya Ufunuo wenyewe kwanini "hekalu" la **Ufu 11:1-2** haliwezi kuwa hekalu halisi la jengo, lakini ni ishara ya kanisa. Kwanza, neno la Kigiriki kwa "hekalu" hapa ni *naos*. *Naos* kamwe haitaji kitu halisi, hekalu la kidunia wakati mwingine wowote linapotumika kwenye Ufunuo. Kwenye Ufunuo, *naos* haizungumzii ama hekalu la Mungu lililopo mbinguni (**Ufu 7:15; 11:19; 14:15, 17; 15:5-6, 8; 16;1, 17**) au Yerusalemu mpya ijayo ambayo Mungu na Mwanakondoo ndio Hekalu (**Ufu 3:12; 21:22**). Kwenye **Ufu 3:12** ahadi kwa watakatifu walioshinda ni kwamba mwatafanywa *"nguzo kwenye hekalu la Mungu Wangu."* Kwa kuwa washindi wameahidiwa kufanywa sehemu ya hekalu la Mungu, siyo jambo la kushangaza kwamba utambulisho wao kama hekalu umethibitishwa kwenye **Ufu 11:1-2** hata wakati wakiwa juu ya nchi.[18]

Pili, asili ya lugha ya ishara ya **Ufu 11:1-2** na utambulisho wa "hekalu" pamoja na kanisa vimeimarishwa kwa ukweli kwamba Yohana aliambiwa "apime" siyo tu hekalu na madhabahu lakini pia *"wale waabuduo ndani yake."* "Kulipima" hekalu kunakuja kutoka **Ezek 40:2-5; Zek 2:1-5**. Kupitia Biblia yote, "kipimo" siyo kitendo tu cha kimwili cha kuamua ukubwa wa kitu Fulani lakini kuna umuhimu wa kitheolojia. "Kupima kunaeleza wazo la kuhifadhi, siyo la kuangamiza. . . . Kwa hiyo wakati Mungu anapima, Hupima, siyo kwa ghadhabu, lakini kitu kinachopimwa chaweza kuwa kwenye kina zaidi ya ufahamu wa kawaida wa makaazi ya Utukufu Wake." (Milligan 1896: 169)[19] Mungu hafurahii kuyahifadhi majengo ya kimwili, kwakuwa Yeye *"hakai kwenye nyumba iliyofanywa kwa mikono ya mwanadamu"* (**Mdo 7:48**). Badala yake, hupendezwa na kuwahifadhi watu Wake, kanisa, ambao ni hekalu Lake (angalia **1 Wakor 3:9, 16-17; 2 Wakor 6:16-7:1; Efe 2:21; 1 Pet 2:5; Ufu 3:12**; angalia pia **Ufu 13:6**).

Tatu, **Ufu 13:6** ni thabiti pamoja na utambulisho wa hekalu kama kanisa kwa kutueleza sisi kwamba mnyama kumtukana *"Jina la Mungu na Hekalu lake, hawa ni,wale wakaao mbinguni."* Hivyo, kwenye **13:6** "hekalu" na "wale wakaao mbinguni" ni sawa, kama vile "hekalu" na watu wa Mungu ni sawa kwenye **11:1**.[20] Utambulisho huu unathibitishwa na ukweli kwamba vyote "miezi arobaini na miwili" na "siku 1260" za **Ufu**

---

[17] Kwenye **Mat 26:61** rejeo la Yesu bila shaka lilikuwa hekalu la mwili wake mwenyewe (angalia **Yoh 2:19-21**) (Nixon 1970:848). Ikiwa kumbukumbu ilikuwa kwa jingo lililojengwa na lililopo, lilikuwa tu kama "aina" ya mwili au kivuli cha Kristo na watu wake kama hekalu la kweli (Beale 2004: 275-76).

[18] Sambamba na hilo Waaminio, wakati bado wapo duniani, hata hivyo wanasemekana kuwa "waliinuliwa" na "kuketishwa" pamoja na Kristo kwenye "ulimwengu wa Roho" (**Efe 2:6**). Zaidi ya hayo, Kristo, akiwa mbinguni, hivyo hujitambulisha na watu wake juu ya nchi kwamba alisema kwa Sauli wa Taso, Sauli, Sauli, kwanini unaniudhi *Mimi*?" (**Mdo 9:4**).

[19] "Kupima kama kuhifadhi" ni sababu nyingine kwanini ama jingo la hekalu la karne ya kwanza au jengo la hekalu linalopendekezwa haliwezi kuwa kwenye mtazamo hapa. Sababu ni kwamba kwenye hotuba ya Mlimani Kristo alitabiri "chukizo la uharibifu" kujitokeza au uonekana ndani, na kuangamizwa kwa hekalu, na siyo kuhifadhiwa kwake na kuwa kwake makazi ya utukufu wa Mungu kama jambo lilivyo hapa (angalia Reader 1982: 410).Jengo la Hekalu la wakati ujao haliwezi kuwa kwenye mtazamo hapa kwa sababu ya nyongeza kwamba itakuwa ni kurudi kwenye "kivuli" cha mfumo wa Agano la Kale, ambao alikwisha kuutimiza milele, kuuondoa au kuufuta, na kuusimamisha (angalia **Waeb 4:145:10; 7:1-10:22**).

[20] Johnson anakumbusha kwamba matumizi ya Biblia toleo la NASB ya maneno "hawa ni wale" baina ya "wale ambao wanakaa mbinguni" na "Hema Lake" mawili yanafanana na "kwa usahihi huakisi maana ya sarufi ya Kigiriki" (Johnson 2001: 166n.12).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

11:1-2, wakati inapoonekana kwenye mazingira yake yote ya Ufunuo, ni, kwa mtiririko huo, kumbukumbu ya mateso ya, na ulinzi wa Mungu kwa, kanisa.

c. *Mji mtakatifu kama fumbo.* Yerusalemu iliitwa "mji mtakatifu" kwenye Agano la Kale na kipindi chote cha huduma ya Yesu juu ya nchi (e.g., **Neh 11:1, 18; Isa 48:2; Math 4:5; 27:53**). Hata hivyo, baada ya Yesu kufufuka na kupaa Yerusalemu haiitwi tena "mji mtakatifu." Kwenye Ufunuo, "mji mtakatifu" ulilitumiwa tu mara nne: hapa, na kwenye **21:2, 10; 22:19** ambapo inazungumzia Yerusalemu mpya, ambao ni sawa na waliokombolewa, bibiarusi wa Kristo, kanisa. Mazingira haya mengi shirikishi na rejea ya msalaba huondoa makosa ya "uhalisia" wakati unapotafsiri kitabu cha mafunuo kama Ufunuo wa Yohana na kuthibitisha maana ya ishara Yohana alizozitumia. Kistemaker anahitimisha, "Nji mtakatifu ni Yerusalemu ya Kiroho ya Watakatifu" (Kistemaker 2000: 437).

d. *Behewa ya nje. "Behewa ya nje"* imefungwa kwenye *"mji mtakatifu"* kwenye **11:2**. Hivyo, kile kinachosemwa kuhusu*"mji mtakatifu"* pia inatumika kwa*"behewa ya nje."* Wengi huona *"behewa au ua ambao upon je ya hekalu"* kama kumbukumbu kwa wale ambao kwa nje ni mali ya kanisalakini siyo waamini wa kweli (Hendriksen 1982: 127; Milligan 1896: 174-75; Reader 1982: 411). Hata hivyo, "kwa kile kilichofuata kwenye sura ya11 hakujatajwa waasi au washiriki, tofauti pekee ya mashahidi wa kweli pamoja na wale ambao huwatesha" (Beale 1999: 560). Kwa hiyo, "behewa ya nje" bila shaka hutofautisha "ukweli wa ndani, uliojificha wa kanisa kama ufalme wa makuhani (cf. 5:10) ambao wanamwabudu Mungu kwenye uwepo wake kutoka kwenye uzoefu wan je wa kanisa kama ulivyowekwa wazi kwa mateso kwa ufalme wa mataifa" (angalia Resseguie 2009:161; Bauckham 1993a: 272). Kwa hiyo, "behewa ya nje" bila shaka unapendekeza uzoefu wan je wa mateso ambayo kanisa linakabiliana nayo, kama unavyopingana na ule wa ndani, usalama wa Kiroho wa kanisa ambao ulikuwa "ukipimwa" na kulindwa na Mungu. Tena, picha hii ni njia nyingine ya kuuona ukweli uleule, kanisa, kutoka kwenye upeo wa mtazamo tofauti (Resseguie 2009: 161).

Utambulisho wa "behewa ya nje" pamoja nay ale yanayoonekana kwa nje, hali ya kimwili ya kanisa na magumu linayopitia, kama kupingana na yaliyo ndani yake, Usalama wa Kiroho ndani ya Kristo, ni madhubuti au wa kuaminika pamoja na maelezo ya Yohana ya kanisa kwenye kitabu chote cha Ufunuo: kanisa linafuata kwenye nyayo za Kristo; litateseka na kufa kimwili kwa muda mfupi tu, lakini litashinda kiroho na milele: "Kama muhuri ambao uliwekwa kwenye vipaji vya nyuso za watumishi wa Mungu, kupimwa kwa hekalu kunaashiria ulinzi wa ndani kinyume na harati za kiroho. Lakini agizo la malaika ni kuuacha wazi bila kupima behewa ya nje, kwa sababu Mungu hatoi kwa kanisa ulinzi kutokana na mateso ya mwilini au kifo. Ni kusudi lake kwamba lazima wabaki wadhaifu kwa nje kwa uadui kamili wa maadui zao, wako salama tu kwenye imani yao kwa Bwana aliyesulubiwa na kufufuka. Kitu kimoja ambacho aliwahakikishia ni kwamba mashahidi wake watakuwa na wigo huru wa kutoa unabii; kwa kuwa kutoa unabii ni kufa kifo cha kuuawa kwa ajili yaneno la Mungu." (Caird 1966: 132)

Mtazamo huu pia unaunganishwa na picha ya Ufunuo ya kanisa kama "mjimtakatifu": Wakati wa "nyakati hizi" kanisa "linapimwa" (i.e., linajulikana na kulindwa na Mungu Kiroho), lakini "ua wake wa nje" haujapimwa, na hivyo ni na"mji mtakatifu" utakuwa *"ukikanyagwa chini ya miguu . . . kwa miezi arobaini na miwili"* (i.e., "nyakati zote hizi" kanisa, ingawa linalindwa kiroho, limetiishwa chini ya mateso ya kimwili hapa ulimwenguni). Pamoja na *parousia* na utimilifu wa "nyakati zijazo," hata hivyo, "mji mtakatifu" kwenye ujumla wake "umepimwa" (**Ufu 21:15-17**). Kwa maneno mengine, kwenye utimilifu, kanisa siyo tu linajulikana na kulindwa kiroho lakini sasa halijatiishwa tena chini ya mateso ya kimwili. Picha hizi mbili pia ni madhubuti pamoja na asili ya "tayari, lakini bado" ya ufalme. Picha za Ufunuo ni sambamba na mtazamo wote wa Agano Jipya wa kanisa. Kuchukulia picha hizo kama "hekalu," "mji mtakatifu," na"behewa ya nje" kama vyombo au vitu vya kimwili, au kama kutofautisha Wayahudi walioamini kutoka kwa wasioamini, kwa hakika kutaangamiza usambamba kwa kushangaza wa mahusiano shirikishi ya ishara za Ufunuo wenyewe sambamba na ushirikiano wa kitabu cha Ufunuo na Agano Jipya lote.

9. Mashahidi wawili (**Ufu 11:3-12**). Kama ishara nyingizo nyingi kwenye kitabu, "mashahidi wawili" wamekuwa somo kuu la tafsiri mbalimbali (angalia Strand 1981: 127n.3). Hata hivyo, yapo makundi mawili ya msingi ya utafsiri: (1) Mtazamo wa kiuhalisia "mashahidi wawili" kama mtu halisi, ama:

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kurejeshwa tena kwa Elia na Musa [ambao] ni wajumbe wa Mungu ambao wataiwakilisha jamii ya Wakristo Wayahudi mwishoni mwa historia" (Pate 1998b: 169); au "watu wawili wa kihistoria wa nyakati za mwisho ambao watatumwa Israeli kuhusiana na kuwaletea wokovu" (Ladd 1972: 154).
(2) Mtazamo ulio bora unawaona "mashahidi wawili" kama ishara kwa kanisa zima, hasa kwenye majukumu yake kama mashahidi waaminifu (Hendriksen 1982: 129; Payne 1980: 617; Beale 1999: 573; Johnson 2001: 171). Sababu za kuwatambulisha mashahidi wawili na kanisa ni kama zifuatazo:

a. *Ishara nyuma ya mashahidi wawili ni pana kuliko kuwa ni manabii tu Elia na Musa* **Ufu 11:6** kwa uhakika inamtaja Elia (angalia **1 Fal 17:1**) na Musa (angalia **Kut 7:14-12:32**). Hata hivyo, kumbukumbu kwa "miti miwili ya mizeituni na vinara viwili vya taa" (**11:4**) vimedhihirika wazi kwenye **Zekaria 4:1-14**. Kumbukumbu ya moto kupitia au ukitiririka kutoka kwenye kinywa chao na kula maadui zao" (**11:5**) kwa karibu msingi wake ni kwenye **Yer 5:14**. Kufufuka kwa mashahidi wawili (**11:11**)—"pumzi ya uhai ikatoka kwao" na "walisimama juu ya miguu yao"—limechukuliwa kutoka **Ezek 37:5, 10**. Ukweli kwamba ishara nyuma ya mashahidi wawili kwenye **Ufu 11:3-11** inapita Musa na Elia kuashiria kwamba mashahidi wawili wenyewe ni zaidi ya Musa na Elia (au watu binafsi kama Musa na Elia).

b. *Sifa za Musa na Elia zimetumiwa kwa pamoja.* Wakati jukumu la kanisa kama shahidi kwenye **11:3-12** limeonyeshwa juu ya Musa na Elia, "mashahidi wawili" "hawafanyi kama watu wawili binafsi, bali tu kama mtu mmoja—wakati wote kwenye umoja na kwenye muungano kamili" (Strand 1981: 130; angalia pia Beale 1999: 575 ["Kwamba manabii hawa wawili siyo watu wawili waliokuja kutoka kuangalia zile nguvu za wote Musa na Elia zimehusishwa sawa kwa mashahidi hao wawili, na hazijagawanywa miongoni mwao"]). Kwa mfano, **11:5** inasema "moto ulipita kutoka kinywani mwao." Maelezo hayawezi kuwa "halisi" na pekee kutosheleza kuashiria kwamba hawa siyo wanadamu binafsi. Zaidi ya hayo, neno "kinywa" ni umoja. Sawa sawa na, **11:8** inasema "mwili wao mfu," siyo "miili." Ingawa tafsiri nyingi zinasema "miili," Kigiriki ni umoja. Hivyo, "mashahidi wawili" wanatendewa kama chombo kimoja siyo watu binafsi.

c. *"Mashahidi wawili" mada iliyopo kwenye kitabu chote cha Ufunuo.* "Kitabu cha Ufunuo kimeweka msisitizo wa jumla juu ya'mashahidi wawili'hili linaanzisha umoja kwenye shughuli za Kiungu—yaani, 'neno la Mungu' na 'ushuhuda wa Yesu Kristo'" (Strand 1981: 134; angalia **Ufu 1:2, 9; 6:9; 20:4;** cf. **12:17; 14:12**). Kwa hiyo, kama Andrew Steinmann alivyohitimisha, "Utambulisho huu wa karibu wa mashahidi pacha pamoja na watakatifu yanaonyesha kwamba mashahidi wawili kwenye eneo la tatu la tarumbeta ya sita wapaswa kueleweka kama kusanyiko la watakatifu, Kanisa" (Steinmann 1992: 75).

d. *Mashahidi wawili ni "miti miwili ya mizeituni na vinara viwili vya taa" (**Ufu 11:4**).* Kwenye **Zek 4:12-14**, mahali ambapo picha hii ilichukuliwa, miti miwili ya mizeituni ilitambulisha kama *"ni hao wana wawili wa mafuta,wasimamao karibu na Bwana wa dunia yote"* Kwenye Zekaria, "hawa wapakwa mafuta wawili walikuwa ni Yoshua na Zerubabeli, ambao walihudumu kama Kuhani mkuu na maliwali kwenye uzao wa kifalme. Baadaye, ofisi hizi mbili zitaunganishwa kwa Masihi ambaye ni Kuhani na Mfalme ([Zek 6:13; Zab 110:4; Waeb 7)." (Yilpet 2006: 1081)

Picha hii ilipelekwa mbele kwenye Ufunuo. **Ufu 1:6; 5:10; 20:4, 6** inalitambulisha kanisa kama Ufalme wa kikuhani ambao utatawala pamoja na Kristo (angalia pia **1 Pet 2:9**). "Kinara cha taa" awali kilitambulishwa kama kuwa makanisa saba (**1:12, 20; 2:1**). Kwa kuwa vinara saba vya taa ni makanisa, hivyo ni vinara viwili vya taa. Pamoja na heshima ya tofauti baina ya "saba" na "mbili," Bauckham anaunganisha matumizi ya Yohana ya picha hizi: "Ikiwa vinara saba vya taa ni viwakilishi vya kanisa lote, kwa kuwa saba ni namba ya utimilifu, vinara viwili vya taa husimama kwa kanisa kwenye jukumu lake la kuwa mashahidi, kulingana na mahitaji ya kibiblia yanayoeleweka sana kwamba ushahidi hukubaliwa tu kwa ushuhuda wa mashahidi wawili (Hes 35:30; Kumb 17:6; 19:15; cf. Math 18:16; Yohana 5:31; 8:17; 15:26-27; Mdo 5:32; 2 Wakor 13:1; Waeb 10:28; 1 Tim 5:19). Siyo sehemu ya Kanisa, lakini zaidi sana kanisa lote kama linavyotimiza jukumu lake kama mashahidi waaminifu." (Bauckham 1993a: 274)

e. *Mashahidi kutoa unabii kwa miaka 3½ (**Ufu 11:3**).* Kama tulivyozungumzia hili awali, kwa kawaida unabii umeunganishwa kwa mfumo wa mazingira shirikishi, mada na neno la msingi.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Yohana alitumia mkakati uo huo kwenye kitabu chote cha Ufunuo. Mashahidi wawili walitoa unabii kwa miaka mitatu na nusu (**11:3**), sawa na urefu wa wakati uleule"mji mtakatifu" ulipokanyagwa (**11:2**), "mwanamke" kuwa jangwani (**12:6, 14**), na "wenye maskani yao mbinguni" walitukanwa na kushambuliwa (**13:6**). Maandiko hayo yote ni ishara ya kanisa lote. Hili limeonyeshwa kwa kumbukumbu ya muda wa miaka mitatu-na-nusu. "Msingi wa miaka mitatu na nusu upo kwenye Dan. 7:25; 12:7, 11 (na labda Dan. 9:27), ambao hutoa unabii wa muda wa dhiki kwa Israeli *kama jumuiya.*" (Beale 1999: 574) **Ufu 11:3** ni thabiti au madhubuti pamoja na mfano huu. Ni picha nyingine ambayo huleta kivuli au kipengele cha Kanisa kama Israeli ya kweli. Zaidi ya hayo, kwa kuwa miaka mitatu na nusu siyo uhalisia wa kipindi cha muda wa miaka mitatu na nusu, bali ni ishara ya uwakilishi wa muda au wakati kutoka kwenye kifo cha Kristo na kufufuka kwake mpaka *parousia* (Kistemaker 2000: 438; Johnson 2001: 189; Beale na McDonough 2007: 1119; Resseguie 2009: 30-31), "mashahidi wawili" haiwezekani kuwa watu binafsi.

f. *Mnyama "atafanya vita pamoja nao" (**Ufu 11:7-10**).* Mtu hawezi *"kufanya vita"* kinyume na mtu binafsi. Mnyama "kufanya vita" kinyume cha mashahidi wawili na "kuwashinda" wao msingi wake ni kwenye **Dan 7:21**, pale pembe ya mnyama wa nne wa Danieli "alipofanya vita" kinyume na watakatifu na "kuwashinda" wao. Kwenye mazingira ya Danieli, vita havikuwa kinyume na mtu mmoja lakini kinyume na watu wote wa Mungu (**Dan 7:18, 22-27**).

Ufu 11:8 pia inatueleza kwamba, baada ya kuuawa kwao, miili yao italazwa kwenye "mji mkuu." Kumbukumbu nyingine yeyote kwa "mji mkuu" kwenye Ufunuo ni kwa "kahaba, Babeli mkuu" (**Ufu 16:19; 17:18; 18:10, 16, 18, 19, 21**). Kama ilivyooneshwa kwenye **11:8-9**, "mji mkuu unawajumuisha wale wote wakaao juu ya uso wa nchi, ambao hutoa utii wao kwa mnyama" (Johnson 2001: 173). Hivyo, "Babeli mkuu" siyo tu mji mmoja lakini ni dunia yote, uchumi wa kijamii, tamaduni za kidini au taasisi ambazo zinapingana na Mungu na Kristo. Vivyo hivyo, "mashahidi wawili" pia ni umbo au fumbo jingine kwa dunia yote, uchumi wa kijamii, taasisi za kidini, Kanisa. Zaidi ya hayo, **Ufu 11:7, 9-10** ni mfanano wa wazi kwa **13:1-2, 7-8**:

11:7, 9-10: *"Yule mnyama atokaye katika kuzimu atafanya vita nao, naye atawashinda na kuwaua . . . Na watu wa hao jamaa na kabila na lugha na taifa wataitazama miziga yao . . . Nao wakaao juu ya nchi watafurahi juu yao na kushangili"*	**13:1-2, 7-8**: *"Na akapewa* [i.e., y*ule mnyama atokaye baharini,* **13:1-2**] *kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na taifa. Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudia"*

"Mnyama" ataokaye katika kuzimu ni sawa kama "mnyama" atokaye baharini. *"Jamaa na makabila na lugha na mataifa"* ya wale ambao wanashangilia kwa kifo cha mashahidi wawili na wale ambao wanamsujudia mnyama wanafanana mmoja na mwingine au wote ni sawa; wao ni sehemu ya kanisa ambalo limekombolewa kutoka katika kila"*kabila na lugha na jamaa na taifa"* (**Ufu 5:9; 7:9**). Wale "wakaao juu ya nchi" wamewekwa kupingana na kanisa lote. Hitimisho haliwezi kuepukika: **Ufu 11:7, 9-10** ni maelezo mfanano sawa na yale yaliyowekwa kumbukumbu kwenye **Ufu 13:1-2, 7-8**.[21] Kwamba zaidi ya hayo yanalazimisha hitimisho kwamba"mashahidi wawili" wa **Ufu 11:3-12** ni picha ya Kanisa la kiulimwengu au Kanisa lote.

[21] Kipo kiunganishi kimoja kwenye mlingano huu. **Ufu 11:7-13** inaonekana kuhusiana na matukio ambayo yatatokea mwishoni mwa historia. Kama ilivyotajwa hapo juu kwenye sehemu "Kumbukumbu ya nyakati kwenye Ufunuo," miezi 42 (**Ufu 11:2**) na siku 1260 (**Ufu 11:3**) huzungumzia kipindi chote cha ushuhuda wa Kanisa ambacho kilianza pamoja na Ufufuo wa Kristo na kupaa kwake. **Ufu 11:7**, hata hivyo, inasimulia matukio "wakati watakapomaliza ushuhuda wao." "Siku tatu na nusu" (**11:9, 11**) zinatofautiana na siku 1260, na sehemu inaishia na *parousia* (angalia sehemu inayofuata kwenye mada kuu). Wakati **Ufu 13:7** yaweza vivyo hivyo kuwa na ombi maalum kwa kipindi mwishoni mwa historia, kanuni inayoelezwa kwenye sura hiyo inatumika kwa historia yote tangu kufufuka kwa Yesu na kupaa. Kama ilivyojadiliwa kwenye sura ya. X, "wanyama" wa **Ufunuo 13** wanawakilisha serikali zisizokuwa za Kikristo, jamii na tamaduni zile ambazo zilianza pamoja na Warumii ya Kale lakini zikidumu kwenye historia yote. Hili linaonekana kwenye **Ufu 13:5** ambayo inasema kwamba *"akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili [mnyama]."* **Ufu 13:7**, tofauti na **Ufu 11:7**, haitaji kwamba *"vita pamoja na watakatifu"* ilifanyika tu baada ya matukio fulani kuwa yamekamilika, na majadiliano ya shughuli za mnyama kwenye **Ufu 13** hayahitimishwi na maelezo ya *parousia*. Hivyo, kikanuni, mnyama *wakati wote* yupo vitani pamoja na watakatifu, ingawa vita hiyo itazidishwa mwishoni mwa historia.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

g. *Kufufuka kwa mashahidi wawili (**Ufu 11:11-13**).* Maelezo yamechukuliwa kutoka **Ezek 37:5, 10.** Kuna mitazamo miwili mikuu kuhusiana na kufufuka na kupaa kwa "mashahidi wawili": ni picha ya uhakikisho wa mwisho wa Kanisa; au ni maelezo ya uhakika wa ufufuo wa waamini wakati wa *parousia*. Beale anazungumzia mtazamo wa kwanza: "Kupaa kwa mashahidi kunathibitisha mwisho kwa siri au fumbo, maamuzi ya ukombozi na kuhakikishwa kwa watu wa Mungu mwishoni mwa nyakati. Uelewa huu wa fumbo unaimarishwa na unabii wa Ezekieli, ambaye anatumia lugha isiyo halisi ya ufufuo kuzungumzia kurudi kwa Israeli kutoka utumwani. . . . Yohana anatumia maneno ya Ezekieli kwa kanisa lililorejeshwa kwa sababu aliona hatimaye wafuasi wake wakifunguliwa kutoka safari yao ya duniani ya utumwa na mateso. Hili linadhihirisha kwamba wao ni watu halisi wa Mungu (cf. Ezek. 37:12-13)." (Beale 1999: 597)

Kwa namna nyingine, ufufuo waweza kuwa ufufuo halisi na unyakuo wa Kanisa wakati wa kurudi kwa Kristo. **Ezek 37:5, 10** ni sehemu ya unabii wa Ezekieli wa mifupa mikavu ambayo, kwenye maono, aliona ikihuishwa tena kwenye uhai. Kwa uhakika picha imechukua wazo la kufufuka, siyo tu kuhakikishwa. Ama **Ufu 11:12** inamaanisha uhakikisho au ufufuo halisi ni kwa muda mfupi, kwakuwa uhakikisho wa mwisho unahusisha kufufuka na *kinyume chake*.

Zaidi, kifungu hiki kinafanana na **Ufunuo 20**. *"Siku tatu na nusu"* (**Ufu 11:11**) za ushindi wa mnyama juu ya "mashahidi wawili" zinashabihiana pamoja na "muda mfupi" Shetani aliopewa *"kuyadanganya mataifa"* na kuleta upinzani duniani kote kinyume na watakatifu (**Ufu 20:3, 79**). Kwenye **Ufu 20:9-10**, Shetani na wafuasi wake wataangamizwa wakati wa *parousia*, wakati ambao ufufuo na hukumu utatokea (**Ufu 20:11-15**). Mfanano huu umeonyeshwa hapa kwa ukweli kwamba ufufuo utatokea *"kwenye muda huo au saa hiyo"* Kwenye hiyo pia *"kutakuwa na tetemeko kuu la nchi"* (**11:13**). "Saa" inaashiria kurudi kwa Kristo mara ya pili na hukumu ambayo itahusishwa (angalia **Ufu 3:3; 14:7, 15**). "Tetemeko la nchi" pia ni wazo linaloashiria *parousia* na hukumu ya Mungu kwa nchi (angalia majadiliano hapo juu kwenye kipengele **G. *Muundo: sambamba hatua kwa hatua; siyo kwa mpangilio madhubuti wa wakati***).

10. <u>"Mwanamke" na "watoto wake" (**Ufu 12:1-17**).</u> Kama ilivyotajwa mwanzoni kwenye sura hii, **Ufunuo 12** ni kifungu kiini kwenye kitabu. Kinairudia historia ya Kanisa na mgogoro wake na Shetani kikianzia angalau na kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo, kama siyoo kabla ya hapo. Picha ya mwanamke kwenye **12:1** ni kutoka **Mwanzo 37:9**. "Kiini cha sura ya mwanamke huyu wa mbinguni ni kwamba yeye ndiye Mama wa Masihi (mstari wa. 2). Baadhi ya wachambuzi hufikiri anamwakilisha Maria, mama wa Bwana Yesu; wengine Israeli, watu waliomzaa Masihi. Ni ukweli kwamba Isaya 66:7 inatupa picha ya Sayuni kama akiwa na utungu wa kumzaa mkombozi mpya wa Israeli (angalia Isa. 26:17; Mik. 4:10); lakini mama huyu wa mbinguni ni mama wa wote Masihi na wa kanisa kamili juu ya nchi ('uzao wake,' vs. 17). Kwa hiyo, ni rahisi zaidi kumwelewa mwanamke kwa uelewa mpana zaidi kama Sayuni *iliyo bora*, mwakilishi wa mbinguni wa watu wa Mungu (Isa. 54:1; 66:7-9)." (Ladd 1972: 167; angalia pia Beale 1999: 630; Carson 2011: 19-20)

Mwanamke *"anamzaa kijana mwanaume"* (**12:5**), ambaye kwa wazi ni Kristo. Yule joka (Shetani, **12:9**) *"akatoka kufanya vita pamoja na watotowake (Yule mwanamke) wote,"* ambao hasa wameelezwa kama wale *"ambao wanashika amri za Mungu na kuushikilia ushuhuda wa Yesu"* (**12:17**). Hili laweza tu kuwa Kanisa, kwa kuwa ni Wakristo tu wanaoyafikia maelezo hayo.[22]

11. <u>Mavuno (**Ufu 14:15-16**).</u> Kukusanywa kwa zabibu iliyoiva kwenye shinikizo la Mungu (**Ufu 14:17-20**) kwa wazi inazungumzia hukumu ya wasiomcha Mungu wakati wa mwisho wa nyakati.[23] Baadhi huona kuvunwa kwa mavuno (**Ufu 14:15-16**) kunawakilisha maelezo mengine ya hukumu ileile ya wasiomcha Mungu ili kusisitiza "ukali na asili mbovu ya adhabu" (Beale 1999: 774-75). Kwa namna nyingine, wengine (bila shaka mtazamo uliobora) hushikilia kwamba mavuno ya nafaka ni ukombozi wa wacha Mungu (Kanisa), kwenye utofauti kwa hukumu ya wasiomcha Mungu, kwa sababu zifuatazo:

[22] Huu ni mfano mwingine wa matumizi ya mafunuo ya ishara mbili tofauti kuelezea taasisi ile ile. Jamii ya Kimasihi, Israeli ya kweli, ubora wa Sayuni (i.e., kanisa lote la Agano la Kale na Agano Jipya) mwanzoni alielezwa kama mama, lakini kisha (angalau kanisa la Agano Jipya) limeelezwa kama "watoto" wake mwenyewe.

[23] Picha hii ya hukumu ya Mungu imechukuliwa kutoka **Isa 63:1-6; Maombolezo 1:15**; angalia pia **Ufu 19:15**.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

- Kama vile kumbukumbu ya mvinyo kwenye **Ufu 14:8, 10** ni kivuli cha "shinikizo" mfano wa **14:19-20**, hivyo "malimbuko" ya **14:4** ni kivuli cha mfano wa mavuno ya nafaka ya **14:15-16**.
- Mavuno ya nafaka yanachukua nafasi kwenye tendo moja tu: kuvuna (hakuna kukusanya au kupepeta kuliko semekana kuchukua nafasi); kwa hiyo, siyo sambamba na mavuno ya nafaka ambayo huchukua nafasi kwenye matendo mengi: kukusanya, kupepeta, na kushona.
- Kulingana na hitimisho la nyakati za mwisho, kuvuna kwenye Agano Jipya wakati wote ni picha chanya ya kuwaleta watu kwenye ufalme (**Marko 4:29; Yoh 4:35-38**), siyo ya hukumu juu ya wasiomcha Mungu (Bauckham 1993a: 290-96; Johnson 2001: 209-12).

12. Ushindi dhidi ya mnyama (**Ufu 15:2-4**). Eneo hili huonyesha ushindi, "kushinda" kwa Kanisa kulikotajwa na Kristo kwenye **Ufu 2:7, 11, 17, 26; 3:5, 12, 21**. Maandalizi ya eneo na picha yameunganishwa na eneo kwenye **Ufu 4:6** (*"bahari ya kioo"*) na **5:9** (wimbo wa kumsifu Mwanakondoo). Hili linaimarisha wazo la kanisa lililoshinda lililoonekana mbinguni.

"Kusimama" kwa watakatifu kunaashiria ufufuo. Kitenzi kwa"kusimama" kilichotumika hapa (*histēmi*) siyo sawa na kile kilichotumika kwa ufufuo.[24] Hata hivyo, kilitumika kwa Kristo*"kusimama mkono wa kuume wa Mungu"* kwenye **Mdo 7:55-56**, kwa Mwanakondoo kusimama kwenye **Ufu 5:6**, kwa makutano makuu kusimama mbele ya kiti cha enzi kwenye **Ufu 7:9**, na "kusimama" kwa mashahidi wawili kwenye **Ufu 11:11** baada ya kufa kwa siku tatu na nusu. Matumizi kama haya yote ya *histēmi* kwa hakika humaanisha ushindi na uhakikisho kama siyo ufufuo pia (au ushindi na uhakikisho *kama ulivyothibitishwa kwa* ufufuo).

Kanisa hili la kiulimwengu limekuwa likijulikanakwa na pia limeashiriwa kwa nyimbo zilizoimbwa. **Ufu 15:3** kwanza unatajwa "wimbo wa Musa," ambao unaturudisha nyuma kwenye wimbo wa ushindi ulioimbwa baada ya safari ya kutoka Misri (**Kut 15:1-21**). Kwenye **Ufunuo 15**, hata hivyo, ipo tofauti. Milligan anakumbusha kwamba wimbo ulioimbwa na washindi "siyo ule wa Musa tu, kiini kikuu cha Safari ya Agano la Kale; pia ni *wimbo wa Mwanakondoo,* kiini na jumla ya Agano Jipya. Mpito wote upo kwenye mawazo ya mwonaji, na kwenye idadi ya wale ambao wanaimba walijumuishwa watakatifu wote, wanachama au wafuasi wa Kanisa moja la kiulimwengu." (Milligan 1896: 261)

13. "Walioitwa na waliochaguliwa na waaminifu" (**Ufu 17:14**). Hapa Kanisa kwa wazi kabisa limetambuliwa, kwa kuwa watu wanaozungumziwa ni*"wale ambao wapo pamoja Naye [Mwanakondoo]."* Zaidi, wameelezewa kama*"walioitwa na waliochaguliwa [wateule]na waaminifu."* Penginepo popote kwenye Agano Jipya, baada ya kufufuka kwa Kristo, wakati maneno hayo yakiwaelezea watu, hutumika kuwaelezea Wakristo (Kanisa): "walioitwa" (**Rum 1:1, 6, 7; 8:28; 1 Wakor 1:1, 2, 24; Yuda 1**); "waliochaguliwa [wateule]" (**Math 20:16; 22:14; 24:22, 24, 31; Marko 13:20, 22, 27; Luka 18:7; Rum 8:33; 16:13; Wakol 3:12; 2 Tim 2:10; Tito 1:1; 1 Pet 1:1; 2:4, 9; 2 Yohana 1, 13**); "waaminifu" (**Math 24:45; 25:21, 23; Luka 12:42; Luka 16:10; 19:17; Yoh 20:27; Mdo 10:45; 16:1, 15; 1Wakor 4:2, 17; 7:25; 2 Wakor 6:15; Efe 1:1; 6:21; Kol 1:2, 7; 4:7, 9; 1 Tim 1:12; 3:1; 4:3, 10, 12; 5:16; 6:2; 2 Tim 2:2; Tito 1:6; 1 Pet 5:12; 3 Yohana 5; Ufu 2:10, 13**).

14. "Watu wangu" (**Ufu 18:4**). "Watu wangu" wanaweza tu kuwa wale walioungana pamoja nawaaminifu kwa Bwana (i.e., Kanisa). Yohana kuwasihi *"tokeni kwake, enyi watu wangu"* bado ni mfano wa kumbukumbu ya mazingira shirikishi. Maelezo yamechukuliwa kutoka **Isa 48:20; 52:11; Yer 50:8; 51:6, 9, 45**.[25] Kwenye vifungu vyote hivyo, yaliyomo yanahusu Babeli halisi. Hivyo hapa, kama maonyo kwenye zile barua za Makanisa saba (**Ufunuo 2-3**), aya hii "imeandikwa kwa wale wanaojiita Wakristo ambao wameshawishika kwa Shetani kupitia ujanja wa malkia kahaba kuuacha utiifu wao kwa Yesu" (Johnson 1981: 56667).

15. "Bibi arusi" (**Ufu 19:7-9; 21:2, 9; 22:17**). Kama alivyofanya kwenye kitabu chote, kwenye picha yake ya Bibi arusi Yohana alichukuwa picha ya Agano la Kale inayohusiana na kurejeshwa kwa Israeli

[24] Kwa upande mwingine, *ansitēmi,* ambalo limetoholewa kutoka *histēmi,* mara nyingi hutumika kwa ufufuo (angalia **Math 12:41-42; 17:9; 20:19; Marko 8:31; 9:9-10, 31; 10:34; 12:23, 25; 16:9; Luka 9:8, 19; 11:31-32; 16:31; 18:33; 24:7; Yoh 6:39, 40, 44, 54; 11:23, 24; 20:9; Mdo 2:24, 30, 32; 3:26; 13:33, 34; 17:3; 31; Warumi 14:9; 1 Wathes 4:14, 16**).

[25] Kwenye **2 Wakor 6:16-17** Paulo sawa na hilo alielezea **Isa 52:11** kwenye kuwahimiza waaminio kuwa wakamilifu. Kwenye kifungu hiki pia aliliita Kanisa *"hekalu la Mungu"* (cf. **Ufu 11:1, 19**). Kwa kuwa 2 Wakorintho iliandikwa takribani mwaka BK 56, upo uwezekano kwamba Yohana aliujua. Bila kujali hilo, Matumizi ya Yohana ya *"kutoka ndani yake huyo mwanamke"* huonyesha mazoea ya kawaida miongoni mwa mitume kutambulisha mada za Agano la Kale na misemo na kuitumia kwenye kanisa.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

(**Isa 49:18; 61:10; 62:5**), na kuitumia kwa Kanisa. Kwenye **Ufu 21:9** Yerusalemu mpya imeelezwa kwa mambo mawili *"Bibi arusi"* na *"Mke wa Mwanakondoo."* Yohana alifanya hivi kusisitiza asili ya mahusiano baina ya Kristo na watu wake. Picha inamaanisha upendo na urafiki wa karibu sana wa kimahusiano: "Mahitaji ya mwanamke kama bibi arusi yanakuja na wazo la umpya na shauku, na kumbukumbu ya Yerusalemu kama mke inamaanisha uvumilivu, uaminifu na kuzaa sana. Hivyo, kwenye kuuonyesha Yerusalemu mpya kama bibi arusi na mke, Yohana anatuambia juu ya uzuri wa mji, na urafiki wa karibu sana kimahusiano na kuzaa sana kwa uhusiano baina ya Mungu na waliokombolewa kwenye nyakati za mafunuo. Zaidi ya hayo, kuonekana kwa lugha inayofanana na hiyo kwenye [**19:7, 9; 20:9; 22:17**] kunaashiria kwamba uhusiano huo ulikwisha kuanza kwenye jamii ya kihistoria." (Deutsch 1987: 112-13)

a. *Bibi arusi wa Kristo anatofautiana na kahaba wa ulimwengu.* Maneno ya **Ufu 17:1** na **21:9** yanafanana. Bibi arusi amevalishwa *"kitani nzuri, ing'aayo safi; kwa maana kitani nzuri hiyo ni matendo ya haki ya watakatifu"* (**Ufu 19:8**). "Mama wa Kahaba" amevalishwa kama kahaba, *"amevalishwa nguo za rangi ya zambarau, na nyekundu,amepambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhanabu mkononi mwake, kilichijawa na machukizo, na machafu ya uasherati wake"* (**Ufu 17:4; 18:16**). Bibi arusi alitukuzwa (**Ufu 21:9-22:5**); kahaba aliangamizwa (**Ufu 17:1-19:6**).

b. *"Karamu ya arusi ya Mwanakondoo" inalinganishwa na "karamu kuu ya Mungu."* Wale wote walioalikwa kwenye *"karamu ya arusi ya Mwanakondoo wamebarikiwa"* (**Ufu 19:9**); kwenye *"karamu kuu ya Mungu"* wale wote waliompinga Kristo waliuawa na kuliwa (**Ufu 19:17-21**).

16. Majeshi (**Ufu 19:14**). Ipo mitazamo tofauti kuhusiana na utambulisho kwa "majeshi" ya **Ufu 19:14**. Mitazamo hiyo mikuu miwili ni ile inayowawakilisha Malaika au ile inayowawakilisha waamini waliokombolewa (i.e., Kanisa, labda kwenye kongamano na Malaika). Kwenye **Ufu 12:7** malaika wanafanya vita na joka na majeshi yake. Penginepo kwenye Agano Jipya, malaika wanasemekana kuambatana na Kristo kwenye *kurudi kwake mara ya pili* na kushiriki katika kutoa hukumu ya mwisho (angalia **Math 13:40-42; 16:27; 24:30-31; 25:31-32; Marko 8:38; Luka 9:26; 2 Wathes 1:7; Yuda 14-15**).

Mtazamo uliobora ni kwamba majeshi ya mbinguni **Ufu 19:14** yanajumuisha watakatifu, siyo tu malaika. Hili linaonekana kwa kulinganisha **Ufu 19:13-15** pamoja na kifungu muhimu kinachofanana cha **Ufu 17:14** ambacho "kinasaidia utambulisho wa majeshi kama watakatifu, siyo malaika, kwa sababu pale ni watakatifu ambao wanafuatana na Kristo, na pale pia Kristo anaitwa 'Bwana wa mabwana na Mfalme wa wafalme' (kama kwenye19:16). 'kitani cheupe, safi' kilichovaliwa na majeshi . . . kinafaa pia kwa malaika (15:6; Dan. 10:5; 12:6; Ezek. 9:2) au watakatifu (19:8). Lakini kwenye Ufunuo, pamoja na mmoja wa kipekee (15:6), ni watakatifu tu waliovaa vazi jeupe (3:4-5, 18; 4:4; 6:11; 7:9, 13-14). Watakatifu hapa na kwenye17:14 wanachukua sehemu kwenye hukumu ya mwisho tu kwamba ushuhuda wao ni ushahidi wa kisheria wa kuwahukumu watesi wao (kwa uelewa kama huu wa mashahidi wanaohukumu angalia Math. 12:41-42 pia.; Rum. 2:27)." (Beale 1999: 960)

Kumbukumbu ya nyongeza ya mazingira shirikishi ndani ya Ufunuo yanaashiria kwamba majeshi ya **19:14**, kwa kiasi kidogo, yanajumuisha Kanisa: "Vazi lililochovywa kwenye damu (Ufu. 19.13) linatukumbusha 7.14, ambapo mavazi la watakatifu waliohudhuria parousia ya Kristo yalielezewa kama yalioshwa na kufanywa meupe kwa damu ya Mwanakondoo . . . Upanga mkali (Ufu. 19.15) unahusishwa na onyo kwa Kanisa la Pergamo kwenye 2.16. . . . Kumbbukumbu ya Kristo kuyatawala mataifa kwa fimbo ya chuma (Ufu. 19.15) kwa karibu linaashiria maneno ya 2.26-27, kwenye hayo Kristo aliliahidi Kanisa la Thiatira kwamba washindi watashiriki pamoja naye kwenye jukumu lake kama kiongozi na hakimu kwenye parousia." (Mealy 1992: 221-22)

17. Wale waketio juu ya viti vya enzi (**Ufu 20:4-6**). Karibia wachambuzi wote wanakubali kwamba Kanisa (au wawakilishi wake, waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu) ndio wanaoelezwa kwenye kifungu hiki. Mfanano baina ya eneo hili na maeneo kwenye **Ufu 6:9** na **7:14-17** yanaashiria kwamba hivi ni viti vya enzi vya mbinguni, siyo vya duniani.[26] Kwamba eneo ni mbinguni, siyo juu ya nchi, pia

[26] Kwa upande mwingine, J. Marcellus Kik anaeleza, "Kiti cha Enzi ni umbo la msemo likiashiria utawala wa watakatifu. . . . Kiti cha enzi kinasimama kwa utawala wa kiroho wa watakatifu ndani yake mwenyewe na juu ya ulimwengu. Ingawa kwa neema ya Kristo wanatawala kwenye uzima dhidi ya mwili, ulimwengu, na mwovu. . . . Anatawala juu ya dhambi kwa sababu dhambi haina utawala juu yake. Anatawala juu ya Shetani ambaye hawezi kumgusa yeye. Anatawala

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

linaonekana kutokana na ukweli kwamba “nukuu zote arobaini na saba za Yohana kwa ‘kiti cha enzi’ au ‘viti vya enzi’ kwenye Ufunuo vimeweka enzi mbinguni, isipokuwa kiti cha enzi cha Shetani (2:13) na kile cha mnyama (13:2; 16:10)” (Ngundu 2006: 1675). Hata viti vya enzi vya Shetani na mnyama “siyo vya kidunia bali vimewekwa kwenye kipimo cha Kiroho” (Beale 1999: 999).

Tafsiri ya lugha ya Kigiriki kwenye kifungu hiki siyo ya kawaida. Kwa hiyo ni vigumu kusema ama kundi moja la watu limeelezewa kwa njia tofauti, au zaidi ya kundi moja limeelezwa: “Kifungu ni tata kwenye suala la ushiriki kwenye utawala huu wa Kimasihi. Ikiwa neno *hoitines* [‘wale’] litahifadhi hisia au akili zake za jadi, litamaanisha mzunguko mpana zaidi ya wale waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu waliotajwa kwenye kifungu cha *tōn pepelekismenōn* [‘wale ambao waliuawa’]. Hivyo ushiriki utaonekana kuwa wazi Wakristo wote waaminifu. Lakini neno *hoitines* kwenye Kigiriki cha Agano Jipya mara nyingi sana hufanya kama vile jamaa au ndugu wa kawaida, hivyo kifungu cha *hoitines* chaweza kuwa sifa nyingine ya ‘nafsi za wale waliouawa.’ Hivyo ushiriki utakuwa na kikomo kwa wale tu waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu. . . . Ingawa haliko wazi ama miaka elfu ya utawala ilikuwa na ukomo kwa wale tu waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu, angalau ni wazi kwamba walichaguliwa kwa msisitizo maalum. Ufufuo wa kwanza na matumizi ya nguvu za kifalme pamoja na Kristo ni Baraka kwa wale ambao walishiriki hatima ya Yesu kwa kuhusiana na mauti yake pia waliwezeshwa kushiriki hatima ya utukufu wake.” (Yarbro Collins 1977: 251)

Kwenye mwanga wa utata wa lugha ya Kigiriki, “baadhi ya wachambuzi huona makundi matatu kwenye kifungu hiki: watakatifu kwa ujumla (wale ambao wanaketi kwenye viti vya enzi), waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu, na watakatifu walio hai (wale ambao hawakumsujudia mnyama wala kupokea chapa yake)” (Ladd 1972: 265). Wengine wanaiona hiyo mahakama ya mbinguni kama pia inajumuisha malaika, kwa kuwa kwenye **Ufu 4:4** wale waketio kwenye viti vya enzi wanaonekana kuwa ni malaika.

18. <u>“Kambi ya Watakatifu na mji upendwao” (**Ufu 20:9**)</u>. Siyo “kambi” wala“mji” wa kuchukuliwa kama kambi au mji halisi. Hizi, kama vile maumbo mengine mengi tuliyoyaona, kwa fumbo na kwa ishara huelezea Kanisa. *“Mji upendwao”* (i.e., Kanisa) ni tofauti na *“mji mkuu”* (i.e., Babeli, ulimwengu wa wapinzani wa Ukristo, taasisi za kidini-na tamaduni). Nyongeza, *“kambi ya watakatifu”* na *“mji upendwao”* ni kitu kile kile, hakuna tofauti. Kama tulivyoona hapo juu na tutakavyoona hapa chini, Yerusalemu mpya ni sawa na*“mji mtakatifu”* ambao ni sawa na waamini (kanisa). **Ufu 3:12** zaidi huwatambulisha waamini wote (i.e., *“Yeye ashindaye”*) pamoja na *“mji wa Mungu Wangu”* (i.e., Yerusalemu mpya). *“Mji upendwao”* hauwezi kuwa tofauti na *“mji mtakatifu”* au *“mji wa Mungu Wangu,”* ambao ni Yerusalemu mpya, i.e., waamini, washindi, *“kambi ya watakatifu.”* Hii yote ni mifano inayoingiliana ambayo ni sawa na kanisa (angalia Kistemaker 2000: 437; Bauckham 1993a: 172; Beale 1999: 1027.).

Usawa wa *“kambi ya watakatifu”* pamoja na *“mji upendwao”* unaonyesha kwa njia nyingine kwamba kanisa la ulimwengu wote limeelezewa. Kwenye **20:9** Biblia tafsiri ya NASB na ESV zinasema kwamba Gogu na Magogu walipanda juu *“upana wa nchi.”* Tafsiri ya Biblia ya NKJV na NIV zinatafsiri mseo huu kama *“upana wa nchi.”*[27] Kwa hiyo Gundry anaona, “Kuja kinyume na mji au kambi, Gogu na Magogu lazima wasambae juu ya upana wa nchi.’ Hivyo mji hauonekani kuwa

---

ulimwengu kwa sababu yake Yeye aliyeushinda ulimwengu. . . . Hivyo enzi hizi siyo halisi wala kitu cha kushikika. . . . Badala yake ni enzi zinazomilikiwa na watakatifu juu ya nchi wakati wa kipindi cha miaka elfu.” (Kik 1971: 210, 213) Kik anaeleza kwamba kwenye **Ufu 20:4** maneno *kuketi, kupewa, kuabudiwa, kupokelewa, na kutawala* vyote vipo kwenye wakati wa kibinadamu. Alihitimisha, “Kwa kuwa vyote vipo kwenye wakati ule ule lazima vizungumzie wakati uo huo. Hili ni, wakati wa kutokumwabudu mnyama na kutokupokea chapa ni wakati uo huo kama ule wa kukaa kwenye viti vya enzi na kuishi na kutawala pamoja na Kristo.” (Ibid.: 228) R. Fowler White anaongeza, “Kusema kwenye [Ufu] 20:6 kwamba wale ambao watachukua sehemu kwenye ufufuo wa kwanza watatawala pamoja na Kristo ni kusema watafanya hivyo kwanza juu ya nchi kabla hawajafa na kasha mbinguni baada ya wao kufa” (White 1992: 13). Kwenye mawasiliano binafsi pamoja na mwandishi, White vivyo hivyo alisema wakati wa kibinadamu wa vitenzi, kuainisha, “Kama Augustine alivyofuundisha, ufufuo wa kwanza *kutaitangulia miili ya wafu waliouawa kwa ajili ya ushuhuda na kuirejesha kwao*. Kuliweka hili kwenye maneno ya andiko lenyewe, mashahidi waliuawa kwa sababu ***hawa****kumwabudu mnyama wala sanamu yake, na* ***hawa****kupokea chapa kwenye vipaji vya nyuso zao wala kwenye mikono yao, na* ***wali****huishwa na* ***wali****tawala na Kristo kwa miaka elfu.* Vitenzi vya kibinadamu hapa vinapaswa kutafsiriwa mara kwa mara kama kuzungumzia matukio yaliyotangulia mauti au kifo cha ashahidi.”

[27] Kwenye maelezo ya kina ya chini toleo la Biblia la NASB linaandika kwamba msemo halisi ni *“upana wa nchi.”*

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

umefungwa mahali pamoja au ni kimji kidogo cha kuzingira kwa dakika moja. walikuwa ni watakatifu wote popote waishipo juu ya uso wa nchi." (Gundry 1987: 256-57)

19. "Watu wake" (**Ufu 21:3**). Ayah ii ni hitimisho la maelezo ya mara kwa mara kwenye Biblia yote (pamoja na tofauti ndogo): *"Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu* (**Mwanzo 17:8; Kut 6:7; 29:45; Walawi 26:12; Yer 7:23; 11:4; 24:7; 30:22; 31:1, 33; 32:38; Ezek 11:19-20; 14:10-11; 36:28; 37:23, 27; Hos 2:23; Zek 8:8; 13:9; 2 Wakor 6:16; Waeb 8:10; Ufu 21:3**). Vifungu vya Agano la Kale vinazungumzia mahusiano maalum baina ya Mungu na watu Wake. Mabnabii waliokwenda utumwani na wale wa baada ya Utumwa walitumia neno hili kuzungumzia urejesho wa Israeli. Agano Jipya limechukua lugha ileile na kuitumia kwa Israeli mpya ya kweli iliyorejeshwa kwa Mungu—Kanisa. Ufunuo unahitimisha hili kwa kulitumia wakati wote kwa "mji mtakatifu," "Yerusalemu mpya," "bibiarusi," "mke wa Mwanakondoo" (**Ufu 21:2, 9-10),** i.e., watu wa Mungu waliobadilishwa na kutukuzwa—kanisa.[28]

Kwenye sentensi *"Nitakuwa Mungu wao, na watakuwa watu wangu,"* Agano la Kale na jipya yote hutumia umoja "watu[mtu]." Pamoja na heshima ya **Ufu 21:3**, hata hivyo, namba muhimu ya maandiko ya awali hutumia wingi "watu" badala ya umoja "watu."[kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili neno la Kiingereza *People na peoples* yote yanamaanisha *watu* hakuna linalomaanisha mtu kama ilivyo kwenye kiingereza] Kudhani kwamba hililaweza kuwa kesi, Yohana anafanya mabadiliko kutoka "watu/mtu" kuwa "watu" ili "kuliweka wazi kwamba nabii zote zililenga juu ya kutimizwa kwa Israeli kwenye 'kila kabila, lugha, jamaa, na taifa' (hivyo 5:9; 7:9)" (Beale 1999: 104647; angalia pia Gundry 1987: 257; Johnson 2001: 305n.2).

20. Yerusalemu Mpya (**Ufu 21:1-22:15**). Kamatulivyoona pamoja na ishara na picha nyingi za Yohana, zipo kambi mbili kuu kuhusiana na tafsiri ya "Yerusalemu mpya": wanaoamini katika uhalisia na wasioamini katika uhalisia. Tafsiri ya Yerusalemu mpya kwa wanaoamini katika uhalisia hutafsiri kama maelezo halisi ya mji halisi wa kimwili. Hata hivyo, *"bibi arusi, mke wa Mwanakondoo"* (**Ufu 21:9**), ambaye kwa wazi ni Kanisa, ni sawa na mji kwenye **Ufu 21:2, 10**. Maelezo ya Yerusalemu mpya yapo "kibinafsi zaidi kuliko kijiografia" (Gundry 1987: 256). Mpango wa Mungu wa milele wakati wote ni umekuwa ni kukaa mahali patakatifu pamoja na watu wake watakatifu (angalia Goldsworthy 1991: 76; Alexander 2008: 29). "Makao ya Mungu pamoja na wanadamu *kwenye muundo wa mji* yaweza . . . kuelezea muunganiko timilifu wa jamii iliokombolewa mmoja na mwingine kama hitimisho la Mungu na jawabu la milele kwa mfululizo wa kijamii wakushindwa kuuchafua msingi wa historia ya binadamu" (Ortlund 1996: 166n.73).

Ambao majina ya mitume kumi na wawili yamesemekana kuwa "msingi" wa kuta za mji tena inasema kwamba imeelezewa kuwa zaidi ya jiografia tu. Beale anaona mahusiano ya kushangaza baina ya kuta za mji na malango yake: "Unaojulikana ni uchunguzi kwenye 21:14 kwamba mitume ni sehemu ya msingi, pale ambapo makabila ni sehemu ya malango kwenye kuta zilizojengwa kwenye msingi. Mtu anaweza kutazamia mtazamo tofauti kwa kuwa Israeli ililitangulia Kanisa kwenye historia ya ukombozi. Lakini siri iliyokuja kinyume inaonyesha ukweli kwamba utimilifu wa ahadi za Israeli hatimaye umekuja kupitia Kristo, ambaye, pamoja na mitume walishuhudia utimilifu wa kazi yake, kuunda msingi wa hekalu jipya, Kanisa, ambalo ni Israeli mpya." (Beale 1999: 1070) Kupewa utambulisho huu wa kaeribu, Yerusalemu mpyainaonekana kuwa ishara kwa watu wa Mungu na Uhusiano wake na wao, badala ya maelezo ya Kijiografia ambao utakuwepo baada ya Kristo kuja mara ya pili.[29]

---

[28] Maelezo kwenye **Ufu 21:3** kwamba *"Maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu"* lilikuwa kivuli kwenye **Ufu 7:15** ambayo inasema kwamba Mungu *"atatanda hema yake juu yao"* (i.e., juu ya "mkutano mkubwa"—kanisa). Rejea hii ya msalaba inathibitisha kwamba kanisa la ulimwengu ndilo lililoko kwenye mtazamo hapa kwenye vifungu vyote viwili.

[29] Yerusalemu Mpya ni maelezo ya kutumia, hali ya umilele ambayo itatumika pamoja na Kristo kwenye *parousia*. Kama vile, umuhimu wake ni mchanganyiko. Unajumuisha kuhuishwa kwa nchi na ulimwengu wa kimwili. Kama lilivyokuwa suala la wale waliokaa kwenye viti vya enzi kwenye **Ufu 20:4-6**, kwa madhumuni ya sasa maana ya ishara ya Yerusalemu Mpya kwa kiwango cha chini yanajumuisha kuangalia hali ya umilele ya kanisa kama *"mji mtakatifu"* na siyo tu maelezo ya mwonekano wa kimwili au kijiografia wa milele *"mbingu mpya nan chi mpya."* R. Fowler White analiweka hili kama hivi, "Watakatifu watatokea kama mji mtakatifu (cf. [Ufu] 3:12), wakati mbingu mpya na nchi hujitokeza kama maskani ya milele ya Mungu na Wanadamu" (White 1999:61).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

VII. Mtazamo wa mawazo makuu na vifungu[30]

Vipengele mbalimbali vya mawazo makuu na vifungu vya Ufunuo tayari vimekwisha kujadiliwa hapo juu, hasa kwenye sura ya **I. Aina** (kuhusiana na namba na vipindi vya wakati kwenye Ufunuo), **V. *Muundo*** (hasa mfanano wamuhuri-tarumbeta-vitasa na maelezo mbalimbali ya *parousia* na hukumu ya mwisho), na **VI. *Kanisa kwenye kitabu cha Ufunuo*** (mitazamo mbali mbali ya kanisa). Kama tunavyoendelea kupitia vifungu vikuu vya Kitabu cha Ufunuo, tafadhali angalia nyuma kwenye mafafanuzi yaliyotangulia kama vipengele hivyo vya kitabu havitakuwa vimerudiwa. Vipengele vingine muhimu vya vifungu vikuu vya kitabu cha Ufunuo ni kama vilivyo hapa chini.

A. *Ufu 1:1-20: Utangulizi*

Yohana anaahidi Baraka kwa wale watakao soma, kusikia, na kuyashika maneno ya kitabu hiki (**Ufu 1:3**). Hata kwenye utangulizi lengo ni kwa Kristo (**Ufu 1:5-8, 13-18**). *"Roho saba walioko mbele ya kiti Chake cha Enzi"* (**Ufu 1:4;** angalia pia **3:1; 4:5; 5:6**) bila shaka ni kumbukumbu ya fumbo kwa Roho Mtakatifu. Kwa uwazi kabisa Roho Mtakatifu ni mmoja (**Ufu 2:7, 11, 17, 29; 3:6, 13, 22; 22:17**; angalia pia **Efe 4:4**) bado anatajwa kama "Roho saba" (**Ufu 1:4; 5:6**; au "Roho mara saba,"kumbukumbu ya NIV) ambazo, kwenye **Ufu 5:6**, ni sawa na "macho saba" ya Mwanakondoo. "Macho saba" na "Roho saba" zimeasiliwa kutoka **Zek 3:8-9; 4:1-10**.[31] Kwenye **Zek 3:9**, "Macho saba" yanahusiana na maelezo ambayo yanahusika na Mungu kuuondoa uovu kutoka katika nchi. Kwenye **Zek 4:2, 10**, "Vinara saba" na "macho saba" yanahusishwa na Roho wa Mungu. "Yohana alitafsiri "macho saba" kwenye Zekaria kama Roho wa Yahwe na alitambulisha vyote kama miliki ya Mwanakondoo. Ni kwa Roho wa Yahwe pekee 'Mtumishi Chipukizi [**Zek 3:8**],'Mwanakondoo wa Ki-masihi, kwamba uovu umeondolewa katika nchi (Zek. 3:9) na upinzani kwa ufalme kushinda (cf. Zech. 4:6–7)." (Beale na McDonough 2007: 1102; angalia pia Bauckham 1993b: 110-15) "Roho saba" zinazungumzia utimilifu wa Roho.

B. *Ufu 2:1-3:22: Barua kwa makanisa saba*

Hata kwenye karne ya kwanza Makanisa walizishuhudia Ishara ambazo Kristo aliwaonya juu yake kwenye hotuba ya Mlimani, ikijumuisha mateso toka kwa Wayahudi (**Marko 13:9; Ufu 2:9-10; 3:9**), mateso kwa ujumla pamoja na kifo (**Math 24:9; Ufu 2:9-10, 13**), manabii wa uongo (**Math 24:5, 11, 23-26; Ufu 2:2, 6, 14-15, 20-24**); kuanguka kutoka kwenye imani (**Math 24:10; Ufu 2:14, 20-24; 3:1-3, 15-17**), na upendo kupoa (**Math 24:12; Ufu 2:4**). Kwenye kifungu hiki, Kristo analitia moyo Kanisa kushuhudia na kuwaonya juu ya kukubaliana ili kwamba waweze kuurithi uzima wa milele.

1. Asili ya maadili ya unabii kwa Makanisa. "Barua saba kwa Makanisa saba" ni kifungu muhimu kwenye kitabu. Zimebeba maneno yote ya Kristo kwa makanisa, jambo pekee linalo ya fanya kuwa muhimu. Yanatia moyo, yanaonya, na kutoa ahadi ambazo zimeendelea kwenye kitabu chote kwa ujumla na hayo yametimizwa mwishoni mwa kitabu. Håkan Ulfgard anakumbusha, "Barua kwa makanisa saba pia zinahusika na ujumbe wa kinabii kwa jamii. Maneno yake ya kutia moyo na matishio hayajaelekezwa kwa watu wa wakati ujao, lakini unazungumza moja kwa moja na maisha ya msomaji/msikilizaji, ukiwatia hamasa kujipambanua wenyewe na 'ishara za kiulimwengu' zilizoorodheshwa kwenye maono ya Yohana, na kutenda kulingana nayo." (Ulfgard 1989: 13)

   Sehemu ya mkakati wa maadili ya kinabii kwa ujumbe wa makanisa saba ni kuonyesha tofauti baina ya "yale yaliyopo kwa sasa nauhakika wa nyakati za mwisho." Richard Bauckham anaelezea: "Bibi arusi ni Yerusalemu mpya, ushukao kutoka mbinguni kwa Mungu (21:2), Kanisa kwenye hitimisho la historia. Bibi arusi ni Kanisa ambalo Mwanakondoo, atakapokuja, atalikuta tayari kwa ajili

[30] Sauti nzuri imerekodiwa ya kitabu cha Ufunuo ambayo yaweza kusikilizwa au kupakuliwa bure, inapatikana kwenye wavuti ya: Arturo Azurdia katika: http://www.monergism.com/thethreshold/articles/onsite/azurdia_revelation.html; G. K. Beale katika: http://resources.thegospelcoalition.org/library?f%5Bbook%5D%5B%5D=Revelation&f%5Bcontributors%5D%5B%5D=B eale%2C+G.K.&page=2&sort=contributors; D. A. Carson katika: http://resources.thegospelcoalition.org/library?f%5Bbook%5D%5B%5D=Revelation&f%5Bcontributors%5D%5B%5D=C arson%2C+D.+A.&sort=contributors; John Fesko katika: http://www.genevaopc.org/audio/fesko-lectures/72-revelation-lectureseries.html; Jonathan Menn katika: http://www.eclea.net/sermons.html#revelation (Vyoye sauti na makala zilizoandikwa); and Kim Riddlebarger katika: http://www.christreformed.org/kim-riddlebarger/#Revelation (sauti, na http://kimriddlebarger.squarespace.com/downloadable-sermons-on-the-bo/ (makala zilizoandikwa).

[31] "Roho saba" pia zaweza kuwa zimeasiliwa kutoka **Isa 11:2** ambayo inazungumzia *"Roho ya Bwana . . . Roho ya hekima na ufahamu, Roho ya ushauri na uweza, Roho ya maarifa na kumcha Bwana."*

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

ya arusi yake, limevaa kitani safi cha matendo ya haki (19:7-8). Bibi arusi ni Kanisa lionekanalo kutoka kwenye mtazamo wa *parousia.* Tofauti mkubwa ipo katika Makanisa yaliyoandikiwa kwenye Ufunuo. ‘nguo zilizochakaa za Wakristo wa Kanisa la Laodikia (3:17) tofauti na kitani safi ya Bibi arusi. Kutokujitayarisha kwa ujumla kwa kuja kwa Bwana huko Efeso, Pergamo, Sardi (3:17) tofauti na maombi ya kina ya Bibi arusi kwa ajili ya kuja kwa Bwana arusi (22:17). Tofauti kweli siyo baina ya waaminifu na wasio waaminifu ndani ya Makanisa. . . . Badala yake tofauti ni baina ya wakati uliopo sasa na uhakika wa nyakati za mwisho, baina ya Makanisa kama yalivyo na Makanisa jinsi yanavyotakiwa kuwa ikiwa yatachukua nafasi yake kwenye sherehe ya arusi ya mwisho.” (Bauckham 1993a: 167) Tofauti hizi hizi lazima zitufanye sisi kutathmini hali ya makanisa yetu wenyewe na maisha yetu kwenye nuru ya ujio wa uhakika wa nyakati za mwisho.

2. Tofauti baina ya Makanisa na “wakaao juu ya uso wa nchi.” Msemo *“wale wakaao juu ya uso wa nchi,”* au tofauti za msemo huu, umetokea kwa kujirudia rudia kwenye kitabu chote (**Ufu 3:10; 6:10; 8:13; 11:10; 13:8, 12, 14; 14:6; 17:2, 8**). Utahbiti wa msemo una maana hasi. Inaashiria kwamba, kwenye mioyo yao, wasioamini wanayaendea maisha kwa mtazamo na ufahamu wa kidunia; wao ni *wa* ulimwengu kwenye nyongeza ya kuwa *ndani* ya ulimwenguni (cf. **Yoh 17:14-18**). Kama vile, wanafuata njia za ulimwengu na kuangukia chini ya hukumu ya Mungu.

Kufuatana na tofauti hizo, kwenye Ufunuo Kanisa wakati wote ni mali ya mbinguni bila kujali wanachama wake wanaishi wapi kimwili (Johnson 2001: 147). Kwenye kitabu chote cha Ufunuo, wanadamu wote (*“kila kabila na jamaa na lugha na taifa”*) wanaonekana kama kuwa wanachama wa moja kati ya mawili, kambi ya wapinzani kwa pande zote: ulimwengu (**Ufu 11:9; 13:7; 14:6**; angalia pia **17:15**), au Kanisa (**Ufu 5:9; 7:9**); wale wakaao juu ya uso wa nchi (**Ufu 3:10; 6:10; 8:13; 11:10; 13:8, 12, 14; 14:6; 17:2, 8**), au wale ambao ni raia wa mbinguni (**Ufu 6:9, 11; 7:9-10; 11:12; 12:10; 14:1-3; 15:24; 19:1-9, 14; 20:4-6**); wale wamwabuduo mnyama (**Ufu 13:3, 4, 8, 12, 15; 14:9, 11; 19:20**), au wale wanaomwabudu au kumsujudia Mwanakondoo (**Ufu 4:8-11; 5:9-14; 6:9; 7:9-17; 11:15-18; 12:11, 17; 14:4, 12; 15:2-4; 17:14; 19:5-9; 20:4; 21:9; 22:3**); wale walioichukua chapa ya mnyama (**Ufu 13:16-17; 14:9, 11; 19:20**), au waleambao wamewekwa muhuri na Mungu (**Ufu 7:3; 9:4; 14:1; 22:4**); wale ambao majina yao hayajaandikwa kwenye kitabu cha uzima (**Ufu 13:8; 17:8; 20:15**), au wale ambao majina yao yameandikwa kwenye kitabu cha uzima (**Ufu 3:5; 21:27**); wale ambao ni sehemu ya “mji mkubwa” (**Ufu 11:8; 16:19; 17:18; 18:10, 16, 18, 19, 21**), au wale ambao ni sehemu ya “mji upendwao” (**Ufu 20:9**). Hakuna “ambaye hatahusika” au mbadala wa tatu.[32] Kwa hiyo, waamini lazima wayakabili maisha kutokana na mtazamo na ufahamu wa mbinguni (**Wafil 3:20**); ingawa *wapo* ulimwengunia hawapaswi *kuwa* wa ulimwengu (**Yoh 17:13-19**). Kitabu chote cha Ufunuo kinatupa mtazamo wa mbinguni wa maana ya kweli ya kile kinachotokea juu ya uso wan chi, ili kwamba waamini waweze kuwa mfano wa sura ya Kristo (**Rum 8:29**).

3. Asili ya mkanganyiko kwenye “kushinda”. Kwenye **Ufu 2:7, 11, 17, 26; 3:5, 12, 21** Kristo alitoa ahadi kwa mtu ambaye “atashinda.” Neno la Kigiriki kwa “mshindi” ni *nika*ō. Istilahi hii imetumika kote kwenye **Ufu 12:11, 15:2,** na kwenye **Rum 8:35-37.** Matumizi ya *nika*ō kwenye **Ufunuo 2-3** (na kitabu chote cha Ufunuo) kinaonyesha wazo mkanganyiko la“kushinda” ambako kumeonyeshwa juu ya ushindi wa Kristo mwenyewe juu ya Shetani na kifo. Kwenye **Ufu 1:5-6**, Yohana anaelezea kazi ya ukombozi ya Kristo. “Kwamba ushindi wa Kristo ulipatikana kwenye kifo chake, ni wazi kutoka kwenye kumbukumbu za Yohana kwa damu yake (1:6). Bila kupingana au kukataa kabisa ushindi wa Kristo kwenye ufufuo, ugumu wa ushindi kwenye kifo cha Kristo ni halali.” (White 2000: 172) Asili ya mkanganyiko wa ushindi wa Kristo vivyo hivyo umeonyeshwa kwenye **Ufunuo 5**. “Alishinda kifo kwa kufufuliwa kutoka kwa wafu. Lakini matokeo ya sasa ya ushindi wa Mwanakondoo hayadumu tu kwenye ukweli kwamba Mwanakondoo anaendelea ‘kusimama’ lakini pia kwenye ukweli kwamba ataendelea kudumu kama Mwanakondoo aliyechinjwa. . . . Huyu ni, Kristo kama Simba alishinda kwa kuwa alichinjwa kama Mwanakondoo, ambalo ni tukio muhimu kwenye sura ya. 5.” (Beale 1999: 352)

Kanisa linafuata nyayo za Bwana wake. Kwa waamini, kile kinachosemwa na Ufunuo, kama White alivyokiweka, ni hiki “kama Yesu’ alivyoanzisha ufalme, ufalme wa Kanisa sasa unahusisha kushinda kwa kushikilia ushuhuda wa uaminifu wake kwenye kukabiliana na majaribu (e.g., 2:9-11, 13; 3:8; 12:11); kwenye kuzishinda nguvu za uovu (e.g., 6:8 kwenye mahusiano na 6:9-11); kwenye kuitiisha dhambi katika maisha ya wanachama wake (angalia sura za. 2-3); na kwenye kuanza kutawala

[32] Kwenye nusu ya pili ya kitabu tunaona uwili unaoelezwa kupitia tofauti ya picha tatu za wazi zikihusisha wanyama, wanawake, na miji: Mnyama—Mwanakondoo; Kahaba—Bibiarusi; Babeli mkuu—Yerusalemu Mpya.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

juu ya kifo na Shetani kwa kutambulishwa pamoja na Yesu (cf. 1:5–6, 18). Uvumilivu wa Kanisa, kisha, ni sehemu ya mchakato wa kushinda." (White 2000: 175)

Tunaliona wazo lilelile mkanganyiko wa "kushinda" kwenye **Ufu 11:7; 13:7** pale mnyama anaposemekana "kuwashinda" watakatifu kwa kusababisha mateso na kifo kwenye miili yao. Wakati uo huo, hata hivyo, Kristo na watakatifu wanasemekana "kumshinda" joka, mnyama, na mawakala wake wote *"kwa sababu ya neno la ushuhuda wao, ambao hawakupenda maisha yao hata kufa"* (**12:11**; angalia pia **15:2; 17:14**). White anahitimisha, "Uvumilivu kwenye imani bila kujali mateso ni ushindi wa kanisa kwenye historia" (Ibid.: 168).

C. ***Ufu 4:1-5:14: Kiti cha enzi, kitabu (gombo), na Mwanakondoo***

Kwenye kifungu hiki, Mungu na Kristo wanatukuzwa kwa sababu kufufuka kwa Kristo kunadhihirisha kwamba ni wenye mamlaka juu ya uumbaji kuhukumu na kukokmboa. "Kitabu' kinaeleweka vizuri kama kimebeba mpango wa Mungu wa hukumu na ukombozi, ambavyo vilianzishwa na kifo na kufufuka kwa Kristo lakini bado kukamilishwa" (Beale 1999: 340). Schüssler Fiorenza anaeleza, "Swali lamsingi la Kitheolojia la sura ya 4-5 kama vile kwenye kitabu chote ni: Ninani ambaye ni Bwana wa kweli wa ulimwengu huu?" (Schüssler Fiorenza 1991: 58)

Ipo mifanano ya muhimu baina ya sura hizi mbili na **Danieli 7:**

Tukio	***Danieli 7***	***Ufunuo 4-5***
1. Maneno ya utangulizi wa maono	**Dan 7:9**	**Ufu 4:1**
2. Kiti cha enzi(vi) kimewekwa mbinguni	**Dan 7:9a**	**Ufu 4:2a**
3. Mungu ameketi juu ya kiti cha enzi	**Dan 7:9b**	**Ufu 4:2b**
4. Mwonekano wa Mungu kwenye kiti cha enzi	**Dan 7:9c**	**Ufu 4:3a**
5. Moto mbele ya kiti cha enzi	**Dan 7:9d-10a**	**Ufu 4:5**
6. Watumishi wa mbinguni kukizunguka kiti cha enzi	**Dan 7:10b**	**Ufu 4:4b, 6b-10; 5:8, 11, 14**
7. Kitabu (vi) mbeke ya kiti cha enzi	**Dan 7:10c**	**Ufu 5:1-5**
8. Kitabu(vi) kufunguliwa	**Dan 7:10c**	**Ufu 5:2-5, 9**
9. Aliye mfano wa mwanadamu akipokea mamlaka kutawala milele	**Dan 7:13-14a**	**Ufu 5:5b-7, 9a, 12-13**
10. Wigo wa ufalme: "jamaa zote, mataifa na lugha"	**Dan 7:14a**	**Ufu 5:9b**
11. Maumivu ya kihisia ya mwonaji juu ya maelezo ya maono	**Dan 7:15**	**Ufu 5:4**
12. Mwonaji kupokea ushauri kutoka kwa mtumishi wa mbinguni	**Dan 7:16**	**Ufu 5:5a**
13. Watakatifu kupokea mamlaka ya Kiungu kuzitawala Falme	**Dan 7:18, 22, 27a**	**Ufu 5:10**
14. Kuhitimisha kutaja Utawala wa milele wa Mungu	**Dan 7:27b**	**Ufu 5:13-14**

Mifanano hiyo inaashiria mawazo manne ya msingi yafuatayo:

"(1) Yohana alikusudia sura. 4-5 kuonyesha utimilifu wa unabii wa Danieli 7 wa utawala wa 'mwana wa adamu' na wa watakatifu, ambao ulizinduliwa na kufa kwa Kristo hasa kufufuka kwake, hili ni, kukikaribia kwake kiti cha enzi kupokea mamlaka.

(2) Kuunganishwa kwa sehemu hii kama Isaya 6 na Ezekieli 1-2 pamoja na sehemu ya kabla ya utawala kutoka Danieli 7 kunaelezea kivuli cha hukumu kwenye maono, kwa kuwa sehemu hii yote inatumika kama utangulizi kwa tangazo la hukumu. . . . Kwa usahihi zaidi, sehemu hizi za Agano la Kalelinawakilisha maono ya utawala na umiliki wa Mungu kwa ulimweng wote ambao ulitolewa kwanza kwenye hukumu, ukifuatiwa na ukombozi. Hii ni historia ya Kitheolojia ya Ufunuo 4-5 na sura zinazofuata.

(3) Wazo la hukumu pia linaletwa na picha ya 'kitabu' ambayo imeelezwa kwenye lugha kutoka Ezekieli 2, Isaya 29, Danieli 7, na Danieli 12. Kila moja ya maandiko haya yana kiini cha wazo la hukumu, lakini tena pamoja na wazo la Wokocu au baraka.

(4) Wazo la Danieli 7 la ufalme ambao watu wote watamhudumia 'Mwana wa adamu' (Dan 7:14) na Mungu (7:27b) linaonekana na Yohana kama kutimizwa Kanisani. Bado Kanisa pia ni utimilifu wa utawala wa Danieli wa watakatifu wa Israeli." (Beale 1999: 314-15 [jedwali]; 368-69 [maandishi])

1. <u>Wazee 24 (**Ufu 4:4, 10; 5:8; 11:16; 14:3; 19:4**)</u>. Wengi huwaona wazee 24 kama wawakilishi wa Agano la Kale lote na Kanisa la Agano Jipya, wakiunganisha idadi ya viongozi au wazee12 wa taifa la Israeli na Mitume 12 (Milligan 1896: 69; Hendriksen 1982: 85). Hata hivyo, kwenye **Ufu 5:8-10, 11:16-18,** na **14:1-3** hapa panaonekana kuwa na utofauti baina ya wazee 24 na walikombolewa (Ladd 1956: 97-98). Zaidi ya hayo, kwenye **Ufu 5:8** na **7:13-14** (cf. **8:3**), wazee wanafanya kazi za malaika na kufunuwa mambo kwa Yohana. Vivyo hivyo, ingawa wameunganishwa na Kanisa, hawaonekani kufanana na kanisa (angalia Ladd 1972: 73-75; Beale 1999: 322; Johnson 2001: 99-100).

2. <u>Kitabu (gombo) kilichofungwa na mihuri saba (**5:1-4**)</u>. Zipo nadharia mbalimbali kuhusiana na utambulisho wa kitabu kilichofungwa. Baadhi hupendekeza kwamba kitabu ni ufunguzi wa majina ya

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

waliokombolewa. Hata hivyo, “kwa kukifungua kitabu Mwanakondoo siyo tu atafunua yale yaliyomo, bali atayaweka kwenye utendaji,” na “hakuna pendekezo hapa au penginepo kwenye kitabu kwamba kusudi la Yohana lilikuwa kufunua utambulisho wa waliokombolewa” (Caird 1966: 71). Wengine wanadai kwamba kitabu ni Agano la Kale. Hata hivyo, maelezo ya kitabu au gombo yamechukuliwa kutoka **Ezek 2:9-3:3**. Kwa hiyo, kiukitazama kitabu au gombo kama Agano la Kale “hupunguza utegemezi wa Yohana kwa Ezekieli . . . na haielezei kwanini kifo cha Kristo lazima kiwe sifa muhimu kwa kiukifungua kitabu.” (Ibid.: 72).

Kenneth Gentry kwa usahihi anakumbusha utegemezi juu ya Ezekieli na kuona kwamba wazo la maono ya Ezekieli lilikuwa “hukumu juu ya Israeli” (Gentry 1998: 51). Kama Utangulizi, inadai kitabu au gombo ni “tangazo la Mungu la talaka dhidi ya mke wake wa Agano la Kale kwa ajili ya uzinzi wake wa Kiroho” (Ibid.: 51-52). Kwenye Agano la Kale, kweli Mungu alizungumza kuhusiana na talaka hiyo (angalia **Isa 50:1; Yr 3:8**). Mwaka BK 70, “mwisho na ukamilifu wa kuangamizwa kwa hekalu kulihitimisha hili” (Ibid.: 52). Hata hivyo, kwa kuyatafakari kwa kina matukio ya mwaka BK 70, utangulizi huona mapungufu mapana kwenye simulizi ya Ufunuo. Hushindwa pia kuona jinsi gani Ufunuo ulivyobadili na kuyalenga mawazo ya Agano la Kale.

Mtazamo mwingine ni kwamba kitabu ni ufunuo wa matukio hayo yajayo ambayo Yohana aliagizwa kuyawasilisha. Hata hivyo, Kristo alishinda haki ya kukifungua kitqbu kwa kifo chake juu ya msalaba. “Haskuna sababu ya wazi sana kwanini, kuishinda haki hiyo mwaka BK 30, alipaswa kuliahirisha zoezi hilo mpaka mwaka BK 95. Dhana ya kiasili ni lile la kufungua kitabu, ambalo kwayo yaliyomo yaweze kufunuliwa na kuwekwa kwenye utekelezaji, kufuatiwa mara na ushindi ambao kwa huo alipata haki ya kukifungua. Hili linamaanisha kwamba kutokana na mtazamo wa Yohana angalau baadhi ya yaliyomo tayari yalikwisha kupita; na kwa kulithibitisha hili tunahitaji tu kurudi kwenye maono yaliyotolewa kwa kuvunjwa muhuri ya tano, ambayo kwayo Yohana aliangalia nyuma juu ya wale waliopita waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu sawa sawa na kuangalia mbeleni.” (Caird 1966: 71-72)

Kwa hiyo, mtazamo ulio bora, ni kwamba “yaliyomo kwenye kitabu ni mpango wa Mungu wa ukombozi, ukitiwa kivuli kwenye Agano la Kale, kwa hili alimaanisha kutangaza utawala wake juu ya ulimwengu wa dhambi na hivyo kulifikia kusudi la uumbaji. Yohana alipendekeza kutazama mchakato wote wa mpango huu kutoka mwanzo wake msalabani mpaka kwenye hitimisho la ushindi kwenye Yerusalemu.” (Ibid.: 72; angalia pia Beale 1999: 340)

3. Simba ambaye ni Mwanakondoo (**5:5-6**). Kwenye maelezo yetu ya awali ya ishara tofauti na picha ya kanisa kwenye Ufunuo, tulijadili sehemu ya “kusikia-kuona” ya utambulisho (angalia maelezo ya “makutano makubwa” ya **Ufu 7:9-17**, hapo juu). Kama vile ufunuo ulivyo na mawazo mkanganyiko ya “ushindi,” hivyo **Ufu 5:5-6** unawakilisha utofauti na mkanganyiko wa utambulisho wa Kristo kama mshindi wa kijeshi na muhanga wa sadaka. Kwenye tofauti baina ya kile alichokisikia (**Ufu 5:5**) na kile alichokiona (**Ufu 5:6**), Yohana: “kwanza anakuja na wazo la Masihi kama ushindi wa jeshi la kitaifa la Wayahudi na kisha kulitafsiri tena kwa maana ya mtazamo wa sadaka ya kifo kwa ukombozi wa watu kutoka mataifa yote (cf. 5:910). . . . Kwa kuweka picha ya muhanga wa sadaka sambamba na ule wa ushindi wa kijeshi, Yohana analenga ishara mpya ya *ushindi* kwa sadaka ya kifo. . . . Yesu Masihi tayari alikwisha shinda uovu kwa sadaka ya kifo. Alishinda kwa ushindi, lakini kwa sadaka, siyo mgogoro wa kijeshi, na aliwakomboa watu wa Mungu, lakini ni kutoka mataifa yote, siyo Wayahudi tu. Ushindi wa kuendelea na wa milele wa Mungu juu ya uovu ambao unaelezwa na unabii wote wa Yohana ni utekelezaji muhimu wa ushindi alioupata juu ya msalaba.” (Bauckham 1993a: 214-15)

D. ***Ufu 6:1-8:5: Mihuri saba***

Kwenye kifungu hiki Kristo anafanyia kazi jukumu lake kama mfalme na mwamuzi au hakimu kwa kutumia nguvu ya uovu ya mbinguni kwa kulazimisha mateso juu ya watu wakati wote kabla ya kurudi kwake, kwa utakaso wa waamini au kwa adhabu ya wasioamini. Ingawa Wakristo wanateswa, hukumu ya mwisho ni majibu ya Mungu ya mwisho kwa maombi ya watakatifu kwenye **6:10** kwamba ataipatia haki damu yao.

1. Wapanda farasi wanne (**Ufu 6:1-8**). Juu ya nyuso zao, muhuri za kwanza nne zinaruhusu “farasi” bianfsi wanne juu ya kila mmoja wao alikaa mpanda farasi mmoja.[33] Hata hivyo, “hakuna hata mmpja kati ya wapanda farasi wane ambaye ni mtu. Kila mmoja ni sababu ya , udhihirisho wa kweli yakini iliyounganishwa na ufalme wa Kristo wakati ufalme huo utakapoonekana kuwa, kwenye asili yake

[33] Umoja, binafsi “yeye” ulitumika kwa kila mpanda farasi.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

yenyewe, hukumu ya ulimwengu. Hata vita, njaa, na kifo na kuzimu, ambavyo vitafuata, siyo vitu halisi. Vimetumiwa tu, kama laana kwa mwanadamu, kutoa maelezo ya jumla ya hukumu ya Mungu." (Milligan 1896: 89)

Kwa nyongeza ya kutambua haya "wapanda farasi wanne wa ufunuo," lipo pia suala la ni lini wapanda farasi hao watakaporuhusiwa. Baadhi wanafikiri kwamba wapanda farasi wataruhusiwa muda mfupi tu kabla ya kurudi kwa Kristo mara ya pili. Hata hivyo, mazingira ya kifungu yanadhihirisha vinginevyo. **Ufunuo 6** kwa karibu sana umeunganishwa na **Ufunuo 5**. **Ufunuo 5** ikiwa tu kwamba Mwanakondoo (Kristo) pekee ndiye aliyestahili *"kukifungua kitabu"* (**Ufu 5:4, 8**) na *"kuzivunja muhuri zake"* (**Ufu 6:1, 3, 5, 7, 9, 12; 8:1**), msingi wake ni kile alichokifanya pale msalabani (**Ufu 5:5-6, 9**). Hali kadhalika, **Ufu 6:1-8** inaelezea nguvu ya uharibifu ambayo iliruhusiwa kama matokeo ya kifo cha Kristo juu ya msalaba na kufufuka kulikoambatana na kupaa. Utambulisho wa muhuri kama kuwa unazinduliwa na kifo, kufufuka na kupaa kwa Kristo, kama kunavyopingana kuwa matukio ambayo yatatukia muda mfupi baada ya *parousia,* inathibitishwa kwa mfanano baina ya "ishara" Yesu aliyoitoa kwenye Hotuba ya Mlimani, ambayo ilihusisha kipindi chote baina ya tukio la kuja kwa Kristo mara ya kwanza na kurudi mara ya pili, na matukio yaliyoorodheshwa kwenye **Ufu 6:1-14**:

Hotuba ya Mlimani (ishara)	***Ufunuo 6 (muhuri)***
Math 24:5, 11, 23-24; Marko 13:6, 22 (Makristo wa uongo)	Inalingana na muhuri wa 1st (**6:2**)
Math 24:7; Marko 13:8; Luka 21:11 (njaa)	Inalingana na muhuri wa 2nd **6:4**)
Math 24:6-7, 12; Marko 13:7-8; Luka 21:10 (vita na matetesi ya vita)	Inalingana na muhuri wa3rd (**6:6**)
Math 24:22; Marko 13:12, 20; Luka 21:24 (kifo); **Luka 21:11** (mapigo)	Inalingana na muhuri wa 4th **6:8**)
Math 24:9; Marko 13:9, 13; Luka 21:12, 16-17 (mateso ya waamini & kuuawa)	Inalingana na muhuri 5th (**6:7-10**)
Math 24:29; Marko 13:24-25; Luka 21:25 (ishara angani & mbinguni)	Inalingana na muhuri 6th (**6:12-14**)

Ingawa matukio ya mihuri minne ya kwanza yaweza kutokea moja baada ya lingine, bila shaka yote yangetokea kwa wakati mmoja kwakuwa: (1) muhuri wa nne unaonekana kutolea maelezo mafupi ya muhuri mitatu ya kwanza; na (2) **Ezek 14:12-21; Zek 6:1-8;** na hotuba ya Mlimani (**Math 24:6-13; Marko 13:7-9; Luka 21:9-12**), ambayo **Ufu 6:1-8** imejengea msingi, kuyaonyesha matukio hayo kama yanayotokea kwa wakati mmoja.

Kama vile **Ufunuo 4-5** ilivyoibua swali "Ni nani Bwana wa kweli wa ulimwengu huu?" Kristo kukipokea kitabu (gombo) na kuivunjaa mihuri yake kunajibu swali hilo. Kwa kukipokea kitabu na kuivunja mihuri yake, Kristo anadhihirisha kwamba Yeye ndiye Bwana atawalaye, akiutendea kazi utawala wakw juu ya ulimwengu na chochote kile kinachotokea ndani yake.[34] Kristo huyu ndiye sababu ya mwisho ya hukumu, inaonekana kwenye ukweli kwamba Kristo kuzivunja mihuri ni msingi wa maagizo kwa wapanda farasi " njoo" (**Ufu 6:1, 3, 5, 7**). Vifungu vikuu vya Agano la Kale nyuma ya **Ufu 6:1-8** pia vinaye Mungu kama sababu ya mwisho ya hukumu (angalia **Zek 6:1-8; Ezek 14:12-21**). Hili ni la muhimu kwa kile kinachofuata kwenye kitabu chote, kwa kuwa mengi ya kile kinachofuata ni maelezo ya ukatili, mapigo, na kifo. Hata kwenye mapigo, Wakristo ni lazima wawe na uwezo wa kutambua kwamba Kristo ni mtawala.[35] Hivyo Kristo wakati wote ndiye mtawala awapaye Wakristo ujasiri na tumaini. Majaribu kama haya, huthibitisha, na kuikamilisha imani ya waamini kwa kitambo, wakati uo huo, yakitenda kama adhabu kwa wale ambao wanamkataa Kristo na kulitesa Kanisa.

2. <u>Aliyempanda Farasi mweupe (**Ufu 6:1-2**).</u> Utambulisho wa mpanda farasi wa kwanza umesababisha mjadala mkubwa. Suala ni ama ni mpanda Farasi mwenye matokeo chanya au hasi.

> a. *Aliyempanda Farasi mweupe kama chanya.* "Baadhi ya wachambuzi [e.g., Irenaeus 1885: 4.21.3; Hendriksen 1982: 93-96] wamemtambulisha mpanda Farasi huyu kama Yesu Kristo, lakini tatizo la mtazamo huu ni kwamba, kwa kuwa Mwanakondoo ndiye afunguaye mihuri mbinguni, asingeweza kuwa mmoja wa wapanda Farasi. Zaidi ya hayo, kitheolojia

[34] **Ufu 1:5, 13-14; 2:26-28; 3:21; 5:1-4** inaonyesha kwamba Kristo tayari alishaanza ufalme wake wa Kimasihi. Angalia pia **Math 28:18; Mdo 2:32-36; Efe 1:18-22** ambavyo vyote vinathibitisha kwamba anatawala sasa kama mfalme wa Kimasihi.

[35] Mamlaka ya wapanda farasi wane yapo kwenye muundo wa "uungu batili, i.e., *"akapewa yeye"* (**Ufu 6:2**); *"alipewa"* (**Ufu 6:4**); *"walipewa mamlaka"* (**Ufu 6:8**). Nguvu walizopewa wapanda farasi siyo tu walipewa na mamlaka ya mbinguni lakini yamewekwa chini ya ukomo wa Kimungu ulioamriwa (angalia **Ufu 6:6, 8**).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

isingewezekana kuwa na malaika, kiumbe, kumwagiza Kristo, muumbaji, kufanya vitu (6:1)." (Ngundu 2006: 1557)

Ya pili "mpanda farasi mweupe kama nguvu chanya" mtazamo huu una nguvu kuliko kumwona mpanda farasi wa kwanza kama Kristo mwenyewe. Wachambuzi mbalimbali ambao humtazama mpanda farasi wa kwanza kama nguvu chanya huhitimisha, "Mpanda farasi siyo Kristo mwenyewe lakini ni ishara ya kuitangaza injili ya Kristo kwenye ulimwengu wote" (Ladd 1972: 99; angalia pia Milligan 1896: 89-90). Mtazamo huu umejikita kwenye ukweli kwamba, mara 14 umetumika penginepo kwenye kitabu, "rangi nyeupe wakati wote ni ishara ya Kristo, au kitu kinachofuatana na Kristo, au ushindi wa kiroho" (Ladd 1972: 98). Pia, "muundo wa mawazo hayo ya msingi umeonekana kwenye hotuba ya Mlimani na kwenye Ufunuo: wakati wa taabu za awali zilizowekewa alama kwa uovu kwenye jamii ya wanadamu na kwenye asili (mihuri saba) . . . hata hivyo, kwenye kipindi cha awali cha uovu ipo kumbukumbu chanya . . . 'injili lazima kwanza ihubiriwe kwa mataifa yote' (Marko 13:10)." (Ibid.: 98-99) Zaidi ya hayo, upinde mara nyingi hutumiwa kama ishara ya ushindi wa kiungu (**Zab 45:4-5; Isa 41:2; 49:2-3; Hab 3:9, 13; Zek 9:13**), na penginepo kwenye Ufunuo, Kristo mahali pengine ameonekana akivaa taji (**Ufu 14:14; 19:12**) na "kushinda" (**Ufu 3:21; 5:5; 17:14**)

b. *Aliyempanda Farasi mweupe kama hasi.* Wachambuzi wengine hushikilia kwamba ni zaidi bila shaka kuwa mpanda Farasi mweupe, kama walivyo wapanda Farasi wengine juu ya Farasi tatu, ni ishara ya mpinga Kristo na nguvu ya uovu. Hta hivyo kumbukumbu ya Mpinga Kristo binafsi, imeonekana kuwa tatizo. "Kama pamoja na usawa binafsi wa mpanda farasi wa kwanza pamoja na Kristo, kujumuishwa kwa Mpinga Kristo hapa kunavunja mpangilio wa sababu ya vinginevyo kutokuwa binafsi ambako kumetajwa wakati wa tukio hili kwenye Ufu. 6" (Smalley 2005: 150).

Kwa hiyo, mtazamo wa "mpanda Farasi mweupe kama mwovu" ni wenye nguvu sana wakati unapomtambulisha mpanda Farasi kama Makristo wa uongo, nabii wa uongo, au nguvu ya uovu kwa ujumla, kuliko kama Mpinga Kristo *hasa au pekee*. Alan Johnson ameitaja hoja kuu kwa fadhila ya nafasi hiyo: "Uungwaji mkono kwa tambulisho wa Farasi mweupe pamoja na Mpinga Kristo na nguvu zake ni sawa na Farasi wengine watatu, ambao ni vyombo au zana za hukumu. Kumbukumbu kwenye 19:11-16 kwa mwenye kumpanda farasi mweupe kama 'Mwaminifu na Mkweli' amna ambaye inasemekana kwamba 'kwa haki alihukumu na kufanya vita' yaweza kusimama kinyume kwa mpanda farasi kwenye 6:2 ambaye siyo mwaminifu au mkweli na ambaye hufanya vita kwa ushindi usiokuwa wa haki. . . . Tena, 'upinde au mshale' kwa wingi ungekuwa kwa asili umeunganishwa na maadui wa watu wa Mungu (Ezek 39:3; cf. Ufu. 20:7-8). Hatimaye, Mfanano wa Hotuba ya Mlimani inaonyesha kwamba matukio ya kwanza yaliyotajwa ni kuinuka kwa 'makristo wa uongo na manabii wa uongo' (Math 24:24)." (Johnson 1981: 473)

Kwa nyongeza, farasi wanne wanaovuta magari ya **Zek 6:1-8** kwa wazi ni chanzo cha Agano la Kale nyuma ya wapanda Farsi wanne wa **Ufu 6:1-8**. Kwenye kitabu cha Zekaria, farasi wanne wanaokokota magari wote ni wa asili ileile. Zaidi, mpanda Farasi wa nne ("Kifo," na "Kuzimu" zinamfuata yeye, **Ufu 6:7-8**) anaonekana kuwa matokeo au ufupisho wa shughuli za mpanda Farasi aliyetangulia. Ikiwa ni hivyo, basi mpanda Farasi wa kwanza, kama walivyo wale wengine watatu, lazima wawe waovu. Kwa hiyo, kwa usawa, "mpanda farasi mweupe kama mwovu" anaonekana kuwa nafasi yenye nguvu.

3. <u>Waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu (**Ufu 6:9-11**)</u>. Kama pamoja na mihuri ya kwanza minne, waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu (muhuri wa tano) ni tukio ambalo linahusika na kipindi chote mpaka kurudi kwa Kristo. Kifungu hiki ni cha umuhimu mkubwa kwenye uelewa wa kitabu, kwa kuwa kitabu chote, kwenye kiini, kinawakilisha na kusimulia majibu kwa maombi ya waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu kwenye **Ufu 6:10**.[36] Kwa upeo huu, ni muhimu kuangalia ni jinsi gani waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu wanavyotenganisha asili ya mkanganyiko wa ushindi wa waamini juu ya Shetani, "mnyama", nguvu ya uovu, na ulimwengu. Asili ya mkanganyiko au makabiliano yenye umaizi ya ushindi wa waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu umeelezewa kwa kina na Bauckham: "Wakati wanyama wanapowaua mashahidi wa neno la Mungu, ni nani hasa mshindi? Jibu, kwenye Ufunuo,

[36] Maombi ya mashahidi, *"Mpaka lini, Ee Bwana?"* yanafanana na kilio cha Habakuki (**Hab 1:2-4**) wakati watu wake mwenyewe walipokuwa wakikandamizwa, haki ilipotoshwa, na Israeli walikabiliwa na nguvu ya Babeli.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

linategemea juu ya ama mtu analiona jambo hili kutoka kwenye mtazamo wa kidunia au wa mbinguni. Kutoka kwenye mtazamo wa kidunia ni wazi kwamba mnyama amewashinda waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu (11:7; 13:7). . . . Hata hivyo maono ya kimafunuo, yanafunua kwamba kutokana na mtazamo wa *mbinguni* mambo huonekana tofauti sana. Kutokana na mtazamo huu waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu ni washindi halisi. Kuwa mwaninifu kuuchukua ushuhuda wa Yesu hata kwenye upeo wa kufa siyo kuwa mwathirika asiye na msaada wa mnyama, lakini ni kuchukua uwanda kinyume chake na kushinda. Yohana anaweza kuuona ushindi wa waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu tu kwenye eneo lililopo mbinguni, kwa sababu linahitaji mtazamo wa mbinguni—ulioanzishwa wakati Mwanakondoo kwa mara ya kwanza alipoonekana ameshinda mbele ya kiti cha enzi cha Mungu (5:6)—kuufanya ushindi wao uonekane, lakini mtazamo wa mbinguni unapelekea ushindi juu ya uso wan chi wakati wa parousia (19:11-21). . . . Ushindi wa waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu siyo kwa kuteswa na kufa kwao kama huko, lakini kwa *ushuhuda* wao wa uaminifu hata kwenye upeo wa kifo (cf. 12:11). Ushuhuda wao kwenye kweli unashinda dhidi ya uongo na udanganyifu wa shetani na mnyama. Kwa wale walioukataa ushuhuda huu, utakuwa ushahidi wa kisheria *kinyume* chao, kupata hukumu yao. Hili jukumu hasi la mashahidi pia uwezekano chanya: watu hawa waweza kusinda kutoka kwenye udanganyifu kuwa kweli." (Bauckham 1993a: 235, 237)

4. Maombi ya waliouawa kwa ajili yaneno la Mungu na majibu yake (**Ufu 6:10-17**). Maombi ya waliouawa na matokeo yake ya pili ni ya kipekee kwenye Ufunuo: "Kwenye kitabu kilichofungwa kwa kumbukumbu ya kuabudu, kufunguliwa kwa muhuri wa tano kwenye [**Ufu 6:9-11**] imebeba mfano tu wa sala na maombi na majibu yake" (Heil 1993: 220). Kama vile, sala hii "huonyesha maombi ya mtakatifu [kwenye **Ufu 5:8**]," na "heshima ya kufanikiwa kwa mazingra, maombi haya ya nafsi yanaandaa ajenda kwa kumbukumbu ya kitabu" (Ibid.: 242).

Majibu ya haraka ya Mungu kwenye **Ufu 6:11** kuwaonya "watumishi" kwa yeyote aliyeandikiwa kitabu (**Ufu 1:1**) kwamba kama "watumishi wenzao" (**6:11**) na ndugu wa nafsi chini ya madhabahu, wangetarajia kuuawa kwa ajili ya neno la Mungu na ushuhuda wa Yesu Kristo. Kwa wakati uo huo, "wamehakikishiwa kwamba Mungu hatimaye atahukumu na kuwathibitisha, ili kwamba waweze kutegemea kushiriki kwenye vazi jeupe na pumziko la mbinguni la nafsi ambazo ziliwatangulia." (Ibid.: 221-22)

Kuhukumiwa kwa *"wale wakaao juu ya uso wa nchi"* na kuthibitishwa kwa Kanisa, ambako kunajibu maombi ya waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu, wanaonekana kwenye maeneo mbali mbali kwenye kumbukumbu ya kitabu. Kwenye **Ufunuo 6** kwenyewe, majibu ya maombi ya **6:10** yanaonekana kwa wazi kwenye **6:12-17**. Mazingira ya maombi ya waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu ya **6:10**, na Mungu kuwaambia waliouawa kwa ajili ya neno lake kusubiri mpaka idadi ya watumishi wenzao watakaouawa kama wao ikamilike (**6:11**), inaonyesha kwamba kile kilichoonekana kwenye **6:12-17** lazima kiwe ni hukumu ya mwisho.[37] "Kifungu cha janga kwenye 6:12-17 kinadhihirisha kwamba mateso kwa Wakristo wote ambao wanapaswa kuteswa hatimaye imehitimisha mwendo wake na kwamba wale wote waliosalia ni kutekeleza adhabu ya mwisho juu ya watesi, ambao watahitimisha andiko la mwisho la historia ya ulimwengu. Hali kadhalika, kifungu hiki hakitajihusisha na hukumu ya kabla ya parousia ya wasioamini wakati wa kuongezwa kipindi cha dhiki, kwa kuwa bado hawajamaliza kuwatesa watakatifu kwa wakati huo." (Beale 1999: 396)

Kwa sababu ya asili ya mfanano wa hatua kwa hatua wa kitabu, kila sehemu ya hukumu juu ya wasiomcha Mungu na kuthibitishwa kwa waamini ni majibu ya maombi ya waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu kwenye **Ufu 6:10**. **Ufu 7:9** inaonyesha jibu kwa maombi yao, kama inavyoonekana *"mkutano mkubwa sana ambao hakuna mtu awezaye kuuhesabu . . .wamesimama mbele za Mwanakondoo . . .na wana matawi ya mitende mikononi mwao,wakilia kwa sauti kuu wakisema,Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwanakondoo.'"*[38] **Ufu 14:3** inawaonyesha 144,000 wakiimba wimbo mpya mbele ya kiti cha enzi. **Ufu 15:2-4** sambamba nayo inawaonyesha *"wale ambao walikuwa*

[37] Wanatheolojia, kwa upande mwingine, wanasema ukweli kwamba watu wanasema milima, *"Tuangukie"* (**Ufu 6:16**) kama ushahidi kwamba "kifungu hiki hakizungumzii juu ya Mwisho wa Ulimwengu, lakini *Mwisho wa Israeli* mwaka BK 70" (Chilton 1987: 198). Sababu ni kwamba mazingira halisi ya maelezo ni unabii wa Hosea kinyume na Israeli (**Hos 10:8**) ambayo Yesu aliyanukuu kwenye njia akiwa njiani kwenda kusulubiwa (**Luka 23:28-30**), hasa inazungumzia kuja kwa uharibifu juu ya Yerusalemu ambo ulitokea mwaka BK 70 (Ibid.: 198-99).

[38] Kwenye **Ufu 6:11**, Mungu aliwaambia wale waliochinjwa kwa ajili ya neno la Mungu wastarehe mpaka itakapotimia hesabu ya wajoli wao na ndugu zao watakaouawa vile vile kama wao. Hii ndiyo hali halisi inayojihusisha na **Ufunuo 7**.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

washinda juu ya mnyama . . . wakisimama juu ya bahari ya kioo, wenye vinubi vya Mungu, nao wauimba wimbo wa Musa . . . na wimbo wa Mwanakondoo." Picha zote hizi zinaonyesha kuthibitishwa kwa watakatifu kama majibu ya maombi ya wale waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu.

Kwenye **Ufu 16:3-6**, maombi yanaonekana kujibiwa kwenye hukumu ya wakaao juu ya uso wa ncho. Maombi ya kumtaka Mungu kulipa kisasi "cha damu yetu" yameelezewa moja kwa moja kwa: **Ufu 16:34** yanaeleza kwamba kitasa cha pili na cha tatu kilichomwagwa na Malaika kuigeuza bahari, mito, na chemchemi kuwa "damu." **Ufu 16:6** inahitimisha, *"Kwa kuwa walimwaga damu ya watakatifu na ya manabii, Nawe umewapa damu wainywe; nao wamestahili."* Vivyo hivyo, kwenye hukumu ya Babeli (**Ufu 18:21-24**), mstari wa 24 unasema kwamba *"Na ndani yake ilionekana damu ya manabii, na ya watakatifu, na ya wale wote waliouawa juu ya nchi."* Wakati wanashangilia juu ya hukumu ya Babeli, mkutano ulioko mbinguni hasa unafurahi juu ya ukweli kwamba Mungu *"kuilipiza damu ya watumwa Wake mkononi mwake"* (**Ufu 19:2**). Haya ni majibu ya moja kwa moja ya maombi ya waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu kwenye **6:10** ambayo kwayo waliuliza *"Hata lini kutokuhukumu, . . . wala kuipatia haki damu yetu kwa hao wakaao juu ya nchi?"* Neno la Kigiriki kwa "kulipiza kisasi" (*ekdike*ō) limeonekana kwenye Ufunuo tu **6:10** na **19:2**, hivyo kuunganisha vifungu viwili. **Ufu 20:4-6** kisha kusisitiza uthibitisho chanya kuongezeka kwa wale ambao waliuawa kwa ajili ya neno la Kristo.

5. <u>Dhiki Kuu (**Ufu 7:14**).</u> Hili ni eneo pekee kwenye Biblia ambapo neno *"dhiki kuu"* limetokea. Kwenye Hotuba ya Mlimani (**Math 24:21**) Yesu alizungumzia *"Dhiki Kuu"* (bila kuwa na makala fafanuzi "the") kwenye kuunganishwa na kuangamizwa kwa Yerusalemu mwaka BK 70. Picha imechukuliwa kutoka D**an 12:1** ambayo inazungumzia ju ya *"kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo."* Wakati mwingine pekee neno *"Dhiki Kuu"* lilitokea ni kwenye **Ufu 2:22** wakati Kristo alipoliambia Kanisa lililokuwa Thiatira kwamba atawatupa wale watakaozini pamoja na Yezebeli kwenye *"Dhiki Kuu."* Matumizi ya makala ("the") kwenye **7:14** wanaeleza kwamba hizi ni taabu za nyakati za mwisho au dhiki iliyotabiriwa na Danieli.

Ingawa msisitizo waweza kuwa juu ya vita ya mwisho itakayofanywa na joka na wafuasi wake kinyume cha Kanisa, taabu hizi za nyakati za mwisho zitakazolitesa Kanisa siyo za ukomo wa kipindi kifupi kabla ya *parousia*. "'Matatizo makuu' yatakayowapata waliokombolewa hayatatokea kipekee mwishoni mwa historia. Nyakati za hukumu tayari zilishaanza kwenye siku za Yohana, na zaweza kuwapata walioamini sawa sawa na wasioamini (cf. 2.22) kwa wakati wowote, mpaka mwisho wa nyakati. Ni uyakinifu uliopo sasa, na siyo uhakika wa wakati ujao, ambao waweza kusadiki aina ya mateso (2.2-3), njaa (6.5-6), kufungwa gerezani (2.10) na hata kufa (2.13; 6.9). . . . Maono ya Kanisa ya Ufu. 7:9-17 yanaelezea kuambatana kwa waaminifu ambao watajumuisha waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu, lakini kuwakumbatia waamini wote." (Smalley 2005: 196)

Hili pia limeelezwa na **Ufu 1:9** na mazingira mapana ya uelewa wa Agano Jipya wa dhiki na mateso. Kwenye **Ufu 1:9** pale Yohana anapojiita mwenyewe *"ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi <u>kwenye mateso</u> na ufalme."* Kwa maneno mengine, Yohana anaamini kwamba mateso au dhiki tayari iliisha kuanza kwenye siku zake mwenyewe: "Kutoka msimamo wa ushindi wa Kanisa mateso yote ya wakati huu yameandaliwa kwenye nuru ya [Dhiki Kuu] ambayo tayari ilishafunguliwa." (Schlier 1965: 143-45) Hili linaeleza asili ya "tayari, lakini bado" ya dhiki, sawa na lile la ufalme: kwa kuwa tupo kwenye "siku za mwisho" kama matokeo ya sadaka ya upatanisho ya Yesu, dhiki tayari iliishaanza; hata hivyo, tunaweza kutarajia muundo uliokithiri wa dhiki hiyo muda mfupi kabla ya Kristo kurudi.

6. <u>"Wamefua mavazi yao na kuyafanya meupe" (**Ufu 7:14**).</u> "Kuwekwa kwenye damu huifanya damu kuwa chombo ambacho kwacho weupe huchukua nafasi" (Porter 1999: 158). Vifungu vingine kwenye Agano Jipya hudhihirisha tofauti kubwa ya mtazamo wa dhiki na mateso ambayo ni ya wazi hapa kuelezea ni jinsi gani damu ya Yesu inavyomfanya mtu kuwa mweupe. Kwenye **Wakol 1:24** Paulo anasema kwambamateso yake mwenyewe kwa niaba ya Kanisa ni *"nayatimiliza yale yaliyopungua kwenye mateso ya Kristo."* Kwenye **2 Wakor 4:8-12** pia alieleza kwamba mateso ya walioamini ni *"twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu"* ili kwamba, kimkanganyiko, *"ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu ya kufa."* Vivyo hivyo, kwenye **Ufu 7:14** na penginepo kwenye Ufunuo, wale ambao wamepitia dhiki, mateso, na kifo kwa ajili ya Kristo wamedhihirisha utambulisho wao wa msingi pamoja naye. Wamevumilia ushuhuda, kwa maneno na kwenye miili yao wenyewe, kwa mateso na kifo ambavyo alivistahimili. Wamedhihirisha kwamba kwa uaminifu kupitia kwenye mateso,

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kwamba imani yao wenyewe ilikuwa dhahiri. Mateso yao yaliwatakasa. Wamefananishwa na mfano wa Kristo (**Rum 8:29**), kwa sababu, kama Kristo, wamekuwa *"watiifu hata mauti"* (**Wafil 2:8**). Kwa sababu Kristo ni haki yote, kujitoa kikamilifu kwa Kristo ni haki na matokeo yake ni vazi lililo safi kabisa (angalia **Ufu 19:8**).

Sawa na hilo, **Ufu 12:11** unaeleza kwamba *"Nao wakamshinda yeye [Shetani] kwa damu ya Mwanakondoo, na kwa neno la ushuhuda waoambao hawakupenda maisha yao hata kufa."* Bauckham anaeleza, "Ushindi haukuhusika tu kwenye kifo kama hiki, lakini kwenye uaminifu wa ushuhuda wao hata kufa (cf. 2:13; 11:7), kudumisha ushuhuda wa Yesu (12:7; 19:10), kuifuata njia ya Yesu ambayo Ufunuo1:5 unaiita 'shahidi mwaminifu'. Thamani ya ushuhuda wao umeigwa au kunakiliwa kutoka hapa, ni kwa kudumisha ushuhuda wake, na hivyo ushindi wa uaminifu wao kama vile kifo kilivyonakiliwa kutoka kwenye ushindi wake." (Bauckham 1993a: 228-29) Tena tunaona mkanganyiko wa mtazamo wa Ufunuo wa kushinda na ushindi. Kama vile Yesu Mwanakondoo alivyoshinda kupitia sadaka ya kifo chake (**Ufu 5:6, 9**), hivyo ushindi wa watu wa Mungu ni wa aina iyo hiyo kama wa Mwanakondoo: kuwa mwaminifu hata kuuawa kwa ajili ya neno la Mungu.

Muunganiko pamoja na **Ufunuo 12** pia unatuonyesha jinsi gani Yohana alivyoliona Kanisa kana Israeli mpya, ya kweli. Tunaliona hili angalau kwa njia mbili. Kwanza, mavazi meupe yaliyofuliwa ya **Ufu 7:14** sawa na **Kut 19:10, 14** pale Wana wa Israeli walipotakiwa *"kuyafua mavazi yao"* kuandaa uwepo wa Mungu juu ya Mlima Sinai. Kwenye maono ya Yohana, "mkutano uliovalia mavazi meupe yaliyofuliwa walionekana kama kusanyiko la kweli la Mungu sawa na Israeli kwenye Mlima wa Sinai" (Ulfgard 1989: 84). Pili, **Ufu 12:6, 14** inamzungumzia mwanamke anayekimbilia "jangwani" mahali ambapo "alinawiri au alistawi." Hili linatumbusha kutanga tanga kwa Israeli jangwani wakati Mungu alipoliendeleza taifa kwa miaka arobaini kufuatia safari. Sikukuu ya vibanda kusherehekea tukio hilo (**Kut 23:16; 34:22; Lawi 23:33-43; Hes 29:12-38; Kumb 16:13-15**). Kwenye **Ufu 7:9**, mkutano mkubwa unaonekana ukisimama mbele ya Mwanakondoo wakiwa na matawi ya mitende mikononi mwao. Matawi ya Mitende hasa yaliambatana na sikukuu ya vibanda (**Lawi 23:40**). Kama vile matawi ya itende yalivyotumika kwenye sherehe ya vibanda kusherehekea ulinzi na uwepo wa Mungu miongoni mwa watu wake jangwani, hivyo "kwa Wakristo katika kuitafsiri tena Biblia huwaambia wasomaji /wasikilizaji kwamba wanashiriki mateso yale yale pamoja na Kristo" (Ibid.: 90). Kutolewa kwa muunganiko huu, mkutano mkubwa ukipaza sauti yake *"Wokovu una Mungu wetu"* (**Ufu 7:10**) yaweza kuonekana kwenye **Zab 118:25**. Zaburi hii ilikuwa ikikaririwa kwenye sherehe ya vibanda, na *lulav* (matawi ya mitende) yalipungwa kwa wakati huo (Ibid.: 91).[39]

E. ***Ufu 8:6-11:19: Tarumbeta saba***

Kwenye tarumbeta za kwanza sita (**Ufu 8:6-9:21**), Mungu alijibu maombi ya watakatifu kwenye **Ufu 6:10** kwa kuwatumia malaika kuleta hukumu juu ya watesi wa Kanisa. Kwenye **10:111** Yohana anaagizwa tena kutoa unabii kuhusu mpango wa Mungu kuleta hitimisho la ufalme. Kwenye **11:1-13** Amri za Mungu kuwahakikishia uwepo Wake pamoja na watu Wake na mafanikio ya ushuhuda wao, bila kujali mateso yao. Kwenye tarumbeta ya saba (**11:14-19**), Mungu analeta hukumu ya mwisho na kuanzisha ufalme wa milele.[40]

1. Hukumu ya Tarumbeta (**Ufu 8:6-9:21; 11:15-19**). Kwenye mtindo wa unabii wa kawaida, kwenye Agano la Kale mapigo ya kutoka yalikuwa yamepanuliwa kutumika kwa Israeli kwenye nchi yao (**Amos 4:10**) na kwa Israeli wakiwa utumwani (**Kumb 28:27-60**). Sasa yanatumika ulimwenguni kote:

Tarumbeta ya 1st (mvua ya mawe) (**8:7**)	Inalingana na pigo la 7th (**Kut 9:22-25**)
Tarumbeta ya 2nd na 3rd (maji kuwa damu) (**8:8-11**)	Inalingana na pigo la 1st (**Kut 7:20-25**)
Tarumbeta ya 4th (Giza) (**8:12**)	Inalingana na pigo la 9th (**Kut 10:21-23**)
Tarumbeta ya 5th (Nzige) (**9:1-11**)	Inalingana na pigo la 8th (**Kut 10:12-15**)

[39] Mwunganisho huu umeimarishwa na ukweli kwamba wakati Yesu alipoingia Yerusalemu kwa mara ya mwisho, watu *"walichukua matawi ya mitende na kwenda kumlaki Yeye"* (**Yoh 12:13**). Kwenye **Ufu 7:9-10** mkutano mkubwa pia *"umesimama . . . mbele ya Mwanakondoo"* wakiwa na matawi ya mitende mikononi mwao. Neno la Kigiriki kwa "mti wa mtende" ni *phoinix*. Kwenye Agano Jipya limeonekana tu kwenye **Yoh 12:13** na **Ufu 7:9**.

[40] "Mashahidi wawili" (**Ufu 11:3-2**) tayari tumekwisha kuwazungumzia hapo juu kwenye mwunganiko pamoja na Kanisa kwenye Ufunuo. TaWarumibeta ya saba ilijadiliwa kwenye mwunganiko pamoja na muundo sambamba hatua kwa hatua wa kitabu. Wazee ishirini na wane wamejadiliwa kwenye mwunganiko pamoja na **Ufu 4:1-5:14**. Kwa hiyo, havitajadiliwa kwa kina chochote hapa.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Tarumbeta pia zinafanana na hukumu ya kutoka kwenye haya, kama vile Wana wa Israeli hawakupata madhara kwa mapigo, lakini ni Wamisri tu (**Kut 7:18, 21, 24; 8:3-4, 8-9, 11-12, 21-23, 29-31; 9:3-7, 10-11, 14, 23-26; 11:4-7**), hivyo Wakristo, lakini siyo wasioamini, wanalindwa kutokana na hukumu ya tarumbeta (**Ufu 9:4**). Kwenye Ufunuo hili halimaanishi kwamba hukumu hizi hazitakuwa na madhara kwa Wakristo kwa njia iwayo yote ile. Wakristo watateseka kimwili kwa njia zile zile kama wasio-Wakristo watakavyoteseka wakati wa hukumu hizo, lakini msingi na asili ya hukumu ni tofauti kati ya Wakristo na wale wasio-Wakristo: "Hukumu za matarumbeta ni hukumu juu ya ulimwengu. Kanisa, katika ukweli wake, laweza kuteseka kwa mapigo hayo. Yaweza kuwa sehemu majaribu yake kwa kuwa limechanganyikana na ulimwengu wakati wa safari yake hapoa juu ya uso wa nchi. Hata hivyo, majaribu siyo hukumu. Kwa watoto wa Mungu ni kurudiwa na mkono wa Baba. Katikati ya haya Kanisa lipo salama, na italisaidia kukua kwa ajili ya utimilifu wa utukufu wa urithi wake mbinguni." (Milligan 1896: 155-56)[41]

Tarumbeta sita za kwanza zinafanana na mihuri mitano ya kwanza. Hata hivyo, malengo ni tofauti: "pale ambapo mihuri mitano ya kwanaza ililenga kwenye majaribu ambayo waamini ni lazima wayapitie, sasa malengo kwenye tarumbeta sita za kwanza ni juu ya hukumu ambayo wasioamini, wote ndani na nje ya Kanisa linaloonekana, lazima kuyavumilia" (Beale 1999: 472-73). Tarumbeta ya saba ni sawa na muhuri ya sita na saba. Yote yanazungumzia *parousia* ambayo itakuja pamoja na hukumu ya mwisho na mwanzo wa ufalme uliokamilika.

a. *"Nyota ilizoanguka" ilipewa funguo za "shimo lisilokuwa na mwisho" au "kuzimu" (**Ufu 9:1-2; 11; 11:7; 17:8; 20:1, 3**).* Kwenye kitabu cha Ufunuo, picha ya "kuzimu" au "shimo lisilikuwa na mwisho" imetokea mara saba (**Ufu 9:1, 2, 11; 11:7; 17:8; 20:1, 3**). Ni nyumba au makazi ya maroho machafu [maroho maovu] na mfalme wao (**9:1-11**); mnyama atakokea huko (**11:7; 17:8**); ndiko alikofungwa Shetani (**20:1-3**; angalia pia **Luka 8:31; 2 Pet 2:4**). *"Nyota iliyotoka mbinguni ambayo ilianguka juu ya nchi"* (**9:1**) inalingana na Shetani *"kutupwa hata nchi"* (**12:9**), na maelezo ya Yesu, *"Nilimwona Shetani akianguka kutoka mbinguni kama umeme"* (**Luka 10:18**). "Nyota hii iliyoanguka' ni kinyume na Mwenzake ambaye ni 'nyota yenye kung'aa asubuhi [**Ufu 22:16**],' na ambaye 'anazo funguo za mauti na kuzimu [**Ufu 1:18**]'" (Milligan 1896: 148). Malaika aliyeanguka "alipewa" funguo kuwafungulia nzige kutoka kuzimu. Huu ni "uungu batili au bandia." Kwa maneno mengine, "ni kwa ruhusa ya Mungu pekee [roho waovu] wanaweza kufunguliwa kuleta uharibifu juu ya nchi (9:1-11; 20:1-3)" (Moo 2009: 157n.22).

Kufunguliwa kwa kuzimu kwenye **Ufu 9:2** kwaweza kuwa, makabiliano yenye umaizi, kuonyesha au kudhihirisha uangalifu na "kufungwa kwa Shetani" kwenye **Ufu 20:1-3**, siyo na "kufunguliwa" au "kuachiliwa" kwa Shetani kwenye **20:3, 7**. Sabau ni kwamba matukio ya **Ufu 9:1-12** siyo matukio yatakayotukia tu mara kabla ya *parousia* lakini kwa wazi ni ya awali. Lililo muhimu sana kitheolojia ni kwamba mapepo ambao walifunguliwa kwenye **9:1** hawatawatesa waamini bali wale tu "ambao hawatakuwa na muhuri wa Mungu juu ya vipaji vya nyuso zao" (**9:4**). Sawa na hili, "kufungwa kwa 'kuzimu' kwenye 20:1–3 kwaweza kuwa au kuleta wazo kwamba Shetani na wafuasi wake hawatafunguliwa kuwadanganya wale 'ambao hawajapokea chapa [ya mnyama] juu ya vipaji vya nyuso zao [**20:4**].' 9:1-10 na 20:1-3 ni kulinganisha na kuonyesha wale ambao Shetani anaruhusiwa kuwadanganya na wale ambao haruhusiwi kuwadanganya." (Beale 1999: 986)

b. *Nzige kutoka kwenye shimo lisilokuwa na mwisho (**Ufu 9:1-12**).* "Nzige" ni mapepo kwa tabia zao. Hili lilidhihirishwa na ukweli kwamba wanaishi na kuibuka kutoka kuzimu kama afanyavyo mnyama (angalia **Ufu 11:7; 17:8**); mfalme wao ni"malaika wa kuzimu" ambao majina yao yanamaanisha "uharibifu" (Abadoni) au "mharibifu" (Apollyon; **Rev 9:11**); na matendo yao ni kuwatesa na kuwaumiza watu (**Ufu 9:5, 10**).

[41] Hili ni ajabu lile lile tulililoliona kwenye **Ufu 7:14**. Dhiki na mateso kwa kujaribiwa kwa Kristo, kunathibitisha, na kutakasa utambulisho wetu pamoja na Kristo kwenye mateso na kifo chake mwenyewe. Hiki hasa ndicho kilichotabiriwa na Kristo kwenye Hotuba ya Mlimani na kwenye vifungu hivi kama **Math 10:16-39** na **Yoh 15:18-25**. Waamini wa Mpito, ambao hufikiri kwamba kanisa litanyakuliwa kabla ya matukio yoyote haya kutokea na litakuwa na "wataketi viti vya mbele" kuyatazama mateso ya wengine, halionekani kuwa na wazo lolote la utambulisho wa haraka wa Wakristo pamoja na Kristo kwenye mateso yake au asili ya kisaikolojia ya ushindi wa sehemu mbili wa Kristo na wetu.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Wakati nzige wanafanana na pigo la nane la Wamisri, picha ya msingi inaonekana kuchukuliwa kutoka kwenye kitabu cha Yoeli. Yoeli anazungumzia juu ya pigo kuu la nzige (**Yoeli 1:4**). Nzige kwenye Yoeli wanao mwonekano "kama mwonekano wa farasi, na kama farasi wa vita" (**Yoeli 2:4**; linganisha na **Ufu 9:7**). Walikuja na sauti za magari ya vita (**Yoeli 2:5**; linganisha na **Ufu 9:9**). Yanafuatana na jua, mwezi na nyota kutiwa giza (**Yoeli 2:10**; linganisha **Ufu 9:2**) na ujumbe wa kuja kwa siku ya Bwana na hukumu inayofuatana nayo (**Yoeli 2:1, 11, 30-32**). "Nzige" wa kipepo hawaruhusiwi kuwadhuru waamini, kwa kuwa waamini wamefungwa kwa muhuri **Ufu 9:4**). Hili linathibitisha mamlaka ya milele ya Kristo juu ya Shetani na uovu wote ambao kitabu cha Ufunuo kimeuona.

Kwa kuwa "miezi mitano" ya **Ufu 9:5, 10** haipaswi kuchukuliwa kiuhalisia, kama ilivyojadiliwa mapema, nyingi kama siyo namba zote na vipindi vya nyakati penginepo kwenye kitabu cha Ufunuo siyo halisi. "Zaidi ni "kwenye makubaliano na mtindo wa Ufunuo kuheshimu hasa vipindi vya nyakati kama vile inavyoashiria kwamba hukumu ina ukomo wa ufafanuzi" (Milligan 1896: 147).

c. *Mto Frati (**Ufu 9:13-14; angalia pia 16:12**).* "Kuufanya kuwa halisi" mto wa Frati ungeondoka kutoka kuwa kanuni iliyo nzuri ya ufafanuzi wakati inapojihusisha na kitabu cha maono na mifano. Mto Frati "ni ishara tu ya hukumu; na malaika wanne ambao walikuwa wamefungwa huko, na sasa wamefunguliwa, ni ishara—nne kuwa namba ya ulimwengu—ambayo hukumu inaizungumzia, ingawa itaathiri moja ya tatu ya watu, kuwafikia watu juu ya uso wote wa dunia." (Milligan 1896: 151) Namba "nne" kama inavyouonyesha ulimwengu inaonekana kwenye ukweli kwamba nchi inasemekana kuwa "pembe nne" (**Ufu 7:1; 20:8)** na "pepo nne" (**Ufu 7:1**). Kumbukumbu ya Frati inashirikisha kitasa cha sita, pale ambapo Frati imetajwa tena (angalia mjadala hapo chini kwenye kuunganishwa na **Ufu 16:12**). Muunganiko huo unapendekeza kwamba upo uwezekano wa tarumbeta hii kufunika au kuchukuwa kipindi chote cha ujio shirikishi na "kubeba sehemu ya adhabu ambayo huleta hitimisho la kitasa cha sita.

d. *"200,000,000" (**Ufu 9:16**).* Ingawa Biblia nyingi hutafsiri idadi ya wapanda farasi kama 200,000,000, hili siyo sahihi. Neno halisi la Kigiriki ni *dismuriades muriadōn* ("mara mbili ya elfu ya milioni" au "mara mbili kumi elfu mara maelfu kumi"). "Bila kuondolewa, *murias* ('kumi elfu') inataja ukubwa usiokokotoleka popote inapotumiwa bila kivumbuzi au kivumishi cha tarakimu. Kwenye LXX wingi pia unayo maana ya siri ya tarakimu isiyokokotoleka, jeshi lisilohesabika au lisilo na kipimo [e.g., **Mwanzo 24:60; Lawi 26:8; Hes 10:36; Kumb 32:30; 33:2, 17 1 Fal 18:7-8; Zab 3:6; Dan 7:10; Mik 6:7**]. . . . Matumizi ya wingi mara mbili *muriades muriadōn* ('maelfu kumi ya maelfu kumi') kwenye Ufu. 5:11 kwenye kuzitaja tarakimu za jeshi zisizokokotoleka kunathibitisha matumizi yale yale ya mfano wa karibia wingi mara mbili unaofanana hapa. Kiambishi awali *dis-* ('mara mbili') huimarisha kipengele cha mfano wa kutokukokotoleka. Kwa hiyo, maana ya mfano inahitajika kwa tafsiri halisi ya namba, kwa kuwa ni mpangilio wa wingi pia iache bila mipaka katika hali ya kukokotolewa kwa usahii." (Beale 1999: 509) Jaribio la baadhi wa Waamini wa mpito kuchukulia namba hizo kiuhalisia na kuzitumia kwa jeshi la kisasa la Kichina ni upumbavu (ang Lindsey 1970: 84-87; Walvoord 1966: 166; ang pia Smith 1980b: 120 [*"wafalme watokao mashariki"* ya **Ufu 16:12** ni majeshi ya China, Japani, na India]; Pentecost 1958: 331 [*"wafalme watokao mashariki"* ni "nguvu kuu ya upinzani ya watu wa mataifa au wasiomjua Mungu ambao watajumuishwa na muungano wa mataifa yaliyoko bara la Asia"]).

e. *Utambulisho na kusudi la wapanda Farasi (**9:17-21**).* Wachambuzi wengi huchukua "farasi" na wapandaji wake kuwa wa kipepo, sawa na "nzige" wa **9:1-11**. Boxall ni mwakilishi: "Kama faida ya asili ya kipepo, farasi hawa wana mseto huo huo kama wa nzige (maono ya Yoeli ya siku ya Bwana imeshawishi vyote: e.g. Yoeli 2:4-5; cf. Ezek. 38:14-16). Vichwa vyao ni kama vichwa vya simba (tena labda mkanganyiko wa Simba wa kweli wa Kimasihi: 5:5; cf. 9:8), na mikia yao ilikuwa kama nyoka, na vichwa ambavyo kwavyo hufanya madhara (cf. kama ya nge mikia ya nzige 9:10, ambayo pia husababisha madhara; katika 12:9 Shetani atatambuliwa kama nyoka wa zamani). Vichwa kwenye mikia bila shaka kuonekana kuwa kama vichwa vya nyoka wakiwagonga wahanga wao." (Boxall 2009: 148)

Kusudi la milele la wapanda farasi linahusika na ukombozi: ama kuwaleta wanadamu kwenye toba (Stylianopoulos 2009: 23n.23); au kuwathibitisha wanadamu kwenye uasherati na

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

dhambi ambazo hazijatubiwa (**Ufu 9:20-21**)—na ikiwa hakuna toba, basi patakuwepo na hukumu. Hili linamfanya Steinmann kuhitimisha kwamba wapanda farasi siyo mapepo bali ni umbo kwa Wakristo kama mashahidi kwenye ulimwengu: "Wanaleta ujumbe wa mauti ya Kiroho kwa wale ambao hawatatubu. Kwamba watashiriki baadhi ya vipengele vya kipepo vya nge kwenye tarumbeta ya tano (vifuani, cf. 9:7, 17; mikia yenye nguvu, 9:7, 19) inafunua kwamba ulimwengu utawaona kama mapepo, kama Yesu alivyoonekana kwenye tukio (cf. Math 12:22–30; Marko 3:23–27; Luka 11:14–23)." (Steinmann 1992: 74)

Ikiwa wote nzige na wapanda farasi ni mapepo, upo uwezekano mkubwa wa picha kuwaonyesha wakifuata kwenye nyayo za baba yao wa milele, ambaye alikuwa *"mwuaji tokea mwanzo . . . mwongo na baba wa huo"* (**Yoh 8:44**). Beale anashikilia kwamba nzige na wapanda farasi hawaonyeshi vita vya kiroho vya sasa bali kwa mfano au kwa siri huonyesha udanganyifu. Ingawa hili laweza kuonekana kuwa na makabiliano yenye umaizi, alielezea, "Mchanganyiko wa joka au majoka (9:19) na nzige (vv 3, 5, 10) huashiria mahusiano mapana kwenye Biblia na mawazo ya zamani, pale ambapo mchanganyiko wa kimifano kwa hukumu kwenye ujumla na udanganyifu au uongo kwenye uhalisia" (Beale 1999: 515; angalia **Hes 21:6; Kumb 8:15; Zab 58:3-6**; angalia pia **Luka 10:17-19**). Hivyo, mapepo huwadanganya na kuifanya mioyo ya wakaaji wa nchi kuwa migumu katika kumkataa kwa Kristo, ibada zao za sanamu, na dhambi zao.

Ufu 9:20 inaashiria kwamba msingi au shina la dhambi ya mwanadamu ni ibada ya sanamu ambayo inajidhihirisha yenyewe kwenye utendaji kama vile mauaji, uchawi, uasherati, na wivi (**Ufu 9:21**). Ibada ya sanamu, kwa asili yake, ni matokeo ya udanganyifu na kugeuka kutoka kwenye ukweli kwenda kwenye uongo. Eneo lote huashiria wimbo wa Musa kwenye **Kumbukumbu la Torati 32**. Pale, Mungu aliwaonya Waisraeli juu ya Ibada ya sanamu (**Kumb 32:21**; linganisha na **Ufu 9:20**), linganisha matunda ya Ibada ya sanamu na *"sumu kama majoka"* (**Kumb 32:33**; linganisha na **Ufu 9:19**), na kusema kwamba atawapelekea*"meno ya wanyama wakali"* na *"sumu ya wadudu watambaao"* (**Kumb 32:24**; linganisha na **Ufu 9:17-19**).

Ikiwa wapanda farasi kwa ishara huonyesha ushuhuds wa Wakristo, matokeo ni sawa. Moto kutoka kwenye vinywa vyao (**Ufu 9:17**) ni sawa na moto ambao unatoka kwenye vinywa vya "mashahidi wawili" kwenye **Ufu 11:5**. Matendo ya wapanda farasi huitwa "mapigo" (**Ufu 9:18, 20**); tena, mashahidi wawili wanayo nguvu ya kuleta "mapigo" juu ya nchi (**Ufu 11:6**). Ukweli kwamba nzige wa kipepo hawawezi kuua, lakini wapanda farasi wanaweza,Steinmann anashauri au kupendekeza kwamba "Shetani anaweza kuwadhuru nafsi lakini wale Wakristo ambao kwa kupitia kuhubiri neno la Mungu la hukumu juu ya wasiotubu wanaweza kutumia nguvu za Mungu za hukumu ya Kiungu ambayo huua nafsi" (Steinmann 1992: 74).

Kwa hiyo, chakushangaza, ama wapanda farasi ni mapepo au ni mashahidi Wakristo haina maana hasa kwenye mwanga wa shughuli zao na makusudi. Hata kama ni mapepo, ni lazima tukumbuke kwamba alikuwa ni Kristo ambaye alizivunja mihuri hivyo kuwaruhushu farasi na wapanda farasi kwenye **Ufu 6:1-8**; ni Mungu ambaye alitoa idhini ya kufunguliwa kwa nzige kwenye **9:1**; ni Mungu ambaye alitoa idhini kwa mnyama kufanya vita na watakatifu na kuwashinda kwenye **13:7**; nan i Mungu atakayemfungua Shetani kwenye **Ufu 20:3, 7**. Hivyo, kwa njia nyingine, wakati wote ni Mungu aliyeidhinisha kufunguliwa kwa farasi na wapanda farasi kwenye **9:13-14** kukamilisha makusudi yake.

Tunauona mkono mkuu wa Mungu ukisimamia kwenye shughuli za wapanda farasi kwenye hizo wapanda farasi walikuwa na *"moto na kiberiti"* ambavyo vinatoka *"kwenye vinywa vyao"* (**Ufu 9:17-18**). "Vinywa" vinawakilisha matamshi ya wapanda farasi: ama udanganyifu ambao huwashawishi wanadamu kwenye ibada ya sanamu (ikiwa wapanda farasi ni mapepo), ambao kutoka huko wanadamu hawatatubu; au ushuhuda wa waamini (ikiwa wapanda farasi ni mashahidi wa Kristo), ambao hawathibitishi kumwongoza mwanadamu kwenye toba. *"Moto na kiberiti"* ni maneno ya wazi ya maandiko yakimaanisha hukumu ya Mungu (angalia **Mwanzo 19:24; Kumb 29:23; Zab 11:6; Isa 30:33; 34:8-9; Ezek 38:22; Luka 17:29**). Hutumika pia kwenye Ufunuo kuelezea mauti ya pili, "ziwa la moto" la milele ambalo katika hili Shetani, mnyama, nabii wa uongo, na wale wote ambao majina yao hayakuandikwa kwenye kitabu cha uzima watatupwa ikiwa ni matokeo ya hukumu ya Mungu juu ya sanamu zao na dhambi (**Ufu 14:10; 19:20; 20:10; 21:8**).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Ufu 21:8 unaonyesha muunganiko wake na **9:20-21** kwa kuwarudia waabudu sanamu hao, wauaji, wachawi, na watu waovu watakuwa kwenye ziwa liwakalo moto na kiberiti. Kama vile kuimarisha muunganiko huo, **21:8** inamalizia orodha yake ya wale ambao watahusika kwenye mauti ya pili kwa kutaja "waongo wote" (i.e., wale ambao hufuata njia ya sanamu kwa kugeuka kutoka kwenye kweli kuuelekea uongo). Hivyo, ama moja kwa moja au vinginevyo, wapanda farasi ni vifaa vya hukumu ya Mungu. Ukweli kwamba wanayo nguvu ya kuua (**9:18, 20**), ambapo nzige awali kwenye surah ii hawakuwa nayo (**9:4-6**), inaashiria "muhuri" wa hukumu ya Mungu kwa waabudu sanamu (i.e., ikiwa waabudu sanamu hana muhuri wa ulinzi wa Mungu [**9:4**], juu ya mauti hali ya umilele wake wa Kiroho ni muhuri au kufanywa yakini). Kwa hiyo, bila kujali utambulisho wa wapanda farasi, kimsingi hamu ya Yohana kwenye **Ufunuo 9** ni kitheolojia, siyo kimwili. Anatumia maono na ishara siyo kuzungumza kuhusiana na mateso au hata mauti ya mwili *hasa* bali kuonyesha mateso na mauti ya mwili na nafsi ambazo zitahakikisha ikiwa waamini watarudi nyuma kwenye kujitoa kwao kwa Kristo. Kama Yesu alivyosema, *"Msiwaogope wauuao mwili, wasiweze kuiua na roho, afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanamu"* (**Math 10:28**). Surah ii yote ni njia nyingine, ya wazi ya kuhifadhi kiini cha suala—Wapi au pamoja na nani utii wetu ulikoegemea?—mbele yetu.

2. Kitabu kidogo (**Ufu 10:2, 8-10**). Kitabu kidogo cha **sura ya. 10** kwa karibu kinafuatana na, kama siyo kufanana na, Kitabu cha **Ufunuo 5**:

- Vitabu vyote vimefunguliwa.
- Vyote vimeshikiliwa na Kristo (kama Malaika wa Bwana kwenye **sura ya 10**).
- Kristo amefananishwa na Simba (**5:5; 10:3**).
- Vyote ni nukuu ya kitabu cha **Ezekieli 2**.
- Vyote vimehusishwa na "malaika mwenye nguvu" ambaye "analia."
- Mungu anaitwa Mmoja ambaye "anaishi milele na milele" (**5:13; 10:15**).
- Vitabu vyote moja kwa moja vinahusika na unabii wa nyakati za mwisho wa **Danieli 12**.
- Kwenye maono yote mtu mmoja anakikaribia kiumbe cha mbinguni na kuchukua kitabu kutoka kwenye mkono wa kiumbe hicho.
- Kwenye maono yote agizo la unabii wa Yohana unajumuisha lugha ya kufanana kwa karibu kwenye kumbukumbu kwa sauti izungumzayo kutoka mbinguni (**4:1; 10:8**).
- Vitabu vyote vinahusika na mwelekeo wa "jamaa, mataifa, lugha, na kabila/falme" (**5:9-10; 10:11**). (angalia Beale 1999: 527; angalia pia Johnson 2001: 159-60)

3. Mji mkubwa au mkuu (**Ufu 11:8**). Kwenye **Ufu 11:8**, Yohana kwanza anautaja *"mji mkuu"* ambao "kimsingi" au "kiroho" umetambulishwa kama *"Sodoma na Misri, pale pia Bwana wao aliposulubiwa."* Hili linatokea kuutambulisha *"mji mkuu"* kama Yerusalemu. Hata hivyo, penginepo kwenye Ufunuo *"mji mkuu"* wakati wote hutumika kuutambulisha "Babeli mkuu" (**Ufu 16:19;17:18; 18:10, 16, 18, 19, 21**; angalia pia **Rev 14:8; 17:1, 5; 18:2; 19:2**. Angalia Reader 1982: 40714).[42] Kwa upeo huu, tunapaswa kukumbuka aina ya mafunuo na ishara inazohusisha na kusudi kuu la Yohana kwenye uandishi: "Tunahitaji kutambua kwambautambulisho wa Roho siyo hadithi rahisi, lakini kufafanua hali ya sasa kuonekana kwenye mtazamo wa nyakati za mwisho. . . . Simulizi inaanzia Yerusalemu kwa sababu Yerusalemu ilivyowatendea manabii hasa Yesu ni dhahiri: haya ndiyo wale ambao wanaubeba ushuhuda wa Yesu wanayoweza kutegemea kutoka ulimwenguni. Wowote na kila Mji ambao mitaa yake maiti za mashuhuda zitawekwa ni hapo utatambuliwa, tabia zake zitaonekana kwenye Roho, kama Sodoma na Misri" (Bauckham 1993a: 172)[43]

4. Wasiomcha Mungu kweli watatubu kabla ya parousia (**Ufu 11:13;** angalia pia **6:14-17; 9:20-21; 16:11**)? Baada ya kifo cha "mashahidi wawili," wataenda mbinguni *"na maadui zao wakiwatazama . . . na waliosalia wakaingiwa na hofu, wakamtukuza Mungu wa mbinguni"* (**Ufu 11:12-13**). Mawazo yamegawanyika kuhusiana na ama hili linawakilisha toba ya kweli au la.

(1) Kumtukuza Mungu kama kukiri utawala au ukuu Wake, lakini siyo kama toba ya kweli.

[42] Waamini wa theolojia wanatambulisha *"mji mkubwa"* na *"Babeli mkuu"* kama Yerusalemu. Mathison 1999: 152-54; Preston 2010: 10203, 167-69, 327n.129. Asili maalum na utambulisho wa Babeli mkuu utajadiliwa hapo chini katika "17:1–19:10: hukumu ya mwisho ya Babeli."

[43] Ukweli kwamba mji mkubwa "kimsingi" na "kiroho" ulitambulishwa kama Yerusalemu yenyewe ni dokezo la maneno kwamba malengo siyo juu ya Yerusalemu halisi.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Sabau nyingi zimetolewa na wachambuzi kama kuashiria kwamba toba ya kweli siyo katika mtazamo huu hapa:

- *Tetemeko kuu la nchi na mazingira ya hukumu ya mwisho.* Historia ya Agano la Kale kwa "tetemeko kuu la nchi" linaonekana kuwa **Ezek 38:19**. Kwenye mazingira hayo, wakati Gogu alipokuja kinyume na Israeli, tetemeko kuu la nchi ni sehemu ya udhihirisho wa uwepo wa Mungu wakati anapokuja kwenye hukumu ya mwisho. Gogu na Magogu wa **Ezekieli 38-39** vile vile ilitumiwa kwenye Ufunuo kama sehemu ya *parousia* na hukumu ya mwisho (**Ufu 20:8-9**). Kama ilivyoelezwa mwanzoni, wazo la "tetemeko la nchi" limetumika kwenye kitabu chote cha Ufunuo, ukijuuisha **Ufu 11:13**, kama udhihirisho wa hukumu ya mwisho. W. Reader anaonyesha kwamba msongamano wa waongofu kwa asilimia 90 ya ulimwengu uliopotea mwishoni mwa historia ni wazo "lisilopatikana penginepo popote kwenye kitabu. Kunashingana au kupingana na wazo kwamba wale waliookolewa ni makundi yenye ukomo (7:1-15; 14:1-5; 18:4) haiwezi kuwa inafanana na maelezo yaliyojirudia kwamba ulimwengu uliolemewa utabaki haujatubu (9:20f; 16:9, 11, 21)." (Reader 1982: 413) Hakika, **Ufu 11:11-12** unaashiria uhakikisho au kufufuka kwa Kanisa mwishoni mwa nyakati wakati wale wale ambao watalitazama wataitwa "maadui zao." Kupewa mazingira na sifa hizi, matendo ya "maadui" kwenye **11:13** hayawezi kuwakilisha toba na waongofu wa kweli.
- *Kumpa Mungu utukufu.* Ingawa "kumpa Mungu utukufu" kwa kawaida humaanisha ibada ya kweli, haionyeshi hivyo wakati wote. Kwenye baadhi ya kesi huonyesha mwitikio wa wasioamini ambao wametambua mamlaka ya Mungu bila kulazimika kutubu au kuwa na mioyo iliohuishwa (angalia **Yosh 7:19; 1 Sam 6:5; Mdo 12:23**). Mfano wa hili ni Nebukadneza kwenye **Dan 2:46-47**. Pale, mfalme aliutambua ukuu wa Mungu na kumheshimu Danieli. Hata hivyo, kumtambua kwa namna hiyo kulikuwa kwa muda tu. Kilichofuatia kwenye **Danieli 3** kwa kujaribu kumlazimisha Danieli na wengine kuabudu miungu ya dhahabu kwa maumivu ya kifo. Hivyo kwenye **Ufu 11:13**, wale wanaotambua ukuu wa Mungu hubaki wasioamini (angalia Beale 1999: 603-04).

b. *Kumpa Mungu utukufu kama toba ya kweli.* Sababu nyingine hupendekeza kuwa hii ni toba ya kweli:

- *Miitikio tofauti.* Kwenye **Ufu 14:6-7** malaika ambao walikuwa wakihubiri injili waliitisha hatua mbili za mchakato wa toba, *"mche Mungu, na umpe Yeye utukufu."* Toba ya **Ufu 11:13** ni thabiti kwa kile malaika walichoitisha na ni tofauti au hakikpothabiti na mwitikio wa watu angalia kwenye **16:9**. Kwenye **16:9**, watu walimtukana au kumlaani Mungu na hawakumpa Yeye utukufu; kwenye **11:13**, watu walitenda sawasawa na kile malaika walichoagiza kwenye **14:7**, i.e., *"wote walitetemeka"* na *"kumpa utukufu Mungu wa mbinguni."* (Resseguie 2009: 166) Bauckham anasema kwamba mwitikio huu unachipuka kutoka ule wa **11:13** kushawishiwa na ushuhuda wa kweli wa "mashahidi wawili" kwa sababu "waliwaona ushiriki wa mashahidi' kwenye ushindi wa Kristo juu ya mauti" kama matokeo ya kufufuka kwa mashahidi wawili (Bauckham 1993a: 281).
- *Hofu; utukufu; Mungu wa Mbinguni.* Wakati "hofu" yaweza au haiwezi kumaanisha heshima kwa Mungu (linganisha **Ufu 1:18; 14:7; 15:4; 19:5** pamoja na **1:7; 2:10; 18:10, 15**), wakati inaposhirikiana na kumpa Mungu utukufu upo uwezekano wa kuwa na maana chanya ibada (Bauckham 1993a: 278). Zaidi ya hayo, kwenye Ufunuo, "kumpa Mungu utukufu" wakati wote "hueleza vyema kumpa Mungu ibada ambayo anaistahili (4:9; 14:7; 16:9; 19:7)" (Ibid.: 278-79).

5. <u>Ujumbe wa kanisa, bila kujali matokeo.</u> Mauaji ya kiimani ya "mashahidi wawili" ni mfano mwingine wa asili ya mkanganyiko wa ushahidi wa Mkristo. *"Kumfuata Mwanakondoo popote aendako"* (**14:4**) kwaweza kupelekea kifo na kuonekana kushindwa kwenye ulimwengu huu lakini, kama paqmoja na Kristo Mwenyewe, hiyo ndiyo inayoleta maana ushindi wa Mungu juu ya dhambi na uovu. Bauckham anaamini kwamba usminifu wa ushuhuda wa Waamini hata kufa ni njia ambayo kwayo mataifa yasiyomcha Mungu yataletwa kwenye toba na imani (Bauckham 1993a: 279-83). Kwa namna nyingine, ikiwa kuongoka kwa wingi kwa wasioamini hakutatokea kabla ya kurudi kwa Kristo, ushuhuda wa mauaji wa Wakristo bado ni wa lazima na muhimu: huthibitisha imani yao kuwa halisi, ambako ni muhimu kwa ustawi wao wenyewe wa milele (angalia, e.g., **Ufu 6:9, 11; 7:9-17; 11:11-12; 15:2-4; 20:4-6**); na kunatupa ushahidi kwa Mungu kuutia hatiani na kuuhukumu ulimwengu wa

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

wasioamini (Beale 1999: 960; angalia pia Johnson 2001: 274; Bauckham 1993a: 237; Schüssler Fiorenza 1991: 78).

Mungu hakujibu kwa haraka kilio cha waliouawa kwa ajili ya imani *"Mpaka lini, Ee Bwana?"* (**Ufu 6:10**). Badala yake, "ujumbe wa Mwanakondoo na ushindi ni lazima uendelee kwa wafuasi wa Mwanakondokoo" (Bauckham 1980: 31). Bila kujali idadi ya waongofu ambao watatokana na ushuhuda huo, "kukawia kwa *parousia* kumejawa na ujumbe wa Kanisa" (Ibid.: 33).

F. ***Ufu 12:1-15:4: Mwanamke, Joka, na Mnyama***[44]

Maono ya **Ufunuo 12-14** yanaanza na kuzaliwa (**12:1, 4-5**)[45] na kupaa (**12:5**) kwa Kristo na hata yaweza kurudi nyuma hata Bustani ya Edeni (**12:9**). Ni kwenye kweli hizi ambapo mgogoro baina ya mwanamke na Joka au nyoka ulikoanzia na ulikuwa wa kimsingi sana na wa pao kwa hapo. Maono ya Yohana kwenye kifungu hiki yanaenea hadi *parousia* na hukumu (**14:14-20**) na uhakikisho wa watu wa Mungu (**15:2-4**). Kama Hendriksen alivyoeleza mwanzoni, kuanzia kwenye **Ufunuo 12** tunapokea maelezo ya historia ya kina ya Kiroho na mapambano ya Kanisa pamoja na nguvu ya uovu (Hendriksen 1982: 23; sawa sawa na, **Rev 13:1-10** hutupa maelezo mengi yaliyokamilika ya **Ufu 11:7**).

Ufu 11:3-13 na **12:1-15:4** "kimsingi huonyesha jambo lilelile kwenye picha tofauti" (Bauckham 1993a: 273n.52). Vifungu vyote vinaonyesha nguvu ya uovu kufanya "vita" kinyume na Kanisa (**Ufu 11:7; 12:17**). Kwenye kesi zote mbili Kanisa linalindwa (kwa muda kwenye **Ufu 11:3-7**; kijiografia kwenye **12:6, 14-16**). Kwenye kesi zote mbili Kanisa linahakikishwa na linaonekana mbinguni (**Ufu 11:11-12; 14:13-16; 15:1-4**). Kwenye kesi zote mbili watesi wao wanahukumiwa (**Ufu 11:13-19; 14:7-11, 17-20**).

Isa 26:16-27:1yaweza kusimama nyuma ya **Ufunuo 12**. Kwenye Isaya, Israeli inaonekana kama mwanamke mwenye utungu ambaye analia kwa sababu ya maumivu (linganisha **Isa 26:16-17** na **Ufu 12:1-2**); ipo ahadi ya ufufuo (linganisha **Isa 26:19** na **Ufu 12:5**); Watu wa Mungu wamehifadhiwa na kulindwa kwa "kitambo kidogo" (linganisha **Isa 26:20** na **Ufu 12:6, 12, 14-16**); na Mungu atamwadhibu "nyoka," "Yule Joka." (linganisha **Isa 27:1** na **Ufu 19:20-21; 20:10**).

1. <u>Kushindwa na kuangushwa chini kwa joka (**Ufu 12:7-12**).</u> "Joka" limetambulishwa kama *"nyoka wa zamani ambaye anaitwa Ibilisi na Shetani"* (**12:9**).

a. *Kushindwa kwa Joka (Shetani) kulitokea Msalabani.* "Kushindwa kwa Joka (12:7-9) bila shaka ni tukio lile lilela ushindi wa Mwanakondoo (5:5-6), na yote kihistoria yaweza kuwekwa kwenye kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo (kuendelea kwenye ushuhuda na mauaji ya kiimani ya wafuasi wake 12:11)" (Bauckham 1993a: 186). Baadaye, "Ushindi wa Mikaeli kimsingi ni wa mbinguni na sehemu ya ishara ya ukweli wa kidunia wa Msalabani." (Caird 1966: 153-54; angalia pia Ladd 1972: 172)

Mazingira ya **Ufunuo 12,** pia yanaweka wazi kwamba Shetani *"kutupwa chini"* siyo tukio lililotokia kabla ya historia kuanza, au tukio litakalotokia mara baada ya hitimisho la historia. **Ufu 12:5-6** linaunganisha kufufuka na kupaa kwa Kristo pamoja na mwanamke kukimbilia jangwani au nyikani. **Ufu 12:9, 11, 13-14** sambamba linaunganisha kufukuzwa kwa Shetani pamoja na *"damu ya Mwanakondoo"* na kukimbia kwa mwanamke. "Kwa kuwa matokeo mara baada ya joka kufukuzwa ni kumfuatilia mwanamke na kukimbilia kwake jangwani (vs. 13-14), maono ya kwanza yanatuongoza kutafsiri kufukuzwa kwa joka na wafuasi wake wasio na hatia kama kutokuzungumzia msingi wa uasi ambao ulitangulia anguko la mwanadamu lakini kwa ushindi na kupaa kwa mtoto wa mwanamke" (Johnson 2001: 388).

---

[44] Kwa kuwa nyanja mbalimbali za **Ufunuo 12:1-15:4** zimekwisha kujadiliwa hapo juu katika sehemu **VI.C.** ***Kanisa kwenye kitabu cha Ufunuo: takwimu kuu na ishara***, mijadala hiyo haitarudiwa kwa kina hapa tena. Wale "wanyama" ambao wanahusika katika **Ufu 13:1-18** watajadiliwa kwa kina katika sehemu inayofuata.

[45] Ingawa kwenye uso wake **Ufu 12:1-5** inaonekana kuzungumzia kuzaliwa kwa Kristo, G. B. Caird anafanya fikra pendekezwa kwamba **Ufu 12:5** kwa hakika haizungumzii kuzaliwa kwa Kristo lakini kifo chake msalabani na kufufuka na kupaa msalaba unafaa. Sababu ni kwamba **12:5** imetajwa kwenye **Zab 2:7-9**. "Kwenye zaburi siyo kwenye kuzaliwa kwake lakini katika utekelezaji wake kwenye Mlima Sayuni kwamba mfalme mpakwa mafuta ametangazwa na Mungu, 'Wewe ni Mwanangu; Mimi leo nimekuzaa', na alipewa mamlaka ya kuwaponda mataifa yote kwa fimbo ya chuma (Zab.2. 7-9). Siku ya kuzaliwa Mfalme ni siku ya kupaa kwake." (Caird 1966: 149; angalia pia **Warumi 1:3-4**; Allison 1985: 72-73) Kama Longman na Reid walivyoonesha, hili siyo tu linafanya hisia kwa kutajwa kwenye **Zab 2:7-9** lakini pia "inaelezea vinginevyo maelezo yaliyorukwa kutoka kuzaliwa hadi kupaa" (Longman na Reid 1995: 183). Kwa hiyo mazingira ambayo pia yanafanya ufahamu kama **Ufu 12:5** yanatuongoza kwa haraka kwenye kutupwa chini kwa Shetani kwenye **12:7-12**, tukio ambalo lilitokea kama matokeo ya kile Kristo alichokikamilisha pale msalabani.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

"Mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache tu" (**12:12**) inaonyesha jambo lile lile: "Kipindi hiki cha wakati hakipaswi kuangaliwa kama kilikuwa kipindi kifupi maalum karibu na nyakati za Kristo, wakati ghadhabu ta Shetani itakapoinuka kwa kiwango cha juu kuliko kawaida yake kwa sababu saa ya mwisho inakaribia kufika. *Ghadhabu kubwa* ambayo anaiendea ni ile iliyochochewa ndani yake kwa kushindwa kwake kupitia kifo, kufufuka, na kupaa kwa Bwana. Iliwaka ndani yake wakati 'alipotupwa duniani,'na kwa hiyo kuanzia wakati huo wa kushindwa kwake 'muda mchache' ulianza." (Milligan 1896: 20910) Hili linathibitishwa na ukweli kwamba kuja kwa Kristo mara ya kwanza kulianzisha "siku za mwisho"; baadaye, kwenye mazingira haya, "muda mchache" wa Shetani ni sawa na "siku za mwisho" (mengi kuhusu hili angalia Menn 2017, kifungu **IV.B.** ***Kuja kwa Kristo mara ya kwanza na "siku za mwisho"***).

Kuanguka kwa Shetani kwenye **Ufu 12:10** (*"sasa . . . ametupwa chini mshtaki wa ndugu zetu"*) inalingana na **Yoh 12:31** (*"sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje"*).[46] Kwenye **Yoh 12**, Yesu anasema kwamba "atainuliwa juu" juu ya Msalaba kunamaanisha kwamba "hatimaye hukumu ya Ibilisi iliyozinduliwa itatekelezwa. Mifanano hii inathibitisha zaidi kwamba picha kwenye Ufu. 12:7-10 inaeleza umuhimu wa Kristo kufa na kufufuka na hakuelezei matukio ya wakati ujao kwa mbali." (Beale 1999: 660)

b. *Asili ya kushindwa kwa Shetani.* Caird alifanya utafiti wa kushangaza, "Kwenye kitabu cha Ayubu mmoja wa malaika kwenye mahakama ya mbinguni aliitwa Shetani (pamoja na makala fafanuzi), kwa sababu alishikilia nafasi kama mshtaki au mtesi kwenye mahakama ya Mungu [**Ayubu 1:6–12**]. . . . Shetani alionekana tena kama mshtaki kwenye maono ya Zekaria, wakati Kuhani mkuu Yoshua akiwa kwenye majaribio [**Zek 3:1–7**]." (Caird 1966: 154)

"Kutupwa chini" kwa Shetani kunaonekana kuhusiana na sehemu muhimu ya uwezo wake wa kuwashtaki ndugu, sawa na kuyadanganya mataifa (**Ufu 12:10**). Shetani analo shitaka moja tu baya zaidi analoweza kulifanya kinyume na watu: dhambi isiyosamehewa. Msalabani Yesu aliuchukua uwezo huo wa Shetani *"akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea Msalabani"* na hivyo *"kuzivua enzi na mamlaka"* (**Kol 2:14-15**). Kwa hiyo kile Kristo alichokifanya juu ya Msalaba, kinamaanisha kuathiri uwezo wa Shetani wa kuwadanganya watakatifu: "Kwenye mwanga wa Ufu. 12:11, mashitaka ya mst. 10 inaonekana kuwa kinyume moja kwa moja na udhalimu wa watakatifu kushiriki kwenye Wokovu. . . . Kifo na kufufuka kwa Kristo kumemwondolea Ibilisi fursa hiyo ambayo mwanzoni Mungu alimpa, kwa sababu kifo cha Kristo kilikuwa adhabu ambayo Mungu aliidhihirisha kwa dhambi za wale wote ambao wameokolewa kwa imani. . . . Kwa hiyo, Ibilisi hana tena msingi wa mashitaka yake kwa watakatifu, kwa kuwa adhabu ambayo walistahili na ile aliyoomba mwishoni imechukuliwa kwenye kifo cha Kristo." (Beale 1999: 659; angalia pia **Rum 3:21-26; 8:1, 33-34, 38-39**)

Matokeo kwa waamini ni mabadiliko muhimu kwenye hali na usalama, ingawa haiwezi kuonekana hivyo kwa macho ya nyama. Hata hivyo, sehemu ya sababu za kwanini Yohana aliandika kitabu chote cha Ufunuo ni kuweka wazi kwa waamini kwamba "mambo siyo kama vile yanavyoonekana kuwa" (Johnson 2001: 9). Magumu ya nje siyo kiashiria cha kukosa kibali cha Mungu au cha kukosa usalama wa Kiroho. Beasley-Murray kwa wazi analishika hili wenye muunganiko na kutupwa chini kwa Shetani kwenye **Ufu 12:7-12**: "Mambo mawili yapo akilini hapa. Kwanza, kwamba Shetani hana nafasi mbinguni kuwakilisha ushindi muhimu uliopewa wanadamu, kwa kuwa Shetani hana uwezo tena kuwashitaki watu mbele za Mungu, ambalo linatudhihirishia kwamba Mungu hasikilizi tena mashitaka yaletwayo kinyume na watu wake, kwa kuwa wamesamehewa. Pili, kushindwa kwa Shetani mbinguni kunamaanisha kwamba nguvu zake zimevunjwa kwa shughuli za watu kwenye historia, hivyo kwamba hata kama atatia bidii na nguvu zake kuyatawala mataifa na kuangamiza kazi ya Mungu, kiwango cha ushawishi wake kina ukomo (kwa mfano hana nguvu juu ya Kanisa), na siku zake zinahesabika (vv. 13ff.)." (Beasley-Murray 1974: 202; angalia pia Beale 1999: 660 ["Uelewa huu wa kuanguka kwa Shetani kutoka mbinguni ni sawa na ule wa [**Luka 10:17-20**]. . . . Kwamba ni, kuanguka kwa Ibilisi kunamaanisha kwamba Wokovu wa wafuasi wa Yesu umehifadhiwa kutokana na tishio la Kishetani, na nguvu zao juu ya mapepo ni kiashiria cha awali cha kushindwa kwa

[46] Kitenzi cha Kigiriki kilichotumika kwenye vifungu viwili vinafanana, maneno yenye nguvu, yaliyotoka kwenye chanzo au lile lile: **Yoh 12:31**—*ekballō* ("kutoa nje; kufukuza"); **Ufu 12:10**—*kataballō* ("tupa chini; angusha chini").

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Ibilisi na usalama wao uletao wokovu."])

2. Bahari na kuzimu (**Ufu 12:12; 9:1-2, 11; 11:7; 13:1; 17:8; 20:1, 3; 21:1**). **Ufu 12:12** inasema, *"Ole wan chi na bahari, kwa maana Yule Ibilisi ameshuka kwenu."* Wakati **12:9** ilisema kwamba Ibilisi alikuwa *"ametupwa hata nchi,"* inaonekana kutoka **12:12** kwamba pia alikuwa ametupwa chini baharini. Mara nyingi bahari imhusishwa na wazo la machafuko na uovu (angalia Beale 1999: 789; Schüssler Fiorenza 1991: 83; angalia pia Schnabel 2011: 279 kwa maana tofauti istilahi "bahari" imehusishwa kwenye Ufunuo). Kama vile wanyama wa **Dan 7:2-8** walipanda toka baharini, hivyo mnyama wa **Ufu 13:1** alipanda kutoka baharini. Penginepo Agano la Kale linaonyesha bahari kama makao ya hayawani waovu, ingawa Mungu ni mtawala juu bahari na wakaaji wake (**Ayubu 38:8-11; Zab 74:12-15; 89:9-10; 104:5-9; Mith 8:27-29; Isa 27:1; 51:9-10; Ezek 32:2**). Bahari kama machafuko na uovu imeonyeshwa zaidi kwenye **21:1** ambayo inasema kwamba, kwenye mbingu mpya nan chi mpya*"hapatakuwa na bahari tena"* bahari kama chanzo cha uovu wa Kishetani ukipingana na kiti cha Enzi cha Mungu vimeondolewa na nafasi yake kuchukuliwa na mto wa ukombozi, ambao chanzo chake ni kutoka kwenye kiti cha Enzi [**Ufu 22:1**]" (Beale 1999: 328).

Bahari inaonekana kuwa sawa na kuzimu "kama inavyowekwa wazi kwenye 11:7 na 17:8, pale ambapo mnyama Yule yule ambaye anakuja kutoka baharini kwenye 13:1 ameelezewa kama atokaye *abussos* [kuzimu]" (Moo 2009: 156). Vivyo hivyo, Shetani *"kutupwa chini mpaka nchi"* (**12:9**) na *"kushuka chini ya nchi na bahari"* (**12:12**) ni sawa na yeye *"kutupwa kuzimu"* (**20:1-3**). Hili linathibitisha kwamba kufungwa kwa Shetani na "kutupwa kuzimu" kwenye **Ufu 20:1-3** kulitokea kwenye muunganiko wa kuja kwa Kristo mara ya kwanza na siyo tukio ambalo litatokea baada ya *parousia* (angalia pia hapo chini kwenye **20:1-3** kwa mahusiano zaidi baina ya "kutupwa" [**12:9**] na "kufungwa" [**20:3**] kwa Shetani).

3. Kifo, lakini mkanganyiko wa ushindi, wa watakaifu (**Ufu 12:11; 13:7**). Kwenye **Ufu 13:7** inasema kwamba mnyama "alipewa" mamlaka kufanya vita kinyume na watakatifu na kuwashinda. Huu ni "uungu batili" (i.e., mamlaka ilitolewa kwa mnyama na Mungu, kama vile Mungu alivyompa Shetani mamlaka juu ya Ayubu kwenye **Ayu 1:12; 2:6**). "Mungu ni mtawala wa vyote, na vita kinyume na watakatifu hakuongezi lengo la mnyama lakini badala yake yanawachanganya wao. Uovu umeshindwa nna ushuhuda wa watakatifu—ushuhuda wao hata kufa. Kristo alishinda kwa kifo chake juu ya Msalaba, nan i mfano wa watakatifu pia (12:11)." (Resseguie 2009: 185)

G. ***Wale "wanyama" wa Ufu 11:7; 13:1-18; 14:9; 15:2; 16:2, 10, 13; 17:3-17; 19:19-20; 20:10***

1. Ile sanamu ya "mnyama" ambayo imechukuliwa kutoka katika kitabu cha Danieli. Maelezo ya yule "mnyama" wa **Ufu 13:1-7** kimsingi yanachukuliwa kutoka **Danieli 7**. Yule "mnyama anayetoka baharini" ni kutoka **Dan 7:2-3**. Zile "pembe kumi" zinahusiana na **Dan 7:7, 20, 24**. **Ufu 13:1-2** hubadilisha tundu la simba la Danieli, dubu, chui, na mnyama wa "kuogopesha na kutisha" katika Danieli huwakilisha dola nne za duniani zilizofuatana na kuwa moja. Kwa hali yoyote, katika Ufunuo mfano wa mnyama pia unachukuwa kutoka katika maelezo ya Danieli ya "pembe ndogo" na Antiochus. Kwa hiyo, Alan Johnson anadokeza kwamba, kwa mujibu wa **Ufu 13:2**, "huyu mnyama alikuwa ana 'katika kila kichwa jina la kukufuru.' Sura hii muhimu inarudiwa katika 17:3 (cf. 13:5-6). Kiburi na kukufuru pia huzungumzia ile 'pembe ndogo' ya mnyama wa nne wa Danieli (7:8, 11, 20. 25) na yule mfalme anayefanya apendavyo wa Danieli 11:36. Yohana anagusia kuhusiana na maono ya Danieli lakini anayabadilisha kabisa." (Johnson 1981: 525) Pembe ndogo ya Danieli (**Dan 7:21**) na mnyama wa Ufunuo (**Ufu 13:7**) hupigana vita na watakatifu na kuwashinda.

2. Agano la Kale kwa kawaida hutumia picha ya "wanyama" kuashiria nguvu ya uovu, falme za dunia, na ushawishi wa kishetani nyuma ya uovu na falme. Ingawa watu wengi hutumia picha ya "mnyama" kwa nadharia ya mwisho wa nyakati binafsi, Biblia wakati wote hutumia picha ya mnyama kwa falme, nguvu, na vyombo vingine ambavyo hujiinua vyenyewer. Kwa nyongeza kwa "wanyama" wa Danieli 7, Agano la Kale limesheheni kumbukumbu nyingine mbalimbali kwa "wanyama" kama kujihusisha na fame ovu (**Zab 74:13-14; 87:4; 89:10; Isa 27:1; 30:7; 51:9; Yer 51:34; Ezek 29:3; 32:2-3**). Kwa hiyo, Sam Storms anahitimisha kwamba "mnyama" wa **Ufunuo 13** "kimsingi ni mshiriki kwenye asili, badala ya binafsi" (Storms 2013: 478). Wakati uo huo, "Vyombo vya kitaifa haviwezi kutenganishwa utambulisho pamoja na ukweli wa aina kuu ya kishetani, mfumo wa kisanamu uliowakilishwa na vichwa saba vya hayawani (Leviathani, Rahabu, na joka) ili kwamba mnyama awakilishwe, siyo nguvu ya kisiasa, lakini mfumo wa uovu ambao unapata maelezo kwenye chombo cha kisiasa" (Johnson 1981:

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

525). Muunganiko huu umewekwa wazi na malinganisho ya "joka" la **Ufu 12:3-4, 713:1** na "mnyama" wa **Ufu 13:1-10**: Shetani ameelezewa kama mwekundu na mwenye vichwa saba na pembe kumi (**Ufu 12:3**). Vivyo hivyo, mnyama ameelezewa kama mwenye wekundu angavu (**Ufu 17:3**) na mwenye vichwa saba na pembe kumi (**Ufu 13:1; 17:3**). Mlinganisho huu kwa wazi unaonyesha utambulisho baina ya falme za ulimwengu usiomcha Mungu na nguvu za kishetani "nyuma ya viti vya enzi vya kifalme." Joka lina taji kwenye vichwa vyake (**Ufu 12:3**) na mnyama ana taji kwenye pembe zake (**Ufu 13:1**). "Kwamba Joka lina taji kwenye vichwa vyake (12:3) na mnyama sasa nanzo kwenye pembe zake kunaonyesha kwamba joka lina sharia mamlaka ya wakati wote na kuamrisha mapenzi yake kupitia kwa mnyama" (Beale 1999: 633-34, 684).

3. Malinganisho ya **Danieli 7, 8, 11**; **2 Wathesalonike 2**; na **Ufunuo 13, 19**. Pamoja na kuchukuwa kutoka katika Danieli, mnyama wa Ufunuo anaonyesha mfanano wa maelezo ya Paulo ya " mtu wa kuasi" katika **2 Wathesalonike 2**. Ulinganifu ufuatao unaonyesha muunganiko wake:

Danieli 7:7-27 (Mnayama wa 4 & pembe ndogo)	***Danieli 8:9-26 (pembe ndogo)***	***Danieli 11:21-45 (mtu astahiliye kudharauliwa)***	***2 Wathes 2 (mtu wa kuasi)***	***Ufunuo 13, 19 (wamnyama wawili)***
Mwenye nguvu nyingi; mkuu kuliko wengine**:** **7:7, 17, 19-20**	Mkuu sana; mwenye uwezo sana, lakini siyo kwa nguvu zake mwenyewe: **8:9-10, 24** Mwenye kufanikiwa na kufanya mapenzi yake: **8:24**	Atakamilisha kile ambacho baba yake hakukifanya kamwe, na atakifanya kama apendavyo: **11:24, 36**	Atakuwa kwenye patano na shughuli za Shetani, kwa nguvu zote: **2:9**	Yule joka akampa yeye nguvu zake, enzi, na uwezo mwingi juu ya mamlaka; mamlaka juu ya watu wote: **13:2-4, 7**
Akinena kwa majivuno makuu: **7:8, 11, 20** Akinena maneno kinyume chake Aliye juu: **7:25**	Akijitukuza nafsi yake: **8:4, 8, 11, 25** Akishindana na Aliye Mkuu wa wakuu: **8:25** Kuondoa sadaka ya kuteketezwa ya daima, kuangushwa chini kwa patakatifu, na kupakanyagisha mahali patakatifu; ni makosa hayo yaliyosababisha hofu: **8:11-13**	Kulikasirikia Agano takatifu: **11:28, 30** Atajitukuza na kujiadhimisha mwenye juu ya miungu yote; atanena maneno kinyme na Mungu, na hataonyesha kumjali Mungu: **11:36-37** Wataondoa sadaka ya kuteketezwa ya kila siku; watalisimamisha chukizo la uharibifu: **11:31**	Mpingamizi na ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; akijionyesha nafsi yake kana kwamba ndiye Mungu**:** **2:4** Yeye mwenyewe kujiketisha katika hekalu la Mungu: **2:4**	Akinena maneno ya kiburi na makufuru: **13:5-6** Anasujudiwa au kuabudiwa: **13:4, 8, 12; 19:20**
Alikula, kusaga, na kuwakanyaga wengine: **7:7, 19** Akifanya vita kinyume na watakatifu, kuwashinda na kuwaangusha chini: **7:21, 25**	Atayakanyaga baadhi ya majeshi ya mbinguni na nyota: **8:10** Ataharibu kwa kiasi cha kustaajabisha, ikiwa ni pamoja na watu watakatifu: **8:24-25**	Atawaua wengi, ikiwa ni pamoja na waaminifu: **11:32-35, 44**	Mtu wa kuasi; mwana wa uharibifu: **2:3**	Akifanya vita na watakatifu na kuwashinda: **13:7, 15; 19:19**
	Mkali na mjuvi wa hila, mkali na ataufanya uongo ufanikiwe: **8:23, 25**	Atauteka ufalme kwa hila; akizungumza uongo; akitumia maneno malaini kuwageuza watu wasimche Mungu: **11:21, 27, 32**	Akitenda kwa uongo wote: **2:10**	Kuwadanganya wakaaji wa duniani: **13:14; 19:20**

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

			Akitenda ishara, na miujiza ya uongo: **2:9**	Akitenda ishara kuu: **13:13**
Mwenye mamlaka kwa wakati, nyakati mbili, na nusu wakati: **7:25**	Mahali patakatifu patatakaswa nyakati za jioni na asubuhi 2,300: **8:14**	Naye atafanikiwa mpaka ghadhabu itakapotimia: **11:36**		Akapewa mamlaka kwa miezi 42: **13:5**
Utawala wake utachukuliwa na kuangamizwa milele; mwili wake utateketezwa kwa moto wakati atakapokuja Mwana wa adamu**: 7:11, 13-14, 22, 26-27**	Atavunjika bila kazi ya mikono: **8:25**	Mwisho wake utakuja kwa wakati ulioamriwa: **11:35, 45**	Atauawa kwa pumzi ya kinywa cha Bwana atakapokuja: **2:8**	Atakamatwa na kutupwa kwenye ziwa la moto wakati atakapokuja Bwana: **19:20**

4. <u>Malinganisho ya maelezo na shughuli za "mnyama" wa Ufunuo.</u> Jedwali lifuatalo limeorodhesha maelezo na shughuli za "mnyama" kwenye Ufunuo:

Ufu 11:7	***Ufu 13:1-8***	***Ufu 13:11-18***	***Ufu 16:10-16***	***Ufu 17:3-17***	***Ufu 19:19-20***
Apandaye kutoka kuzimu.	Apandaye kutoka baharini: **1**	Atokaye katika nchi: **11**		Apandaye kutoka kuzimu: **8**	
	Anazo pembe 10, vichwa 7: **1**	Anazo pembe 2 kama mwanakondoo: **11**		Anazo pembe 10 (=wafalme), vichwa 7 (=milima= wafalme): **3, 9-10**	
	Majina ya makufuru kwenye vichwa vyake: **1**			Amejawa na majina ya makufuru: **3**	
	Akinena maneno ya kiburi na kufuru: **5-6**	Akinena kanma joka na kuwadanganya wakaaji wa dunia: **11, 14**	Roho chafu zikatoka kwenye vinywa vya mnyama na nabii wa uongo: **13**		
	Wakaaji wa Dunia washangazwa, kumfuata na kumwabudu mnyama: **3-4, 8**	Kuwafanya wakaaji wa dunia kumwabudu mnyama wa 1: **12, 14**		Kumshangaa mnyama: **8**	
Kupigana, kushinda, na kuwaua mashahidi 2	Kupigana na watakatifu na kuwashinda: **7**	Mamlaka ya kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama wa 1st na kuwaua wale ambao hawaiabudu sanamu ya mnyama: **15**	Roho chafu kutoka kwa mnyama na nabii wa uongo kuwakusanya wafalme wa dunia kufanya vita kinyume na Mungu: **13-14**	Mnyama na wafalme kukusanyika kwa vita kinyume na Mwanakondoo: **14**	Mnyama na wafalme kukusanyika kwa vita kinyume na mpanda farasi mweupe na jeshi lake: **19**
				Mwanakondoo atawashinda: **14** Mnyama atauendea uharibifu: **8**	Mnyama & nabii wa uongo watakamatwa na kutrupwa kwenye ziwa la moto: **20**

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

5. Tabia za “mnyama” zaweza kuashiria sehemu ya karne ya kwanza ya Rumi na watawala wake. Baadhi ya vipengele au sehemu za “mnyama” mazingira ya Rumi ya karne ya kwanza ambayo kwayo Yohana aliandika. “Vyeo vya kufuru kwenye vichwa saba vya mnyama vyaweza kutaja sifa na heshima walizopewa watawala wa Kirumi kwenye karne ya kwanza BK, ili kusaidia matakwa yao ya kuheshimiwa kama miungu ndani ya ibada za au madhehebu ya Kaisari. Sarafu za kifalme za wakati huo zilibeba ushuhuda wa wazi wa matamanio hayo; na, wakati wa kufa kwao, Julius Caesar, Augustus, Claudius na Vespasian walitangazwa kwenye sherehe kuwa ni ‘mungu’ (*divus*). . . . Haya yote yaweza kueleza kwamba mnyama wa Ufu. 13.1 anawakilisha Dola ya Rumi, mnyanyasaji au mkandamizaji katili wa Kanisa la Kikristo.” (Smalley 2005: 336) Wanatheolojia humtambulisha “mnyama” atukaye baharini pamoja na Rumi, kama ilivyowakilishwa na mfalme Nero (Chilton 1985: 175-81; DeMar 1999: 255-59).

6. “Mnyama” wa Ufunuo aliinuka karne ya kwanza ya Rumi na watawala wake. Ingawa mwonekano wa “mnyama” kwenye Ufunuo yaweza kufungiwa kwenye Rumi ya karne ya kwanza, maana na umuhimu wake vinaenda zaidi ya hali ambayo Wakristo waliipitia kwa wakati ule na mahali. Kuunganishwa na Yohana kwa wanyama wanne wa Danieli kuwa mmoja kunapendekeza kwamba mnyama anampita kila mtawala kihistoria (Resseguie 2009: 182, 191; hili ni sambamba kwenye picha ya Yohana ya “Babeli mkuu” kwenye **Ufunuo 17-18** kama ilivyokuwa na msingi kwenye karne ya kwanza ya Rumi lakini kama ilivyoipita Dola ya Rumi). Hili linathibitishwa na Agano la Kale ambalo “hutumia *picha ile ile ya hayawani wa baharini* kuwakilisha falme ovu zilizofuatana zikitawala kwa mamia ya miaka” (Beale 1999: 686, fafanuzi imeongezwa.; “Rahab” ni mbadala kwa Misri kwenye **Zab 87:4** na kwa Babeli kwenye **Yer 51:34**). Johnson anahitimisha kwamba utambulisho wa mnyama wa bahari na joka—mtawala kandamizi mwenye nguvu za kishetani nyuma yake—“hutusaidia sisi kuona kwamba mnyama mwenyewe hapaswi kutambulishwa pamoja na muundo wowote wa kihistoria wa mwonekano wake au pamoja na kipengele cha taasisi yeyote ile kwa udhihirisho wake. Kwa maneno mengine, mnyama anaweza kuonekana sasa kama Sodoma, Misri, Rumi, au hata Yerusalemu na yaweza kujidhihirisha yenyewe kama nguvu ya kisiasa, nguvu ya kiuchumi, nguvu ya kidini, au ya kutokuamini (1 Yoh 2:18, 22; 4:3).” (Johnson 1981: 525; angalia pia Storms 2013: 488; Rushdoony 1970: 170 [“Mnyama, mfano wa serikali ya kibinadamu na mamlaka, ya hali ya mpinga Kristo na kitamaduni kwa ujumla, zikiwakilisha Dola ya Rumi wakati wa siku za Yohana, na amri nyingine zote za wapinzani wa Kikristo. Mnyama anawakilisha ujumla wa mamlaka hizi kwenye ulimwengu wa zamani, na vyote vijavyo. Vichwa vyake saba na pembe kumi zinasisitiza ujumla wake.”]) Yohana alimtumia “mnyama” kile alichokifanya penginepo kwenye kitabu: aliiona misukumo ikitenda kazi kwenye ulimwengu wake na kuwajumuisha wote na kuufunua ukweli wao na maana zake za kina. Yohana aliona kile ambacho watu wengi hawaoni, yaani, ingawa kwa nje tunaweza “tusimwabudu mnyama” (**Ufu 13:8**), ikiwa Yesu Kristo siyo Bwana wetu wa kweli basi kwenye kiwango cha utambulisho wetu kimsingi sisi kwa, uhakika ni “wakaaji wa dunia” ambao hufanya, kwa uhakika, kumwabudu mnyama. Amefunua hatari za wakati wote zinazohusika kwenye mahusiano yetu pamoja na jamii na tamaduni.

7. Maelezo ya “mnyama” atokaye baharini (**Ufu 13:1-10**) ni ubunifu wa Kristo. Kama vile *“mtu wa kuasi”* wa **2 Wathes 2:3-12**, kipengele muhimu sana cha mnyama wa Ufunuo siyo kisiasa au kiuchumi lakini ni kitheolojia. **Ufu 13:5-6; 17:3** hutilia mkazo kiburi cha mnyama na makufuru. Kwamba mnyama ni “mpinga Kristo” wa kweli—mshiriki mkuu wa Kitheolojia kwa Kristo na kile Kristo alichokiwakilisha—anaonekana kwenye usambamba mwingi baina ya Kristo na mnyama: (1) Mwenye upanga (linganisha na **Ufu 1:16; 2:12, 16; 19:15, 21** na **13:10**); (2) Mwenye pembe (linganisha na **Ufu 5:6** na **13:1, 11**); (3) Waliuawa, kwa neno lile lile la Kigiriki (*sphagizō*) lililotumika kuelezea vifo vyao (linganisha na **Ufu 5:6** na **13:3, 8**); (4) Kuinuka kwenye maisha mapya (linganisha na **Ufu 2:8; 5:6, 9; 13:8** na **13:3, 12**); (5) Walipewa mamlaka (linganisha na **Ufu 2:27; 5:1-9** na **13:2, 14**); (6) Wakivaa taji nyingi (linganisha na **Ufu 13:1** na **19:12**); (7) Wana kiti cha enzi (linganisha na **Ufu 13:2** na **3:21**); (8) Wenye mamlaka juu ya “kila kabila, lugha, watu, na mataifa” (linganisha na **Ufu 5:9; 7:9** na **13:7**); (9) Wenye wafuasi ambao majina yao yameandikwa kwenye vipaji vya nyuso zao (linganisha na **Ufu 13:16-17** na **14:1**); (10) Wakiabudiwa na ulimwengu (linganisha na **Ufu 5:8-14** na **13:4, 8**).

Kwa nyongeza, maelezo ya mnyama kama mmoja ambaye *“alikuwa na siyo na siyo na ndiye ajaye”* (**Ufu 17:8**) sambamba na maelezo ya Mungu kama mmoja *“ambaye ndiye na ambaye alikuwa na ambaye atakuja”* (**Ufu 1:4, 8; 4:8**). Kinyume na mmoja na mwingine, mnyama anayo majina ya kufuru yaliyoandikwa kwenye vichwa vyake (**Ufu 13:1; 17:3**); Kristo analo jina lililoandikwa juu yake ambalo hakuna alijuaye isipokuwa yeye mwenyewe (**Ufu 19:12**). Wale ambao wanalo jina la

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Mwanakondoo kwenye vipaji vya nyuso zao wamenunuliwa (Kigiriki. = *agoradzō*) kutoka duniani (**Ufu 14:1, 3**); wale ambao hawana jina la mnyama lililoandikwa kwenye vipaji vya nyuso zao hawawezi kununua (*goradzō*) duniani (**Ufu 13:17**).[47]

8. Mnyama atokaye duniani (**Ufu 13:11-17**). Mnyama wa pili "pia na ubunifu wa Mwanakondoo wa Kimasihi wa 5:6 na anao uhusiano wa kidhihaka pamoja na Mwanakondoo huyo. Yeye pia, ni Mwanakondoo mwenye pembe [**Ufu 13:11**]." (Beale 1999: 707) Mnyama wa pili kimsingi anayo majukumu ya kidini na ndiye baadaye aliyeitwa *"nabii wa uongo"* (**Ufu 16:13; 19:20; 20:10**). Mnyama huyu sambamba na *"mtu wa kuiasi"* mwenye heshima ya ushawishi wa kishetani (**Ufu 13:11; 2 Wathes 2:9**), ishara (**Ufu 13:13-15; 2 Wathes 2:9**), udanganyifu (**Ufu 13:14; 2 Wathes 2:10**), na kuabudu (**Ufu 13:12, 15; 2 Wathes 2:4**). Wanatheolojia humtambulisha mnyama atokaye duniani ("nabii wa uongo") kama "Viongozi wa dini ya Kiyahudi ambao walitafuta kuwashawishi Wakristo" kabla ya mwaka BK 70 (Chilton 1985: 181; angalia pia DeMar 1999: 259-60). Wengine humwona mnyama huyu kama "ibada au madhehebu ya kifalme" ya Rumi ya zamani ambayo sasa inaizidi Rumi au kama "udanganyifu wa kidini" (Johnson 2001: 196, 338). "Pale ambapo nabii wa kweli walipaswa kuwaongoza watu kumwabudu Mungu, nabii huyu aliwaongoza kuiabudu nchi. Mnyama huyu anaweza kuchukua maumbo mengi na anaweza kwa nyakati hata kuwa sawa na nchi, sawa sawa na manabii wa uongo kanisani (kama kwenye 2:2, 14-15, 20-24). Madhihirisho haya ya kinyama ya nabii wa uongo yaliyotukia kanisani pia yalionekana kwenye Agano la Kale, pale ambapo karibia unabii wa uongo huchukua nafasi kwenye jamii ya agano. Hili liliimarishwa na unabii wa Kristo kwamba manabii wa uongo na masihi watainuka kwenye jamii ya waamini yenyewe (Math. 24:5, 11 na sambamba na hayo). Yesu aliwafananisha manabii wa uongo na wanyama na kutabiri kwamba 'manabii wa uongo' 'watakuja . . . kwenye ngozi ya mwanakondoo lakini ndani yao ni mbwa mwitu wakali' (Math. 7:15). Picha ya mbwa mwitu kwenye ngozi ya mwanakondoo inaonyesha usaliti ndani ya makundi ya kanisa. . . . Kwa hiyo, picha hii na msingi wake unaonyesha udanganyifu ndani ya jamii ya Agano yenyewe. Pale ambapo mnyama wa kwanza alinena kwa sauti kuu na kwa ujasiri kinyume na Mungu, mnyama wa pili aliyafanya madai ya mnyama wa kwanza kusikika vizuri na yenye ushawishi. . . . Kwa hiyo, itachukua utambuzi wa Mkristo kutambua tabia ya uovu ndani ya mnyama wa pili." (Beale 1999: 707-08)

9. Jeraha la mauti kichwani na kupona kwa mnyama (**Ufu 13:3, 12, 14**).

a. *Jeraha la mauti kichwani mwa mnyama.* Neno la Kigiriki lililotumika kwa jeraha la mnyama ni *plēgē*, ambalo wakati wote hutafsiriwa "pigo." Penginepo popote kwenye Ufunuo neno hilo humaanisha hukumu au adhabu ya Kiungu iliyotolewa (**Ufu 9:18, 20; 11:6; 15:1, 6, 8; 16:9, 21; 18:4, 8; 21:9; 22:18**). **Ufu 13:14** inaongeza kwamba jeraha la mauti la mnyama lilitolewa kwa "upanga". Kwenye Ufunuo wakati wote upanga hufananishwa na hukumu ya Kimungu ya Masihi (**1:16; 2:12, 16; 19:15, 21**). Kumbukumbu ya upanga pia huonekana kwenye **Isa 27:1** ambayo inasema: *"Katika siku hiyo ya Bwana, kwa upanga wake ulio mkali, ulio mkubwa, ulio na nguvu, utamwadhibu lewiathani, nyoka yule mwepesi, na lewiathani, nyoka Yule mwenye kuzonga-zonga; naye atamwua yule joka aliye baharini."* Kumbukumbu zote hizi zinatuelekeza kwenye maana halisi ya *"jeraha la mauti"* linalomtesa mnyama: "Mahali popote kwenye kitabu ushindi wa kutosheleza pekee wa mnyama na joka ni Mwanakondoo aliyechinjwa, pamoja na watakatifu waaminifu (12:11; 19:19-21). Zaidi ya hayo, ni tukio la maisha na hasa kusulubiwa, kufufuka na kuinuliwa kwa Yesu ambalo linahusika na pigo hili la mauti kwa joka na mnyama (1:5; 5:9; 12:11). Mawazo sambamba na haya yanafanana kwenye mafundisho mengine ya Agano Jipya (Luka 10:17-24; 11:14-22; Yohana 12:31-33; Kol 2:15)." (Johnson 1981: 526) Vivyo hivyo, "pigo" la mauti kwa "upanga" kwenye **Ufu 13:3, 12, 14** "haliwezi kuelezea kifo halisi na kufufuka kwa mtu wa kihistoria [au wa (mtu) wakati ujao]" (Beale 1999: 689).

b. *Kupona kwa mnyama.* Yote yaliyo sambamba baina ya "mnyama" wa kwanza na Kristo, na usambamba wa nafasi ndani ya jamii ya Agano baina ya "mnyama" wa pili na *"mtu wa kuasi,"* huangazia umuhimu wa kitheolojia au asili ya Kiroho ya "Mpinga Kristo." Kwa maneno mengine, mambo yote ya kisiasa, kiuchumi, na masuala ya kijamii yanayoibuliwa na serikali na

[47] "Chapa ya mnyama" (**Ufu 13:16-17; 14:9-11**), kama muhuri wa Mungu juu ya Kanisa (**Ufu 7:3**), siyo "mchoro wan je wa tatuu au rangi juu ya mwili lakini badala yake ni ishara ya umiliki wa mnyama na utawala wa mawazo ya wafuasi wake (kipaji cha uso) na matendo (mkono wa kuume)" (Johnson 2001: 196). Chapa ya mnyama na muhuri wa Mungu "vimewekwa wazi kwenye kanuni za watu, vithaminisho, na imani" (Resseguie 2009: 136).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

tamaduni hukabiliana nasi pamoja na swali la msingi: Uaminifu wangu umeegemea wapi—pamoja na Kristo au pamoja na dunia? Suala hilo hilo, kwenye muundo tofauti, limeibuliwa na jeraha la mauti kichwani mwa mnyama na kupona kwake. Richard Bauckham anachunguza, "Usambamba baina ya 'kifo' na 'kufufuka' kwa mnyama na kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo kunaleta suala la ni kipi hasa kilicho cha Kimungu. Ni udhahiri wa mnyama kufanikiwa ambako kunastahili kuaminiwa na dini na kuabudu? Au ni udhahiri wa kushindwa kwa Kristo na kuuawa kwa mashahidi wa kweli kwa Mungu ambaye wakati wote anaweza kuaminiwa na Yeye pekee anastahili kuabudiwa?" (Bauckham 1993a: 452)[48]

10. Namba ya mnyama: 666 (**Ufu 13:18**).

a. *Nero na matumizi ya gematria.* Gematria ni mbinu ya siri ya kutafsiri maandiko kwa kuyawekea mbadala wa namba kwa herufi kweye baadhi ya maneno au majina. Wakati mwingine hutumika kujaribu kutafuta ni nani ambaye ni Mpinga Kristo. Toleo lililo maarufu sana la hli ni lenye msingi wake kwenye Nero *redivivus* ("Nero kuurudia uhai au kuwa hai tena") hadithi ambayo ilizunguka kwenye karne ya kwanza, i.e., Mfalme Nero kweli hakufa lakini alitorokea Parthia upande wa mashariki na atarudi pamoja na jeshi kubwa kuwatiisha wapinzani wote (Minear 1968: 248-50).[49] Ikiwa neno "Caesar Nero" likitafsiriwa kwenye Kiebrania, lingekuwa na namba zenye thamani ya 666 (Resseguie 2009: 191). Kwa hiyo, baadhi ya wasomi huamini kwamba Yohana alimtambulisha Nero kama mnyama (angalia Chilton 1985: 180-81; DeMar 1999: 26061).[50]

b. *Gematria ilishindwa kama mbinu ya utambulisho.* Hata hivyo kulifanyia rufaa wazo la Nero kwa baadhi, gematria wakati wote ilishindwa kama mbinu ya kumtambua mpinga Kristo. Kwanza, kujaribu hesabu halisi za baadhi ya majina ya binafsi ni kinyume na njia ya mfano ambayo kwayo tarakimu zimetumika kwenye Ufunuo na kwenye fasihi nyingine za mafunuo. Pili, yapo majina mengi, ya zamani nay a sasa, ambayo yatakuja kwenye 666 wakati yatakapotiishwa kwenye gematria (angaliaBeale 1999: 720-21; DeMar 1999: 231-38). Hta neno "mnyamat," wakati litakapofasiriwa kwenye Kiebrania, litafikia kwenye 666 (Resseguie 2009: 191). Kama ilivyo mbali nyuma kama karne ya pili, Irenaeus alitambua jambo lile lile: "Kwa hiyo lilikuwa la uhakika zaidi, na lenye hatari ndogo, kusubiria utimilifu wa unabii, kuliko kufanya majaribio, na kutoa kuhusika kwa kila majina ambayo yanaweza kujiwakilisha yenyewe, kwa hiyo kama majina mengi yanaweza kupatikana yakimiliki tarakimu zilizotajwa; na swali lile lile litabaki, baada ya yote, kubaki halijajibiwa" (Irenaeus 1885: 5.30.3).

Tatizo ni la kina zaidi ya uongo mwingi wa utambulisho wa Mpinga Kristo wenye msingi kwenye gematria kwa zaidi ya miaka elfu mbili iliyopita. Tatizo halisi ni matumizi ya gematria yenyewe. Matumizi yake yanafanana na kiinimacho au uchawi. Beale anaonyesha kwanini mbinu yenyewe siyo kile Yohana alichokuwa nacho kwenye ufahamu wake: "Hakuna ushahidi wa tarakimu nyingine yeyote kwenye kitabu iliyotumika kwa njia kama hiyo. Tarakimu zote zina maana ya fumbo na kufananishwa na baadhi ya kweli za Kiroho na kamwe hazihusishi aina yeyote ya hesabu halisi ya gematria . . . Ikiwa mfumo wa gematria wa Kiebrania au Kigiriki wa hesabu za uhalisia ungetumika kwa kiasi kikubwa hapa, kasha Yohana angewaonya wasomaji wake kwa kuandika kitu kama vile 'na tarakimu ya jina lake *Kiebrania* (au *Kigiriki*) ni 666.'" (Beale 1999: 721) Hili linapendekeza kwamba mbinu ya hesabu halisi kamwe haitatoa tafsiri sahihi, na kwamba kumbukumbu ya Yohana kwa 666 kamwe haikuwa na lengo la kusaidia kukuza matumizi ya gematria kabisa.

---

[48] Bila kujali mfanano, Beale anaeleza tofauti za msingi baina ya ufufuo wa mnyama na ufufuo wa Mwanakondoo: "Mwanakondoo kwa hakika alishinda ushindi wa mauti kwa ufufuo, lakini kuendelea kuwepo kwa mnyama siyo mabadiliko ya halisi ya kushindwa" (Beale 1999: 689). Hakika, **Ufu 17:8** inasema kwamba alikuja kutoka kuzimu tu kwa *"kwenda kwenye uangamivu."*

[49] Richard Bauckham (1993a: 384-452) amefanya utafiti wa kina wa matumizi ya Yohana ya hadithi ya kurudi kwa Nero, akijumuisha na kumbukumbu za kihistoria, Matumizi ya Yohana ya maneno ya Kiyahudi na ufunuo wa Kikristo Kupanda au kuinuliwa kwa Isaya, na utafiti wa kina wa umuhimu wa namba. Alieleza, "Simulizi ya kurudi kwa Nero kunathibitisha matumizi kwa Yohana kwa sababu angeyaasili kwenye mahitaji ya maono ya unabii wake wa ushindi wa Ufalme wa Mungu dhidi ya vidokezo vya dola ya Warumii kwa utawala wa Mungu" (Ibid.: 450-51).

[50] Schnabel, hata hivyo, anaona kwamba Yohana asingemtambulisha Nero kama Mpinga Kristo wa "mwisho" kwa kuwa Nero alifariki mwaka BK 68, wakati ambao Yohana aliandika Ufunuo miaka kadhaa baada ya hilo (Schnabel 2011: 190).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

11. Kuinuka kwa asili ya uovu. Kwa sababu mnyama anaonekana kuinuka kupita historia binafsi na falme, hesabu ya mnyama vile vile bila shaka imepita historia binafsi na falme. Hili limeonyeshwa kwa njia mbili.

a. *"Hesabu ya kibinadamu" (**Ufu 13:18**).* Msemo wa Kigiriki *"hesabu ya kibinadamu"* haina makala fafanuzi (i.e., neno (ya) "the") kabla ya "binadamu au mtu." Vivyo hivyo, "ingeweza kutafsiriwa kawaida kama 'hesabu ya kibinadamu' (i.e., hesabu ya ubinadamu), au isivyo kikawaida, ikimaanisha mtu binafsi, 'hesabu ya kibinadamu' (i.e., mtu binafsi maalum)" (Resseguie 2009: 189). Ufahamu wa "kawaida" wa "hesabu ya kibinadamu" kwenye **Ufu 13:18** imeonyeshwa kwa ukaribu wa mfanano wa Kibiblia—**Ufu 21:17**. Kwenye ayah ii Malaika alikuwa akiupima ukuta wa Yerusalemu mpya "kulingana na kipimo cha kibinadamu." Neno "binadamu" kwenye **21:17** halina makala fafanuzi mbele yake. Msemo "kipimo cha kibinadamu" kwa wazi hakionyeshi kipimo cha au kwa mtu maalum. Badala yake, lina maana ya kawaida. (Ibid.: 189-90)

Usambamba baina ya **Rev 13:18** na **21:17** inaonyesha kwa jinsi gani *yametofautiana*: kwenye **13:18** "mtu" au "binadamu" limetambulishwa na mnyama; kwenye **21:17** "mtu" au "binadamu" limetambulishwa na Malaika. "Usambamba na utofauti kwa hakika vinapendekeza kwamba alipo mnyama ubinadamu hupotea, Yerusalemu mpya huwakilisha kuinuliwa kwa binadamu kwenye nafasi ya Malaika" (Bauckham 1993a: 398). Hivyo, upo uwezekano mkubwa kwamba "kuondolewa kwa makala kwenye 13:18 huonyesha wazo la kawaida la kibinadamu, siyo baadhi ya watu binafsi maalum ambao wanaweza kutambuliwa tu kwa kutumia mbinu ya siri ya ukokotozi. Kwa hiyo, kwenye vifungu vyote *anthrōpou* [neno la Kigiriki kwa "mtu au binadamu"] ni maelezo au ubora wa kisasa, ili kwamba msemo hapa uweze kutoa'hesabu ya binadamu' (so RSV) au 'hesabu ya kibinadamu.'Ni hesabu ya kawaida kwa anguko la kibinadamu." (Beale 1999: 724)

b. *Umuhimu wa namba 666.* Namba sita hutangaza kutokutimia na kutokukamilika. "Namba saba inahusu ukamilifu na imerudiwa kwenye kitabu chote. Lakini 666 imeonekana hapa tu. Hili linatangaza kwamba sita tatu zinakusudiwa kama kuwa kinyume na saba za Mungu kwenye kitabu chote na kumaanisha kutokutimia na kutokukamilika. . . . Marudio ya sita tatu kunajulisha kuongezeka kwa kutokutimia na kushindwa ambako kunahitimishwa kwa mnyama zaidi ya penginepo pote ambako limeshuhudiwa angako la kibinadamu." (Beale 1999: 721-22) Au, kama Resseguie alivyoliweka, 666 ni mfano wa "kinyume cha sifa ya kibinadamu" (Resseguie 2009: 190). Milligan anafupisha: "Namba sita yenyewe huamsha hisia za hofu kwenye kifua cha Myahudi ambaye anahisi maana au umuhimu wa hesabu. Inaangukia chini ya namba saba ya utakatifu kama vile namba nane inavyoenda mbele yake. Namba hii ya mwisho humaanisha mengi zaidi ya umiliki rahisi wa Kiungu. Kama ilivyokuwa kwenye suala la tohara siku ya nane, 'siku kuu' ya sherehe ya siku ya nane, au ya kufufuka kwa Bwana wetu siku ya kwanza ya juma, ikifuatia siku saba za nyuma au zilizopita, huelezea mwanzo mpya wa utendaji wenye nguvu. Kwa mchakato unaofanana na huo namba sita ilichukuliwa kumaanisha kutokuwa na uwezo wa kufikia hoja ya utakatifu na bila matumaini kupungukiwa na huo. Kwa Myahudi kulikuwa na adhabu ya namna hiyo kuhusiana na namba sita hata pale iliposimama peke yake. Iandike mara tatu; acha iwepo mara nyingi mara kumi na kasha mara ya pilimara kumi mpaka utakapopata siri ya *sita* tatu zinazofuatana moja na nyingine, 666; na tutakuwa tumewakilisha nguvu ya uovu kuliko ule ambao unaweza kuwa hakuna mmoja ulio mkuu zaidi, ukali wa mauti kuliko ambao ungeweza kuwa hakuna ulio mbaya zaidi." (Milligan 1896: 235) Kwenye karne ya pili Irenaeus alifikia kwenye hitimisho linalofanana na hili. Alichukulia kwamba 666 humaanisha "inahitimisha uovu wote ambao uliwahi kuwepo katika kipindi cha miaka elfu sita" (Irenaeus 1885: 5.28.2).

H. *Ufu 15:5-16:21: Hukumu za vitasa saba*

Kwenye kifungu hiki Mungu anawaadhibu wasiomcha kipindi cha nyakati za mwingiliano wa matukio na kuleta hukumu ya mwisho siku ya mwisho kwa sababu ya mateso yao na Ibada ya sanamu au Uasherati. Kama tulivyoona mwanzoni kwenye mapigo ya tarumbeta na vitasa yalitokea kwenye mpangilio ule ule na kuhusisha: (1) nchi; (2) bahari; (3) mito; (4) jua; (5) ulimwengu wa uovu; (6) Frati; na (7) hukumu ya mwisho ya ulimwengu pamoja na "umeme, sauti, radi, na tetemeko la nchi' na 'dhoruba kuu." Kwa upeo huu, ni lazima tena tuone kwamba Ufunuo *siyo* simulizi ya mtiririko wa nyakati. Kama na mihuri na tarumbeta, vitasa siyo

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

lazima uwe ni mtiririko lakini yaweza kuwa ni ya wakati uo huo. Hivyo, kuhusiana na kitasa cha sita (giza), "Tunaambiwa juu ya *maumivu yao na vidonda vyao.* Lakini maumivu na vidonda siyo athari zilizosababishwa na giza. Kwa hiyo, waweza kuwa tu, wale wa kitasa cha kwanza, hitimisho linalothibitishwa na neno 'mapigo' badala ya pigo [**16:9**]." (Milligan 1896: 268, fafanuzi imeongezwa.)

Kama ulivyokuwa ukweli kwenye tarumbeta, hukumu za kitasa zimechukuliwa kwenye picha ya mapigo ya kitabu cha Kutoka:

kitasa cha 1 (vidonda) (**16:2**)	linalingana na pigo la 6 (**Kut 9:8-11**)
vitasa 2 na 3 (maji kuwa damu) (**16:3-6**)	linalingana na pigo la 1 (**Kut 7:20-25**)
kitasa cha 5 (giza) (**16:10-11**)	linalingana na pigo la 9 (**Kut 10:21-23**)
kitasa cha 6 (vyura) (**16:12-16**)	linalingana na pigo la 2 (**Kut 8:2-9**)
kitasa cha 7 (dhoruba) (**16:17-21**)	linalingana na pigo la 7 (**Kut 22-26**)

1. Vitasa vya sita na saba (**Ufu 16:12-21**). Vitasa vya sita na saba vimeunganishwa. Kitasa cha sita kinauandaa ulimwengu kwa vita ya mwisho kinyume na Mungu; matokeo yake yanaonekana kwenye kitasa cha saba, ambacho ni *parousia.* Lengo juu ya Shetani, "kusanyiko la vita" ya ulimwengu kinyume na Mungu na watu wake, na kukamilika na kushindwa kwa mwisho kwa maadui wa Mungu, kunaonyesha kwamba vitasa vya sita na saba vinalingana na **Ufu 20:7-10** (pia vinafanana na **19:17-21**). Milligan anaonyesha sababu ya uwezekano wa kwanini kitasa cha saba kilimwagwa juu ya anga: "Kitasa cha saba au cha mwisho kilimwagwa juu ya anga, wazo hapa la kama ulimwengu wa huyo mfalme wa ulimwengu ambaye pia ni 'mfalme wa uwezo wa anga' [**Efe 2:2**]" (Milligan 1896: 268, fafanuzi imeongezwa.).

Kwamba Kanisa litakuwepo wakati wa kipindi hiki kunaonekana kutoka **16:15** ambayo inasema, *"Tazama. Naja kama mwivi. Heri akeshaye, na kuyatunza mavazi yake, asiende uchi hata watu wakaione aibu yake."* Kama vile tulivyoona mbeleni muunganiko baina ya mihuri na Hotuba ya Mlimani, hapa tunaona muunganiko ule ule baina ya vitasa na Hotuba ya Mlimani. *"Naja kama mwivi"* kunarudia onyo la Kristo kwa Kanisa kwenye **Math 24:43** na **Ufu 3:3**. *"Heri akeshaye"* kunarudia mashauri ya Kristo kwa Kanisa kwenye **Math 24:42-44**, **45-51**; **Math 25:1-13**, **14-30** kwamba tunapaswa kuchukua tahadhari, kuwa tayari, tumejiandaa, na waaminifu kufanya kile tupaswacho kufanya.

2. Kukauka kwa mto Frati kuandaa njia kwa wafalme watokao katika maawio ya jua (**Ufu 16:12**). Kama ilivyo kwenye mengi katika Ufunuo, picha ya kitasa cha sita msingi wake ni kwenye kiolezo cha kihistoria ambacho kimetumiwa kitaipolojia. Kukauka kwa mto Frati na wafalme kutoka maawio ya jua yanaonekana kuchukuliwa kutoka kwenye hukumu ya Mungu juu ya Babeli, ambayo yenyewe inafuata mfano wa kukauka kwa bahari nyekundu na mto Yordani na kufuatiwa na Kutoka (angalia **Kut 14:21-22; Yosh. 3:16; 4:23**). Isaya na Yeremia walitabiri kwamba hukumu juu ya Babeli itahusisha kukauka kwa mto Frati (**Isa 11:15; 44:27-28; Yer. 50:38; 51:36**). Nabii zilitimizwa kwa maji kugawanyika kwa ajili ya Waashuru (angalia **Isa 44:27-28**). Hili liliyaruhusu majeshi ya Waashuru kuingia Babeli kusikotarajiwa na kuishinda (Beale 1999: 827). Ashuru, watawala na wafalme wake, "walitoka kwenye maawio ya jua yaani mashariki" (**Isa 41:2, 25; 46:11; Yer 50:41; 51:11, 28**).

Yohana alichukulia kuanguka kwa Babeli ya kihistoria na kuijumuisha kuifanya ya kiulimwengu kwenye Ufunuo: "Kama kwenye Kutoka na hasa kwenye anguko la Babeli ya kihistoria, kukauka tena kwa mto Frati kunaonyesha utangulizi wa kuangamizwa kwa Babeli ya siku za mwisho. Na kama vile Babeli ilivyofanywa ya kiulimwengu na kuwa ishara [angalia majadiliano juu ya Babeli hapo chini], hivyo mto Frati hauwezi kuwa kumbukumbu halisi ya kihistoria kwa mto Frati wa kisasa uliopo Iraki, Syria na Uturuki lakini lazima liwe fumbo na la kiulimwengu, bila kujali wale wasemao au wanaodai kwamba kumbukumbu ni uhalisia. Hili limeonyeshwa kwa 17:1, pale kahaba wa Babeli 'alipokaa juu ya maji mengi,' ambayo ni njia nyingine ya kuzungumzia'mto Frati na maji yake' (16:12) 'Maji mengi' ya 17:1 ni fumbo lililotafsiriwa kama 'watu na makutano . . . na mataifa na lugha' kwenye 17:15. . . . Kwa hiyo, kukauka kwa maji yam to Frati ni picha ya jinsi mkutano mkubwa wa waamini wa dini za Babeli duniani kote watakavyoacha kuwa waaminifu kwa Babeli [angalia **17:15-18**]. Kupuuzwa kwa Babeli ni utangulizi wa hukumu ya Babeli, na hukumu ya mwisho yenyewe." (Ibid.: 828)

Kuna kutokukubaliana kuhusiana na utambulisho wa *"wafalme wa maawio ya jua au wa Mashariki":*

a. "Wafalme wa Mashariki" kama wasioamini. Wengi huwaona "*wafalme wa Mashariki"* kama "ujumla wa ulimwengu kwa fumbo na siyo tu Babeli na mto Frati lakini pia Ashuru na wafuasi

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

wake, 'wafalme kutoka maawio ya jua,' ambao kitafsiri waliongezwa kwenye 'wafalme wa wakaaji wa dunia au nchi yote' (16:14; cf. 18:18)" (Beale 1999: 828). Mtazamo kama huo ni kwamba "wafalme wa mashariki—makundi ya wapagani—wataunganisha nguvu na wafalme wote wa ulimwengu (wakaaji) kufanya vita na Masihi, kwa kuwa vita vya nyakati za mwisho juu ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi ni wazi ' (vs. 14)" (Ladd 1972: 213).
b. "Wafalme wa Mashariki" kama waaminio. Wengine huwaona *"wafalme wa mashariki"* kwenye istilahi chanya. Sababu ni kama zifuatazo: Neno la Kigiriki kwa "mashariki" (Kigiriki = *anatol*ē; ambalo pia linamaanisha "kuinuka" au "nafasi ya kuchomoza kwa jua") "lilizoelewa kama ishara ya Masihi kwenye nyakati za Agano Jipya. Lilionyesha kitu Fulani au mtu wa asili ya Mbinguni. Penginepo Ufunuo ulitumia neno hili kwa maana hii [**7:2**], na uwezekano mkubwa kwamba kuandikwa kitabu kwa umakini kusibadilishe maana ya ishara kwenye sura zitakazofuata. . . . 'wafalme wa mashsriki' waweza kuwa wamekusudiwa kama tofauti ya moja kwa moja ya 'wafalme wa dunia yote' waliotajwa kwenye kifungu hicho hicho, na wanaweza kuwawakilisha viumbe wa mbinguni ambao walikuja kuwaokoa watakatifu, kama wafalme wa Midiani kutoka mashariki walivyokuja pamoja na Ashuru kuokoa Israeli ya zamani kutoka Babeli." (Ford 1979: 268) Kwa kuwa kitasa cha sita ni maandalizi kwa vita ya mwisho na *parousia,* Kwa hiyo *"wafalme wa mashariki"* wanaweza kuzungumzia majeshi ya mbinguni ambayo yanafuatana na Kristo kwenye **Ufu 19:11-16**.

I. ***Ufu 17:1-19:10: Hukumu ya mwisho ya Babeli***

Kama ambavyo ilionekana penginepo kwenye kitabu chote cha Ufunuo, ubinadamu umehusisha vitu viwili, na viwili pekee, aina au makundi: hayo mawili ni waliojitoa kwa ajili ya Kristo na wale ambao hawajajitoa kwa ajili ya Kristo. Babeli inawakilisha mfumo na mtazamo wa ulimwengu wa kila kitu na kila mtu ambaye siyo wa Kristo. Mfumo wa ulimwengu unaonekana wenye nguvu nyingi lakini ukibeba mbegu za kuuangamiza wenyewe. Hukumu ya Mungu juu ya uchumi wa wasiomcha Mungu, tamaduni, na mfumo wa kidini wa dunia unaongoza kwenye kuanzishwa kwa utawala wa milele wa Mungu (**Ufu 19:6**) na kuungana pamoja na watu wake (**Ufu 19:7-9**). **Ufu 13:4** unaibua swali, *"Ni nani awezaye kufanya vita naye [mnyama]?"* Hili ni jibu kwenye **Ufu 17:14**: Mwanakondoo na wale walio pamoja naye (*"walioitwa na wateule na waaminifu"*) watamshinda mnyama kwa sababu Mwanakondoo ni *"Bwana wa mabwana na Mfalme wa wafalme."* Kwenye bado picha nyingine inajirudia, watakatifu wanahakikishwa, damu ya waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu inalipizwa, na maombi ya **Ufu 6:10** yanajibiwa.

1. Babeli mkuu, mama wa makahabas (**Ufu 17:1-5, 9, 15, 18**) kwenye mazingira yake ya karne ya 1st.
Wachambuzi wengi waliitambulisha Babeli kama Rumi, msingi ukiwa juu ya kumbukumbu ya milima saba (**Ufu 17:9**) (e.g., Bauckham 1991: 52; Schüssler Fiorenza 1991: 97; Beale 1999: 869-70). Neno la Kigiriki ambalo Biblia Toleo Jipya la Kimataifa (NIV) limelitafsiri kama "vilima" ni wingi wa *oros* ambalo ni "mwonekano wa kiasi cha juu wa nchi ambao unaonekana kwa juu kuliko bounos ('mwonekano mdogo wa kilima')" (Danker 2000: *"oros,"* 724). Vivyo hivyo, tafsiri nyingi za Biblia (e.g., ESV, NAS B, NKJV, and RSV) hutafsiri istilahi hiyo kama "milima" badala ya "vilima." Ingawa kumbukumbu bila shaka ni kwa Rumi, matumizi ya *oros* kwenye **17:9** yanapendekeza kwamba "Babeli mkuu" ipo juu zaidi ya Rumi ya kihistoria kwa kuwa vilima vya Rumi kwa hakika ni vyenye mwonekano mdogo sana ukilinganisha na vilima vya Palestina.[51] Kwa hakika, ukweli kwamba Yohana alitumia jina "Babeli mkuu" badala ya "Rumi" kunaashiria kwamba hakuufunga au kuuwekea ukomo utambulisho wake kwa dola ya Rumi iliyopo au jamii. Wakati Yohana akitumia nguvu ya Rumi, uchumi, na tamaduni kama mazingira ya kihistoria kwa mtazamo wake wa Babeli mkuu, Rumi inaonekana kama mfano au "aina". Hasa hasa, Rumi au Babeli inaonekana kama *kishawishi cha uovu* juu ya watu (i.e., ni "kahaba").[52]

Vipo vyanzo viwili vikuu kwa mtazamo wa Yohana juu ya Babeli mkuu: Unabii wa Yeremia kinyume na Babeli ya kihistoria (**Yeremia 50-51**) na unabii mkuu wa Ezekieli kinyume na Tiro

[51] "Mwinuko au urefu wa sehemu ya kati ya Warumii inafikia kutoka urefu wa mita 13 au (futi 43) juu ya usawa wa bahari (katika msingi wa au sehemu ya chini ya Pantheon) hadi mita 139 au (futi 456) juu ya usawa wa bahari (kilele cha Monte Mario)" ("Rome" 2012: n.p.).

[52] Babeli iliitwa *"Mama wa Makahaba"* (**Ufu 17:5**). Hii ni lugha ya fumbo ikionyesha "yeye ambaye anavutia, kushawishi, kudanganya na kuwavuta watu mbali na Mungu" (Hendriksen 1982:167). Kuvutiwa kama huku kunafunua kwamba msingi wa kujitoa kwa watu na uaminifu wao ni kwa ulimwengu (Schnabel 2011: 208).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

(**Ezekieli 26-28**).[53] Utafiti wa kina wa Richard Bauckham wa sehemu hii ya Ufunuo ilimpelekea kuhitimisha kwamba kile kinachoonekana hapa kimsingi ni mafungu mawili ya uovu: kwanza, utamaduni, unyonyaji wa kiuchumi na rushwa; na pili, uovu au rushwa ya kidini (Bauckham 1991: 4790). Bila shaka, vilihusiana: Yesu wakati wote aliwaonya waaminio kuhusu ukweli kwamba mtego wa utajiri unaweza kumgeuza mtu, kulisonga neno kwenye maisha ya mtu, na hivyo kuwa Bwana mpya wa kweli wa mtu huyo (e.g., **Math 6:19-24; 13:7, 22; 19:16-30; Marko 4:7, 18-19; 10:17-25; Luka 8:7, 14; 12:13-21; 16:13**). Paulo alifanya jambo lile lile (e.g., **Kol 3:5-6; 1 Tim 3:3; 6:6-11**).

Picha za kahaba, zimechukuliwa kutoka kwenye nabii za Agano la Kale kuhusiana na Tiro (**Isa 23:15-18; Ezekieli 26-28**), kimsingi inazungumza kwa ya kwanza kati ya miundo miwili ya rushwa au uharibifu: "Kumbukumbu hapa zipo wazi kwa shughuli mabalimbali za kibiashara ambazo kwazo mji wa Tiro ulipata utajiri. Shughuli za kibiashara za Tiro zililinganishwa na kahaba au Malaya kwa sababu ziliyahusisha mataifa mengine kwa ajili ya kupata faida. . . . Kwa maneno mengine, Rumi ni kahaba kwa sababu mahusiano yake na watu wa dola yake ni kwa faida yao wenyewe ya kiuchumi. . . . Rumi inapendekeza umoja wa ulimwengu wa Mediterania, usalama, utulivu au uimara, hali ya kufanikiwa. Lakini mtazamo wa Yohana wa faida hizi siyo kile kinachoonekana: ni fadhila za kahaba, zilizonunuliwa kwa gharama kubwa." (Bauckham 1991: 54-56)

2. <u>Orodha ya bidhaa (**Ufu 18:12-13**).</u> Bauckham analinganisha na maelezo ya Ezekieli ya biashara ya Tiro kwenye **Ezek 27:12-25** na maelezo ya Yohana juu ya biashara ya Rumi na kuhitimisha kwamba maelezo ya Ezekieli yalikuwa mwonekano sahihi wa biashara ya Tiro kwenye karne ya sita KK na orodha ya Yohana ya bidhaa ni orodha sahihi ambayo Rumi iliagiza kwenye karne ya kwanza BK (Bauckham 1991: 59).

Yohana anahitimisha orodha ya bidhaa zake kwenye **18:13** kwa kuwataja watumwa. Utumwa ulikuwa ni msingi wa mfumo wa uchumi wa Rumi. Bado jinsi Yohana alivyoelezea tangazo la utumwa kama sehemu ya bidhaa za Babeli mkuu ni kwa kina cha kitheolojia: "Kwamba Yohana anatoa maneno yote ya kawaida ya utumwa kwenye soko la utumwa ['miili'] na maelezo ya kimaandiko ya utumwa ['nafsi za watu'] lazima imaanishe kwamba alikusudia kuzungumzia juu ya biashara ya utumwa. Analiweka wazi kwamba watumwa siyo tu mizoga ya wanyama kununuliwa na kuuzwa kama bidhaa au mali, lakini ni wanadamu. Lakini kwenye nafasi ya fafanuzi mwishoni mwa orodha, hili ni zaidi ya maelezo ya biashara ya utumwa. Ni maelezo juu ya orodha nzima ya bidhaa. Inahusisha ukatili usio wa kibiadamu, dharau kwa maisha ya wanadamu, ambayo kwayo mafanikio na anasa zote za Rumi zilikaa." (Bauckham 1991: 79)

3. <u>Wale waombolezao juu ya Babeli (**Ufu 18:3, 9-11, 14-19**).</u> Kwenye **Ufunuo 18**, Yohana anaona kwamba makundi matatu ya watu wanaomboleza kwa ajili ya kuangamizwa kwa Babeli mkuu: *"wafalme wa nchi"* (**18:9**); *"wafanyabiashara wa nchi"* (**18:11**); na *"kila nahodha, msafiri, baharia, na wote watendao kazi baharini"* (**18:17**). "Hawa hasa ni watu ambao kibinafsi walinufaika kutokana na unyonyaji wa kiuchumi wa dola ya Rumi. Wanachokiombolezea ni kuangamizwa kwa chanzo cha utajiri wao wenyewe." (Bauckham 1989: 97)[54]

4. <u>Ukomo wa Babeli siyo Rumi bali ni ulimwengu wote.</u> Ingawa mazingira ya **Ufunuo 17-18** yaweza kuwa kijamii, kiuchumi, kisiasa, na mazingira ya kidini kwa siku zake mwenyewe, Ufunuo wa Yohana ni mbali zaidi ya Rumi. Ingawa kuna baadhi ya alama za kuitambua karne ya kwanza ("vilima saba"; orodha ya bidhaa), "ni vichache toshelevu kufanya matumizi mapya ya picha kulinganisha kirahisi na mazingira" (Bauckham 1993b: 156). Hili linaonekana kwenye lugha aliyoitumia Yohana. Kwenye maelezo yake ya Babeli kama *"kahaba mkuu"* na *"mama wa makahaba"* (**Ufu 17:1, 5**; angalia pia **Ufu 17:2, 4, 15; 18:3, 7, 9**), Yohana anasimama kwenye mstari mrefu wa manabii ambao walitumia lugha ya mahusiano ya kingono yasiyokuwa halali kuhukumu udhalimu wa kiuchumi, rushwa ya kitamaduni, na uasi wa kidini. Kwa mfano, **Isa 23:1-18** anaihukumu Tiro kama kahaba kwa mazoea yake ya

[53] Maelezo pia yamefanywa kwa wale wote weye maneno machache kinyume na Babeli na Tiro wanaopatikana miongoni mwa manabii wa Agano la Kale (Babeli: **Isa 13:1-14:23; 21:1-10; 47; Yer 25:12-38**; Tito: **Isa 23**) (Bauckham 1991: 54). Kwenye maelezo kwa maneno haya ya Agano la Kale lakini yalitafsiriwa tena kutumika kwa Warumii ya siku zake na zaidi ya Warumii ya siku zake, Yohana amesimama kwenye mstari wa manabii wa Kibiblia, na Yesu mwenyewe, ambaye aliyachukua maneno yaliyovuviwa ya tamaduni za kinabii na kuyapa maana na matumizi mapya.

[54] Bila shaka, mtazamo wa Yohana, siyo ule wa watu wa *nchi* na *bahari* (**Ufu 18: 9, 11, 17**) lakini ni ule wa *mbinguni* (**18:20**). Kwa mtazamo wake, kuanguka kwa Babeli ni sababu ya kufurahi na kuabudu na kumsifu Mungu (**18:20; 19:1-6**).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kibiashara. Ezekieli anaihukumu Yerusalemu kama kahaba kwa uasherati wake, rushwa ya kitamaduni, na udhalimu wa kiuchumi (**Ezek 16:1-59**). Kitabu chote cha Hosea ni picha ya mwonekano wa "ukahaba" wa Israeli kwenye matumizi yake ya fedha na rasilimali (**Hos 2:5-9**), uasherati wake (**Hos 2:11-13; 4:11-13; 13:1-2**), na rushwa yake ya kitamaduni kwa ujumla (**Hos 4:1-2, 7-8, 14; 10:13**).

Zaidi ya hayo, Yohana wakati wote alizungumza kwenye lugha ya "kiulimwengu": majaribu yatarajiwayo *"iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote"* (**Ufu 3:10**); mnyama anayo mamlaka *"juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa"* na *"na wote wakaao juu ya nchi watamwabudu au kumsujudia yeye"* (**Ufu 13:7-8**);[55] wafalme "*wa ulimwengu wote"* watakusanyika kwa vita ya mwisho (**Ufu 16:14**); Uovu wa Babeli na kuyadanganya*"mataifa yote"* (**Ufu 14:8; 18:3, 23**) na hatia yake ya damu*"ya wale wote waliouawa juu ya nchi"* (**Ufu 18:24**).

Kama vile mnyama wa **Ufu 13:1-2** inajumuisha vipengele vyote vya wanyama wanne wa **Dan 7:3-8** pamoja, hivyo Babeli mkuu anajumuisha mwenyewe uovu wote wa miji mikuu miwili iliyojaa uovu (Babeli na Tiro) ambayo juu yake msingi wa unabii umewekwa. Hivyo, Babeli siyo mji binafsi au pekee, au hata dola pekee au binafsi, lakini inaonekana kuwa taasisi ya kidunia. Inaweza kuonekana kuwa kama "maelezo ya mwisho ya ushawishi wa watenda maovu wa kidunia" (Smalley 2005: 427), au "madhihirisho ya mwisho ya historia yote ya mataifa yasiyomcha Mungu . . . ambayo yataishawishi dunia yote kuabudu kile ambacho siyo Mungu" (Ladd 1972: 222), au vifaa vya ushawishi na anguko la tamaduni za kibinadamu (Johnson 2001: 17, 246, 268-69n.2, 339). Hakika, "Babeli ya Yohana ni kilele cha mwisho cha biashara iliyoanzia Babeli kwenye Mwanzo 11: miaka mingi ya biashara ya kibinadamu ya kuunganisha jumuiya za kibinadamu kumpinga Mungu. . . . Hivyo Babeli ya Ufunuo siyo maono pekee maalum ya picha ya Rumi ya sasa, lakini pia picha ya nyakati za mwisho. Kwa maneno mengine, ni zaidi ya kumbukumbu yake ya asili na kuwa ishara ya historia yote ya kuwaunganisha watu waovu ambao anguko lao litakuwa mwisho wa historia." (Bauckham 1989: 93)[56]

Kwenye mwonekano wake wa Babeli mkuu, Yohana tena anawakabili wasikilizaji wake na uchaguzi baina ya mnyama au Mwanakondoo, dunia au kanisa, wale wakaao juu ya nchi au wale ambao uraia wao ni mbinguni, kwa sababu Babeli ni "kinyume na ufalme"—ya kuvutia au inayoshawishi, mbadala wa kuzungukia wageni kwenye ufalme wa Mungu.[57] Thomas Torrance anahitimisha, "Inaonekana kwamba Babeli ni ustaarabu wa dunia yote na tamaduni, zenye kushangaza kwenye sayansi na sanaa na biashara zake, lakini ikiburuzwa na kiburi na kuleweshwa na mafaikio yake makubwa. Wakati uo huo ni ajabu kuchanganya nguvu ya dunia na dini, ya Upagani na Ukristo, ambavyo vitakuwa kikwazo kikubwa kwa Injili ya kikristo. Siri yake ya ndani imefunuliwa mwishoni kama utawala mkuu wa Shetani ambao unatamani kujiimarisha wenyewe milele kwenye uumbaji wa Mungu, kwenye uhasama mkubwa kwa utawala ambao huwa juu ya ulimwengu kutoka juu, Ufalme wa Mungu." (Torrance 1959: 115)

5. <u>Asili ya kiroho ya Babeli.</u> Kama ilivyozungumzwa hapo juu, vipo vipengele viwili vya uovu wa kibinadamu kwa Babeli mkuu: uchumi wa kitamaduni na dini. Kipengele cha kidini cha nguvu ya ushawishi wa uovu wa Babeli mkuu chaweza kuonekana kutoka kwenye kumbukumbu za Agano la Kale "Ikijumuishwa na ukweli kwamba Babeli ni kahaba, kuangamizwa kwa moto [**Ufu 18:8**] kunatuongoza moja kwa moja kwenye wazo la tabia za mji za kiroho, na siyo tu la kijamii, au kisiasa,

[55] Sawa na hilo, *"maji mengi"* ambayo juu yake aliketi kahaba mkuu wa Babeli (**Ufu 17:1**) wazi wazi imefafanuliwa kuwa *"jamaa na makutano na mataifa na lugha"* (**Ufu 17:15**); cf. **Ufu 5:9; 7:9** pale kanisa linapotolewa *"kutoka kila kabila na lugha na jamaa na taifa."*

[56] Babeli mkuu inapita Warumii ya kihistoria na kuwakilisha udanganyifu wa wote wa ulimwengu ni madhubuti pamoja na kumbukumbu ya *"wafalme saba ambao mmoja ni wa nane"* kwenye **Ufu 17:9-11**. Hii yaweza kuwa "kiashiria cha nahau ya Kiebrania, 'nambari iliyopangwa katika daraja la usemi,' ambayo inatumia namba mbili zinazofuatana sambamba. Kwenye jambo hilo hilo nahau hiyo inaonyesha kwamba tarakimu ni kielelezo badala ya ukamilifu (Mith 6:16; 30:15, 18, 21, 29), lakini wakati namba saba na nane zinapotumika kwa njia hii, zinaonekana kuonyesha kusikokuwana mipaka lakini namba toshelevu (Mhubiri 11:2; Mik 5:4[5]). . . . Matumizi haya yaweza uthibitisha nini tutakachokihesabia haki kwenye hukumu ya kila kesi: kwamba namba saba na nane za Yohana hazipaswi kuchukuliwa kiuhalisia, kama kufafanua ni watawala wangapi wa Warumii watakaokuwepo kwa uhakika kabla ya parousia, lakini kama kiashiria cha uovu wote, watawala wanaopinga Ukristo wanaweza kuwepo kabla ya kuongezeka kwa uovu wao wenyewe kutakakoleta uharibifu wake wenyewe." (Bauckham 1993a: 405)

[57] Hivyo Yohana annawachangamoto Wakristo kutafakari jamii yao wenyewe. Kama Bauckham anavyosema, "Kila jamii ambayo kofia ya Babeli inawakaa ni lazima waivae. Kila jamii itakayopendelea mafanikio ya uchumi wake wenyewe kwa gharama za wengine itajiweka chini ya hukumu ya Babeli." (Bauckham 1993b: 156; angalia pia Schnabel 2011: 211-12)

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

au kibiashara. Kulingana na sharia za Musa, kuchomwa moto kulikuwani adhabu ya uasherati kwenye kesi ya binti wa kuhani [**Lawi 21:9**]. . . . Hitimisho la kufikiwa ni kwamba Babeli ni mji wa Kiroho." (Milligan 1896: 309, 310)

Kwenye Biblia yote, lugha ya ukahaba, uzinzi na uongo ni sawa na uzinzi wa kiroho (i.e., kumwacha Mungu na kuiandamia miungu mingine na kutokumcha Mungu) (angalia, e.g., **Yer 3:6-10; Ezek 16:15-22; Hos 2:2; 4:12; Mal 2:13-16; 1 Wakor 6:15-18; Yak 4:4; Ufu 2:18-22; 14:8; 17:1-5; 18:1-3; 19:1-2**). Desmond Ford anaonyesha, "Wakati ni kweli kwamba Maandiko yanatumia ishara ya kahaba kwa miji kama vile Tiro na Ninawi [kuonyesha uchumi na uovu wa kitamaduni] ni zaidi sana mara nyingi hutumika kuwapotosha watu wa Mungu" (Ford 1979: 270). Ford anaendelea kujadili kile alichokiona kama historia halisi ya ishara alizozitumia Yohana kuhusu Babeli mkuu: "'Kahaba' na siyo 'mzinzi' *ni* mfano wa kukubalika zaidi, kwa kuwa msisitizo ni juu ya wapenzi wengi na ujira upatikanao. Asili ya uhalisia wa ishara kwenye Ufu. 17, unapatikana kwenye Yer. 2:33-34 na 3:1-11, pale ambapo Yuda ni kahaba (Yer. 2:20) mwenye alama juu ya kipaji chake cha uso (Yer. 3:3), ambaye husababisha makosa kwa wengine (Yer. 2:33), na 'ambaye juu ya nguo zake imeonekana damu ya roho zao maskini wasiokuwa na hatia' (Yer. 2:34). Amejivika vazi jekundu (Yer. 4:30) na mapambo ya dhahabu. Wapenzi wako wanakudharau (Yer. 4:30) na kutafuta maisha yake. . . . *Porn*ē [malaya; uzinzi] limetumika kwenye LXX [Agano la Kale la Kigiriki] kwa uchache mara hamsini kuelezea uzinzi wa Kiroho wa Israeli na Yuda. . . . Hoja hii, kama ilivyotumiwa kwenye utafiti huu, haimaanishi kukataa hoja zinazojulikana sana kwa Rumi. . . . Badala yake zinamaanisha kuonyesha kwamba Yohana aliona mbali zaidi ya Rumi pekee, na kwamba hasa alijihusisha na uasi wa mwisho ambao utakuwa kama kiini chake kwa mambo ya mahusiano na Mungu badala ya mambo ya kisiasa. Zaidi ya hayo, aliandika kuwatambua Wakristo, na siyo wenyeji wasioamini wa Rumi. Kwa hiyo, alikusudia kwa mwonekano wake kulionya kundi, kwa kuhofia kwamba wanachama wake wasiongozwe na Mpinga Kristo kwenye uzinzi wa Kiroho." (Ibid.: 270, 304n.159)

Kwa hakika uovu wa kidini na kiroho wa Babeli mkuu ulikuwepo kwenye karne ya kwanza. Bauckham anajadili asili ya uovu na ustaarabu wa kidini kwenye mazingira ya karne ya kwanza ambayo Yohana aliandika: "Kutokana na mtazamo wa Wakristo Wayahudi wa wakati wa Yohana, siasa ya dini ya Rumi ilikuwa aina mbaya zaidi ya dini ya uongo, kwa kuwa iliyapendelea madai ya Rumi juu ya malengo yake na kufunika uovu wake kwenye vazi la uaminifu wa kidini. Hivyo, kwa Yohana, uovu wa kiuchumi wa Rumi na ushawishi wake movu wa dini ya kitaifa unaenda mkono kwa mkono. . . . Kwenye mtazamo wa Yohana, maovu ya Rumi yalionekana kwenye mateso yake kwa Wakristo, kwa sababu hapa maelezo ya Rumi yenyewe yanapingana na ubwana wa Mwanakondoo ambao kwa huo Wakristo waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu walibeba ushuhuda na hivyo kile kilichofunikwa na polisi wa dola yote ya Rumi kuwekwa wazi." (Bauckham 1991: 57-58)

Moja ya kipengele hiki cha uovu wa kidini waweza pia kuwa ushirikiano baina ya Wayahudi wa karne ya kwanza na Warumi. Baadhi ya wachambuzi wanamtambulisha kahaba na kutokutii kwa Israeli, hasa Yerusalemu (McDurmon 2011: 2; Chilton 1985: 187-88 [Yerusalemu ni kahaba; ameonekana kama "aketiye juu ya mnyama" (Ufu 17:3) inawakilisha "utegemezi wake juu ya Dola ya Rumi kwa uwepo wa taifa lake na nguvu"]). "Maelezo yaliyopo kwenye [**Ufu 17:6; 18:24**] ya kahaba kuwaua watetezi wa neno la Mungu ni kumbukumbu ya wazi ya madai au mashitaka ya Yesu kinyume na Yerusalemu (Mt 23:29–39). . . . Wakati Yohana anazungumzia juu ya mnyama kumgeukia kahaba na kumwangamiza [**Ufu 17:16-18**], kwa uwezekano wote alizungumzia hukumu ya Mungu ambayo itaipata Yerusalemu kwa ushirikiano wake na utawala mwovu." (Pate and Haines 1995: 43)

Kama ilivyokuwa kweli na kuheshimiwa na tamaduni na rushwa ya kiuchumi, rushwa ya kidini ya Babeli mkuu haikuishia kwenye Rumi ya karne ya kwanza. Yohana hasa hakuwa anavutiwa na siasa zasasa na hali ya kiuchumi *hasa*, ingawa bila shaka aliichukulia tahadhari kubwa. Badala yake, "Kwake yeye Babeli ni dini Muhimu na inayohusisha ulimwengu wote ulio kinyume na Mungu. . . . Yohana aliona zaidi ya Rumi tu, na . . . alijihusisha hasa na uasi wa mwisho ambao utakuwa na kiini cha mambo ya mahusiano na Mungu badala ya mambo ya kisiasa. Zaidi ya hayo, aliwaandikia Wakristo walioamini, na siyo raia wasioamini wa Rumi. Kwa hiyo, alikusudia kwa mtazamo wake kulionya kundi, kwa kuhofia kwamba wanachama wake wasijeongozwa kwenye uasherati wa Kiroho na Mpinga Kristo." (Ford 1979: 269, 304n.159)[58]

[58] Asili ya kiroho ya kahaba imewafanya baadhi ya wachambuzi kuiona Babeli kama manabii walivyoiona Israeliisiyokuwa na imani: "Babeli siyo Yerusalemu tu ya 'Wayahudi.' Ni kanisa kubwa la Mungu ulimwenguni pote

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

6. Kahaba wa Babeli ni mwenzake na Mwanamke safi wa **Ufu 12:1**. Asili ya jumla ya Babeli mkuu inaonekana kwenye uwazi wa tofauti yake na mwanamke wa **Ufunuo 12**. "Kama mwanamke wa Ufu. 12 kwa wazi ni mfano wa watu wa Mungu wakati wote, hivyo mwanamke kwenye Ufu.17 anawakilisha au anahusisha waasi wa nyakati zote. Lakini Yohana hasa analitumia kwa mwanamke au bibi-arusi wa nyakati za mwisho [angalia **Ufu 19:7-8; 21:2, 9**], hivyo na kahaba. Paulo alizungumzia [uasi] na Babeli kwa Yohana kufupisha uasi uliozungumziwa na mtume kwa watu wa Mataifa. Babeli ilianzia kwenye uasi, na hivyo itaishia." (Ford 1979: 269) Jedwali hapo chini linaonyesha jinsi gani mwanamke, Sayuni iliyo bora, mwakilishi wa mbinguni wa watu wa Mungu (**Ufu 12:1-2, 5-6, 13-17**), ni wazi tofauti na "kahaba mkuu" wa **Ufunuo 17-18**:

Mwanamke wa Ufunuo 12	***Kahaba mkuu wa Ufunuo 17-18***
Amefunikwa na jua (**12:1**)	Amevikwa nguo za zambarau na nyekundu (**17:4; 18:16**)
Mwezi upo chini ya miguu yake (**12:1**)	Amekaa juu ya maji mengi (**17:1, 15**)
Amevaa taji ya nyota 12 (**12:1**)	Aepambwa na dhahabu, mawe ya thamani na Lulu (**17:4; 18:16**)
Akamzaa mtoto mwanaume (**12:5**)	Ni mama wa makahaba (**17:5**)
Alikimbilia jangwani (**12:6, 14**)	Maisha ya kusikitisha pamoja na wafalme na wafanyabiashara wa nchi (**17:2; 18:3, 9**)
Alitunzwa na Mungu (**12:6, 14**)	Alichukuliwa na mnyama (**17:3, 7**)
Aliteswa na Joka (**12:13, 15**)	Alilewa kwa damu ya watakatifu (**17:6; 18:24**)

7. Babeli ni mwenzake na Yerusalemu Mpya. Vyote, Babeli na Yerusalemu Mpya ni ishara. Asili ya kiulimwengu ya Babel mkuu inaonekana kwenye uwazi wa tofauti yake na Yerusalemu Mpya. Ukweli kwamba Babeli imeelezwa kama mwanamke na mji, na Yerusalemu Mpya hali kadhalika imeelezwa kama mwanamke na mji (**Ufu 21:2**), haionyeshi tu asili ya ulinganishi ya kiulimwengu lakini pia muunganiko wa tamaduni, uchumi, na dini: vinaingiliana kwa karibu, na vyote vinaamua na kumfunua mwaminifu mmoja wa kweli. "Babeli, mji wa ulimwengu huu, mahali pa utumwa na ugeni kwa Wakristo, ni mji mkuu wa kiroho kwa wale ambao ni wakaaji wa nchi, ambao mtazamo wao ni wa kutoka chini (ambao ni, kutoka kwenye ulimwengu huu). Wakaaji wan chi hawajumuishi tu wale walio nje ya kanisa lakini pia wale waliopo ndani. Babeli ni pale 'wakaaji wa nchi wanapokaa na wafuasi wa mnyama kupafanya nyumbani kwao. Bado Babeli siyo tu nyumbani kwa wakaaji wa nchi; pia ni mahali Wakristo wanapoishi, ingawa hapawezi kuitwa nyumbani kwao." (Resseguie 2009: 35) Mfanano baina ya Babeli na Yerusalemu Mpya unaonyesha asili ya ushawishi wa ulimwengu na uthamani wake; tofauti inaonyesha kwamba ulimwengu na uthamani wake mwisho wake ni mauti:

Babeli (Ufu 17-18)	***Yerusalemu Mpya (Ufu 21-22)***
Utangulizi	**Utangulizi**
Kuja kwa malaika (**17:1**)	Kuja kwa malaika (**21:9**)
Mwaliko: "Njoo huku, Nitakuonyesha" (**17:1**)	Mwaliko: "Njoo huku, Nitakuonyesha" (**21:9**)
Mwonaji kuchukuliwa na malaika katika Roho (**17:3**)	Mwonaji kuchukuliwa na malaika katika Roho (**21:10**)
Hata jangwani (**17:3b**)	Hata mlima mrefu (**21:10**)
Kufunguliwa kwa maono (**17:3**)	Kufunguliwa kwa maono (**21:10b**)
Ulinganishi	**Ulinganishi**
Amevaa kitani safi, zambarau na nyekundu (**17:4; 18:16**)	Amevaa kitani safi, angacu na safi (**19:8**)
Amepambwa na dhahabu (**17:4; 18:16**)	Amejengwa kwa dhahabu safi (**21:18, 21**)
Amepambwa kwa vito vya thamani (**17:4; 18:16**)	Mng'ao wake ni kama kito cha thamani-yaspi safi (**21:11**); kuta za mji ni Yaspi (**21:18**); msingi wa kuta za mji umepambwa na kila aina yam awe ya thamani (**21:19-20**)

wakati ambapo kanisa hilo litakuwa halina imani kwa Bwana wao wa kweli na mfalme. . . . Babeli ni ulimwengu ndani ya Kanisa." (Milligan 1896: 295-96) Hata hivyo, kamwe Babeli haikuwahi kuitwa *moichalis*, 'wazinzi'; *mbunifu* wakati wote, 'kahaba'. Hivyo, Babeli hakuwa kamwe mke wa Mwanakondoo." (Hendriksen 1982: 167n.3) Pia, "Ufu. 18—hasa mst. 11, 13—inafaa maelezo ya mji wa ulimwengu; itakuwa vigumu kusema kuhusianisha pamoja na wazo la kanisa la uongo." (Ibid.: 167n.1) Babeli kama Warumii na Babeli kama kanisa la uongo lina vipengele vya kweli; lakini mawazo yote yanaonekana kuwa na ukomo kabisa.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Amepambwa kwa dhahabu (**17:4; 18:16**)	Milango kumi na miwili ni Lulu kumi na mbili (**21:21**)
Tofauti	**Tofauti**
Kahaba mkuu (**17:1**)	Bibi-arusi, mke wa Mwanakondoo (**21:2, 9**)
Maskani ya mapepo (**18:2**)	Maskani ya Mungu (**21:3, 22**)
Jina limeandikwa kwenye kipaji cha uso wake (**17:5**)	Jina la Mungu limeandikwa kwenye vipaji vya nyuso zao (**22:4**)
Wafuasi wake hawapo kwenye kitabu cha uzima (**17:8**)	Wakaaji wake wapo kwenye kitabu cha uzima cha Mwanakondoo (**21:27**)
Ameshikilia kikombe cha dhahabu kilichojawa na machukizo na machafu ya uasherati wake (**17:4**); maskani ya roho wa chafu na kila ndega mwenye kuchukiza (**18:2**)	Hakuna kinyonge kitakachoingia (**21:27**)
Mvinyo yake huwafanya mataifa kulewa (**17:2; 18:3**)	Maji ya uzima yanatolewa bure, na mti wa uzima huwaponya mataifa (**21:6; 22:1-2**)
Uovu & na udanganyifu wa mataifa; wafalme wan chi wamezini naye (**17:2; 18:3, 9, 23**)	Mataifa watatembea katika nuru yake; na wafalme wa dunia wataleta utukufu wao ndani yake (**21:24, 26**)
Watu wa Mungu wanaitwa kutoka Babeli (**18:4**)	Watu wa Mungu wanaitwa kuingia Yerusalemu Mpya (**22:14**)
Kuteketezwa kabisa (**17:16-17; 18:8-23**)	Watakatifu watatawala milele na milele (**22:5**)

8. <u>"Tokeni kwake, enyi watu wangu" (**Ufu 18:4**).</u> Kwa kuunganisha na kanisa kwenye Ufunuo, tuliyoionyesha mapema nukuu ya **Isa 48:20; 52:11; Yer 50:8; 51:6, 9, 45** kama msingi wa mwito wa Yohana wa *"tokeni kwake, enyi watu Wangu."* Kwenye mazingira ya karne ya kwanza ya Yohana, Maagizo au mwito wa Yohana "siyo wa kutoka kimwili lakini kwa usahihi wa njia ya maisha ya upinzani wa kitamaduni katikati ya jamii ya Wagiriki wa Rumi" (Stylianopoulos 2009: 26; angalia pia Bauckham 1993a: 377 ["Hakuna hata mmoja wa wasomaji wa Yohana waliokuwa wakiishi kwenye mji wa Rumi. Agizo ni kwa wasomaji kutokujihusisha wenyewe na uovu wa Rumi, wasije wakashiriki hatia na hukumu yake."]).

Kwa kuwa Babeli mkuu imepita Rumi ya karne ya kwanza, Mwito wa Yohana unatumika kwa wakati wote na mahali pote kwa Wakristo ambao wakati wote wapo kwenye hatari ya ushawishi na mvuto wa zawadi nyingi za ulimwengu: "Hata kwenye muundo wa Agano la Kale, hili halikuwa tu onyo la kuondoka mji wa Babeli. Yohana, kama manabii wa Agano la Kale, anawaita watu wa Mungu kukimbia mvuto na mitego ya mji wa kikahaba. Babeli ipo kila ulipo uasherati, ukahaba, kujitukuza mwenyewe, kujikinai, kiburi na kukata tama, kutumainia anasa na utajiri, na ukatili kinyume na maisha (18:4-8, 24). Waamini wanapaswa kujitenga wenyewe nkutoka kwenye kila muundo wa Babeli. Wakati ambao bado wanaishi na kufanya kazi ulimwenguni, pia wanahitaji kudai utambulisho tofauti na kuendeleza tabia ya upinzani ambayo itawezesha ushuhuda kupata nafasi." (Ngundu 2006: 1572)

9. <u>Hukumu ya Babeli imetengenezwa juu ya hukumu ya Babeli ya kihistoria (**Ufu 18:1-24**).</u> Kwenye muunganiko wa kitasa cha sita (Ufu 16:12), tuliona ni jinsi gani hukumu ya Mungu kwenye Ufunuo ilivyotengenezwa kwa sehemu juu ya kuangamizwa kwa Babeli ya kihistoria. Sasa, **Ufu 18:7** imenukuu **Isa 47:7-8** kuhusiana na utamaduni wa Babeli. Hata hivyo, ulinganishi baina ya Babeli ya kihistoria na Ulimwengu wa Babeli mkuu wa **Ufunuo 18** hauna ukomo kwenye hiyo nukuu moja. **Ufunuo 18** hutumia **Isaya 47** kitu kama kibao cha kutangazia hukumu ya Mungu juu ya Babeli mkuu kwa kiburi chake, utamaduni, uchawi, na kutokumcha Mungu, kama vile sawa na hilo Mungu aliihukumu Babeli ya kihistoria. Jedwali lifuatalo linaonyesha mfanano baina ya Babeli mbili:

Babeli ya kihistoria—Isaya 47	***Babeli mkuu—Ufunuo 18***
Alijiita mwenyewe malkia, siyo mjane (**47:7-8**)	Alijiita mwenyewe malkia, siyo mjane (**18:7**)
Akifikiri yuko salama (**47:8, 10**)	Akifikiri yuko salama (**18:7**)
Kujitukuza mwenyewe (**47:8, 10**)	Kujitukuza mwenyewe (**18:7**)
Mpenda anasa (**47:8**)	Mpenda anasa (**18:3, 9**)
Anayetumia uchawi (**47:9, 12-13**)	Anayetumia uchawi (**18:23**)
Mwenye dhambi (**47:10**)	Mwenye dhambi (**18:4-5**)
Hukumu itakujia ghafla (**47:9, 11**)	Hukumu itakujia ghafla (**18:8, 10, 17**)

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Utateketea (**47:14**)	Utateketea (**18:8-9, 18**)
Walalao naye hawatamwokoa (**47:15**)	Walalao naye hawatamwokoar (**18:3, 9-19**)

Beale anafupisha ulinganifu baina ya Babeli mbili: "Kama penginepo kwenye Ufunuo, kiburi na anguko la Babeli ya kihistoria limechukuliwa kama aina ya mfano wa kiburi kilichopitiliza na kuanguka kwa mfumo wa Ki-Babeli ulimwenguni pote mwishoni mwa historia. Kama pamoja na Babeli ya zamani, Babeli ya siku za mwisho inajiona yenyewe kama mama wa wakaaji wake wote, ambao aliwasitawisha. Anao ujasiri kabisa kwamba hataacha kuwa na usaidizi wa watoto wake. Kama pamoja na taifa la Wababeli, siku za mwisho siasa na usalama wa uchumi wa Babeli utaondolewa ghafla. Na kiburi cha ujasiri wake kwenye usalama huo utafunuliwa kama usio na msingi na kama udanganyifu (kama kwenye Isa. 47:9-11; Yer. 50:31-32). Ujasiri kama huu ni uasherati binafsi, ambao lazima uhukumiwe. Kanisa lazima lichukue tahadhari waumini wake wasijewakahukumiwa pamoja na ulimwengu." (Beale 1999: 903)

10. **Ufu 18:1-19:6:** hukumu juu ya Babeli. **Ufu 18:1-19:6** ina muundo wa muunganiko shirikishi

18:1-3: Malaika anatangaza hukumu juu ya Babeli
18:4-20: Sauti kutoka mbinguni ikitabiri anguko la Babeli
18:21-24: Malaika akitangaza hukumu juu ya Babeli
19:1-6: Sauti mbinguni zikimsifu Mungu kwa anguko la Babeli

(Angalia Bauckham 1993a: 338-43; kwa muundo unaofanana mpangilio angalia Beale 1999: 891)

Ingawa **Ufu 18:6** yaweza kuhukuliwa kama kuipa Babeli adhabu iliyostahili mara mbili, kumbukumbu ya "maradufu" na "mara mbili" ni kitendawili cha Kiebrania kuelezea malipo "yaliyo sawa" (Kline 1989: 171-79; angalia pia **1 Tim 5:17**; Ladd 1972: 238 ["Adhabu kwenye kipimo kilichokamilika"]; Beale 1999: 900-02). Hili limethibitishwa na **Ufu 18:7** ambayo inasema, *"Kwa kadiri alivyojitukuzana kufanya anasa, mpeni maumivu na huzuni kadiri iyo hiyo."*

J. *Ufu 19:11-21: Kurudi kwa Kristo mara ya pili*

Kwenye kipengele hiki Kristo anafunua utawala na uaminifu kwa ahadi Zake wakati atakapokuja tena kuleta hukumu juu ya wale wote waliompinga Yey na kuwakandamiza watu Wake. Kwenye kuweka usambamba wa muundo hatua kwa hatua wa kitabu, *parousia* au athari zake zimetajwa au kuelezwa kwenye **Ufu 1:7; 6:12-17; 8:1-5; 11:11-19; 14:1420; 16:17-21** (*parousia* au athari zake pia zitaelezwa kwenye **20:7-10, 11-15;** na **21:1-2**). **Ufunuo 19** Ki-ishara inaelezea *parousia* kwa kina. Matukio ya **Ufunuo 19** yameunganishwa pamoja na vifungu vya nyuma vya *parousia*. Mealy anaelezea muunganiko huu: "Kwenye Ufunuo 19, inatangulia ufunuo wa Yesu juu ya farasi mweupe, Yohana anaelezea liturujia ya ushindi mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, ambayo ina mwendelezo pamoja na maeneo yote ya 7.9-12 na pamoja na ule wa 11.15-17. Sifa zinatolewa kwa 'Mungu ambaye ameketi juu ya kiti cha enzi yake' kwa sababu ya haki ya hukumu yake kwenye kuipindua Babeli (19.1-3); na kasha, kama kwenye 16.17, 'Sauti ikatoka kwenye kiti cha enzi'. . . . Hukumu ya kwanza [**19:5**] kwa wazi inasikika kurudi nyuma hadi Ufu. 11.18, pale ambapo parousia kulitabiriwa kama wakati wa kuwapa thawabu 'Watumwa wako manabii na watakatifu, na hao walichao jina lako, wadogo kwa wakubwa'. Sawa na hilo, kumsifu Mungu kwa sababu amechukua utawala wake wa nyakati za mwisho (v. 6) inaonyesha nyuma hadi 11.15-17. . . . Kwenye Ufunuo 19, kiti cha enzi cha Mungu kinaonyeshwa kwa mara ya tatu [**19:1-6**] (cf. 7.9-17; 11.15-18) kumaanisha kwamba parousia siyo tu kama tukio la hasira, lakini pia moja ya shangwe. Yote yatategemea ni juu ya kundi lipi la watu wanaokikabili kiti cha enzi." (Mealy 1992: 156)

Kama kuanza kwa *parousia* yenyewe, Yohana anaona *"mbingu zikifunguka"* (**Ufu 19:11**) ambayo inaturudisha nyuma kwenye vifungu vilivyopita vya *parousia* na hukumu (**Ufu 6:14; 11:19; 15:5**; cf. **4:1**). Asili ya ukamilifu wa eneo hili umeonyeshwa kwenye hili kama silaha pekee inayohusika kwenye vita kuelezewa ni, *"Na upanga mkali hutoka kinywani mwake"* (**Ufu 19:15;** angalia pia **1:16; 2:12; Isa 11:4; 49:2; Waeb 4:12**): "Wazo linarudi nyuma hadi kwenye uumbaji. Mungu aliumba ulimwengu kwa neno Lake. Alizungumza na ikafanyika. Uumbaji huu ulipatanishwa au kuunganishwa kupitia neno lililo hai, Kristo (Yohana 1:3; Waeb. 1:2). Hukumu ya mpango wa zamani pia utaunganishwa kupitia neno la Kristo." (Ladd 1972: 255) Jina la Yesu, *"Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana"* (**Ufu 19:16**), linaonyesha utawala wake wa milele juu ya mamlaka nyingine zote.

Parousia inahusisha vitu tofauti. Inaweza kuelezewa kama kuwa na asili mbili, ambazo Yohana alizielezea kwa njia tofauti. *Parousia* inahusisha vyote kuhakikishwa kwa wenye haki na hukumu kwa wasio haki. *Parousia* pia inaelezwa kama mahakama inayoendelea na kama mashindano au vita.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

1. *Parousia* kama uhakikisho wa wenye haki. Wakati Yesu atakaporudi atakuja, ki-ishara, siyo juu ya punda (angalia **Yoh 11:13-15**) lakini juu ya *"farasi mweupe"* akiambatana pamoja na majeshi yake *"juu ya farasi weupe"* (**Ufu 19:11-14**). Kwenye Rumi ya zamani, ushindi wa jumla kwenye vita kuu mara nyingi huwa na "mashangilio" ya hadhara ambayo kwayo huingia Rumi kwa magari yanayovutwa na farasi wannne weupe, pamoja na kufuatiwa na majeshi ya ushindi nyuma yao (Ramsay 1875: 1163-67). Rangi nyeupe inaashiria ushindi.

Rangi nyeupe pia inabeba wazo la haki, utakatifu, na uhakikisho: "Kupitia Ufuno wote 'rangi nyeupe' imewakilisha thawabu kwa walio safi au usafi wenyewe, itokanayo na uvumilivu wa imani uliojaribiwa kwa mateso [**3:4-5**]. . . . 19:7-8 imelihuisha wazo hili kwa kuelewa vazi 'jeupe' siyo tu kwamba linawakilisha haki lakini pia kama thawabu ya *uhakikisho* kwa wale waliovumilia kupitia mateso. Uhakikisho bila shaka umejumuishwa kwenye matumizi mengi ya awali ya 'rangi nyeupe' (e.g., Mwana wa adamu na watakatifu waliosimama kuhakikishwa na Mungu baada ya uaminifu wa ushuhuda wao kukataliwa na ulimwengu na waliteswa: 1:14; 2:17; 3:4-5; 4:4; 6:11; 7:9, 13; 14:14). Hasa kwenye 14:14 na 20:11 'rangi nyeupe' imebeba wazo siyo tu la utakatifu na usafi lakini pia uhakikisho wa kisheria wa ukweli kupitia hukumu. Sambamba na hilo, rangi nyeupe ya farasi hapa inaashiria wazo lile lile la kuhakikishwa kwenye utangulizi wa maeneo ya hukumu yafuatayo, hasa kwa sababu ya ukaribu wa kuunganishwa kwake na mst. 7-8 na hasa kwa 'kitani nyeupe' ya mst. 14, ambayo pia imebeba wazo la kuhakikishwa au kuthibitishwa." (Beale 1999: 950)

Kama tulivyoona kupitia Ufunuo, utambulisho wa Mungu pamoja na uhakikisho wa watu wake kunafuatia mfano wa utambulisho wake pamoja na Kristo aliyehakikishwa: waamini watateseka, kufa, na kuonekana kushindwa katika ulimwengu huu, lakini uaminifu wao hata kufa umesababisha ushindi wao wa milele na uthibitisho (**Ufu 2:9-10, 13; 6:9-11; 7:9-17; 11:7-13; 12:11; 14:1-5, 13; 17:14; 18:20-24; 19:1–9; 20:4-6**).

2. *Parousia* kama hukumu kwa wasio haki. Kwenye nyongeza kwa uhakikisho wa wenye haki, *parousia* inahusisha hukumu ya wasio haki. **Ufu 19:15-21** inaangalia kwa makini juu ya *parousia* kama hukumu juu ya wasio haki.

3. Hukumu wakati wa *parousia* kama vyote, mashindano na mahakama inayoendelea. Kwenye kuelezea *parousia* **19:11** inasema, *"Kwa haki ahukumu na kufanya vita."* Hili ni hakikisho pamoja na picha ya hukumu ya Mungu kwenye Biblia yote kwa kuja Kwake kama mahakama ya sharia na vita au mashindano: "Picha ya majaribu na vita ni maelezo ya kimafumbo ya utawala wa Mungu. Anatawala kwenye hukumu zake na kwenye mashindano au vita vyake. Kwenye hasira yake, hulithibitisha jina Lake, lakini pia huwathibitisha wale wote walio wake na wale wanaomwamini kwa ulinzi na ukombozi." (VanGemeren 1990: 220)

> a. *Hukumu ya Bwana kama mahakama ya sheria.* Kwenye Agano la Kale, "kuja kwa Bwana kwaweza kulinganishwa na eneo la mahakama. Kwenye mahakama yake Yahweh ni *Mwendesha mashitaka, Shahidi,* na *Hakimu.* Ni hakimu huru akikaa juu ya uumbaji wake: 'Lakini Bwana yupo kwenye hekalu lake takatifu; nchi yote na inyamaze kimya mbele zake' (Hab. 2:20; angalia Zefa. 1:7). Wakati atakapokuja, atayakusanya mataifa yote na 'na kuingia kwenye hukumu kinyume nao' (Yoeli 3:2). Ataleta mashitaka (Hos. 4:1-3), atahudumu kama shahidi kwenye mashitaka (Yer. 29:23; 42:5; Mik. 1:2), kuhukumu, na kutekeleza maamuzi. Msingi wa mashitaka na hukumu ni kiburi cha mwanadamu, kuukataa ufalme wake, na ubinafsi na maisha ya choyo [**Mal 3:5**]." (VanGemeren 1990: 219)
>
> Kwenye Agano Jipya, tunaona hukumu ikielezwa kwenye maneno au istilahi ya chumba cha mahakama katika **Math 25:3146; Mdo 10:42; 17:31; Rum 14:10; 1 Wakor 4:4-5; 2 Wakor 5:10**. Kwenye Ufunuo, hukumu kama mahakama inayoendelea kwa wazi imeonekana katika **11:18; 20:11-15**. Kwenye **Ufunuo 19**, hukumu kama mada ya chumba cha mahakama imeelezwa kwa mfano *"Macho yake ni kama mwali wa moto"* (**Ufu 19:12**). Hili linaonyesha majukumu ya Kristo kama Mungu, hakimu aonaye yote. Imeonekana pia kwenye **Ufu 2:18-23** ambapo, kwa mfano ule ule, macho ya Kristo yaonayo vyote hupenya kupitia nje hadi ndani (Yeye *"huchunguza mawazo na mioyo,"* **Rev 2:23**) kwa Kanisa la Thiatira na nabii mke Yezebeli na wafuasi wake. Matokeo ni uthibitisho na thawabu ya waaminifu na hukumu kwa wasioamini.
>
> b. *Hukumu ya Bwana kama mashindano au vita.* Kwenye mandhari ya mashindano, "Yahweh ni Mungu Mshindi, ambaye anakuja utaratibu penye machafuko, vurugu, na kujitawala kwa ufalme mwanadamu. Ushindi hufungua hasira yake kinyume na upinzani wote kwenye ufalme

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

wake [**Isa 13:13**]. Kwenye hasira yake atakuja pamoja na malipizi, ikifananishwa na vita na mauaji [**Jer 46:10**].” (VanGemeren 1990: 220) Vos anafafanua hili: “Maandalizi ni ya kijeshi; yale mazingira ya vita vikali na ushindi muhimu. Kwenye Agano la Kale hili ni aina ya ushindi wa muda mrefu wa uwakilishi, kuanzia Danieli na Zaburi kuendelea mbele picha ya upasuaji rasmi huja kuongezea ushahidi, hata hivyo, bila kuingilia mengine yote. Kwenye hukumu ya kijeshi hakuna kifaa cha kuhifadhia kumbukumbu na kuzikagua, na hakuna maamuzi makini yanayotangazwa kwa msingi wa haya. . . . Hakuna kipengela kimoja cha kipekee kuhusiana na huku kukamilishwa kwa hukumu . . . uharaka wa atahri zake. Huu ni uthibitisho ulio bora kwa maelezo ya kuondolewa kwa ‘Mtu wa dhambi’ [**2 Wathes 2:8**]; italetwa kwa pumzi ya kinywa cha Kristo, kwa madhihirisho madogo ya kuja Kwake. Kwa wazi kipengele hiki kimeazimwa kutoka [**Isa 11:4**]. Kwenye Isaya ni moja tu maelezo ya mawazo ya nabii ya papo kwa papo ya nguvu itendayo kazi isiyokuwa ya kawaida hasa kwenye hukumu.” (Vos 1979: 262-63) Kwenye Ufunuo, hukumu kama mashindano inaonekana katika **6:12-17; 11:18; 14:17-20; 16:14-21; 17:14; 18:17-24; 19:11-21; 20:7-10**. Kwenye **Ufunuo 19**, kumbukumbu ya Kristo akiwa amepanda farasi mweupe (**19:11**) na “majeshi” yake pia yakimfuata juu ya farasi weupe (**19:14**) inaonyesha *parousia* na hukumu kama mandhari ya vita (angalia Schnabel 2011: 236, 288). Hili limefanywa wazi kwenye**Ufu 19:17-21**. Kwenye **19:17**, *“karamu ya Mungu iliyo kuu”* huendana na *“karamu ya harusi ya Mwanakondoo”* (**19:9**). Muunganiko huo unaonekana kwenye ay azote mbili **Ufu 19:9** na **19:17** zimebeba msemo ule ule, *eis to deipnon* (“kwenye karamu”). “Muunganiko unaashiria kwamba hukumu ni upande mwingine wa shilingi ya Wokovu” (Beale 1999: 965).[59]

K. ***Ufu 20:1-15: Kufungwa kwa Shetani, kutawala kwa Watakatifu, hukumu ya Shatani, na hukumu ya mwisho***

“Miaka elfu” au “milenia” ni kipindi cha kati ya Kuja kwa Kristo mara ya kwanza mpaka mudsa mfupikabla ya kurudi Kwake mara ya pili. Wakati wa kipindi hiki, Mungu anaiwekea ukomo nguvu ya udanganyifu ya Shetani na Wakristo waliokufa wanahakikishwa kwa kutawala mbinguni. Kipindi hiki kitaishia kwa kuzaliwa upya shambulio la uongo la Shetani kinyume na Kanisa. Hili, kwa upande mwingine, litahitimishwa na *parousia* na hukumu ya mwisho.

Ingawa vipo vifungu au vifungu vidogo vine kwenye **Ufunuo 20** (**20:1-3**, kufungwa kwa Shetani; **20:4-6**, kutawala kwa Watakatifu; **20:7-10**, hukumu ya mwisho ya Shetanii na nguvu zake; na **20:11-15**, hukumu ya mwisho), kwa hakika hivyo ni vifungu vidogo vya vifungu viwili vikuu: matukio kabla ya *parousia* (**20:16**); na matukio yaliyounganishwa na *parousia* (**20:7-15**).

Matukio yaliyoandikwa kwenye **ufu 20:1-15** hayafuati mtiririko wa nyakati kutoka pale **19:21** ilipoishia. Badala yake, inafuata hatua kwa hatua mfanano wa muundo wa kitabu, **Ufunuo 20** inarudia historia kutoka kuja kwa Kristo mara ya kwanza hadi kwenye *parousia* na hukumu ya mwisho, kuongezea kina na msisitizo mpya.[60] *“Kutupwa kwa Shetani,* na siyo utawala wa miaka elfu, ni mada kuu kwenye aya kumi za mwanzo wa sura. Kufikia hapo ni, ni kuwa ya mwisho kutoka kwenye upeo wa hitimisho la kitabu chote, hili hata halikuelezwa mwanzoni mwa kifungu chochote kipya na muhimu.” (Milligan 1896: 336). Shetani ndiye adui mkuu wa Kristo. Kwenye **Ufunuo 19** Yohana ameelezea hatima ya mnyama na nabii wa uongo. Kwa hiyo, ni sahihi kwamba ni mwisho wa Shetani (“nguvu iliyo nyuma ya kiti cha enzi”) kuwa imeelezwa peke yake kwenye sura hii.

1. <u>Kufungwa kwa Shetani (**Ufu 20:1-3**): lugha ya ki-ishara.</u> Beale anaazisha mjadala wetu wa **Ufunuo 20** kwa kutukumbusha hatari ya “uhalisia” (kwenye ufahamu wa kimwili) wakati Yohana anaandika kuhusiana na kweli za Kiroho kwenye aina ya mafunuo: “Ni makosa kumwona Ibilisikuwa ‘anatupwa juu ya nchi’ kwenye baadhi ya hisia za vipimo vitatu, hivyo basi hayupo tena juu ya nchi. Hili litakuwa ni kuichukulia ‘kuzimu’ kwenye uhalisia usiokuwa wa kawaida. Badala yake, kama ‘mbingu’ kwenye

[59] Picha ya ndege walao miili ya wale waliokufa (**19:17-21**) kimsingi limetolewa kutoka **Ezek 39:4, 17-20**. Ni “ombi la kanuni ya laana ya kale” ambayo inaashiria “maana ya kale kwa kuumiza na kumdhalilisha adui hata baada ya kufa” (Aune 1998b: 1067-68; angalia **Mwanzo 40:19; Kumb 28:26; 1 Sam 17:44, 46; 1 Fal 14:11; 16:4; 21:24; 2 Fal 9:10; Ayubu 39:27-30; Yer 7:33; 15:3; 16:4; 19:7; 34:20; Hab 1:8; Math 24:28; Luka 17:37**).

[60] Angalia **Nyongeza 2—MILENIA: Kumbukumbu za awali za Kibiblia za kutokuwepo kwa milenia** kwenye Menn 2016 ndiyo sababu kwanini **Ufunuo 20** inarudia **Ufunuo 19** badala ya kufuata mpangilio wa wakati na kwa majadiliano zaidi ya “miaka elfu”, “fufuo mbili” na utawala wa watakatifu (**Ufu 20:4-6**).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kitabu chote cha Ufunuo, inawakilisha kipimo cha Kiroho kilichopo pamoja na yaliyopo katikati ya mambo ya kidunia, siyo juu yake au chini yake (kama pamoja na, e.g., hali ya kimbingu kwenye 2 Kings. 6:15-17 na hali ya Kishetani kwenye Efe. 6:10-17; cf. 2 Wakor. 10:3-5).” (Beale 1999: 987) Upeo wa Beale unaonekana wakati tunapotafakari lugha Yohana aliyoitumia kwenye **20:1-3**. “Shetani siyo Joka halisi ambaye anaweza kufungwa kwa mnyooror wa kawaida au kufungiwa kwenye shimo la kawaida” (Johnson 2001: 283). Kuishikilia miaka 1000 “kiuhalisia” kunahitaji kuwa na uthabiti, kwamba “funguo” na Mnyororo” ulioshikiliwa na malaika kwenye **Ufu 20:1** ni funguo na mnyororo wakawaida tuujuao, na kwamba “kuzimu” ya **Ufu 20:3** ni shimo halisi lililopo kwenye uso wa nchi ambalo lina kufuli ya kawaida ya kufunguliwa kwa ufunguo na “muhuri” wa kawaida kama tuujuao kwenye maofisi (Waltke 1988: 273; Jackson 2001: n.p.). Hili, bila shaka, siyo kile kilichokusudiwa kwa lugha kama hii. Shetani ni roho, siyo kiumbe chenye mwili. Lugha aliyotumia Yohana ni fumbo au ishara.

Kuna kipengele kingine muhimu kwa lugha ya Yohana kuhusiana na “kufungwa” kwa Shetani na uhusiano wake jinsi inavyoonekana kwenyehistoria, yaani, Yohana anahusisha “lahaja au nahau za kitenzi” kuuelezea ushindi wa Mungu juu ya joka (White 1999: 62).[61] Baada ya kuchunguza mifano mingi ya Kibiblia ya matumizi ya lahaja za kitenzi, White anaelezea, “kwenye kila jambo . . . hatima ya hayawani kwenye lahaja za kitenzi ni sawa tu, siyo sawa sawa na hatima yake kwenye historia. Hili litakuwa hivyo, ama watamkuta mnyama mwovu kuwa amekamatwa au amechinjwa. Kwenye mambo yote haya, hatima ya joka inawakilisha ukweli kwamba jitihada za maadui wa Mungu kuzuia uumbaji wake na kazi ya ukombozi mbinguni na duniani yenyewe imezuiliwa kwa ufanisi na Mungu ama kwa muda au kwa maana ya milele.” (Ibid.) Alihitimisha kwamba “hatima ya jokwa kwenye Ufu 20:1–3 ni *sawa lakini haifanani* na hatima ya Shetani kwenye historia. Imeelezwa tofauti, wakati joka limekamatwa na kufungwa kwenye utenzi wa picha na njama ya maono ya Yohana, Kwenye historia Shetani hakukamatwa wala kufungwa gerezani. Badala yake, kama nyoka majoka ya Babeli na giza na kina, Shetani ameondolewa kwenye jukumu lake kama mdanganyifu wa mataifa ya dunia.” (Ibid.: 63, fafanuzi imeongezwa)

2. <u>Kufungwa kwa Shetani kulitokea wakati wa Kristo kuja mara ya kwanza.</u> Jambo la kwanza ni *lini* huku “kufungwa” kutatokea? Waamini wa mpito wanadai kwamba kufungwa kutatokea baada ya *parousia*. Wengine wote wanakubaliana kwamba kufungwa kulitokea kwenye muunganiko wa kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo. Agano Jipya na ushahidi wa kimazingira ndani ya Ufunuo wenyewe unafanya uwazi kwamba kufungwa kwa Shetani kulitokea kwenye muunganiko wa kuja kwa Kristo mara ya kwanza. Hoekema anatueleza kwanini: “Kipo kiashiria chochote kwenye Agano Jipya kwamba Shetani alifungwa wakati wa kuja kwa Kristo mara ya kwanza? Kwa hakika kipo. Wakati Mafarisayo wakimshtaki Yesu kwa kutoa mapepo kwa nguvu za Shetani, Yesu aliwajibu, ‘Ama awezaje mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuviteka vyombo vyake, asipomfunga kwanza Yule mwenye nguvu?’ (Math. 12:29). Chakufurahisha zaidi, neno lililotumiwa na Mathayo kuelezea kufungwa kwa mtu mwenye nguvu ndiyo hilo hilo lililotumiwa kwenye Ufunuo 20 kuelezea kufungwa kwa Shetani (neno la kigiriki *de*ō).” (Hoekema 1979: 228-29)

Maneno ya Yesu mwenyewe kwenye **Yoh 12:31** yanafanana na **Ufu 20:3**: **Yoh 12:31** (*“Sasa hukumu ya ulimwengu huu ipo; sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje* [Kigiriki = *ekball*ō]”); **Ufu 20:3** (*“Akamtupa* [Kigiriki = *ball*ō] *yeye katika kuzimu”*). Hivyo, Agano Jipya mara nyingi huzungumzia hukumu ya Shetani, kuanguka, kuwa na ukomo, na kushindwa kwenye muunganiko pamoja na kuja kwa Kristo mara ya kwanza na kwa kipindi cha nyakati hizi.[62]

---

[61] Kile Yohana anachokifanya ni kukopa “picha na mbinu kutoka hadithi za ulimwengu wa Wapagani . . . ili kwamba Elohim Mwumbaji wa kweli aweze kuonekana kwenye kupambana pamoja na Joka asiyekuwa mwumbaji, nyoka, au bahari. Kwa hakika, lazima tulielezee jambo hili kitofauti: kufanya tafakari kwa usahihi kwa hadithi za kitamaduni kwenye kurekebisha uumbaji wao na ukombozi, waandishi wa maandiko ya mungu mmoja walikuwa “wakizitafsiri tena” tamaduni hizo.” (White 1999: 61) Hili ni sawa na kile Yohana alichokifanya mwanzoni kwenye **Ufunuo 13** na **17** kwenye kugawa na kubadilisha simulizi za Nero na jinsi alivyo, kama manabii na waandishi wengine wa Agano Jipya, wakati wote huzigawa tena picha za unabii wa Agano la Kale kwa madhumuni yake mwenyewe na mazingira.

[62] Kwa aya zingine juu ya mada ya “kutupwa” angalia Math 12:28; Marko 3:22-23; 9:38; 16:17; Luka 9:49-50; 10:18; Yoh 12:31; Mdo 5:16; 16:16-18; 19:11-12; 2 Pet 2:4.

Kwa aya zingine juu ya mada kuu ya ukomo wa Shetani angalia Math 12:29; Marko 3:24-27; Yoh 16:11; 17:15; Mdo 26:18; Warumi 8:33, 38-39; 16:20; 1 Wakor 15:25; Efe 1:20-23; 3:8-12; 6:10-16; Col 1:13; 2:10, 15; Waeb 2:14; Yak 4:7; 1 Pet 3:21-22; 1 Yoh 2:13; 3:8; 4:3-4; 5:18; Yuda 6.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Yesu kuwapa Wanafunzi wake Agizo Kuu (**Math 28:18-20**) kunaashiria mwanzo wa shughuli mpya: "Mamlaka ya kisiasa ya kidunia ambayo kwa kiburi Shetani huyadai, kwa hayo huyakandamiza mataifa, na ambayo alimpa Kristo [**Math 4:8-9; Luka 4:5-6; Efe 2:1-2]** kwa haki alishinda kwa kazi tukufu ya ukombozi wa Kristo. . . . Ni lazima tukumbuke kwamba Agizo Kuu lilifunguliwa kwa tamko hili zuri la heshima: 'Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani' (Math. 28:18b). Mamlaka hayo yamezingira mbingu na dunia na ni 'juu ya kila jina litajwalo [**Efe 1:21; Wafil 2:9-10; 1 Pet 3:22**].'" (Gentry 1990: 58, 94)

3. Kufungwa kwa Shetani kwenye **Ufu 20:1-3** ni sambamba na kutupwa chini kwa Shetani kwenye **Ufu 12:7-12**. "Ufunuo wenyewe pia unatupa ushahidi wa usahihi wa tafsiri hii [kwamba kufungwa kwa Shetani kulitokea wakati wa kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo], kwa sura ya kumi na mbili, ambayo inaunda kiini cha kitabu, inaonyesha maadili ya Kristo kama kuhusiana na kuleta kutolewa kwa Shetani kutoka mbinguni" (Grenz 1992: 162). Kwa maneno mengine, kufungwa kwa Shetani kwenye **20:1-3** ni sambamba na Shetani kuwa *"akatupwa hata nchi"* (**12:9**) na kuja chini kwenye nchi na bahari (**12:12**). Majina yote manne ya Shetani (*"joka, nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani"*) "yametokea kwenye mpangilio ule ule kwenye vifungu vyote kwenye maandiko ya Kigiriki [**12:9; 20:2**], Na vifungu hivi viwili ni mahali pekee kwenye kitabu chote ambapo mfuatano wa hili kama wote umetumika kwake. Mfanano huu wa kipekee baina ya vifungu hivi viwili vinatupa baadhi ya ushahidi unaotusaidia kuamua kuunganisa simulizi hizi mbili." (Shea 1985: 45) Usambamba baina ya sura mbili unathibitishwa na asili ya kujirudia kwa kitabu kizima. Kama pamoja na mwingiliano wa mengine mengi na rejea ya msalaba kwenye kitabu chote, mfanano baina ya **sura ya 12** na **20** unaashiria kwamba wanaangalia tukio lilelile kwenye mtazamo tofauti, kuleta kivuli au msisitizo tofauti.[63] Mfanano baina ya **Ufunuo 12** na **20** umeonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo:

Ufu 12:7–12	***Ufu 20:1–6***
Mpinzani mwovu wa malaika ni *"Joka kuu . . . nyoka wa zamani aitwaye Ibilisi na Shetani"* (**12:9**)	Mpinzani mwovu wa malaika ni *"joka, nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani"* (**20:2**)
Shetani kutupwa hata nchi [na bahari] (**12:9; 12**)	Shetani kutupwa hata kuzimu (**20:3**)
Shetani *"anajua muda wake ni mfupi"* (**12:12**)	Shetani "*kufunguliwa kwa muda mfupi"* (**20:3**)
Kuanguka kwa Shetani kuna matokeo kwenye ufalme (**12:10-11**)	Kuanguka kwa Shetani kuna matokeo kwenye ufalme (**20:4-6**)
Ufalme wa watakatifu misingi yake siyo tu kuanguka kwa Shetani bali kwenye ushindi wa Kristo na uaminifu wao kwa *"neno la ushuhuda wao"* hata kufa (**12:11**)	Ufalme wa watakatifu misingi yake siyo tu kuanguka kwa Shetani bali kwenye ushindi wa Kristo na uaminifu wao kwa *"ushuhuda wao kwa Yesu na kwa ajili ya neno la Mungu"* hata kufa (**20:4**)

Maeneo ya mwanamke na joka (**Ufu 12:1-17**) na kufungwa na kufunguliwa kwa Shetani (**Ufu 20:1-3**) nayo pia ni eneo madhubuti pamoja na mashahidi wawili na mnyama (**Ufu 11:3-12**). Maeneo yote matatu yanatumia picha tofauti kuonesha kipindi kile kile na matukio yale yale (Ulinzi wa Kiroho wa Kanisa bila kujali upinzani uliopo juu yake na mateso yake kwenye ulimwengu huu): mashahidi wawili walilindwa na Mungu mpaka walipomaliza ushuhuda wao; mwanamke alilindwa akiwa jangwani; Shetani amefungwa kwa miaka elfu kumzuia asiyadanganye na kuyakusanya mataifa kuliangamiza Kanisa (Johnson 2001: 286-87;pia angalia kwenye 4445).

Hata hivyo, "kufungwa" ya **Ufu 20:3** hakufanani kwa vyovyote vile na "kutupwa" ya **Ufu 12:9**, lakini ni kipengele chake. Sababu ni kwamba Shetani "atafunguliwa" kutoka kwenye "kifungo chake" (i.e., kutoka kwenye zuio ambalo limewekwa juu ya uwezo wake wa "kuyadanganya mataifa") kwa muda mfupi kabla ya Kristo kurudi (**Ufu 20:3, 7**, angalia hapo chini). Kwa namna nyingine, "ushindi wa [Kristo] alioshinda dhidi ya Shetani alishinda mara moja na kwa wakati wote" (Ladd 1972: 263). Shetani hataweza tena kamweata kupanda kwenye nafasi, hali, au mamlaka aliyokuwa nayo kabla "hajatupwa chini" kwa kile Kristo alichokamilisha pale Msalabani.

[63] Misisitizo miwili ambayo lazima ibainishwe ni: (1) "Muda mfupi" kwenye **Ufu 12:12** na **20:3** ni tofauti: kwenye **Ufu 12:12** "muda mfupi" ni kipindi cha muda wote kutoka kufufuka na kupaa kwa Kristo hadi kwenye *parousia*, pale ambapo "muda mfupi" kwenye **20:3** tu ni mwisho wa kipindi hicho, muda mfupi kabla ya *parousia*. (2) Shughuli za udanganyifu wa Shetani zinazozungumziwa kwenye **Ufu 12:9** na **20:8** vivyo hivyo ni tofauti: ya kmwanzo ilitokea kipindi chote kutoka kupaa hadi *parousia*, wakati ambao iliyofuata ilitokea tu kwa muda mfupi kabla ya *parousia* na pia haipo chini ya vikwazo sasa ambavyo vimewekwa juu ya Shetani. Angalia sehemu mbili zinazofuata kwenye mada kuu kwa majadiliano zaidi ya masuala haya.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

4. Kusudi la kufungwa kwa Shetani. Shetani amekuwa wakala mtendaji ulimwenguni tangu Adamu na Hawa kwenye Bustani ya Edeni (**Mwanzo 3:1-13**). Yesu alimwita *"baba wa uongo"* (**Yoh 8:44**). Ni mshitaki wa waamini na *"mdanganyifu wa ulimwengu wote"* (**Ufu 12:9-10**). Hata hivyo, upeo wa mamlaka ya udanganyifu wake yamewekewa ukomo, nguvu zake kwa uhakika zimevunjwa, na kushindwa kwake kwa milele kumehakikishwa. Kufungwa kwa Shetani wakati wa Kristo kuja mara ya kwanza kunahusiana, siyo kabisa, kuzuiliwa au kufupishwa kwa shughuli za Shetani kwa kusudi maalum wakati wa kipindi maalum.[64] Shetani amefungwa *"ili kwamba asiweze kuyadanganya tena mataifa"* (**Ufu 20:3**). Gentry anafafanua hili: "Kwenye Agano la Kale ni Israeli pekee waliomjua Mungu wa kweli (Zab. 147:19-20; Amos 3:2; Luka 4:6; Mdo 14:16; 17:30). Lakini kuzaliwa kwa Kristo kulibadilisha hili kama injili ilivyoanza kuenea kwa mataifayote (e.g., Isa. 2:2-3; 11:10; Math. 28:19; Luka 2:32; 24:47; Mdo 1:8; 13:47)." (Gentry 1998: 83) John Sittema anaongeza kwamba kupaa kwa Yesu "kunadhihirisha ushindi na kuwekwa kwenye kiti cha enzi, na kwa hivyo, kufungwa kwa Shetani 'ili kwamba asiyadanganye tena mataifa.' Haya ni matokeo ya lazima kwa lugha za siku ya Pentekoste [**Mdo 2:1-11**] hili liliwezesha kuenea kwa ufalme hadi mwisho wa nchi (angalia Luka 11:20-21)." (Sittema 2013: 86n.3) Paulo anaelezea hili kwenye **Mdo 26:17-18** pale aliposema kwamba Kristo alimtuma yeye kwa watu wa mataifa *"nikikuokoa na watu wako, na watu wa Mataifa, ambao nakutuma kwao; uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi.."*

Ufu 20:7-8 pia unaelezea asili ya kufungwa kwake kwa kuwa **mst. 7** inachukulia pale **mst. 3** ilipoachia.[65] **Ufu 20:3** inaeleza kwamba Shetani amefungwa *"ili kwamba asiyadanganye mataifa tena, mpaka miaka elfu itakapokamilika."* **Mst. 7-8** kisha zinalichukua wazo, *"Wakati miaka elfu itakapokamilika, Shetani atafunguliwa . . .na atatoka kuyadanganya mataifa . . . kuyakusanya pamoja kwa ajili ya vita."* Johnson ananonyesha umuhimu wa **20:7-8** juu ya maana ya **20:3**: "Ingawa ni ukweli kwenye historia yote kwamba Shetani, nyoka wa zamani, 'ataudanganya ulimweng wote' (Ufu. 12:9), kwenye maono haya uongo maalum kufikia lengo maalum linatazamwa. Tunaliona lengo hili wakati, mwishoni mwa miaka elfu, joka linafunguliwa na kutoka 'kuyadanganya mataifa ambayo yapo kwenye pande nne za nchi, Gogu na Magogu, kuwakusanya pamoja kwa ajili ya vita' (20:8). . . . Kwenye mwanga wa mafafanuzi haya ya kusudi lililo nyuma ya udasnganyifu wa joka (20:8), kufungwa kwake wakati wa kipindi cha miaka elfu kunamzuia Shetani asiweze kuyakusanya mataifa kwenye njama ya dunia yote ya kulifuta Kanisa." (Johnson 2001: 284-85)[66]

5. Kufunguliwa kwa Shetani (**Ufu 20:3, 7**). **Ufu 20:7** inaeleza, *"Wakati miaka elfu itakapokamilika, Shetani atafunguliwa kutoka katika kifungo chake."* Beale ananelezea mazingira Biblia inayoonyesha wakati Shetani atakapofunguliwa muda mfupi kabla ya Kristo kurudi tena: "Kwa kipindi chotebaina ya kuja kwa Kristo mara ya kwanza na mara ya pili, Shetani hatakuwa na uwezo wa hata mmoja wa 'idadi kamili' (6:11) ya wale walionunuliwa na Kristo kwa sababu watakuwa 'wamewekewa muhuri'. Wakati 'idadi kamili' itakapokuwa imekusanyika, kasha Ibilisi ataruhusiwa kuwadanganya wengi waishio mwishoni mwa historia, kuwasababisha siyo tukuwa vipofu kwenye kweli ya Kristo lakini pia kutafuta

---

[64] Ingawa hakubaliani kuhusiana na muda wa "kufungwa," muumini wa kabla ya milenia Ladd anakubali kwamba kufungwa kwa Shetani "ni njia ya kiishara ya kuelezea kuzuiliwa kwa nguvu na shughuli zake; haimaanishi isiyohamishika kabisa. Kufungwa kwake kuzimu hakumaanishi kwamba shughuli zake na nguvu zake zimeondolewa." (Ladd 1972: 262)

[65] Schüssler Fiorenza kwa usahihi anaonyesha, "Ingawa mwanzoni sura iligawanywa kwenye migawanyiko mitatu, pamoja na 20:7-10 kama sehemu ya maono yaliyoanzia kwenye 20:4ff, kimazingira 20:7-10 kuyaleta kwenye hitimisho 20:1-3" (Schüssler Fiorenza 1991: 106).

[66] Ukweli kwamba kanisa halikuharibiwa lakini lilienea kujumuisha watu *"kutoka kila kabila na lugha na jamaa na taifa"* ya ulimwengu (**Ufu 5:9**) ni "sawa lakini haifanani" madhihirisho ya kihistoria ya maono ya Yohana ya kufungwa kwa Shetani, yamejadiliwa hapo juu na White (angalia White 1999: 66n.41).

Lugha ya **Ufu 20:3, 7-9** inaweka wazi madhumuni maalum ya "kufungwa" kwa Shetani, i.e., kumzuia yeye ili asiweze kusimamisha kuenea kwa kanisa ulimwenguni kote na kumzuia yeye asieneze njama zake ulimwenguni kote kuliangamiza kanisa. Hata hivyo, tulikwisha kuona mwanzoni kwamba, kama matokeo ya kuja kwa Kristo mara ya kwanza, nguvu za Shetani pia ziliwekewa ukomo kwa njia nyingine: hana tena nafasi ya kuingia mbinguni, hana uwezo tena wa kuwashtaki waaminio, na hana uwezo tena wa kuwatawala waaminio kwa kuwa wamekwisha kuhamishwa kutoka kwenye utawala wake hadi kwenye ule wa Kristo; hivyo, waaminio wanaweza *"kumpinga Shetani naye atawakimbia*" (**Yak 4:7**).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kuwashinda wafuasi wa Kristo. . . . Mwishoni mwa nyakati, mateso kupitia wengi waliodanganywa yatalipuka kinyume cha Kanisa, kiasi kwamba yangewaangamiza kama siyo Mungu kuingilia kwa niaba yake (hivyo pia Marko 13:19-22; Math. 24:21-24)." (Beale 1999: 986-87) Mazingira haya yanatusaidia kuona tofauti baina ya "muda mchache" ambao Shetani amepewa kufuatia kufunguliwa kwake kwenye **Ufu 20:3** na "muda ['mdogo']mfupi" aliokuwa nao wakati anatupwa hata nchi kwenye **Ufu 12:12**. Muda mfupi wa **Ufu 20:3** ni hatua ya mwisho kabisa ya muda Shetani aliokuwa nao kwenye **Ufu 12:12** (angalia ibid.: 993).[67]

6. Kufungwa na kufunguliwa kwa Shetani kabla ya parousia na kuangamizwa kwake wakati wa parousia ni sambamba na kuzuiliwa, kufunuliwa, kuangamizwa kwa "mtu wa kuasi" kwenye **2 Wathes 2:6-12**. Kufungwa kwa Shetani sasa, lakini kufunguliwa kwake muda mfupi kabla ya *Prousia*, pia mfanano na **2 Wathes 2:6-12** pale ambapo *"siri ya kuasi tayari inatenda kazi,"* lakini *"Yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake Shetani"* amezuiliwa kwa sasa. Wakati kizuizi *"kitakapoondolewa . . . yule asi atafunuliwa."* Kwa kweli, vyote **Ufunuo 20** na **2 Wathesalonike 2** zinafanana kwa sababu nyingi, zikijumuisha mpangilio muhimu wa matukio yanayoelezwa:

2 Wathes 2:6–12	***Ufu 20:1–15***
Mtu wa kuasi (MOL) kwa sasa amezuiliwa (**2:6-7**)	Shetani amefungwa na malaika (**20:1-3**)
Mzuiaji ataondolewa (**2:7**)	Baada ya miaka "1000" Shetani atafunguliwa (**20:3, 7**)
Mtu wa kuasi atafunuliwa & kuja kwake ni mfano wa kutenda kwake Shetani (**2:8-9**)	Shetani atatka (**20:8**)
Mtu wa kuasi atawadanganya wale wa kuangamia (**2:8-12**)	Shetani atayadanganya mataifa na kuwakusanya pamoja kwa vita (**20:8-9**)
Mtu wa kuasi atauawa kwa ujio wa Kristo (**2:8**)	Shetani ataangamizwa [kwa ujio wa Kristo] (**20:9-10**)
Wale ambao hawataiamini kweli na kujichukulia anasa kwenye uovu watahukumiwa (**2:12**)	Wafu watahukumiwa; wale ambao majina yao hayapo kwenye kitabu cha uzima watatupwa kwenye ziwa la moto (**20:11-15**)

Sydney Page anaonyesha mfanano baina ya vifungu viwili: "Vifungu vyote vikizungumzia kizuizi ambacho kinazuia mlipuko mkubwa wa uovu kwa kipindi kifupi lakini hili hatimaye kitaondolewa, pamoja na matokeo kwamba kutakuwa na kipindi cha upinzani mkali kwa Mungu ambacho kitahitimishwa kwa kuingiliwa na Mungu mwenyewe. Pamoja na kuwa na msingi wa mpangilio wa matukio kwa kawaida, Ufunuo 20 na 2 Wathesalonike 2 zinathibitisha hesabu ya mfanano kwa kina. Utawala huru wa Mungu umesisitizwa kwenye maelezo yote. . . . Maelezo yote piayameonyesha jukumu la udanganyifu kwenye muunganiko pamoja na nyakati hizi za mwisho za uovu au uasi. . . . Siyo tu kwamba vifungu vyote viwili vina mada ya udanganyifu kwa pamoja, lakini kwenye vyote Shetani anachukua nafasi maarufu kuhusiana na hili. Kwenye Ufunuo anawakilishwa kama mmoja adanganyaye, na kwenye 2Wathes 2:9 anaonekana kama nguvu halisi nyuma ya mpango wa udanganyifu wa mtu wa kuasi. Hatimaye, upo mfanano wa muhimu baina ya wazo la Yohana na Paulo la jinsi gani uasi ilivyohitimishwa. . . . Lakini hata mfanano ni wa karibu kuliko hili, kwa kuwa kwenye [**2 Wathes 1:79**] Paulo, kama Yohana, anaambatanisha kurudi kwa Kristo pamoja na moto na kutolewa kwa hukmu ya mwisho juu ya maadui za Mungu." (Page 1980: 40-41) Mifanano hiyo inaonyesha kwamba matukio ya vifungu vyote viwili vinaishia (havianzii) katika *parousia*.

7. Kutawala kwa watakatifu (**Ufu 20:4-6**). Kwa sababu kutupwa na kuangamizwa kabisa kwa adui mkuu wa Kristo ndiyo mada kuu ya kitabu cha **Ufu 20:1-10**, hakuna taarifa maalum zilizotolewa kuhusiana na asili ya "miaka elfu" zaidi ya ufupisho wa ukweli kwamba watakatifu *"waliketi juu ya [viti vya enzi], na hukumu ikatolewa kwao"* (**20:4**). Waamini wa Mpito huliweka eneo hili *baada* ya kurudi mara ya pili kwa Kristo, fikiri kwamba "Ufufuo wa kwanza" ni ufufo wa waaminio katika *parousia,* na shikilia kwamba *"wengine wote waliokufa"* ambao*"watahuishwa"* kunazungumzia

[67] Maneno ya Kigiriki ya aya hizi mbili ni tofauti: **Ufu 12:12** = *oligon kairon*; **Ufu 20:3** = *mikron chronon.* Kimsingi maneno hayo ni sawa. Hata hivyo, Zodhiates anaonyesha utofauti kuhusiana na maneno ya "wakati": *Chronos* "anautazama muda kwa kiasi kama kipindi kilichopimwa kwa upatikanaji wa vitu na matukio na inaashiria kupita kwa kipindi au wakati. Neno lingine, *kairos* . . . hutafakari ubora wa muda kama kipindi kilichojihusisha na ushawishi au kuenea kwa kitu." (Zodhiates 1993: *"chromos,"* 1487) Tofauti hiyo ni thabiti pamoja na jinsi Ufunuo unavyotumia msemo "wakati mchache": kwenye **Ufu 12:12** "wakati mchache" (*kairos*) ambayo inaashiria, ubora, kipindi kilichofuatia Shetani kutupwa ulimwenguni ni wakati unaohusika na ushawishi au kuenea kwake juu ya nchi; kwenye **Ufu 20:3** "wakati mchache" (*chronos*) ambacho kinaashiria, ubora, wakati uliobaki wa ushawishi wa Shetani utaisha muda siyo mrefu.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kufufuliwa kwa kila mmoja, waaminio na wasioamini pamoja, miaka 1000 baada ya *parousia*. Wasioamini katika milenia hushikilia kwamba "miaka 1000" ni maelezo ya siri au fumbo ya wakati huu, baina ya kufufuka kwa Kristo lakini *kabla* ya kurudi mara ya pili. Wanang'ang'ana kwamba "ufufuo wa kwanza" huzungumzia maisha mapya ya Wakristo ndani na kwenye muunganiko pamoja na Kristo (Augustine 1950: 20.6-.10; White 1992: 22; Shepherd 1974: 36-38; Venema 2000: 331-36), Ufufuo wa Kristo ambao kwao waaminio wataushiriki Kiroho (Hughes 1977b: 315-18), au kuhamishwa kwa Wakristo kwenda mbinguni kupitia kifo cha miili yao (Kline 1975: 366-75). *"Wengine wote waliokufa"* ambao*"watahuishwa"* inazungumzia wasioamini ambao hawakushiriki kwenye " ufufuo wa kwanza" lakini ambao ufufuo wao ni ufufuo wa kimwili tu ambao utatokea wakati wa *parousia* (Beale 1999: 1013-14; White 1992: 10-11; kwa maelezo ya kina zaidi juu ya mambo haya yote angalia Beale 1999: 991-1017).

8. Muda wa "Miaka Elfu." "Kwamba utawala wa Milenia ulioelezwa kwenye mst. 4-6 utatokea kabla ya kurudi kwa Kristo mara ya pili ni ushahidi kutokana na ukweli kwamba hukumu ya mwisho, iliyoelezwa kwenye mst. 11-15 za sura hii, inaonekana kama kuja baada ya utawala wa miaka elfu. Siyo tu kwenye kitabu cha Ufunuo lakini penginepo kwenye Agano Jipya hukumu ya mwisho imeambatana na kurudi kwa Kristo mara ya pili. (Angalia Ufunuo 22:12 na vifungu vifuatavyo: Mt. 16:27; 25:31-32; yuda 14-15; na hasa 2 Wathes. 1:7-20.) Hili kuwa jambo muhimu, ni wazi kwamba utawala wa miaka elfu ya Ufunuo 20:4-6 lazima litokee *kabla* na *siyo baada* ya kurudi kwa Kristo mara ya pili." (Hoekema 1977: 160)[68]

Utawala wa watakatifu kama *wakati huu*, siyo baadaye, mambo ya kushangaza yamethibitishwa pamoja na kitabu chote cha Ufunuo na Agano Jipya, ambayo yanaonyesha Kanisa kwa sasa kama limeinuliwa pamoja na Kristo mbinguni (**Efe 2:5-6; Wafil 3:20; Waeb 12:18-24; Ufu 1:6; 5:9-10; 6:9-11; 7:9-17; 13:6; 14:1-4; 15:2-4**). Kwa mfano, **Ufu 20:4b** kwa wazi unafanana na **Ufu 6:9** (Gourgues 1985: 680 [jedwali na maneno]):

Ufu 6:9	***Ufu 20:4b***
Nikaona (*eidon*) chini ya madhabahu	Nikaona (*eidon*)
Roho (*tas psuchas*)	Roho (*tas psuchas*)
Zao waliochinjwa	Zao waliokatwa vichwa
Kwa ajili ya neno la Mungu (*dia ton logon tou theou*) na kwa ajili ya ushuhuda (*kai dia tēn marturian*) waliokuwa nao.	Kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu (*dia tēn marturian Iēsou*) na kwa ajili ya neno la Mungu (*kai dia ton logon tou theou*).

Kwa kifupi, "Aya za ufunguzi za surah ii zinatangaza ushindi wa kiulimwengu alioushinda Kristo katika ujio wake wa kwanza. Aya za 4-6 zinazungumzia ushindi wa pili wa ushuhuda wa uaminifu wake, bila kujali kuonekana kama kushindwa, ama ushindi huu utakuwa kwenye ufalme wa mbinguni wa hali ya kati au ufalme wa kidunia wa maisha ya Kikristo." (Grenz 1992: 163) Hivyo, "Wakati watakatifu wakichukuliwa kwenda mbinguni katika kifo hujumuika na Kristo kwenye liti chake cha hukumu kutawala juu ya adui kwenye uzinduzi wa utimilifu wa ahadi iliyotolewa kwa "washindi" kwenye 3:21 na 2:26-27, ingawa ahadi hizo pia zitafikia utimilifu kamili katika ufufuo wa mwisho wa Watakatifu [angalia **Math 19:28; Luka 22:30; 1 Wakor 6:2-3**]" (Beale 1999: 996).

9. Maangamizi ya mwisho ya Shetani na nguvu zake (**Ufu 20:7-10**).

a. *Mashindano au vita ya **Ufu20:7-10** ni sawa na mashindano au vita ya **Ufu 16:14-16** na **19:17-21**, ambavyo vytatokea muda mfupi kabla ya parousia.* Waamini wa mpito huona mashindano au vita ya Har-Magedon (**Ufu 16:14-16**) na mashindano au vita ya **Ufu 19:19-21** kama maelezo mawili ya tukio lile lile ambalo litatokea muda mfupi kabla ya *parousia* (e.g., Ladd 1972: 256-57). Hata hivyo, huona mashindano au vita ya **Ufu 20:7-10** kama nyingine, mashindano sawa na hayo au vita ambavyo vitatokea baada ya *parousia* na baada ya Kristo kutawala juu ya nchi kwenye ukamilifu wa haki kwa miaka 1000 (Ibid.: 269-70). Wazo hilo

[68] "Ikiwa Ufu. 20:11-15 ni kuhusiana na mfuatano wa wakati kwa Ufu. 20:1-10 (kama ilivyo kwa waamini wa kabla ya milenia [e.g., Thomas 1995: 581]) basi mfano wa imani (ambao unafundisha kwamba hukumu ya wote itakuja wakati wa Kristo kurudi mara ya pili) itategemea kwamba 'miaka 1000' na 'msimu mdogo'kutangulia kurudi mara ya pili" (Waldron 2000b: n.p.).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

linaikanganya asili ya kurudi mara ya pili ambayo inahusisha, ufufuo, hukumu, na kuhuishwa kwa nchi na kuanza *"nyakati zijazo"* ambazo kwazo milele hakutakuwepo na dhambi au uovu tena. "Kipimo kingine kigumu cha nyakati za kabla ya milenia ni wazo lake la ushindi wa milele wa Kristo. Kulingana na Paulo, adui wa mwisho wa Kristo ni kifo, na Bwana atamwangamiza adui huyu wa mwisho katika kufufuliwa kwa waaminio (1 Wakor 15:25-26, 50-55 [ambako kutatokea kama sehemu ya *kurudi kwake mara ya pili*]). . . . Kwa sababu ya uaminifu wao kwa fundisho la kabla ya Milenia, wanafundisha kwamba kifo hakitaangamizwa hadi mwishoni mwa utawala wa Milenia. Kwa hiyo, nyakati za waamini wa kabla ya milenia, huuweka ushindi wa mwisho wa Kristo miaka elfu kamili baada ya kufufuka na hivyo miaka elfu baada ya tukio ambalo Paulo alilitangaza kama alama ya ushindi wa Bwana." (Grenz 1992: 143-44)

Nyongeza ya athari ambazo kurudi kwa Kristo mara ya pili inazo kwenye kuondoa dhambi na kifo, mazingira ya Ufunuo yenyewe yanafunua kwamba mashindano au vita ya **20:7-10** ni sawa kama ile ya **16:14-16** na **19:17-21**. Vifungu vyote vitatu vimechukuliwa kwenye unabii wa Gogu na Magogu wa **Ezekieli 38-39**. Meredith Kline anajadili mwingiliano wa kimahusiano wa **Ezekieli 38-39; Ufu 16:14-16; 19:17-21**; na **20:7-10**. Anaelezea kwa kina jinsi Ufunuo viashiria vyake lazima vyote view vinazungumzia mashindano yale yale ambayo yatatokea wakati wa *parousia*: "Vita (*polemos*) ya Ufu 20:8 kwa uhakika ni 'vita ya siku ile kuu ya Mungu, Mwenyezi,' mashindano au vita ya Har Magedon yameelezwa kwenye 16:14-16. Kwenye kila tukio ni vita ambayo Shetani, joka, watayakusanya mataifa yote ya ulimwengu. . . . Mahusiano ya Ufu 20:7-10 kwa Ezekieli 38-39, kwa uwazi wa kutosha yameasiliwa kutoka yale ya istilahi ya Gogu-Magogu kwenye Ufunuo 20, pia yameshuhudiwa kwa kuwekwa msingi wa mifanano: kupanga makundi kutoka pande nne za nchi (Ezek 38:2-7, 15; 39:4; Ufu 20:8); kutembea kwa majeshi yaliyokusanyika kuwazunguka Watakatifu kwenye mji wa Mungu, kiini cha ulimwengu (Ezek 38:7-9, 12, 16; Ufu 20:9); kuandaliwa kwa tukio na Mungu (Ezek 38:4, 16; 39:2, 19; Ufu 20:3, 7); muda wa tukio baada ya kipindi kirefu ambacho watu wa Mungu walihifadhiwa kutokana na shambulio hili la kiulimwengu (Ezek 38:8, 11; Ufu 20:3); hitimisho la mgogoro wa nyakati za mwisho (Ezek 39:22, 26, 29; Ufu 20:10ff.); na kuangamizwa kwa moto kwa nguvu za uovu (Ezek 38:22; 39:6; Ufu 20:9-10). Kama ilivyo wazi, unabii wa Ezekieli juu ya Gogu-Magogu Ezekieli 38-39 ni chanzo cha msingi kilichochukuliwa na Ufu 16:14-16; 19:17-21 na nabii nyingine za Ufunuo za mgogoro wa mwisho. Yaliyojitokeza kwenye vifungu hivi ni vipengele vikuu ambavyo huwekea alama utegemezi wa Ufu 20:7-10 juu ya unabii wa Ezekieli—yaani, kusanyiko la kiulimwengu la majeshi ya adui (Ufu 16:14-16; 17:1214; 19:19; linganisha na 6:15 pamoja na Ezek 39:18-20), pia jumuisha mpangilio wa kihistoria wa tukio hilo mwishoni mwa nyakati za dunia (Ufu 6:12-17; 11:7-13; 16:16-17 [cf. 17:10-14]; 19:15-21), kufuatiliwa na kipindi ambacho kimetolewa kwa Kanisa kukamilisha ujumbe wake wa ushuhuda wa injili (11:3-7; cf. 12:6, 14). . . . Kwa hiy kufuatia hiyo miaka elfu ambayo itatangulia mgogoro wa Gogu-Magogu wa Ufu 20:7-10 kutanguliwa na tukio Har Magedon-*parousia* kwenye vifungu vingine. Har Magedon siyo kabla ya milenia, lakini kuacha. Har Magedon inaashiria mwisho wa milenia. Na hitimisho hilo kuelezea mwisho wa kabla ya milenia." (Kline 1996: 219-20)

Kwa kuwa Ufunuo wote una muundo mfanano endelevu, kwenye marudio hayo ya angamizo la mwisho la kwa Shetani na nguvu zake tunaona maendeleo ya hila ya wazo ambalo lilikuwa limejadiliwa hapo nyuma kwenye **sura za 16** na **19**: "Kwenye Ufu.16.14 watawala wa kidunia wanakusanyika kwa vita au mashindano, kwa roho chafu, kwenye Siku ya Bwana; kwenye 19.19 mnyama, pamoja na watawala wa dunia na majeshi yake, watafanya vita kinyume na Masihi na wafuasi wake; wakati ambao kwenye 20.8 Shetani mwenyewe atakusanya kusanyiko lisilohesabika na mataifa hasidi kutoka pande nne za dunia . . . kufanya vita na watu wa Mungu juu ya nchi na mbinguni (20.9)." (Smalley 2005: 513) Kwa maneno mengine, mwonekano wa mwisho wa tukio hili humfunua Shetani kuwa na "nguvu nyuma ya kiti cha enzi" ambaye huwaongoza wote mapepo na mnyama.

Inawezekana kuonekana "kiasili" kuyaona matukio ya **Ufu 20:7-10** kama mashindano ya kimwili (au vita) baina ya Shetani na wafuasi wake na Kanisa, vikihusisha silaha za kimwili za vita. Kuungwa mkono kwa kipengele cha "kimwili" cha vita baina ya dunia na Kanisa kinapatikana kwenye **Math 24:22** ambacho kinasema, *"Na kama siku hizo zisingalifupizwa,*

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

asingeokoka mtu yeyote;lakini kwa ajili ya wateulezitafupizwa siku hizo" (angalia pia **Marko 13:20**). Hata hivyo, bila shaka, kwa hakika hili siyo lengo la kifungu hiki. Kwenye maoni yake juu ya kifungu hiki, J. Marcellus Kik anaonyesha, "Lugha ni wazi kiasi ambacho ni vigumu kwetu kutambua hii siyo mashindano ya silaha—ya upanga na bunduki. Bwana wetu kwa uwazi anaonyesha kwamba mashindano kwa Ukristo havipiganwi kwa silaha za kimwili. Ni mashindano baina ya Injili ya kweli na Injili ya uongo. Ni mashindano ya kweli kinyume na makosa. . . . Siyo vita ya damu na nyama 'lakini kinyume na falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho' [**Efe 6:12**]. . . . Bila shaka kutakuwa na mateso. Adui anaweza kutumia nguvu za kimwili. Lakini silaha kuu zitakuwa kwenye ulimwengu wa roho." (Kik 1971: 238. 240-41)

Tunahitaji kukumbuka kwamba kwenye kitabu chote cha Ufunuo, msisitizo umekuwa juu ya suala la ni yupi aliye Bwana wa kweli na kubakia mwaminifu hata kufa. Tumeona kwamba kipengele muhimu sana cha Babeli Mkuu kilikuwa ni uovu wake wa *kiroho*, siyo uovu wa kisiasa au wa kiuchumi. Huo pia ndio ukweli kuhusiana na "Mpinga Kristo"—Msisitizo wa Biblia juu ya asili yake ya *kiroho,* siyo suala la kisiasa au kiuchumi. Hivyo shauku ya msingi ya Kristo kuhusiana na kurudi kwake ni, *"Wakati atakapokuja Mwana wa adamu je! Ataiona imani duniani?"* (**Luka 18:8**) Kama tulivyoona pia, hukumu ya Mungu wakati wote imeonekana kama mashindano au vita, na wakati Mungu atakapotuma *"moto kutoka mbinguni"* (**Ufu 20:9**) wakati wote unaashiria hukumu yake.[69] Vivyo hivyo, **Ufu 20:9-10** na vifungu vingine kwenye kitabu ambavyo vinaonekana kuelezea Mungu akihitimisha kwa kasi mashindano ya kimwili yaliyo kinyume na watakatifu kwa uhakika yaweza kuwa maelezo ya fumbo au yak i-ishara ya hukumu ya mwisho yenyewe ambayo itatokea kwenye muunganiko na *parousia*.

b. *Shetani "ametupwa kwenye ziwa la moto . . . alipo mnyama na nabii wa uongo (**Ufu 20:10**).* Waamini wa kabla ya mpito wanang'ang'ana kwamba mnyama na nabii wa uongo wamekuwa kwenye ziwa la moto kwa miaka elfu kabla ya Ibilisi kutupwa huko. Tafsiri nyingi za Kiingereza zinaonekana kukubaliana na hilo kwa kusema kwamba Shetani ametupwa kwenye ziwa la moto *"alipo mnyama na nabii wa uongo"* (NASB; NKJV), au *"walipo"* (ESV; RSV), au hata *"alipokuwa ametupwa"* (NIV). Kwa uhakika, hukumu ya Shetani, mnyama, na nabii wa uongo ni wakati uo huo, siyo utaratibu wa kudumu. Hukumu kwenye **Ufu 20:10** ni marudio ya hukumu kwenye **Ufu 19:20**, pamoja na maelezo ya ziada ya Shetani, kwa kuwa kushindwa kwa Shetani ndilo lengo la **Ufu 20:1-10**.

Sarufi ya Kigiriki ya kifungu hiki ni yenye wasiwasi na kiasili inaunga mkono mtazamo wa kurudiwa wakati uo huo, siyo mtazamo wa hukumu ya utaratibu wa kudumu. Andrew Steinmann anaelezea kwanini: "20:10 inapaswa kuonekana kama marudio ya hukumu kwenye 19:20 ikiwa na nyongeza ya hukumu ya Shetani. 20:10 kiuhalisia inasomeka: 'Na Yule Ibilisi mwenye kuwadanganya akatupwa (*eblēthē*, kiashiria batili cha kibinadamu) katika ziwa la moto na kibiriti, alimo Yule mnyama na nabii wa uongo. . . . Nao watateswa mchana na usiku milele na milele.' Kitenzi cha umboyai kinachotawala 'mnyama' na 'nabii wa uongo' kinamtaka mtafsiri kuchukulia chanzo kimoja kwenye Kiingereza. Watafsiri wengi huleta au huandika 'alimoau walipo mnyama na nabii wa uongo'—kama vile hukumu zote mbili ni zaq utaratibu wa kudumu, siyo sawa. Lakini umboyai la wingi wa mtu wa tatu kuunda *einai* ni nadra (BDF 71). Muundo wa kawaida wa umboyai utakuwa ni kuondolewa kwa kitenzi kulingana na kitenzi kilichotangulia. Hivyo tafsiri nyingi za asili za 20:10 zinaweza kuwa: 'Na Ibilisi ambaye alikuwa akiwadanganya alitupwa kwenye ziwa la moto na kibiriti mahali alipo alipotupwa mnyama na nabii wa uongo' (cf. NIV). (Kumbuka: 'Walitupwa' [kibinadamu] = kwa wakati uo huo, siyo 'alikuwa ametupwa' [akiwa na kingamwili] = kabla ya wakati ambao Ibilisi alitupwa huko.)." (Steinmann 1992: 77-78n.18; angalia pia Beale 1999: 1030 [Shetani, mnyama, na nabii wa uongo wote wanaweza kuonekana "kama wametupwa kwenye ziwa la moto kwa wakati ule ule ama imekwisha [i.e., kiliondolewa] kitenzi ni 'alitupwast' au 'walitupwa' (herufi ambayo ingefanana na kitenzi kilichotangulia kuhusiana na Ibilisi"])[70]

[69] Angalia Menn 2017, sehemu ya **VIII.J.**1.a. *"Kumbukumbu ya Yesu kwa "umeme" kwenye Math 24:27 pia yaweza kuashiria hukumu"* kwa vifungu ambavyo Mungu alituma moto kutoka mbinguni.

[70] Kwa nyongeza, "Uwezekano kwamba 20:7-10 ni marudio ya 19:17-21 kunafanya uwezekano wa dhana kwamba

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

10. Hukumu ya mwisho (**Ufu 20:11-15**). “Yohana tayari alishaandaa wazo tangulizi kwamba hukumu ile ile ingeweza kwanza kuonekana kama mashindano au makabiliano, na kisha kama mandhari ya chumba cha mahakama. . . . Mandhari ya 20.1-15 inaualika uelewa kama kurudia, kutumia picha tofauti, ya hukumu ya mwisho kama vile simulizi kwenye 20.7-10.” (Mealy 1992: 177, 179) Hivyo, wakati **Ufu 20:7-10** na **20:11-15** vyote vikielezea hukumu ya mwisho, kila maelezo yanao msisitizo wake: “Awali ya viwili [**20:7-10**] inasisitiza kuangamizwa kwa Ibilisi na mawakala wake, labda kwa sababu simulizi yote ya Ufu 20 inaanza na yeye kama somo lake. Kisha mandhari ya mwisho ambayo inafuata [**20:1-15**] imeweka msisitizo wake juu ya Mungu kama hakimu, ambaye anawakilisha hukumu yake ya mwisho kwa wakati huu.” (Shea 1985: 49) Ukweli kwamba **20:11** inaeleza *“mbingu nan chi zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana”* yote yenarudia mwonekano wa awali wa hukumu ya mwisho (**Ufu 6:12-14; 11:13; 16:17-21**) na kuhitimisha asili ya mabadiliko ya uumbaji ya *parousia* na hukumu ile itakayotokea kwenye mwunganisho pamoja nayo.

a. *Hukumu ya mwisho itatokea kama sehemu ya matukio yanayohusiana na parousia.* Kuna mlingano wa wazi baina ya **Ufu 20:11-15** na **1 Wakor 15:20-54**. Kwenye **1 Wakor 15:26** Paulo alisema, *“Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti.”* **Ufu 20:14** inasema kwamba *“Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto.”* “Maelezo yak i-ishara ya kuangamizwa kwa Mauti na Kuzimu [katika hukumu ya nyakati za mwisho] yanalingana na maelezo ya Paulo kwenye 1 Wakor 15:26. . . . Kwa wote Paulo na Yohana mandhari ya mwisho kwenye mchezo wa ukombozi kabla ya kuzinduliwa kwa hali ya mwisho ni kuondolewa kwa Mauti.” (Page 1980: 42) Ambako kutatokea kwenye muunganiko pamoja na *parousia* (angalia **1 Wakor 15:50-54**). Kama tulivyoona, Injili, Nyaraka, na Ufunuo vinazungumzia simulizi sambamba: *parousia* inahusisha kufufuka na hukumu; ni upeo wa mgawanyiko baina ya *“nyakati hizi”* na *“nyakati zijazo.”*

b. *Hukumu ya wasioamini tu, au watu wote?* Baadhi ya watu, kimsingi waamini wa mpito, hufikiri kwamba kutakuwepo na hukumu nyingi tofauti kwenye Agano Jipya: hukumu ya “mataifa” kuona ni nani atakayeingia ufalme wa milenia (**Math 25:3146**); hukumu ya kuwatenganisha waaminio mbele ya “kiti cha hukumu cha Kristo” kupokea thawabu (**2 Wakor 5:10**); na hukumu ya “kiti cha enzi kikubwa cheupe” ya **Ufu 20:11-15** ambayo wanafikiri itawahusu wasioamini pekee yao (e.g., Scofield 1967: 1036-37n.2, 1375n.1; Thomas 1998: 223; MacDonald 1995: 1299; Smith 1980b: 193). Vingine angalia **Ufu 20:1115** kama hukumu ya jumla kwa watu wote, waaminio sawa na wasioamini (e.g., Hendriksen 1982: 196; Ladd 1972: 271; Ngundu 2006: 1576).[71] Ingawa msisitizo kwenye kifungu hiki waweza kuwa juu ya wasioamini, watu wote wamejumuishwa, kwakuwa, kama tulivyojadili hapo nyuma, Biblia inaonyesha kwamba kutakuwa na hukumu moja tu ya jumla kwa watu wote (angalia Menn 2017, sura ya **V. Umuhimu wa nyakati za mwisho na kurudi kwa kwa Kristo mara ya pili**). “Mambo ya mwisho ya hukumu ya mataifa siyo ufalme wa milenia lakini ni ama uzima wa milele au adhabu ya milele (Math. 25:46). Hii ni hukumu ya mwisho ya wazi itakayoamua mwelekeo wa mwisho wa mwanadamu. Kiti cha hukumu cha Kristo pia ni Kiti cha hukumu cha Mungu ambacho mbele yake waaminio wote watapaswa kusimama (Rum. 14:10).” (Ladd 1972: 271)

Kwenye kuweka mfanano wa hatua kwa hatua wa asili ya kitabu, **Ufu 20:11-15** ni mafafanuzi ya hukumu ambayo tayari ilikwisha kutajwa, ingawa haijaelezewa, katika **Ufu 11:18**. Maelezo *“wafu wakahukumiwa”* yanaonyesha kwamba **Ufu 20:11-15** “ni upanuzi wa maelezo mafupi ya awali ya adhabu ya mwisho kwenye 11:18 (‘wakati [ulifika] kwa wafu kuhukumiwa’). 11:18 pia inalenga juu ya hukumu ya waovu, lakini inajumuisha ‘thawabu’ kwa ‘watumishi wa Mungu manabii na watakatifu na wale wamchao’ Mungu.” (Beale1999: 1033; angalia pia Johnson 2001: 298)

---

alitupwa motoni miaka mingi baada ya washiriki wake wa Kishetani kwenda kwenye moto mwishoni mwa sura ya. 19. Baaadhi hufikiri kwamba kwa 20:10 kurudia matukio yanayofuatana pamoja na kufariki kwa mnyama na nabii wa uongo tutahitaji lugha ya wazi zaidi, kitu kama ‘Baada ya vita ya Gogu na Magogu, Shetani alitupwa kwenye ziwa la moto akiwa pamoja na mnyama na nabii wa uongo.’Lakini hili siyo tarajio la lazima, hasa kwa kuwa mtindo wa kujirudia kwenye fasihi ya kinabii ya Agano la Kale haihusishwi na uwazi kama huo, wala kujirudia penginepo kwenye Ufunuo kunakojihusisha hivyo.” (Beale 1999: 1028)

[71] Baadhi, wakati wanashikilia kwamba ipo hukumu moja tu ya jumla ya watu wote, wanang’ang’ana kwamba **Ufu 20:11-15** unaelezea tu hukumu ya wasioamini (Johnson 1981: 589-90; Milligan 1896: 357).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Maneno ya **20:11-15** (i.e., *"wakubwa kwa wadogo"*), wakati unapoilinganisha na ukomo au sifa ya msemo huu wakati unapotumiwa penginepo kwenye Ufunuo, inatupeleka kwenye hitimisho kwamba watu wote, waaminio na wasioamini, watahukumiwa. Hivyo, kwenye **Ufu 11:18** na **19:5** *"wadogo kwa wakubwa"* huzungumzia waaminio wote, na kwenye **Ufu 13:16** na **19:18** *"wadogo kwa wakubwa"* huzungumzia wasioamini. Kwa upande mwingine, "kwenye kifungu kilichopo mbele yetu, ni sehemu tu ya ambao ni 'wadogo kwa wakubwa' wanaohusika—kama inavyoonekana—ni *'wafu.'* Hatujaongozwa bila kushindwa, kasha kuhitimisha kwamba maana inayokusudiwa ni, wafu—ulimwenguni kote, au angalau bila ubaguzi?" (Brown 1882: 200)

Kwenye kumbukumbu yake ya "vitabu", **Ufu 20:12** inaashiria **Dan 7:10; 12:1-2**. Kumbukumbu ya vifungu hivyo viwili vya Danieli tena vinaonyesha kuhusishwa kwa asili ya vyote ya hukumu kwenye **Ufu 20:11-15**: "Fikra ya vitabu kwenye Dan. 7 ni kulenga juu ya matendo maovu ya watesi wa watu wa Mungu wa nyakati za mwisho, ambayo kwayo watesi watahukumiwa. Kitabu kwenye Dan. 12:1 pia kinahusika na nyakati za mwisho, lakini ni picha ya ukombozi. Wale walioandikwa kwenye kitabu watapewa uzima, bali wale wasioandikwa kwenye kitabu watapata hukumu ya milele (12:1-2). Nabii hizi mbili za Danieli zinaonekana kutafuta kutambuliwa kwa nyakati wakati wa hukumu ya mwisho." (Beale na McDonough 2007: 1150)

Hatimaye, Agano Jipya limeweka wazi kwamba watu wote lazima wafike mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu (e.g., **Rum 14:10; 2 Wakor 5:10; Waeb 9:27**). **Ufu 3:5** hasa inazungumzia waaminio walioko kwenye kitabu cha uzima (angalia pia **Ufu 13:8**). Hakuna penginepo kwenye Ufunuo zaidi ya **20:11-15** inayofanya hukumu kama chumba cha mahakama kikitanguliwa na kuonekana kwa kitabu cha uzima. "[Ufu] 3:5 inasadiki kwamba waaminio katika Kristo watatokea mbele ya mahakama ya Mungu kwa hukumu, kabisa kama ilivyo hapa. Ikiwa Kanisa limeondolewa kutoka kwenye hukumu ya mwisho, inawezekana kuwa tu kwa sababu tayari lilikwisha kuonekana mbele ya Mungu kwenye hukumu. Yohana mwenyewe hatupi dokezo lolote kwamba tukio hili lilishatokea. Ni hekima kutambua kwamba Yohana anafundisha kwamba wote ni lazima wafike kwenye hukumu ya Mungu, watakatifu na wenye dhambi pia (Beasley-Murray 1974: 301) Kwa sababu hukumu ya **Ufu 20:11-15** inatumika kwa waaminio na wasioamini, kimsingi imetajwa kwenye **3:5** kwa hiyo majina ya waaminio ambayo hayakufutwa kwenye kitabu cha uzima yamefungwa na kutimizwa.

c. *Asili ya hukumu.* **Ufu 20:12** inaeleza kwamba watu watahukumiwa *"kulingana na matendo yao."* Hatuwezi kuiona njia ya mbinguni au kufanya "matendo mema" ya kutosha kupata haki ya kuachiliwa kwenye hukumu ya Mungu; tunaokolewa kwa neema tu kupitia imani katika Kristo (**Yoh 3:16-18; 6:28-29; Rum 2:16-17; 10:8-13; Wagal 3:1-14; Efe 2:8-9**). Kwa hiyo, "KAzi ni kielelezo cha hali ya kiroho ya moyo wa mtu. . . . Hukumu itafunua uaminifu wa mtu umekuwa na Mungu na Mwanakondoo au na maadui wa Mungu. Theolojia ya imani ya Yohana na mahusiano yake na kazi haviwezi kutenganishwa ni sawa kama yale ya Yesu Kristo (Yoh 5:29), Paulo (Rum 2:6-8) na Yakbo (Yak 2), nah ii ndiyo maana ya kitabu kingine, *kitabu cha uzima,* kinaonekana kuwa na maamuzi (20:12, 15; 3:5; 13:8; 17:8; 21:27). Wale ambao majina yao yapo kwenye 'kitabu cha uzima' cha Mwanakondoo watakuwa pia na kumbukumbu ya matendo ya haki au mema. Upande wa pili pia utakuwa sahihi. Picha inaonyesha uwiano dhaifu baina ya neema na dhambi." (Ngundu 2006: 1576) Beale anahitimisha, "'Uzima' waliopewa watakatifu kwenye muunganiko na kitabu unatokana na utambulisho wao na matendo ya haki ya Mwanakondoo, na hasa kifo chake, ambayo pia yanamaanisha kwamba yanatambuliwa na maisha yake ya ufufuo (cf. 5:5-13). Hawatapata hukumu kwa matendo yao maovu kwa sababu Yeye (Kristo) alikwisha kuyapata kwa ajili yao: alichinjwa kwa niaba yao (hivyo hasa. 1:5 na 5:9). Mbele za Mungu, Mwanakondoo anawatambua wale wote walioandikwa kwenye kitabu (3:5) na wanatambuliwa pamoja na haki yake na kifo." (Beale 1999: 1037)

L. *Ufu 21:1-22:5: Mbingu mpya nan chi mpya: Yerusalemu Mpya*

Kwenye kifungu hili uumbaji mpya na Kanisa unakamilishwa kwenye utukufu. Neno "mpya" (**21:1-2, 5;** pia kwenye **2 Pet 3:13**) ni *kainos. "Kainos* inazungumzia kitu kipya kwenye *ubora* na ni kikilinganishwa na kile ambacho kinaonekana kutumika—nje nje, kilichochoka, au kile ambacho kilifunikwa kwa nyakati. . . .

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Hivyo, kwenye ufalme wa utukufu, kila kitu kitakuwa kipya: 'Yerusalemu mpya' (Ufu. 3:12; 21:2), 'jina jipya' (2:17; 3:12), 'wimbo mpya' (5:9; 14:3), 'mbingu mpya na nchi mpya' (21:1; cf. 2 Pet. 3:13), 'kila kitu kipya' (Ufu. 21:5)." (Trench 1989: 233-34) Kwa hiyo, "kifungu hiki hakifundishi kwamba mbingu nan chi sasa zinaletwa kwenye uwepo kwa mara ya kwanza, lakini kwamba zitamiliki tabia mpya" (Smith 1962: 1521).

1. Mbingu mpya nan chi mpya ni za sasa au za wakati ujao? Wanatheolojia, baadhi ya waamini wa baada ya milenia, na baadhi ya waamini wa ubora wa mawazo hung'ang'ana kwamba kwenye Yerusalemu Mpya, "tunayo picha ya muhimu, siyo ya wakati ujao, lakini ya wakati wa sasa; ya hali ya ubora wa watu halisi wa Kristo, na 'kundi lake dogo' juu ya nchi, kwenye kila nyakati. Picha haitakuwa imetambuliwa kikamilifu bado; lakini kila Baraka zinazoendana nayo juu yake ni kanuni ya waamini sasa, na zita zidi kuwa zake kwenye uhalisi wa uzoefu kadri atakavyoendelea kufungua macho yake na moyo wake kupokea." (Milligan 1896: 373; angalia pia Chilton 1985: 203-09; Mathison 1999: 157-58) Hivyo, "*maji ya uzima*" atoayo Kristo (**Ufu 21:6**) yanahusiana na ahadi Zake kwenye **Yoh 4:13-14; 7:37-39** kuwapa waamini wa sasa, "*maji ya uzima."* Kumbukumbu kwa*"mataifa"* (**21:24**) kiuhalisia imechukuliwa kuwa mataifa yasiyoongoka, kama ilivyo kumbukumbu kwa "wasio safi" (**21:27**), ambao "lazima walidhani kuwa hai juu ya nchi baada ya Yerusalemu mpya kuonekana" (Milligan 1896: 373; angalia pia Preston 2010: 266). Nafasi hiyo inasifa kwenye hili, kwamba kwenye kanuni, Yerusalemu Mpya ipo sasa. Uraia wa Wakristo upo mbinguni (**Wafil 3:20**); tayari tumekwisha kuufikia Mlima Sayuni, Yerusalemu yya mbinguni (**Waeb 12:22**).[72]

Kwa upande mwingine, kama ilivyopendekezwa hapo juu kwenye kifungu **XI.B.** ***Mbinu za tafsiri***, ingawa Ufunuo unasisitiza kanuni ambazo zinatumiwa na Waaminio sasa na kwenye nyakati zote, unafanya zaidi ya hilo: unatupa sisi maelezo ya mwisho wa nyakati hizi na mwanzo wa nyakati zijazo. Maelezo ya mbingu mpya na nchi mpya kama hali ya umilele ya wakati ujao ni sehemu ya lazima kwa maelezo ya awali ya Ufunuo ya mwisho wa historia. **Ufu 17:1-19:6** inaelezea kutupwa kwa mji wa kahaba wa ulimwenguni na mashangilio au shangwe ambayo ilitokea mbinguni kama matokeo yake. **Ufu 19:11-21** unaelezea *parousia*. **Ufu 20:1-15** unarudia nyakati za Kanisa, ukiishia na hukumu wakati wa *parousia*. Vifungu hivyo vinaonyesha kwamba upo mwisho wa historia. Moja ya makusudi ya Yohana kuandika kitabu ilikuwa ni "kuwahamasisha wasomaji wake kwenye imani kwamba utawala wa MpingaKristo na wafuasi wake unaelekea kupokelewa na utawala wa Kristo na watakatifu wake. Asingeweza, lakini aliamini kwamba kutupwa kwa mji wa kahaba na mpinga Kristo kungefuatiwa na kuanzishwa kwa mji wa Bibi-arusi kwenye utawala wa Kristo." (Beasley-Murray 1974: 315) Ikiwa **Ufu 21:1-22:5** hauelezi kwa muundo wa maono nyakati zijazo, basi hatutakuwa na maelezo ya nyakati zijazo kabisa lakini ingekuwa yameachwa katika upeo wa hukumu ya mwisho. Kwenye kitabu hili limebuniwa kwenye sehemu ya mwisho ya simulizi ya Mungu na kuleta hitimisho la Biblia yote, hili halisadikiki.

Kwahiyo kwenye sehemu hii ya mwisho ya kitabu, kila tishio linaloonekana na lisiloonekana kwa watu wote wa Mungu, wote wa kiroho na kimwili, limeondolewa: maumivu yote yaliyopita, huzuni, na masikitiko yamefutiliwa mbali, na yote yamefanywa kuwa mapya. Hakuna tena dhuluma yoyote, dhambi, au kupingana, lakini utakatifu kamilifu, furaha, na umoja utatawala miongoni mwa watu na baina ya watu na Mungu. Hii siyo tu ndoto au uwezekano wa kubuni wa "tayari" ya ufalme lakini ni mwonekano wa maono ya "bado" ya ufalme. Kwa hiyo, mtazamo wa wengi huona **Ufu 21:1-22:5** kama unazungumzia kile kitakachotokea nyakati zijazo, kuanzia na *parousia.*

2. Matukio yaliyoelezwa kwenye **Ufu 21:1-4** yatatokea katika *parousia.* **Ufu 21:3** unaelezea kurudi kwa Kristo katika nchi. Kwa kufanya hivyo, unatumia msemo *"maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu."* Neno la Kigiriki kwa "maskani" ni *skēnē*. Hili ni la muhimu kwa sababu, yote yanahusiana na *parousia* na kuja kwa Kristo mara ya kwanza, kwa wakati uo huo, inaonyesha ni jinsi gani *parousia* kunavyotimiza tumaini la Wayahudi la kuja kwa Mungu kukaa pamoja nao. "Wayahudi wanatazamia kurudi kwa *Shekinah* kwenye ufalme wa Mungu. Wayahudi wanaozungumza Kigiriki wanajua kwamba istilahi *Shekinah* lina konsonanti ile ile kama ya Kigiriki skēnē, na hili linawawezesha wao kuungana na *skēnē* wazo la Shekinah. Mfano maarufu wa hili umetokea kwenye Yohana 1:14, 'Naye neno alifanyika

[72] Ingawa malengo ya Yerusalemu mpya ni maono ya *"nyakati zijazo,"* pia ina kusudi la kimaadili kwenye hilo inaonyesha *kwenye kanuni* kile maisha yetu ndani ya Kristo yanavyopaswa kuonekana sasa: "Maelezo yote ya mji kwenye 21:9-22:5 yanakubalika kwa wazi kwa wazo la ufalme wa Kristo kufunuliwa kwenye ulimwengu huu" (Beasley-Murray 1974: 316); "Kile tunachokipata hapa kwenye Ufunuo 21:1-22:5 ni maelezo ya ulimwengu uliookolewa wa wakati ujao kama ulivyofunikwa na Kanisa lililoookolewa la wakati wa sasa" (Hendriksen 1982: 197)

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mwili, akakaa kwetu (Kigiriki *eskēnōsen*, kutoka *skēnē*), nasi tukauona utukufu wake.' Kwenye mwili, Bwana tumaini la kurudi kwa Mungu kwenye *Shekinah* utukufu wake kulitimizwa. Ufunuo uo huo wa utukufu wa Mungu umefikia hitimisho lake kwenye ujumbe wetu." (Beasely-Murray 1974: 311) Umuhimu wa *parousia* kwa watu wa Mungu kumeongezwa zaidi ya ukweli kwamba sasa *"maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu"* (**Ufu 21:3**). Watu wa Mungu wameelezewa kama bibi-arusi (**Ufu 19:78; 21:2, 9**) na mji. Ishara ya bibi-arusi na mji "kimsingi unaonyesha kitu kile kile, yaani, watu wa Mungu kwenye ushirika na Mwokozi wao" (Ibid.: 316). Kwenye **Ufu 19:7-8** Bibi-arusi *"amejitayarisha mwenyewe"*; kwenye **21:2** anaonekana *"akishuka kutoka mbinguni kwa Mungu."* Beasley-Murray wanahitimisha, "Kwa uwazi Yohana alitaka kuonyesha kwamba bibi-arusi atatokea katika utukufu akiwa pamoja na Bwana-arusi, na hivyo karamu ya ndoa itasherehekewa." (Ibid.: 315)[73]

3. <u>**Ufu 21:1-22:5** inatimiza ahadi za Agano Jipya kwamba kurudi kwa Kristo mara ya pili kutaleta pamoja nako uhuisho wa uumbaji.</u> Nchi mpya ni kipengele muhimu cha mpango wa Mungu wa ukombozi. Hitaji la kukombolewa uumbaji linachipuka kutoka kwenye anguko la mwanadamu na "laana" ambayo iliathiri uumbaji wote (**Mwanzo 3:14-19**): "Mungu sasa amemtumwa Mwanae kwenye ulimwengu huu kuukomboa uumbaji huo kutokana na matokeo ya dhambi. Kwa hiyo, kazi ya Kristo, siyo tu kuokoa watu Fulani binafsi, hata siyo kuokoa umati usiohesabika wa watu waletao damu. Kazi yote ya Kristo siyo pungufu kuliko kuuokoa uumbaji wote kutokana na madhara ya dhambi." (Hoekema 1979: 274-75)

Awali tuliona *parousia* ya Kristo ikiihusisha kuangamizwa au kutakaswa kwa dunia ya sasa. Kwamba asili ya Yerusalemu Mpya—i.e., kuhuishwa kwa uumbaji—kunatokea kama sehemu ya matukio tata ya *parousia* yanaonekana kwenye **Ufu 21:1** ambayo inasema kwamba *"mbingu mpya nan chi mpya zimekwisha kupita."* Uumbaji uliokombolewa unaoelezewa kwenye **Ufu 21:1-22:5** siyo tu picha ya ndoto ya *"nyakati hizi."* Badala yake, "mbingu mpya nan chi mpya" ni "vipya," i.e., upya kwenye ubora. Haifanani na "nchi ya kwanza" au "mambo ya kwanza" ambayo *"yamekwisha kupita"* (**Ufu 21:1, 4**). Kwa hiyo, **Ufu 21:4** inasema kwamba, kwenye nchi mpya, *"wala mauti haitakuwepo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu."* **Ufu 22:3** unaongeza, *"Wala hapatakuwa na laana yoyote tena."*

Kweli hizi zinawaondoa waamini wa kabla ya milenia na wanatheolojia kwa kuwa wote hushikilia kwamba dhambi na mauti bado zitakuwa na madhara au athari baada ya kurudi mara ya pili. Kwa sababu kuhuishwa kwa uumbaji wakati wa kurudi kwa Kristo mara ya pili kunajumuisha kuondolewa kwa mauti, maombolezo, kilio, maumivu, na laana, kwa umuhimu huo hakutakuwepo na uwezekano wa dhambi yoyote. Kwa hiyo, wazo la kwamba kutakuwepo na umati wa waasi wenye dhambi miaka elfu baada ya kurudi kwa Kristo haliwezi kuwa sahihi.

4. <u>*Parousia* na hukumut: mambo au vipengele hasi na chanya.</u> Ingawa hukumu imeelezwa kwenye **Ufu 20:11-15** ikijumuisha wote wenye haki na wasio na haki, lengo hapa lilikuwa juu ya hukumu ya wasiomcha Mungu ambao watatupwa kwenye*"ziwa la moto."* **21:1-22:5** sawa na hiyo, inaonyesha mambo hasi ya hukumu yanayohusiana na *parousia,* lakini picha tofauti zilitumiwa: "Ziwa la moto halimaanishi kupotezwa kwenye upinzani kwa kuwepo, lakini kuwepo kwa upotofu kwenye jamii ya waovu inayopingana na uzima kwenye jamii ya Mungu. Kwa sababu hiyo Yohana anaweza kuwasilia ukweli ule ule kwa ishara tofauti sana ya uzima nje ya mji (21:27) kwenye utofauti wa uzimandani ya mji (21:24ff.), kujitenga kuliathiriwa na ukuta wa mji (21:14)." (Beasley-Murray 1974: 304)

Kwenye **Ufu 21:1-22:5**, wakati athari hasi za *parousia* na hukumu vikitajwa, kumbukumbu kwa wale ambao waliondolewa kutoka Yerusalemu Mpya karibia inaanzia kama pembeni. Badala yake, msisitizo upo juu ya athari chanya za *parousia*. Mengi ya **Ufunuo 21-22** yanaelezea tena kuondolewa kwa mateso yote na mauti, kuponywa kwa mataifa, uwepo wa Mungu na Mwanakondoo, na utukufu mkuu, na mwangaza, na uzima wa upya, ufalme wa milele. Mealy anajadili jambo moja la hila ya msisitizo "chanya" wa *parousia* kwamba, tena inaonyesha mfanano wa hatua kwa hatua wa asili ya kitabu: "Kwenye Ufu. 21.6, mmoja Aliyeketi kwenye Kiti cha Enzi alitangaza kwamba 'imekuwa' (kiuhalisia, 'Wamekuwa' [*gegonan*]). Hili linaleta mwangwi wa msemo wa kufanana ambao ulisikika kutoka kwenye kiti cha enzi wakati wa kumiminwa kwa kitasa cha saba cha mwisho wa hasira ya Mungu kwenye 16.17 (*gegonen*). Ikiwa maana ya kulia 'Imekuwa' kwenye mazingira ya kitasa cha saba yaliashiria utimilifu wa parousia kama hukumu ya ulimwengu, kisha bila shaka chanya 'Wamekuwa'

[73] Mealy ameorodhesha sababu zingine sita kuonyesha kwamba asili ya Yerusalemu Mpya kwenye **Ufu 21:1-6** itatokea wakati wa *parousia*, siyo miaka elfu baada ya *parousia* (Mealy 1992: 223-25).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

hapa kunazungumzia utimilifu wa pande zote mbili za mpito wa ufalme wa Mungu wa nyakati za mwisho, vyote hasi na chanya. Kama 21.4 inavyothibitisha, 'Mambo ya kwanza yamekwisha kupita'. Bado siyo tu kwamba ya zamani yamehukumiwa na kuondolewa, lakini mapya yameanzishwa kwenye mahali pake." (Mealy 1992: 225)

5. **Ufu 21:1-22:5** utimilifu wa kile kilichoahidiwa kwa waaminio mapema kwenye kitabu. Mapema, wakati tunajadili kujirudia kwa mada, misemo, na ahadi kwa Kanisa, tuliona ni jinsi gani **Ufu 21:1-22:5** ilivyotimiza ahadi zilizofanywa kwa Kanisa kwenye sura tatu za kwanza za kitabu. Sawa sawa na, kwenye **Ufu 7:16-17** waaminio waliahidiwa kwamba hawataona njaa wala kiu tena, Mwanakondoo "*atawaongoza kwenye chemchemi ya maji yaliyo ya uzima,"* na *"Mungu atafuta kila chozi kwenye macho yao."* Ahadi hizo vivyo hivyo zimetimizwa kwenye **Ufu 21:4; 22:1-2**. Kwa nyongeza, mifano yote ya mateso, kukandamizwa, na maovu yatendwayo kinyume na Kanisa kupitia kwenye kitabu chote sasa yamebadilishwa. Kanisa limepata fidia ya milele—hakika, zaidi ya fidia—kwenye ulimwengu mpya wa Yerusalemu Mpya: "Siyo watawala katili na wasaidizi wao lakini mtoa uzima na nguvu ya kuendeleza uzima ya Mungu ikihusisha ufalme na utawala wa Mungu wa nyakati za mwisho" (Schüssler Fiorenza 1991: 113).

6. **Ufu 21:1-22:5** inatimiza **Isa 65:17-66:24**. Mahali pekee kwenye Agano la Kale ambapo *"mbingu mpya na nchi mpya"* vilitajwa ni kwenye **Isa 65:17** na **66:22**. **Isa 65:18-19; 66:10, 13, 20** pia inazungumza kuhusiana na Yerusalemu iliyorejeshwa. Kama alivyofanya kwenye Ufunuo wote, Yohana anachukuwa kutoka kwenye picha za Agano la Kale lakini anazifanya za kiulimwengu na kuzitafsiri tena kutumika kwenye watu wapya wa Mungu, watu wa kweli—Kanisa. Mfanano baina ya **Isaya 65-66** na **Ufunuo 21-22** unaashiria kwamba Yohana anauelezea utimilifu wa ufalme baada ya *parousia*.[74] Kwa uhakika, mfanano baina ya **Ufunuo 21** na **Isaya 65** unafunua kwamba *"Yerusalemu Mpya"* ni sawa na *"nchi mpya."* Kwenye**Isa 65:17-18** "Yerusalemu" inaonekana kuwa sawa na *"mbingu mpya nan chi mpya."* Sawa na, Yohana alivyoelezea*"mbingu mpya nan chi mpya"* (**Ufu 21:1**) lakini kisha mara anaelezea *"mji mtakatifu, Yerusalemu Mpya"* (**Ufu 21:2-3, 10-22:5**) kwa sababu Yerusalemu Mpya *ni* mbingu mpya nan chi mpya (angalia Beale 1999: 368; Levenson 1988: 89-90, 107).

7. Kumbukumbu kwenye **21:24-27** kwa "mataifa," "chochote kilicho najisi," na kuingia mjini" ni mwonekano wa fumbo wa ukamilifu wa haki wa uumbaji mpya. **Ufu 21:24-27** ni lugha ya fumbo. Wafalme na mataifa hawajatengwa kutoka au nje ya mji bali ni njia nyingine ya kuielezea asili ya mji. Gundry anaonyesha, "'Lete ndani yake [i.e., ndani ya mji (**Ufu 21:24**)]' ni lugha ya nafasi, lakini maana yake ni isiyokuwa na nafasi, kama vile vipimo vya mji ni nafasi lakini maana yake ni isiyokuwa na nafasi. . . . Maana ya 'lete ndani yake' inafanyika pamoja na utukufu na heshima ya mataifa ya watakatifu ya wafalme ambao waliufanya mji, siyo na mwenendo wa wasio haki kutoka mashambani kuingia mjini. . . . Kuingia mjini ni kusaidia kuujenga—na hakuna namna ya kuondoka au kuuacha mara utukufu na heshima inapokuwa imeletwa humo." (Gundry 1987: 264; angalia pia **Ufu 3:12** pale Yesu alipoahidi kwamba yeye ashindaye atafanywa nguzo kwenye hekalu la Mungu *"na wala hatatoka humo tena kabisa"*) **Ufu 21:24-27; 22:14** inamaanisha kwamba ni wale tu ambao majina yao yameandikwa

[74] Yohana ametoa maana ya kimamlaka na uvuvio ya kumbukumbu ya Isaya kwa *"mbingu mpya nan chi mpya"* (angalia pia **2 Pet 3:13**). Maana moja ya hili ni kwamba maelezo ya Isaya kwenye **Isa 65:20** kuhusiana na kijana kufa akiwa na umri wa miaka mia moja *haiwezi* kuchukuliwa kiuhalisia na *haiwezi* kuwa inazungumzia "milenia" ya muda mfupi wa miaka 1000. Sababu ni kwamba Yohana anazungumza kuhusiana na *hali ya umilele* baada ya *parousia,* ambayo kwayo *"mauti haitakuwepo tena."* **Isa 65:19** yenyewe inasema kwamba *"sauti ya kulia haitasikiwa ndani yake tena [Yerusalemu], wala sauti ya kuomboleza."* Arthur Lewis kwa wazi wazi anauliza, "Ni jinsi gani wazazi kwenye siku hizo watakuwa na furaha yoyote au tumaini, wakijua kwamba watoto wao watakufa wakati watakapofikia umri wa miaka mia moja?" (Lewis 1980: 37) Kumbukumbu ya Isaya kwa vijana kufariki wakiwa na umri wa miaka mia moja ni mfano wa "nahau ya kinabii", i.e., Manabii wa Agano la Kale wanazungumzia ufalme wa milele wa Masihi wakitumia lugha na kumbukumbu ya muundo wenye ukomo wa miili yao wenyewe, Mazingira ya Wana wa Israeli. Hata hivyo, Agano Jipya kwa kurudia rudia limeweka wazi kwamba Israeli ilikuwa tu kimwili "aina au mfano" au "kivuli" cha ukweli mkubwa sana. Hivyo, Lugha ya Agano la Kale ya kijana kuishi kufikia umri wa miaka 100 ni kimwili, lugha ya kimfano ambayo inaonyesha maisha ya ufufuo—maisha ya milele—kwa watu wa Mungu kwenye hali ya umilele (angalia Lee Irons n.d.; angalia pia Lewis 1980: 37 ["Isaya mara nyingi aliona utawala wa Bwana wa wakati ujao kwenye ukomo na kilelezo cha maneno "]). Muumini wa kabla ya milenia Greg Bahnsen anachukua "kufa katika umri wa miaka 100" kwenye **Isa 65:20** kwa uhalisia lakini anang'ang'ana kwamba Isaya anazungumza kuhusiana na muda ambao "kwa sababu ya Baraka za Mungu juu ya watu wake, umri wa maisha utarefushwa sana kwamba kufa ukiwa na miaka 100, unaonekana umekufa ukiwa mtoto bado [i.e., 'nyakati za dhahabu' waamini wa kabla ya milenia wanaamini kitatokea kwenye historia kabla ya *parousia*]" (Bahnsen 2015: 58).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kitabu cha uzima cha Mwanakondoo ndio watakaoweza kuingia mbingu mpya nan chi mpya, kwa sababu **Ufu 20:15** inasema, *"Iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto."*[75]

Martin Kiddle anasema, "*Mataifa ni* wale waliokombolewa, ambao ni wa kiroho lakini siyo wa kitamaduni kwa makabila kumi na mawili. Kristo hakuwakomboa 'watu kutoka kila kabila na lugha na jamaa na taifa'? Vizuri sana, *kwamba* ndivyo Wakristo wanavyopaswa kuusoma nabii hizi za zamani: wao ni *mataifa*. Sawa na, *wafalme wa nchi* . . . (hivyo ni lazima tuhitimishe) ni watawala mashahidi, ambao walitawala kama warithi wa watawala wa kipagani au watu wa mataifa (cf. xx. 4–6); au labda Wakristo wote waaminifu, ambao majeshi ya mbinguni yalikuwa yakiwalilia: *twatatawala juu ya nchi* (v. 10)." (Kiddle 1940: 439)[76] Hapa tena ni lazima tuweke akilini kusudi kuu la uandishi wa Yohana: ubaya Yohana aliouorodhesha kwenye **Ufu 21:8, 27; 22:11, 15** na maelezo yake kuhusu kuingia mjini (**Ufu 21:24-26; 22:14**) au hawataweza kuuingia mji (**Ufu 21:27; 22:15**) zote zinawaonya waaminio kutokuikana au kuisaliti imani yao na vithaminisho vyake na kuwasihi kuishi maisha ya kujitoa ya uaminifu, kwa kuwa mwisho wenye utukufu upo wazi sana machoni pao.

Ufu 21:24-26 imechukulia kutoka **Isaya 60**. Isaya 60 inazungumzia juu ya Sayuni iliyotukuzwa. **Isa 60:3** inasema kwamba kwenye Sayuni iliyotukuzwa *"mataifa wataijia nuru yako."* **Ufu 21:24** sawa na hiyo inasema, *"Mataifa watatembea kwenye nuru yake [Yerusalemu Mpya]."* **Isa 60:11** inasema, *"Malango yako nayo yatakuwa wazi daima; hayatafungwa mchana wala usiku."* **Ufu 21:25** sawa na hiyo inasema, *"Wakati wa mchana (kuwa kuwa hapatakuwa na usiku kule) [Yerusalemu Mpya] malango yake hayatafungwa kamwe."* **Isa 60:20** (angalia pia **Isa 60:19**) inasema, *"Jua halitakuwa nuru yako tena wakati wa mchana, wala mwei hautakupa nuru, kwa mwangaza wake; bali BWANA atakuwa nuru ya milele kwako."* **Ufu 21:23** sawa na hilo inasema, *"Na mji ule hauhitaji jua wala mwezi kuuangaza, kwa maana utukufu wa Mungu huutia nuru, na taa yake ni Mwanakondoo."* **Isa 60:21** inasema, *"Watu wako naowatakuwa wenye haki wote, nao watairithi nchi milele."* **Ufu 21:27** sawa na hiyo inasema, *"Na ndani yake hakitaingia kamwe kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwanakondoo."*[77] **Isa 60:3-14** inasema kwamba wafalme wa mataifa watakuja kuleta utajiri wao ndani ya Sayuni. **Ufu 21:24-26** sawa na hiyo inasema, *"Wafalme wan chi wataleta utukufu wao ndani ya [Yerusalemu Mpya]"* na *"wataleta utukufu na heshima ya mataifa ndani yake."* Ulinganishi huu unaonyesha ni jinsi gani, kama alivyofanya kwenye kitabu chote, Yohana alichukua vifungu vya Agano la Kale na nabii zilizohusiana na Israeli, na alizifafanua na kuzitumia tena kwa umilele, Kanisa la kiulimwengu.[78]

Ufu 22:1-2 inasema kwamba *"mti wa uzima"* ambao upo kwenye mto ulioundwa na *"maji ya uzima"* ni kwa*"uponyaji wa mataifa."* Picha ya maji ya uzima kuyaponya mataifa haisemi kwamba, kwenye Yerusalemu Mpya, "kulisalia mataifa ambayo hayakuponywa yenye uhitaji wa kuponywa" (Johnson 2001: 321). Badala yake, ni "lahaja ya kinabii" ambayo inasimulia ni nini kilichoelezwa kwenye **Ufu 22:3**, kwamba "hapatakuwa na laana yeyote tena" (angalia pia **Rev 21:4**).

8. <u>Yerusalemu Mpya ni hitimisho la mpango wa milele wa Mungu kukaa mahali patakatifu pamoja na watu wake watakatifu.</u> Lengo la mungukwenye historia yote ya Kibiblia imekuwa ni kujaza kila sehemu

---

[75] Angalia pia **Ufu 21:7-8** ambao unaeleza kwamba *"ni washindi pekee watakaoyarithi mambo haya"* wakati wale ambao wanatenda dhambi na uovu *"watakuwa kwenye ziwa la moto."* **Ufu 21:27** inafanya jambo lile lile lakini inatumia picha tofauti: *"Na ndani yake hakitaingia kamwe cho chote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, [i.e., ndani ya mji]."*

[76] Maelezo yote (mataifa na wafalme) yanahusiana na vipengele vya watu wa Mungu na maisha pamoja naye kwenye hali ya umilele. Kwa njia iyo hiyo, kwenye **Ufunuo 12** mwanamke na watoto wake wote walikuwa ni njia ya kielelezo ya kuzungumzia taasisi ile ile, Kanisa. Tena, kwenye **Ufu 19:7-9** kanisa lilizungumziwa kama bibiarusi na karamu ya arusi na pia kama wageni kwenye karamu iyo hiyo.

[77] Kama Kiddle alivyoonyesha, "Malango wakati wote yapo wazi, lakini kwa watu wenye haki tu. Hayatafungwa kamwe, kwa sababu hakuna usiku wa kuogofya, na hakuna watenda maovu watakaoweza kukaribia mwangaza wa milele." (Kiddle 1940: 440)

[78] Msemo *tēn doxan kai tēn timēn* ("utukufu na heshima") wa **Ufu 21:26** umetokea penginepo kwenye Ufunuo tu kwenye **4:9, 11** na **5:12, 13**. Kwenye vifungu hivyo unazungumzia kumsifu Mungu na Mwanakondoo kunakofanywa na viumbe wenye uhai, wazee ishirini na wane, na Malaika mbinguni. Kwa hiyo, wakati mataifa wasiomcha Mungu mwanzoni watakapotoa kila kitu walichokuwa nacho kwa Babeli mkuu, sasa, kinyume chake, kumbukumbu ya "utukufu na heshima" kwenye **Ufu 21:26** itaonyesha kumsifu na kuabudu kwa moyo wote, na kujinyenyekesha kwa Mungu kwa mataifa yote, kwa milele yote, kote katika mbingu nan chi mpya yote.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

ya uumbaji wake na uwepo wake. Kuanzia kwenye Bustani ya Edeni, Mungu alitamani kuufanya ulimwengu wote mahali pake pa kukaa ambapo angeweza kushirikiana na watu wake watakatifu. Kwa sababu ya dhambi, utukufu wa Mungu usingeweza kabisa kukaa kwenye uumbaji wa zamani. Ingawa Mungu alitembea Bustanini pamoja na Adamu na Hawa (**Mwanzo 3:8**), kwa sababu ya dhambi zao aliwafukuza nje ya Bustani (**Mwanzo 3:23-24**). Kisha Mungu, hatua kwa hatua aliufunua uwepo wake maalum juu ya nchi miongoni mwa watu wake kwenye hema na kwenye hekalu la Sulemani, ambako alihudumu kama *"nakala ya kivuli cha mambo ya mbinguni"* (**Waeb 8:5;** angalia pia **Zab 78:69; Waeb 8:1-10:1**).

Kisha Mungu alizindua hatua ya mwisho ya uwepo wake kwa mwanadamu Yesu Kristo. Kupitia Roho Mtakatifu akaaye kanisani, uwepo wake sasa umeenea duniani kote. Wakati wa "vivuli" vya hekalu la kutengenezwa na wanadamu umekwisha, na ni wakati wa hekalu mpya la kweli—uwepo wake halisi ndani ya Kristo na kanisa—umekuja. Hata hivyo, ingawa uhakika wa kweli wa kiroho ambao hema na hekalu la Agano la Kale lililoonyesha linemzinduliwa, halijakamilishwa bado. Ukamilifu huo utatokea wakati Kristo atakaporudi duniani. Wakati atakapofanya hivyo, uumbaji wote utakuwa umekombolewa (**Rum 8:15-25**).

Wakati dhambi itakapokuwa imeondolewa kabisa kwenye uumbaji, ulimwengu wote (i.e., *"mbingu mpya nan chi mpya"*) utakuwa kama Bustani ya Edeni/mji/hekalu—chombo kikamilifu kwa uwepo wa utukufu wa Mungu. Uwepo wa Mungu hautakaa tena kwenye hekalu la kujengwa kwa mikono. Badala yake, Bwana Mungu Mwenyezi na Mwanakondoo utajaza, siyo sehemu tu ya uumbaji, lakini wote kama ulivyo (**Ufu 21:22**). Hi indo sababu kiini cha maono ni nchi—mbingu kuja *juu ya nchi*. Kwa maneno mengine, "'mbingu mpya' na 'nchi mpya' vitakuwa ukweli mmoja, ukihusishwa na kujazwa, mara na uwepo wa Mungu miongoni mwa watu wake" (Schnabel 2011: 280).

a. *Kuupima mji.* "Upimaji" wa mji (**Ufu 21:15-17)** umetofautiana na upimaji wa hekalu, madhabahu, na waabuduo, lakini umeuacha ua wa nje, kwenye **Ufu11:1-2**. Kama matokeo ya upimaji huo, Kiroho Kanisa lililindwa lakini kimwili liliwajibika kwa matesho na manyanyaso. "Hapa mji mzima ulepimwa kama ishara nyingine ya usalama wake kamili kutoka kwa kila adui ambaye mwanzoni alitishia utakatifu na furaha yake" (Johnson 2001: 312).[79]

b. *Yerusalemu Mpya kama Patakatifu pa Patakatifu.* Ukamilifu wa utakatifu wa Yerusalemu Mpya unaonekana kwa ukweli kwamba Yerusalemu Mpya ni Patakatifu pa Patakatifu:

- Kama vile Patakatifu pa Patakatifu (**1 Fal 6:16-20; 2 Nyak 3:8**), mji ni mchemraba kamili (**Ufu 21:16**).
- Kama vile Patakatifu pa Patakatifu palivyokuwa pamefunikwa kwa dhahabu safi (**1 Fal 6:16-20; 2 Nyak 3:8**), *"dhahabu safi, mfano wa kioo safi"* (**Ufu 21:18**).
- Kama vile Patakatifu pa Patakatifu palivyokuwa mahali maalumu kwa uwepo na utukufu wa Mungu, mji sasa ni mahali pa uwepo na utukufu wa Mungu (**Ufu 21:22-23; 22:1, 3-5**).
- Ni Patakatifu pa Patakatifu pekee, hakuna mahali pengine pa hekalu la Israeli (i.e., mahali patakatifu na ua wa nje), panapopatikana kwenye **Ufunuo 21.** Uwepo maalum wa Mungu, ambao awali ulikuwa na unaishia au kukomea Patakatifu pa Patakatifu, sasa unawazunguka uumbaji wake mpya wote.

Kwa upande mwingine, utimilifu wa Yerusalemu Mpya unapazidi Patakatifu pa Patakatifu kwa heshima ya sisi kumfikia Mungu.

- Ni Kuhani Mkuu pekee ambaye aliingia Patakatifu pa Patakatifu, na alikuwa akitoa sadaka kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe na kwa ajili ya dhambi za taifa (**Lawi 16:1-28**). Kwenye Yerusalemu Mpya, watu wote wa Mungu hawana dhambi na watamtumikia Bwana na kutawala milele na milele (**Ufu 21:7-8, 27; 22:3-5**).
- Kuhani Mkuu angepaingia Patakatifu pa Patakatifu mara moja tu kwa mwaka, kwa siku ya upatanisho (**Lawi 16:29-31**). Kwenye Yerusalemu Mpya, hatutamfikia Mungu moja kwa

[79] Vipimo havipaswi kuchukuliwa "kiuhalisia" kama kwamba vilikuwa vipimo vya mji wa kimwili lakini kwa wazi vilikuwa ni ishara, msingi wake ukiwa kwenye wingi wa namba 12 (angalia Johnson 2001: 312-13). Kama Gundry alivyoeleza kwa heshima ya watue "kuingia ndani" ya mji, hii ni "lugha ya nafasi, lakini maana yake siyo ya nafasi." Vivyo hivyo, "ni uongo kuhitimisha kwamba mji ulichukua eneo la mita za eneo 144,000,000 za nchi lakini siyo nchi yote au kwamba Waisraeli 144,000 hawawezi kujumuisha mkutano usiweza kuhesabika." (Gundry 1987: 264) Kimsingi kusudi la Yohana siyo kuelezea "eneo." Badala yake, "Anaelezea usalama wa watu milele" (Ibid.: 260).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

moja tu, bali wakati wote tutakuwa kwenye uwepo wake (**Ufu 21:3-4, 22-23; 22:3-5**).

- Kwenye siku ya upatanisho Kuhani Mkuu alipaswa kutoa sadaka ya uvumba ambayo ilifanya wingu jembamba ambalo lilifunika Kiti cha Rehema ili kwamba asiweze kuuona utukufu wa Mwonekano wa Mungu, au vinginevyo angekufa (**Lawi 16:13**; angalia **Kut 33:20**). Kwenye Yerusalemu Mpya, watu wote wa Mungu watauona "uso wake" (**Ufu 22:4**).

M. ***22:6-21: Hitimisho***[80]

Hitimisho la kitabu linaendana na kitabu chote na unabii kwa ujumla. Manabii walinena maneno ya hukumu na maneno ya wokovu kuwaonya watu na kuwasihi kubadili njia zao na kugeuka au kuwa waaminifu kwa Bwana. Kwa upekee kitabu cha Ufunuo kiliandikwa kutoa taarifa, kusihi, kufariji, na kulitia Kanisa moyo. Kwa hiyo Beale anachunguza: "Aya hizi za mwisho hasa zimefungwa kwenye utangulizi 1:1-3: zote zinakitambulisha au kukitambua kitabu kama utimilifu utokao kwa Mungu (kikitumia maneno yale yale kutoka kwa Dan. 2:28-29, 45); yote yanamlenga Yohana kama 'shahidi' kwa ufunuo ambao alipewa; na vyote vinauzungumzia ufunuo kama 'unabii' uliowasiliana na 'wasikilizaji' . . . Hitimisho linaonyesha kwamba kusudi la kitabu chote ni kushawishi utii mtakatifu miongoni mwa watu wa Mungu ili kwamba waweze kupokea thawabu ya wokovu. . . . Kurudia kuwasihi kuwa watakatifu ni jambo kuu kwenye hitimisho, kwa kuwa walisaidiwa na mshangao au kelele za kuhusiana na kuja kwa Yesu. Siyo chini ya nane kati ya aya kumi na tano za mwisho zinazosisitiza kusudi la kitabu kutia moyo utii ama kupitia kuwasihi watii, kupitia Baraka zilizoahidiwa kwa maisha matakatifu, na kupitia maonyo ya hukumu kwa maisha yasiyo matakatifu." (Beale 1999: 150)

VIII. <u>Ufunuo umefungwa pamoja na kukamilisha Biblia yote</u>

A. ***Uumbaji mpya wa Ufunuo umeungana na uumbaji asili wa Mwanzo***

Sura za mwisho mbili za Ufunuo zimeunganishwa kwa wazi, mara nyingi kwa tofauti, na sura tatu za kwanza za Mwanzo kama ifuatavyo:

Mwanzo	***Ufunuo***
"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi" (**Mwanzo 1:1**)	*"Nikaona mbingu mpya nan chi mpya"* (**Ufu 21:1**)
"Giza aliliita usiku" (**Mwanzo 1:5**)	*"Kwa maana humo hamna usiku"* (**Ufu 21:25; 22:5**)
"Makusanyiko ya maji akayaita bahari" (**Mwanzo 1:10**)	*"Wala hapana bahari tena"* (**Ufu 21:1**)
"Na iwe mianga katika anga la mbingu. . . itie nuru juu ya nchi" (**Mwanzo 1:14-15**)	*"Mji ule hauhitaji jua wa mwezi kuuangaza"* (**Ufu 21:23; 22:5**)
"Kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika" (**Mwanzo 2:17**)	*"Wala mauti haitakuwapo tena"* (**Ufu 21:4**)
"Adamu na Mkewe wakajificha wenyewe kutoka kwenye uwepo wa Bwana Mungu" (**Mwanzo 3:8**)	*"Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao . . . nao watamwona uso wake"* (**Ufu 21:3; 22:4**)
"Hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako" (**Mwanzo 3:16**)	*"Wala hapatakuwapo tena . . . maumivu"* (**Ufu 21:4**)
"Ardhi imelaaniwa kwa ajili yako" (**Mwanzo 3:17**)	*"Wala hapatakuwapo na laana tena"* (**Ufu 22:3**)

"Kwenye Mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi; kwenye Ufunuo tunasoma juu ya mbingu mpya na nchi mpya (21:1). Kwenye Mwanzo mianga iliitwa kuwapo; kwenye Ufunuo utukufu wa Bwana unaangaza mji [**21:23; 22:5**]. Kwenye Mwanzo tunasoma nguvu ya ushawishi wa Shetani; kwenye Ufunuo Ibilisi amefungwa nakutupwa kwenye ziwa la moto (20:10). Kwenye Mwanzo tunasoma paradiso iliyopotea; kwenye Ufunuo paradiso inarejeshwa. Mwanzo unaelezea kutengwa kwa mwanadamukam Adamu na Hawa walivyomkimbia Mungu; kwenye Ufunuo waliokombolewa wanafurahia ushirika wa karibu wa ndoa ya Mwanakondoo [**19:7-9; 21:2-4; 22:4**]. Kwenye Mwanzo asili zinatishia usalama na kuwaumiza wanadamu; kwenye Ufunuo asili zinaendelezwa na kuwafariji watu [**22:1-2**]. Kwenye Mwanzo mti wa uzima unalindwa na malaika asje hata

[80] Ingawa wachambuzi wengi wanadhani kwamba kwenye **Ufu 22:6** malaika ambaye aliyemwonyesha Yohana Yerusalemu mpya anazungumza, kwenye **22:7** mzungumzaji kwa wazi ni Kristo mwenyewe. Hili linaongeza uwezekano kwamba alikuwa ni Kristo ambaye alikuwa akizungumza kwenye **22:6** na kote kwenye maeneo mengi ya **sura ya 22** (angalia Schüssler Fiorenza 1991: 114).

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mmoja akala matunda yake; Ufunuo unarejesha mwanadamu kuyafikia matunda (22:14). Mahusiano haya ya wazi baina ya kitabu cha kwanza na cha mwisho cha Biblia kinasimulia utimilifu wa unabii wa kwanaza wa Kimasihi (Mwanzo. 3:15) na uaminifu wa Mungu kwenye agano (Ufu. 21:3).” (Hamstra 1998: 123)

B. ***Uumbaji mpya wa Ufunuo ni zaidi ya uumbaji wa asili wa Mwanzo***

Douglas Moo anahitimisha uchunguzi wetu juu ya Ufunuo kwa kuzungumzia uwezo wa uumbaji kabla ya utimilifu, jinsi uwezo huo unavyohusika kwenye historia, na jinsi gani Mungu alivyouleta ulimwengu kwenye utukufu mkubwa kuliko ule wa uumbaji wa asili: “Ukweli kwamba hapatakuwa na bahari au usiku kwenye mbingu mpya na nchi mpya [**21:1, 25**] kunapendekeza njozi kwenye uumbaji wa kwanza kwa kuwa kwenye mifano yote miwili vipengele hivi vipo kwenye baadhi ya njia kushinda, kugawanyika, au kuzuiliwa. . . . Ni kama uumbaji wa kwanza, wakati ukiwa mzuri wenyewe, ulikuwa na uwezo wa kuendelea kwenye mwelekeo wa aina miwili: kama mwanadamu angetimiza jukumu lake na kuishi katika mahusiano mema na Mungu na uumbaji wote, nguvu iliyositirika ya machafuko iliyowakilishwa hasa na bahari na giza milele ingekuwa kwenye upeo wa utawala wa mwanadamu na bila shaka ingekuwa vyanzo vya nguvu ya ubunifu na furaha—kama vile vilivyokuwa kwa Mungu, Kwake pia hata lewiathani angekuwa kitu cha kuchezea [angalia **Ayubu 41:17; Zab 74:14; 104:24-26**]. Lakini ikiwa agano la Mungu na viumbe wake lilivunjika na wanadamu kushiriki wenyewe na nyoka na ufalme wake, nguvu ya machafuko ingeachwa ishindwe na bahari ingekuwa kitu cha kutisha, kukaa na uovu na chombo cha hukumu. Maandiko kwa sehemu kubwa yangeweka kumbukumbu ya mwanadamu kuchagua njia hii mwishoni, lakini kusudi la Yohana ni kuyahakikishia Makanisa kwamba hayajaachwa kwenye ulimwengu wa huzuni, maumivu na maombolezo. Badala yake, Ushindi wa ‘Mwanakondoo aliyechinjwa’ ulimaanisha kwamba uaminifu wa Muumba kwa uumbaji wake—uligusia kwenye upinde wa mvua kuzunguka kiti chake cha enzi [**4:3**], ishara ya agano la Nuhu—hatimaye unaelezwa kupitia siyo kingine chochote kilicho kidogo zaidi ya kurejeshwa kwa ulimwengu, tukio ambalo ulimwengu utaletwa zaidi ya tishio lolote la uasi wa wakati ujao au dhambi.” (Moo 2009: 166-67)

IX. <u>Maana ya Kitabu cha Ufunuo</u>

Makusudi ya kitabu cha Ufunuo, m.y., kuelezea kwa kanisa jinsi ambavyo Mungu anashughulika na dunia, kuwaita waamini kuvumilia katika kupambana na nguvu za uovu, na kuwafariji na kuwatia moyo Wakristo kwa kuwa Kristo ni mshindi, yanatenda kazi leo kama yalivyofanya katika karne ile ya kwanza. Mfano wa hili ulionyeshwa katika maisha ya Mkristo aliyeuawa kwa ajili ya imani yake Dietrich Bonhoeffer. Wakati akiwa amefungwa na Wanazi katika Vita ya Pili ya Dunia, Bonhoeffer aliandika kwamba aligundua kwamba vitabu vya Zaburi na Ufunuo vilikuwa “vya msaada sana kuliko alivyotarajia” (Bonhoeffer 1997: 128). Kinyume chake, aligundua kwamba wafungwa wenzake ambao hawakuwa na misingi ya mtazamo wa Kikristo waliyagawa maisha yao na kupotoka katika ushirikina au falsafa ya majaliwa katika jitihada zao za kushughulika na shida za maisha ya gerezani na hofu ambazo zilitokana na mashambulio ya angani (Ibid.: 231, 310-11).

Kwa kuongezea, kitabu cha Ufunuo “hutupa njia tofauti za kuutazama ulimwengu ambao huwaongoza watu kuzuia na kuzichangamoto athari za mawazo yanayoongoza” (Bauckham 1993b: 159). Maono haya mbadala ya ulimwengu ni yenye nguvu inayokaribiana na ya kitheolojia—hakika, kiini chake ni Kristo. “Mwishoni ni maono yaliyotakasika ya ukamilifu wa Mungu ambayo yanaweza kwa ufanisi kuizuia tabia ya mwanadamu ya uasherati ambayo inahusisha kuvipendelea vipengele vya ulimwengu huu. Kumwabudu Mungu wa kweli ni nguvu ya kuzuia kuabudu nguvu ya jeshi nay a kisiasa (mnyamat)na mafanikio ya kiuchumi (Babeli).” (Ibid.: 160) Kama tulivyoona kuhusiana na mjadala unaohusu Babeli mkuu, Yohana anawakabili wasomaji wake ili wahakiki jamii zao wenyewe. Kama Richard Bauckham anavyoiweka, “Kila jamii ambayo kofia ya Babeli inawakaa ni lazima waivae. Kila jamii itakayopendelea mafanikio ya uchumi wake wenyewe kwa gharama za wengine itajiweka chini ya hukumu ya Babeli.” (Bauckham 1993b: 156; angalia pia Schnabel 2011: 211-12)

Mtazamo kama huu hutupatia msingi wa kukabiliana na ukandamizaji, udhalimu, na ubinadamu. Kama Theodore Stylianopoulos anavyosema, “Ufunuo ni zaidi ya mwito wote wa haki, kuulilia ufalme, maombi ya kufunuliwa kwa utawala wa Mungu juu ya nchi kama ulivyo mbinguni” (Stylianopoulos 2009: 28). Akitolea maoni yake juu ya **Ufu 18:24**, Bauckham anakumbusha “hisia za mshikamano zinazungumza baina ya mashahidi wa Kikristo na wahanga wengine wote wasio na hatia wa Rumi. Ikiwa Yohana aliyasihi Makanisa yake kujitenga yenyewe kutoka kwenye nguvu ya muundo wa kisisa na kiuchumi ya Rumi, hili siyo kuwageuza wao kwenye kuangalia mambo ya ndani ya kundi la kidini, kuhusiana tu na hatima yao wenyewe. Kwa sababu badala yake, kwenye unabii wao wa ushuhuda kwa ulimwengu, wafusi hawa wa Mwanakondoo, yeye

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mwenyewe ni mhanga wa Rumi, hawezi kujihusisha na wauaji lakini ni lazima ashuhudie kinyume na wauaji." (Bauckham 1989: 101)

Mwitikio wakati wote hutokea kwa waliokandamizwa na waliopotea. Mara nyingi hutambua kile ambacho matajiri na wenye nguvu hawakitambui: kwamba utamaduni unaoongoza kwenye nchi yoyote huwa na mbegu zake ndani yake, na hubeba alama, ya Babeli Mkuu. Elisabeth Schüssler Fiorenza anaona, "Wakristo waliokandamizwa na waliopotea husoma mazingira ya Ufunuo kama kundi la kisiasa la kidini ambalo huzungumzia hali zao wenyewe. Theolojia ya uhuru wa Amerika ya Kusini au Afrika ya Kusini huthamini ulimwengu wa kisiasa wa maono ya Ufunuo kwa mashtaka yake rasmi yaliyoandikwa kiufunuo ya unyanyasaji na ukandamizaji sambamba na mwendelezo wa maono yake ya haki." (Ibid.: 7) Mfano wa hili ni uasi ulioongozwa na John Chilembwe Januari mwaka 1915 kwenye nchi ya Nyasaland (Malawi ya sasa) kinyume na mamlaka ya kikoloni ya Uingereza kupinga udhalimu na unyanyasaji wa mfumo wa kikoloni. Chilembwe mwenyewe alikuwa kasisi au mhudumu wa Kanisa la Baptist. Philip Jenkins anaandika, "Kwa kiwango kikubwa aliandika mengi kwenye mawazo ya mafunuo wa Kibaptist" (Jenkins 2015: 45).[81] Schüssler Fiorenza anatupa mifano mingine mitatu yenye kutambulika ya mtazamo kama huo na ushuhuda uliochukuliwa kutoka nyakati za mwisho za Ufunuo: "Kwenye barua yake kutoka gereza la Birmingham, Martin Luther King, Jr., alinukuu lugha ya picha za Ufunuo wakati anatafsiri uzoefu na matumaini kwenye kupigania haki za kijamii za Waafrika Wamarekani; Ufafanuzi wa Allan Boesak wa mazingira ya kulaumu na kufariji ya Ufunuo kwenye kupigana kinyume na ubaguzi wa rangi wa Afrika ya Kusini; na Danieli Berrigan aliandika mtazamo wake juu ya Ufunuo, Jinamizi la Mungu, wakati akiwa kifungoni au gerezani kwa shughuli zake kwenye kusaidia waandamanaji waliopingana na matumizi ya Nyuklia vitani." (Schüssler Fiorenza 1991: 11)

Vile vile, Ufunuo hutupa msingi wa sisi kuhakiki kanisa lenyewe ambalo, mara nyingi kwa kupitiliza katika historia, limeonyesha kwamba "limeuacha upendo wake wa kwanza" na limejiweka katika muafaka wa kukubaliana na dola, utamaduni unaokubalika, na dunia.[82] Katika hali hizi, kitabu cha Ufunuo kinakabiliana nasi kikiwa na maswala ya msingi tuliyoyaona yakijirudia katika kitabu chote: Uaminifu wangu wa msingi unasimamia wapi na ni nani aliye Bwana wangu hasa? Miitikio yetu kwenye tamaduni zetu na kwa mitazamo ya dunia na ushawishi huonyesha majibu yetu kwa maswali haya.

Mwisho, tumeona maswali makuu yakiulizwa na Ufunuo tena na tena: Uaminifu wangu wa msingi uko kwa nani? Ni nani au ni nini ambacho ni Bwana wangu atendaye ambaye hufinyanga na kuhamasisha mienendo yangu na tabia? Watu wanaweza kuyajibu maswali hayo kwa ajili ya wao wenyewe, lakini wanahitajika kujua kwamba mazingira yao ya kiuchumi na kijamii huwakabili na maswali kama hayo hatahivyo. Hii haimaanishi kwamba wale tu wanaoipinga dola, waliofanikiwa, matajiri, na wenye nguvu, kwamba ndio wao walio sahihi. Kiwango kikubwa mno cha uovu usioneneka umefanyika katika jina la kuwapinga waliofanikiwa, matajiri, wenye nguvu na waliobahatika—shuhudia, kwa mfano, Mapinduzi ya Ufaransa, mauaji ya Rwanda, na kila mapinduzi ya kikomunisti. Maswala ni ushawishi wa mtu mwenyewe na ni nani ndiye Bwana wake hasa: Yesu, au mtu au kitu kingine. Hayo ndiyo maswala ambayo kitabu cha Ufunuo kinayaibua. Yanaenda hadi kwenye kiini cha maisha yetu, ya sisi ni nani. Ikiwa tunaelewa Kristo ni nani na tunaelewa kupitia kitabu hiki jinsi Mungu kwa njia ya Kristo anashughulika na dunia, tutaweza kuvumilia kwa urahisi zaidi katika mapambano na nguvu za uovu na kupata faraja na kutiwa moyo kwa sababu Kristo ni mshindi. Ndio maana kitabu cha Ufunuo ni muhimu sana

BIBLIOGRAPHIA

Alexander, T. Desmond. 2008. *From Eden to the New Jerusalem.* Nottingham, England: Inter-Varsity.

Allison, Dale. 1985. *The End of the Ages Has Come: An Early Interpretation of the Passion and Resurrection of Jesus.* Philadelphia: Fortress.

[81] Uasi ulizimwa lakini "uliachilia nyuma urithi wa utaifa na hisia za kiafrika. Chilembwe leo ni shujaa mkubwa wa taifa la Malawi. Uso wake unaonekana kwenye fedha za Malawi, na kila Januari 15 taifa husherehekea siku ya John Chilembwe." (Jenkins 2015: 45)

[82] Schüssler Fiorenza observes, "Whereas mainline Christianity has often co-opted or neutralized Revelation's political-religious language and vision by identifying God's empire with the institutional church or with the interior salvation of the soul, messianic-prophetic Christian movements have again and again affirmed Revelation's visions of salvation as a vision of total well-being and freedom from oppression. They have read it as promising liberation from oppressive ecclesiastical structures and from the destructive domination of those who have power in the world." (Schüssler Fiorenza 1991: 128)

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Augustine. 1950 (reprint). *The City of God.* Translated by Marcus Dods. New York: Random House. Online: http://www.ccel.org/ccel/schaff/npnf102.toc.html.

Aune, David. 1983. *Prophecy in Early Christianity and the Ancient Mediterranean World.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

_____. 1997. *Revelation 1-5* (WBC 52A). Dallas: Word.

Azurdia, Arturo. Not dated. *Sermon Series on the Book of Revelation.* Audio mp3. Online: http://www.monergism.com/thethreshold/articles/onsite/azurdia_revelation.html.

Bauckham, Richard. 1989. *The Bible in Politics: How to Read the Bible Politically.* London: SPCK.

_____. 1991. "The Economic Critique of Rome in Revelation 18." In *Images of Empire* (JSOTSup 122), edited by Loveday Alexander, 47-90. Sheffield, England: Sheffield Academic Press.

_____. 1993a. *The Climax of Prophecy: Studies on the Book of Revelation.* Edinburgh: T&T Clark.

_____. 1993b. *The Theology of the Book of Revelation.* Cambridge, England: Cambridge University Press.

Bahnsen, Greg. 2015. *Victory in Jesus,* 2nd ed. Nacogdoches, TX: Covenant Media Press.

Bandstra, Andrew. 1992. "'Kingship and Priests': Inaugurated Eschatology in the Apocalypse," *Calvin Theological Journal* 27: 10-25.

Beale, G. K. 1999. *The Book of Revelation* (NIGTC). Grand Rapids, MI: Eerdmans.

_____. 2006. "The Purpose of Symbolism in the Book of Revelation." *Calvin Theological Journal* 41: 53-66. Online: http://www.calvin.edu/library/database/crcpi/fulltext/ctj/CTJ06Ap/124804.pdf.

_____. 2008. *Sermon Series on the Book of Revelation.* Audio mp3. Online: http://resources.thegospelcoalition.org/library?f%5Bbook%5D%5B%5D=Revelation&f%5Bcontributors%5D%5B%5D=Beale%2C+G.K.&page=2&sort=contributors.

Beale, G. K., and Sean McDonough. 2007. "Revelation." In *Commentary on the New Testament Use of the Old Testament,* edited by G. K. Beale and D. A. Carson, 1081-1161. Grand Rapids, MI: Baker Academic.

Beasley-Murray, G. R. 1974. *The Book of Revelation* (NCBC). Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Bell, William Everett, Jr. 1967. "A Critical Evaluation of the Pretribulation Rapture Doctrine in Christian Eschatology." Ph.D. diss., New York University.

Bonhoeffer, Dietrich. 1997. *Letters and Papers from Prison,* enlarged ed. New York: Touchstone.

Boxall, Ian. 2009. *The Revelation of St. John* (BNTC). Grand Rapids: Baker Academic.

Bruce, F. F. 1938. "The Earliest Latin Commentary on the Apocalypse." *Evangelical Quarterly* 10: 352-66. Online: https://biblicalstudies.org.uk/pdf/eq/1938-4_352.pdf.

Caird, G. B. 1966. *A Commentary on the Revelation of St. John the Divine* (HNTC). New York: Harper & Row.

Carson, D. A. 1994-2010. *Sermons and Lectures on the Book of Revelation.* Audio mp3. Online: http://resources.thegospelcoalition.org/library?f%5Bbook%5D%5B%5D=Revelation&f%5Bcontributors%5D%5B%5D=Carson%2C+D.+A.&sort=contributors.

_____. 2009. *Preaching Apocalyptic.* Audio mp3. Online: http://resources.thegospelcoalition.org/library?utf8=%E2%9C%93&query=carson+preaching+apocalyptic.

_____. 2011. "This Present Evil Age." In *These Last Days: A Christian View of History,* edited by Richard Phillips and

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Gabriel Fluhrer, 17-37. Phillipsburg, NJ: P&R. Online: https://thelogcollege.files.wordpress.com/2013/09/2011_present_evil_age.pdf.

Chilton, David. 1985. *Paradise Restored.* Tyler, TX: Dominion. Online: http://www.garynorth.com/freebooks/docs/pdf/paradise_restored.pdf.

_____. 1987. *Days of Vengeance: An Exposition of the Book of Revelation.* Ft. Worth, TX: Dominion. Online: http://www.garynorth.com/freebooks/docs/pdf/days_of_vengeance.pdf.

Danker, Frederick, ed. 2000. *A Greek-English Lexicon of the New Testament and Other Early Christian Literature*. Chicago: The University of Chicago Press.

DeMar, Gary. 1999. *Last Days Madness,* 4th ed. Powder Springs, GA: American Vision. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0915815354.

Deutsch, Celia. 1987. "Transformation of Symbols: The New Jerusalem in Rv 21:1-22:5." *Zeitschrift fur Die Neutestamentliche Wissenschaft* 78: 106-26.

Elwell, Walter. 1989. "Revelation." In *Evangelical Commentary on the Bible,* edited by Walter Elwell, 1195-1229. Grand Rapids, MI: Baker.

Fesko, John. 2010. *Lecture Series on the Book of Revelation.* Audio mp3. Online: http://www.genevaopc.org/audio/fesko-lectures/72-revelation-lecture-series.html.

Ford, Desmond. 1979. *The Abomination of Desolation in Biblical Eschatology.* Washington, DC: University Press of America.

Gentry, Kenneth. 1989. *Before Jerusalem Fell: Dating the Book of Revelation.* Powder Springs, GA: American Vision. Online: http://www.garynorth.com/freebooks/docs/pdf/before_jerusalem_fell.pdf.

_____. 1990. *The Greatness of the Great Commission.* Tyler, TX: Institute for Christian Economics. Online: http://www.garynorth.com/freebooks/docs/pdf/the_great_commission.pdf.

_____. 1998. "A Preterist View of Revelation." In *Four Views on the Book of Revelation,* 37-92. Grand Rapids, MI: Zodervan. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0310872391.

Goldsworthy, Graeme. 1991. *According to Plan: The Unfolding Revelation of God in the Bible.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Green, Joel. 1984. *How to Read Prophecy.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Gourgues, Michel. 1985. "The Thousand-Year Reign (Rev 20:1-6): Terrestrial or Celestial? *Catholic Biblical Quarterly* 47: 676-81.

Grenz, Stanley. 1992. *The Millennial Maze.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Gundry, Robert. 1987. "The New Jerusalem: People as Place, Not Place for People." *Novum Testamentum* 29: 254-64.

Hamstra, Sam. 1998. "An Idealist View of Revelation." In *Four Views on the Book of Revelation,* 95-131. Grand Rapids, MI: Zodervan. Online: https://books.google.com/books?isbn=0310872391.

Harvey, Paul. 1998. "'Yankee Faith' and Southern Redemption: White Southern Baptist Ministers, 1850-1890." In *Religion and the American Civil War*, edited by Randall Miller et al., 167-86. New York: Oxford University Press.

Heil, John. 1993. "The Fifth Seal (Rev 6.9-11) as a Key to the Book of Revelation." *Biblica* 74: 220-43.

Hendriksen, William. 1982 (reprint). *More Than Conquerors.* Grand Rapids, MI: Baker.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Hoekema, Anthony. 1977. “Amillennialism.” In *The Meaning of the Millennium: Four Views,* edited by Robert Clouse, 155-87. Downers Grove, IL: InterVarsity.

_____. 1979. *The Bible and the Future.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Hooker, Morna. 1967. *The Son of Man in Mark.* Montreal: McGill University Press.

Hughes, Philip Edgcumbe. 1977. “The First Resurrection: Another Interpretation.” *Westminster Theological Journal* 39: 315-18.

Irenaeus. 1885. *Against Heresies*. In *The Ante-Nicene Fathers*, vol. 1, edited by Alexander Roberts and James Donaldson, revised by A. Cleveland Coxe, 315-567. New York: Christian Literature Publishing Company. Reprint, Peabody, MA: Hendrickson, 1994. Online (another edition): http://www.ccel.org/ccel/schaff/anf01.ix.i.html.

Ironside, Harry. 1943. *The Great Parenthesis*. Grand Rapids: Zondervan. Online: http://bartimaeus.us/pub_dom/the_great_parenthesis.html.

Jackson, Wayne. 2001. “Examining Premillennialism.” No pages. Online: http://www.christiancourier.com/articles/322-examining-premillennialism.

Jenkins, Philip. 2015. “Chilembwe’s rising.” *Christian Century* (February 18): 45.

Johnson, Alan. 1981. “Revelation.” In *The Expositor’s Bible Commentary,* vol. 12, edited by Frank Gaebelein, 399-603. Grand Rapids, MI: Zondervan.

Johnson, Dennis. 2001. *Triumph of the Lamb: A Commentary on Revelation*. Phillipsburg, NJ: P&R.

Kiddle, Martin. 1940. *The Revelation of St. John* (MNTC). London: Harper and Bros.

Kik, J. Marcellus. 1971. *An Eschatology of Victory.* Phillipsburg, NJ: Presbyterian and Reformed.

Kistemaker, Simon. 2000. “The Temple in the Apocalypse.” *Journal of the Evangelical Theological Society* 43: 433-41. Online: http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/43/43-3/43-3-pp433-441_JETS.pdf.

Kline, Meredith. 1975. “The First Resurrection.” *Westminster Theological Journal* 37: 366-75. Online: http://www.meredithkline.com/klines-works/articles-and-essays/the-first-resurrection/.

_____. 1989. “Double Trouble.” *Journal of the Evangelical Theological Society* 32: 171-79. Online: http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/32/32-2/32-2-pp171-179_JETS.pdf.

_____. 1996. “Har Magedon: The End of the Millenium.” *Journal of the Evangelical Theological Society* 39: 207-22. Online: http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/39/39-2/39-2-pp207-222_JETS.pdf.

Korner, Ralph. 2000. “‘And I Saw . . .’ An Apocalyptic Literary Convention for Structural Identification in the Apocalypse.” *Novum Testamentum* 42: 160-83.

Ladd, George Eldon. 1956. *The Blessed Hope.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

_____. 1972. *A Commentary on the Revelation of John.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Levenson, Jon. 1988. *Creation and the Persistence of Evil.* San Francisco: Harper & Row.

Lewis, Arthur. 1980. *The Dark Side of the Millennium: The Problem of Evil in Rev. 20:1-10.* Grand Rapids, MI: Baker.

Lindsey, Hal. 1970. *The Late Great Planet Earth.* Grand Rapids, MI: Zondervan.

Longman III, Tremper, and Daniel Reid. 1995. *God is a Warrior.* Grand Rapids, MI: Zondervan.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

MacDonald, William. 1995. *Believer's Bible Commentary*, edited by Art Farstad. Nashville, TN: Thomas Nelson.

Mathison, Keith. 1999. *Postmillennialism: An Eschatology of Hope*. Phillipsburg, NJ: P&R.

McDurmon, Joel. 2011. *Jesus v. Jerusalem.* Powder Springs, GA: American Vision.

Mealy, J. Webb. 1992. *After the Thousand Years: Resurrection and Judgment in Revelation 20.* Sheffield, England: Sheffield Academic Press.

Menn, Jonathan. 2016. *Biblical Theology*. Online: http://www.eclea.net/courses.html#theology.

_____. 2017. *Biblical Eschatology.* Online: http://www.eclea.net/courses.html#eschatology.

_____. Not dated. *Sermon Series: Revelation*. Online: http://www.eclea.net/sermons.html#revelation.

Milligan, William. 1893. *Discussions on the Apocalypse.* London: Macmillan. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=155635763X.

_____. 1896. *The Book of Revelation.* New York: Armstrong. Online: https://books.google.com/books?id=98DYAAAAMAAJ.

Minear, Paul. 1968. *I Saw a New Earth.* Washington, DC: Corpus.

Moo, Jonathan. 2009. "The Sea that is No More: Rev 21:1 and the Function of Sea Imagery in the Apocalypse of John." *Novum Testamentum* 51: 148-67.

Mounce, Robert. 1998. *The Book of Revelation* (NICNT), rev. ed. Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Ngundu, Onesimus. 2006. "Revelation." In *Africa Bible Commentary,* edited by Tokunboh Adeyemo, 1543-79. Nairobi: WordAlive.

Nixon, R. E. "Matthew." 1970. In *The New Bible Commentary*, 3rd ed., edited by D. Guthrie et al., 813-50. Carmel, NY: Guideposts.

Noe, John. 2006. "An Exegetical Basis for a Preterist-Idealist Undersanding of the Book of Revelation." *Journal of the Evangelical Theological Society* 49: 767-96. Online: http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/49/49-4/JETS_49-4_767-796_Noe.pdf.

Ortlund, Raymond. 1996. *God's Unfaithful Wife: A Biblical Theology of Spiritual Adultery* (NSBT 2). Downers Grove, IL: InterVarsity.

Osborne, Grant. 2002. *Revelation* (BECNT). Grand Rapids, MI: Baker Academic.

Page, Sydney. 1980. "Revelation 20 and Pauline Eschatology." *Journal of the Evangelical Theological Society* 23: 31-43. Online: http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/23/23-1/23-1-pp031-043_JETS.pdf.

Pate, C. Marvin. 1998. "A Progressive Dispensationalist View of Revelation." In *Four Views on the Book of Revelation,* 135-75. Grand Rapids, MI: Zodervan. Online: https://books.google.com/books?isbn=0310872391.

Pate, C. Marvin, and Calvin Haines. 1995. *Doomsday Delusions: What's Wrong with Predictions About the End of the World.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Pate, C. Marvin, Kenneth Gentry, Sam Hamstra, and Robert Thomas. 1998. *Four Views on the Book of Revelation.* Grand Rapids, MI: Zodervan. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0310872391.

Payne, J. Barton. 1980 (reprint). *Encyclopedia of Biblical Prophecy.* Grand Rapids, MI: Baker.

Pentecost, J. Dwight. 1958. *Things to Come: A Study in Biblical Eschatology.* Grand Rapids, MI: Zondervan.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Porter, Stanley. 1999. *Idioms of the Greek New Testament,* 2nd ed. Sheffield, England: Sheffield Academic Press.

Preston, Don. 2010. *Like Father, Like Son, On Clouds of Glory,* 2nd ed. Ardmore, OK: JaDon Management, Inc.

_____. 2013. *AD 70: A Shadow of the "Real" End?* Ardmore, OK: JaDon Management, Inc.

Ramsay, William. 1875. "Triumphus." In *A Dictionary of Greek and Roman Antiquities,* edited by William Smith, 1163-67. London: John Murray. Online: http://penelope.uchicago.edu/Thayer/E/Roman/Texts/secondary/SMIGRA*/Triumphus.html.

Reader, W. 1982. "The Riddle of the Identification of the Polis in Rev. 11:1–13." In *Studia Evangelica*, vol. VII, edited by Elizabeth Livingstone, 407-14. Berlin: Akademie-Verlag.

Resseguie, James. 2009. *The Revelation of John: A Narrative Commentary.* Grand Rapids, MI: Baker Academic.

Riddlebarger, Kim. 2001-2002. *Sermon Series on the Book of Revelation.* Online: http://www.christreformed.org/kim-riddlebarger/#Revelation (audio mp3); http://kimriddlebarger.squarespace.com/downloadable-sermons-on-the-bo/ (written transcripts).

Rist, Martin, and Lynn Harold Hough. 1957. "The Revelation of St. John the Divine." In *The Interpreter's Bible,* vol. 12, edited by George Buttrick, 345-613. New York: Abingdon.

"Rome." 2012. Wikipedia. No pages. Online: http://en.wikipedia.org/wiki/Rome.

Rushdoony, R. J. 1970. *Thy Kingdom Come.* Vallecito, CA: Ross House.

Schaff, Philip. 1990. *The Creeds of Christendom, With a History and Critical Notes,* 6th ed. 3 volumes. Grand Rapids, MI: Baker. Online: http://www.ccel.org/ccel/schaff/creeds1.html.

Schlier, Heinrich. 1965. "Thlibō, Thlipsis." In *Theological Dictionary of the New Testament,* vol. 3, edited by Gerhard Kittel, 139-48. Translated by Geoffrey Bromiley. Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Schnabel, Eckhard. 2011. *40 Questions About the End Times.* Grand Rapids: Kregel. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0825438969.

Schreiner, Thomas. 2003. *1, 2 Peter, Jude* (NAC 37). Nashville, TN: Broadman & Holman.

Schüssler Fiorenza, Elisabeth. 1980. "Apokalypsis and Propheteia: The Book of Revelation in the Context of Early Christian Prophecy." In *L'Apocalypse Johannique et l'Apocalyptique dans le Nouveau Testament,* edited by J. Lambrecht, 105-28. Leuven: University Press.

———. 1991. *Revelation: Vision of a Just World* (PC). Minneapolis: Fortress, 1991.

Scofield, C. I., ed. 1967. *The New Scofield Reference Bible.* New York: Oxford.

Shea, William. 1985. "The Parallel Literary Structure of Revelation 12 and 20." *Andrews University Seminary Studies* 23: 37-54. Online: https://www.andrews.edu/library/car/cardigital/Periodicals/AUSS/1985-1/1985-1-04.pdf.

Shepherd, Norman. 1974. "The Resurrections of Revelation 20." *Westminster Theological Journal* 37: 34-43.

Silva, Moisés, ed. 2014. *New International Dictionary of New Testament Theology and Exegesis,* 2nd ed. 5 volumes. Grand Rapids, MI: Zondervan.

Sittema, John. 2013. *Meeting Jesus at the Feast: Israel's Festivals and the Gospel.* Grandville, MI: Reformed Fellowship.

Smalley, Stephen. 2005. *The Revelation to John.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Smith, Christopher. 1990. "The Portrayal of the Church as the New Israel in the Names and Order of the Tribes in

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Revelation 7.5-8." *Journal for the Study of the New Testament* 39: 111-18.

Smith, Chuck. 1980a. *The Tribulation and the Church.* Costa Mesa, CA: The Word for Today.

_____. 1980b. *What The World Is Coming To.* Costa Mesa, CA: The Word for Today.

Smith, Wilber. 1962. "Revelation." In *The Wycliffe Bible Commentary,* ed. Charles Pfeiffer and Everett Harrison, 1491-1525. Chicago: Moody.

Stefanovic, Ranko. 2002. "Finding Meaning in the Literary Patterns of Revelation." *Journal of the Adventist Theological Society* 13: 27-43. Online: http://www.atsjats.org/publication_file.php?pub_id=60&journal=1&type=pdf.

Steinmann, Andrew. 1992. "The Tripartite Structure of the Sixth Seal, the Sixth Trumpet, and the Sixth Bowl of John's Apocalypse (Rev 6:12-7:17; 9:13-11:14; 16:12-16)." *Journal of the Evangelical Theological Society* 35: 69-79. Online: http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/35/35-1/JETS_35-1_069-079_Steinmann.pdf.

Stephens, Mark. 2011. *Annihilation or Renewal?* Tübingen, Germany: Mohr Siebeck.

Storms, Sam. 2013. *Kingdom Come: The Amillennial Alternative.* Tain, Scotland: Mentor.

Strand, Kenneth. 1981. "The Two Witnesses of Rev 11:3–12." *Andrews University Seminary Studies* 19: 127-35. Online: http://digitalcommons.andrews.edu/cgi/viewcontent.cgi?article=1526&context=auss.

Stylianopoulos, Theodore. 2009. "'I Know Your Works': Grace and Judgment in the Apocalypse." In *Apocalyptic Thought in Early Christianity,* edited by Robert Daly, 17-32. Grand Rapids: Baker Academic.

Summers, Ray. 1960. "Revelation 20: An Interpretation." *Review and Expositor* 57: 176-83.

Thomas, Robert. 1967. "The Chronological Interpretation of Revelation 2-3." *Bibliotheca Sacra*: 321-31.

_____. 1992. *Revelation 1-7: An Exegetical Commentary.* Chicago: Moody.

_____. 1994. "An Analysis of the Seventh Bowl of the Apocalypse." *The Master's Seminary Journal* 5:73-95. Online: https://www.tms.edu/m/tmsj5d.pdf.

_____. 1995. *Revelation 8-22: An Exegetical Commentary.* Chicago: Moody.

_____. 1998. "A Classical Dispensationalist View of Revelation." In *Four Views on the Book of Revelation,* 179-229. Grand Rapids, MI: Zodervan. Online: https://books.google.com/books?isbn=0310872391.

Torrance, Thomas. 1959. *The Apocalypse Today.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Travis, Stephen. 1982. *I Believe in the Second Coming of Jesus.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Trench, Robert. 1989 (reprint). *Synonyms of the New Testament.* Grand Rapids, MI: Baker. Online (9th edition): https://books.google.com/books?id=WzdNAAAAMAAJ.

Ulfgard, Håkan. 1989. *Feast and Future: Revelation 7:9-17 and the Feast of Tabernacles*. Stockholm: Almqvist & Wiksell.

VanGemeren, Willem. 1990. *Interpreting the Prophetic Word.* Grand Rapids, MI: Zondervan.

Venema, Cornelis. 2000. *The Promise of the Future.* Carlisle, PA: Banner of Truth.

Victorinus of Pettau. 2012. *Commentary on the Apocalypse*. In *Ancient Christian Texts: Latin Commentaries on Revelation*, translated and edited by William Weinrich, 1-22. Downers Grove, IL: IVP Academic. Online (another edition): http://www.bombaxo.com/victapoc.html.

Hakimiliki © 2010-2017 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Vos, Geerhardus. 1979 (reprint). *The Pauline Eschatology.* Grand Rapids, MI: Baker.

Waldron, Samuel. 2000. "Preterism." In *Lecture Notes on Eschatology,* no pages. Online: http://www.vor.org/truth/rbst/escatology00.html.

Waltke, Bruce. 1988. "Kingdom Promises as Spiritual." In *Continuity and Discontinuity: Perspectives on the Relationship Between the Old and New Testaments,* edited by John Feinberg, 263-87. Westchester, IL: Crossway.

Walvoord, John. 1966. *The Revelation of Jesus Christ.* Chicago: Moody.

White, R. Fowler. 1992. "Death and the First Resurrection in Revelation 20: A Response to Meredith G. Kline." Unpublished paper presented at the Eastern Regional meeting of the Evangelical Theological Society held in Lanham, Maryland on 3 April 1992. Theological Research Exchange Network No. ETS-0524 (www.tren.com).

_____. 1999. "On the Hermeneutics and Interpretation of Rev 20:1-3: A Preconsummationist Perspective." *Journal of the Evangelical Theological Society* 42: 53-68. Online: http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/42/42-1/42-1-pp053-068_JETS.pdf.

_____. 2000. "Agony, Irony, and Victory in Inaugurated Eschatology: Reflections on the Current Amillennial-Postmillennial Debate." *Westminster Theological Journal* 62: 161-76.

Witherington, Ben. 2003. *Revelation* (NCBC). Cambridge, England: Cambridge University Press. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0521000688.

Yarbro Collins, Adela. 1977. "The Political Perspective of the Revelation to John." *Journal of Biblical Literature* 96: 241-56.

_____. 1998. "The Book of Revelation." In *The Encyclopedia of Apocalypticism,* vol. 1, edited by John Collins, 384-414. New York: Continuum.

Yilpet, Yoilah. 2006. "Zechariah." In *Africa Bible Commentary*, edited by Tokunboh Adeyemo, 1077-92. Nairobi: WordAlive.

Zodhiates, Spiros. 1993. *The Complete Word Study Dictionary: New Testament,* rev. ed. Chattanooga, TN: AMG.

MWANDISHI

Jonathan Menn anaishi Appleton, WI, USA. Alipokea shahada ya kwanza elimu ya siasa (B.A. in political science) kutoka Chuo kikuu cha Wisconsin-Madison, ambapo alitunukiwa shahadaa ya heshima kutokana na kufaulu kwa viwango vya juu, mnamo mwaka wa 1974, akajumuika na Phi Beta Kappa ambayo ni taasisi ya heshima katika kijamii. Baadae akapata J.D. ambayo ni shahada ya juu ya sheria kutoka Shule ya sheria, Cornell magna cum laude, mnamo mwaka wa 1977, na akajumuishwa kwenye "Order of the Coif legal honor society" ambayo ni taasisi inayoheshimika katika jamii inayofanya kazi za kisheria. Akaitumia miaka 28 iliyofuata akifanya kazi za uanasheria, kama wakili, wa huko Chicago na baadaye kama mmiliki mwenza wa Shirika la mawakili liitwalo Menn Law Firm kule Appleton, WI. Akawa muamini na mfuasi wa Yesu Kristo tangu mwaka wa 1982. Alifundisha masomo ya Biblia darasa la watu wazima kwa miaka kadhaa. Kukua kwa pendo lake katika Thiolojia na Huduma vilimfanya aende akatafute Shahada ya Uzamili ya mambo ya Mungu (Master of Divinity) katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity School huko Deerfield, IL. Alipokea shahada yake ya M.Div. kutoka kwa TEDS, summa cum laude, mnamo Mei 2007. Kati ya mwaka 2007 – 2013 alikuwa mkurugenzi wa Afrika Masahariki wa huduma ya Equipping Pastors International (EPI). Na sasa Jonathan ni mkurugenzi wa huduma ya kuwawezesha viongozi wa kanisa Afrika Mashariki Equipping Church Leaders East Africa. (ECLEA). Kwa ujumla, kazi zake za mafundisho aliyoandika ya masomo ya Bibilia, yanapatikana kwenye: **www.eclea.net**. Unaweza kuwasiliana na Jonathan kupitia na anuani hii: **jonathanmenn@yahoo.com**.